ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi – Tarehe 2 Julai, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 37

Ukosefu wa Vyombo vya Usafiri kwa Majaji Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante sana kabla ya yote naomba uniruhusu kwa dakika moja tu kumshukuru Mwenyezi Mungu na vile vile nimshukuru Mwenyekiti wangu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) nilipokuwa sipo alikuwa akiniwakilisha, namwambia aendelee na uzi huo huo.

Mahakama Pemba zinakabiliwa na uhaba wa gari kwa Majaji wanaokwenda kusikiliza kesi kisiwani humo na kulazimika kutumia gari inayokabiliwa na uchakavu kinyume na hadhi yao.

a) Je, serikali ina mpango gani wa kuweka gari japo mbili kwa ajili ya Majaji wa Mahakama Kuu.

b) Ni muda gani sasa tangu mazingira ya uhaba wa gari kujitokeza Kisiwani humo na lini tatizo hilo litaondoka.

c) Kutokana na mazingira hayo serikali haioni ndio chanzo cha Majaji kutokwenda kwa wakati kusikiliza kesi na kuzitolea hukumu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mahakama zetu zimekuwa zikikabiliwa na matatizo mbali mbali, likiwemo tatizo la usafiri hususan kwa upande wa Pemba. Katika kukabiliana na tatizo hilo, wizara yangu kupitia Mahakama imeshapeleka gari moja huko Pemba ili kupunguza tatizo la usafiri kwa matumizi ya Mahakama Kuu. Wizara itahakikisha kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari mpya na matengenezo ya magari chakavu yaliyoko Mahakama Kuu Pemba ili kupunguza tatizo hilo.

(b) Mhe. Spika, suala la uhaba wa gari kwa matumizi ya Mahakama Kisiwani Pemba ni la muda mrefu na litaondoka mara tutakapoweza kupata fedha za kununulia magari mapya.

(c) Mhe. Spika, uhaba wa usafiri sio chanzo cha Majaji kutokwenda kusikiliza kesi Kisiwani Pemba. Aidha, Majaji wa Mahakama Kuu wamekuwa wakienda Pemba mara kwa mara kwa lengo la kusikiliza kesi kwa mujibu wa utaratibu uliopangwa na Mahakama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama sikumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kusema kweli na niombe Mawaziri na Manaibu Waziri wafate nyayo zake kwa kuliwezesha Baraza hili. Mheshimiwa baada ya shukurani hizo naomba kuuliza swali moja lenye fungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri Majaji ni watu wenye hadhi kubwa, lakini kutokana na hali yao hasa Kisiwani Pemba panapokuwa na Majaji wawili katika utekelezaji wa majukumu yao ya kazi huwa kuna usumbufu wa gani. Je, wizara yako itachukua hatua gani ya dharura kusimamia tatizo hilo.

b) Mhe. Naibu Waziri ulipokuwa unajibu swali la msingi ulisema Mahakama zetu zinakabiliwa na matatizo mbali mbali, hilo nikushukuru sana kwa maneno yangu niliyosema jana mimi kutounga mkono bajeti nafikiri utayaafiki. Je, umejipanga vipi kuongeza bajeti mwaka huu ukijua kwamba Mahakama zetu ndio kimbilio la wanyonge wa nchi hii. Hivyo, umejipanga vipi kuongeza bajeti hii baada ya kukwambia kwamba ni ndogo haikidhi na umeyaona mwenyewe leo ushahidi wake hata masaa 24 hayajafika umekiri mwenyewe mbele yetu. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nakubali kuwa Majaji wana hadhi kuu miongoni mwa watu ambao wanahitajika kuwa na hadhi. Sasa kwa kuwa Majaji wa hadhi kama Mhe. Mwakilishi ulifatilia swali langu mama ni kwamba tayari wizara imeshapeleka gari moja, gari hiyo kwa ajili ya kuwahudumia hao Majaji. Kwa hivyo, tumepeleka gari hilo kwa sababu tunajua kwamba Majaji wana hadhi kubwa na wao wanahitaji usafiri kule Pemba, kwa hiyo gari moja Mhe. Mwakilishi tayari tumeshapeleka na nyengine tunafatilia.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali namba (b) amesahau.

Mhe. Spika: Swali la (b) hujalijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa bajeti ya Mahakama ni ndogo na umeniomba kukueleza tumejipanga vipi ili kuhakikisha kwamba bajeti inakuwa na mvuto katika Mahakama.

Mhe. Spika, bajeti ambayo tunayo ya Mahakama kipindi hiki pamoja na kwamba inaonekana ni haba lakini tutajitahidi kadiri tuwezavyo kuhakikisha kwamba bajeti inayofuata tunahakikisha Mahakama inakuwa na kiwango kikubwa na fedha ili kuyatatua yale yote ambayo mwaka huu yatakuwa bado hayajafanyiwa kazi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimpongeze sana na mimi Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini mbali na majibu yake amesema kwamba wizara imeshanunua gari moja na inatenga fedha kununua gari jengine. Lakini vile vile kuna magari machakavu ambayo yanahitajika kutengenezwa. Je, ni magari mangapi machakavu ambayo yanahitajika kutengenezwa katika Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli katika jawabu langu mama nilieleza kwamba kuna baadhi ya magari machakavu ambayo yanahitajika kufanyiwa matengenezo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi aniruhusu kumletea hiyo idadi ya hayo magari machakavu yaliyokuwepo huko Pemba ambayo yanahitaji kufanyiwa matengenezo kwa maandishi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante nashukuru kwa kuweza kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, na mimi sina budi nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, kwa kuwa amesema wizara hii imejipanga kuhusina na suala la usafiri wa Majaji. Je, vipi kuhusiana na makaazi ya Majaji hao Kisiwani Pemba zipo nyumba zinazostahiki kukaa Majaji hao au wanaishi mahotelini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ningependa kumjuulisha Mhe. Mwakilishi kwamba serikali haina utaratibu wa kuwakodia Majaji wengine ukiondoa Mhe. Jaji Mkuu, Majaji wetu wote wanaishi katika makaazi yao binafsi na serikali hutoa posho mbali mbali kwa Majaji hao ikiwemo posho la nyumba.

Nam. 61

Gharama za Kuunga Umeme Bado Kubwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kumekuwa na kilio kwa wananchi wanyonge masikini kushindwa kumudu gharama kubwa ya kuunga umeme, ambapo hivi sasa umeme umekuwa na umuhimu zaidi kwa kuwa ni sehemu ya wananchi kujifanyia miradi ya kuongeza vipato vyao.

Je, kwa nini shirika halipeleki nguzo za umeme kama sehemu ya miundombinu halafu mwananchi akalipia gharama za kuunga peke yake, badala ya kubebeshwa mzigo wa kulipa nguzo na uungaji ambazo ni kubwa sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imezingatia ushauri wa Mhe. Mwakilishi huyo wa kuwasogezea wananchi huduma ya umeme karibu na maeneo yao. Hata hivyo, kutokana na gharama kubwa za uendeshaji zinazolikabili Shirika la Umeme hivi sasa ni vigumu kutekeleza kikamilifu zoezi la kusogeza huduma kwa mwananchi mmoja mmoja. Kutokana na hali hiyo inapelekea haja kwa wananchi kuendelea kuchangia gharama za uungaji umeme. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa ya chombo hiki, unajua binadabu siku zote hutakiwa kumaliza maneno mengine huweka akiba. Mhe. Naibu Waziri alijibu swali Nam. 8 akajibu na Waheshimiwa Mawaziri waliokuwepo mbele wakampigia makofi sasa sijui makofi yake yaliashiria vipi, naomba nisome *hansard*.

"Mhe. Spika, serikali haiogopi hasara kwa kunufaisha wananchi wake". Unatujibu nini Mhe. Naibu Waziri, uko tayari kujiuzulu baada ya kushindwa kusimamia matatizo yako. Hii hapa si maneno yangu" serikali haiogopi hasara kwa ajili ya wananchi wake", leo unatujibu nini humu ndani.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku naomba ukae ili waziri mwenyewe atoe ufafanuzi hapo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli serikali haiogopi hasara na sisi nataka tumuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Shirika la Umeme linabeba mzigo mkubwa kwa sababu ya kuwahudumia wananchi wake. Bei ya umeme ambayo tunaitoa basi serikali ina-*subsidize* kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata umeme kwa bei nafuu. Lakini mzigo tunauchukua ni mkubwa tunahakikisha tunafikisha umeme na tunahakikisha kwamba wananchi wanapata umeme kwa bei nafuu. Kama tukisema gharama ambazo tunazikabili zote tuwabebeshe wananchi basi wananchi wengi watakuwa hawawezi kupata hiyo huduma. Kwa hiyo, nataka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi sisi tupo kwa sababu ya watu na watu hawa tutawahudumia ipasavyo na ndio maana tunafika pahala kama shirika tubebe mzigo, kama serikali tubebe tuhakikishe wananchi wanapata huduma iliyo bora. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, mimi nataka kuuliza lifuatalo. Kwa kuwa sera ya serikali ni ya kuwasaidia wananchi katika huduma za umeme na maji safi na salama, na kwa kuwa sasa hivi Shirika la Umeme wanazo nguzo nyingi.

Je, wizara yake iko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi na hasa wa Jimbo la Mfenesini kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri wa mkopo ambao atachukua mwenyewe Mhe. Mwakilishi dhamana ili kuangalia upelekaji wa nguzo katika Jimbo la Mfenesini na kuondoa tatizo la wananchi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kweli sisi tuko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi na hilo kila siku

tunalisema, na kusema kweli sisi tupo kwa sababu ya watu. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi kama anataka mashirikiano mazuri na anataka wananchi wake wafikishiwe umeme haraka iwezekanavyo, basi watu wangu wapo kwa ajili yake tunamkaribisha na taasisi yangu iko wazi tunamkaribisha sana ili aweze kuja kushirikiana na nasi na nguzo tunahakikisha tunazo ili wananchi waweze kupata hizo huduma. Ahsante.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Waziri ningependa kujua juu ya kwamba wananchi wa Zanzibar ni masikini sana lakini wanakubali kulipa ile gharama ya kupelekewa umeme ndani kwao ikiwemo kununua mita na umeme. Ni sababu zipi hasa licha ya umasikini wao, wameshatafuta pesa wamelipa na ni kwa nini wanacheleweshwa kwa muda mrefu kupelekewa huduma hiyo.

b) Ni kiasi gani hasa serikali inawa-*cost* kununua nguzo hizi huko wanakozitoa mpaka kufika hapa na ni kiasi gani wanauziwa wananchi wa Zanzibar bei ya hapa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ucheleweshwaji wa mita na vifaa vyengine inatokana na *transport* kutoka huko ambako tunavichukua hadi kufika Zanzibar, lakini kwa kiasi kikubwa suala hili limetatuka. Sasa kama wapo watu ambao wamelipa na hawajapatiwa hiyo huduma tunaomba tuonane, ili lifanyiwe haraka suala hilo. (*Makofi*)

Nam. 22

Ongezeko la Maradhi ya Kipindupindu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ugonjwa wa kipindipindu umeingia Zanzibar tangu Oktoba mwaka jana na umeathiri baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na baadae kuenea vijijini na watu kadhaa kuugua maradhi hayo na baadhi yao kupoteza maisha.

(a) Watu wangapi walipata maradhi ya kipindupindu na wangapi wamepoteza maisha kuanzia Oktoba mwaka jana hadi April mwaka huu.

b) Wizara kwanini inashindwa kuweka mazingira ya usafi katika masoko, maeneo ya biashara pamoja na maeneo ya makaazi ya watu kwa kutumia kanuni za afya.

c) Sababu gani ugonjwa huu unaendelea kusambaa hadi vijijini licha ya kuwepo wataalamu wa afya pamoja na watumishi wanaotakiwa kutoa elimu ya afya na kusimamia kanuni zake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli visiwa vyetu vinakabiliwa na ugonjwa wa kipindupindu kuanzia mwezi wa Septemba 2015 na sio Oktoba.

(a) Mhe. Spika, takwimu tulizonazo zinaonyesha kwamba hadi kufikia tarehe 30 April, 2016 jumla ya wananchi 4,148 walipata maradhi hayo na kulazwa katika vituo 18 vilivyofunguliwa, ambapo wananchi au wagonjwa 64 walipoteza maisha katika kipindupindu hicho.

(b) Mhe.Spika, suala la kuweka mazingira ya usafi katika masoko, sehemu za biashara na maeneo ya makaazi ya watu si jukumu la Wizara ya Afya pekee, hili ni jukumu la kila mmoja wetu zikiwemo taasisi mbali mbali za Serikali na wananchi wenyewe. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na taasisi hizo zina jukumu la kusimamia utekelezaji wa kanuni za afya kama zilivyoelezwa katika Sheria ya Afya na Mazingira Namba 11 ya 2012. Katika kutekeleza jukumu hilo Wizara inafuatilia kwa makini usafi wa maeneo katika mahoteli, maskuli, vyoo katika makaazi ya wananchi. Aidha Wizara inaendelea kutoa elimu ya Afya juu ya kujikinga na maradhi hayo kwa njia mbali mbali ikiwemo redio, simu, mikutano ya jamii, televisheni n.k.

(c) Mhe. Spika, sababu kuu ya kuenea kwa ugonjwa huu wa kipindupindu mjini na Vijijini licha ya juhudi kubwa zinazotolewa na maafisa wa Afya ni pamoja na :-

i. Uharibifu katika miundo mbinu na upatikanaji mdogo wa maji safi na salama kwa baadhi ya maeneo, ambapo hadi sasa kuna baadhi ya wananchi wanatumia maji kutoka vyanzo visivyo salama.

ii. Matumizi madogo ya vyoo ikiwemo utupaji mbaya wa kinyesi katika mazingira yanayotuzunguka hususan utupaji ovyo wa pempasi zenye kinyesi cha watoto na watu wazima.

ii. Muitiko mdogo wa wanajamii juu ya kinga na tahadhari ya ugonjwa huu juu ya kuchemsha maji ya kunywa au kuweka dawa *water guard,* kuosha mikono kabla ya kula na baada ya kutoka chooni, kutumia vyoo pamoja na kutunza usafi wa mazingira kwa maeneo yanayotuzunguka.

Mhe. Spika, naomba kuchukuwa nafsi hii kuwaomba wananchi kufuata kanuni na taratibu za afya ili kuepusha ugonjwa wa kipindupindu kuendelea kusambaa katika nchi yetu. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuishajihisha jamii katika maeneo yao juu ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize masuala madogo sana ya nyongeza, moja yenye kifungu (a) na (b).

Serikali imetumia kanuni gani za afya kupiga karantini watu wasiuze chakula badala ya kwenda katika maeneo ya biashara kutoa elimu ya kuweka usafi ukizingatia ajira nchi hii ni ngumu, hilo la kwanza.

La pili ugonjwa wa kipindupindu umeathiri Unguja na Pemba. Sababu gani za mikahawa na wauza chipsi Pemba wakaruhusiwa kuuza wakati Unguja wakafungiwa, na hivi sasa tayari sehemu nyengine zishafunguliwa na wengine hawataki kufunguliwa, ni sababu gani Wizara yako imechukuwa ubaguzi wa aina hiyo.

Isitoshe Pemba kuna wagonjwa waathirika sehemu ya vitongoji, Wizara yako imeshindwa kuwapokea, jamaa zao ndio ikawatibu. Hebu toa kauli hiyo ya Serikali ili wananchi wapate kufahamu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mwakilishi wa Jimbo la Paje, swali lake la nyongeza ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Wizara ya Afya imetumia kanuni ya afya ya sheria ya mazingira nambari 11 ya mwaka 2012 na inafanya juhudi kubwa na inaendelea na juhudi hizo za kuwaelimisha wananchi kufuata kanuni za afya, ili kuepukana na maradhi na janga kubwa la kipindupindu lililoikumba nchi yetu. *(Makofi)*

(b) Mhe. Spika, si kweli kwamba Serikali imewaachia wananchi wa Pemba wauze biashara zao wafanya wanavyotaka. Tamko lililotolewa na Mhe. Waziri, la kupiga karantini katika kuhusu uuzaji wa biashara lilikuwa linahusu Zanzibar nzima yaani Unguja na Pemba. Sasa kama kuna Pemba ambao wanafanya hili jambo wanafanya biashara zao ni ukaidi wa binaadamu tu, lakini tamko lilihusu kisiwa cha Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nitampa Mhe.Shadya nafasi, halafu nitampa Mheshimiwa mwenye kilemba cha manjano nyuma kule. Mhe. Shadya suala la nyongeza tafadhali.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu, suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Ugonjwa wa kipindupindu tayari umeshakuwa tishio kwa kisiwa cha Pemba baada ya kupunguwa kwa kasi katika kisiwa cha Unguja na hivi sasa imepelekea mwananchi mmoja kupoteza maisha katika kijiji cha Mgogoni, Wilaya ya Chake Chake na kuendelea kuathiri familia katika nyumba ya mtu huyo na Daktari wako kukiri kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi katika kituo cha Vitongoji ambacho wanalazwa wagonjwa hawa.

Je, Mheshimiwa Waziri, Wizara yako imejipangaje kukabiliana na tatizo hili katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya, naomba kumjibu Mhe. Shadya Mohammed, Muwakilishi wa Viti Maalum, suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwa takwimu ya juzi na jana kuna ongezeko kidogo la wagonjwa wa kipindupindu katika kisiwa cha Pemba. Wizara yangu imejipanga kama ilivyojipanga mwanzo kupambana na tatizo la kipindupindu. Itaendelea kutoa huduma kwa wananchi wanaopata kipindupindu lakini pia itaendelea kutoa elimu ya hali ya juu kuhakikisha wananchi wanafuata kanuni za afya na kuepukana na maradhi ya kipindupindu.

Tunawaomba sana, tunawasihi sana Waheshimiwa Wawakilishi kusaidia Wizara yetu ya kutoa elimu katika majimbo yenu, kusaidia kutoa elimu katika familia zenu, kusaidia kutoa elimu katika sehemu mbali mbali kwa sababu nyinyi ni sehemu ya Serikali. *(Makofi)*

Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza suala moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, ametuelezea kwamba wagonjwa 4148 waliopata kipindupindu na 64 walifariki dunia.

Naomba kumuuliza Naibu Waziri, je mpaka sasa ni wagonjwa wangapi ambao wamepata ugonjwa huu wa kipindupindu na ni wagonjwa wangapi ambao wamefariki kwa upande wa Unguja na wangapi kwa Pemba. Naomba kujua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya, napenda kumjibu suala lake la nyongeza Mhe. Maryam, Mwakilishi wa Jimbo la Gando kama ifuatavyo:-

Jumla ya wagonjwa 4148 ni jumla ya Unguja na Pemba lakini kwa Unguja peke yake ni wagonjwa 2576 waliopata maradhi na kutibiwa na kwa Pemba ni 1572. Wagonjwa waliokufa kwa Unguja na Pemba ni 64, kwa Unguja peke yake ni wagonjwa 48 na kwa Pemba ni wagonjwa 16.

Nam. 60

Faida za Mji Mkongwe Kujiunga na UNESCO

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wananchi wamefarijika sana kwa Mji Mkongwe, kuwa hifadhi ya Kimataifa inayotambuliwa na UNESCO.

Je, wananchi wanaweza kuelezwa angalau faida kumi (10) zilizopatikana tangu Mji Mkongwe uwekwe katika hifadhi ya UNESCO.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, uingizwaji wa Mji Mkongwe wa Zanzibar katika orodha wa Mji iliyo ndani ya Uhifadhi wa UNESCO kwa ujumla wake umesaidia sana kuitangaza Zanzibar kiutalii duniani. Aidha, kwa kuzitaja moja baada moja, faida (10) zilizopatikana nazo ni:-

1. Kuingizwa ndani ya tovuti ya Urithi wa Kimataifa. Tovuti hii hutembelewa na watu 80,000 kwa wiki, ambayo inatoa ushawishi mkubwa kwa watalii kutembelea sehemu hizo za urithi ikiwemo Zanzibar. Hivyo ni rahisi zaidi mtalii wa urithi wa utamaduni kuja Zanzibar kuliko mji jirani usio wa Urithi wa Dunia.

2. Mhe. Spika, Zanzibar imepata mvuto mkubwa kwa vyombo vya habari duniani. Mji Mkongwe umeshatangazwa sana CCN, BBC (Heritage Heros), TBS (Japan), DWTV (Ujerumani), France 2 (Ufaransa) n.k. Filamu kadhaa za kumbukumbu *documentary* zimeshatengenezwa, sambamba na tafiti zilizo ndani ya vitabu, *Urban Design, Chaos and Colonial power in Zanzibar* (William C Bissel, Indiana University Press 2011).

3. Mhe. Spika, huwavutia wawekezaji kwa imani ya biashara zao kutangazwa zaidi Kimataifa kwa mfano:-

   (a) Bustani ya Forodhani (Aga Khan Trust for Culture);

   (b) Uhuishaji wa ukingo wa bahari Mizingani (Benki ya Dunia);

   (c) Kuukuza na kuutangaza Mji Mkongwe kama Urithi wa Dunia Sida, Sweden na;

   (d) Kupata maombi mengi mfululizo ya wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kwa mvuto huo.

4. Thamani ya majengo ya Mji Mkongwe imeongoezeka kutokana na hadhi hiyo.

5. Matamasha makubwa yanayotambulika kama: Tamasha la nchi za Majahazi, Sauti za Busara, *Film Festival*, kukubali kuyafanya kwenye eneo finyu la Ngome Kongwe badala ya Amani au Mao Tse Tung, kutokana na hadhi yake.

6. Kuwafundisha wanafunzi uhifadhi, kinadharia na kivitendo na uhuishaji maeneo ya Mji Mkongwe.

   Wanafunzi kutoka Minnesota University, kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Mji Mkongwe wamefanya zoezi la kitaalam. Kuziorodhesha *open spaces* zote na kuzitengenezea kitabu.

7. Mji Mkongwe wa Zanzibar umejenga heshima na hadhi ya Taifa letu kutambuliwa dunia nzima (Brand Name).

8. UNESCO imeweza kujenga uhusiano wa mji wetu na miji mingine ya kihistoria iliyosajiliwa Kimataifa, ulimwenguni.

9. UNESCO inasaidia kusimamia miradi mbalimbali ndani ya Mji Mkongwe kupitia World Bank, European Union (EU) na Mashirika mengine kwa mfano ukarabati wa Bharmal Building (Manispaa) na ukarabati mkubwa wa Kanisa la Mkunazini na ukarabati wa jengo la forodha ya zamani.

10. UNESCO inasaidia kuongeza ujuzi wa wafanyakazi wa Mamlaka kwa kuwajengea uwezo wa kiutendaji kwa kuandaa program za muda mfupi na mrefu nje ya nchi, kwa mfano: Baadhi ya wafanyakazi wamepata nafasi ya kwenda Sweden, Italy (ICCROM) na nchi nyengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika;

(a) Wananchi hasa wakaazi wa Mji Mkongwe yaani wapiga kura wako Mhe. Naibu Waziri, wamenufaika vipi moja kwa moja na uhifadhi wa Mji wakati huduma za maji bado upatikanaji wake ni wa shida wakati unatakiwa uwe njia ya mfano mji huo kuutangaza na vile vile Mji huo taa hauna. Mheshimiwa wapiga kuwa wako wanakusikia.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuyalinda majumba ya Mji Mkongwe ambayo yako katika hali ya hatari na usalama wa watu na majumba hayo kuwa machakavu, yanazidi kuporomoka majumba kule na Wizara inayosimamia hayo haijachukuwa hatua yoyote mpaka hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, napenda kumjibu Mhe. Jaku Ayoub Hashim, Muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Paje suala lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na yeye kwamba kwa kipindi hiki mimi ndiye Muwakilishi halali wa Jimbo la Malindi na ninaahidi Baraza hili tukufu nitakuwa muaminifu kwa wananchi wote wa Jimbo langu la Malindi bila ya kujali itikadi zao chama na yale maendeleo ambayo nimeyatangaza nakutoa ahadi basi tutayatekeleza kwa

ukamilifu. Na kama vile alivyoniuliza Mji Mkongwe kwa kuwa katika Jimbo langu, basi mimi naahidi kwamba wananchi wangu wa Jimbo la Malindi watafaidika na ajira zilizokuwepo, kwa sababu kuna mahoteli mengi pale na vile vile kuna ajira zilizokuwa si sekta rasmi kama vile watu wanaokodisha magari na vile vile kuna ajira zinazopatikana katika Beit-el-ajaib na sehemu nyengine nitahakikisha kwamba na wananchi wangu wa Jimbo la Malindi na wenye uwezo wa kupata hizo kazi basi na wao wanafaidika na hayo.

Swali (b) la nyogeza napenda kumuarifu Mhe. Hashim Jaku kwamba matengenezo ya Mji Mkongwe yanapofanyika, basi vile vile wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe wanashirikishwa na matatizo hayo anayosema kwamba taa hazipo. Inawezekana yakawa ni matatizo ya kiufundi lakini mimi nitahakikisha kwamba mji wetu ule unaghara na sehemu zenye kasoro zozote zile tutaziondosha kwa kushirikiana na yeye ambaye ni mdau mkubwa wa Jimbo la Malindi.

Mhe. Spika: Mhe. Shihata sijakusikia leo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, kwa ruhusa yako ninaomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa maelezo mazuri aliyoyaeleza juu ya faida zinazopatikana katika kulinda au kuuendesha Mji Mkongwe. Lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, suala langu lipo kama ifuatavyo:-

Watalii wanaotoka katika nchi za nje na Wazanzibari mpaka wanafunzi wetu na sie watu wazima huwa wanapendelea sana Forodhani - Beit-el-ajaib kuona hadhi ya jumba lile na historia zilizokuwemo ndani yake. Lakini kwa bahati mbaya jengo hili hivi sasa liko katika hali mbaya na huo urithi tunaosema kwamba ni moja wapo ambapo UNESCO wanatusaidia. Je, Wizara ina mpango gani wa kulijenga jengo lile upya vile lilivyo alau kulikarabati uzuri, ili lilete faida zaidi kwa Serikali yetu na wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, napenda kumjibu suala lake Mhe. Ali Suleiman Shihata, lakini naomba radhi kabla ya kumjibu Mhe. Ali Suleiman Shihata, Mhe. Jaku aliuliza kuhusu majengo yale kuwa katika hali ya hatari. Ni kweli majengo mengi yapo katika hatari na sisi tumeorodhesha majengo 40 ambayo hayawezi kukalika

sasa hivi na tumeshawaarifu watu wake waondoke katika majengo hayo. Kwa hiyo napenda kumjibu suala lake lile ambalo nilimuona alitaka kuuliza utaratibu.

Nikiendelea na suala la Mhe. Ali Suleiman Shihata, Mwakilishi wa Jimbo la Kijito Upele ni kama ifuatavyo:-

Tunafahamu fika kwamba Beit-el-ajaib hivi sasa kuna baadhi ya sehemu limeanguka na lipo katika hatari ya kuanguka zaidi. Kwa hiyo sisi kama Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Oman tayari wameshaleta wachunguzi wa kuja kuliangalia lile jengo na ilikuwa mwezi huu wa Juni uanze ukarabati. Kama kawaida utengenezaji wa majengo yote yaliyoko katika Mji Mkongwe lazima kwanza tupate kibali kwa UNESCO. Tayari tumeshapeleka ramani ya kuhusu ukarabati wa jengo UNESCO na wamesema wakati wowote watatujibu na baada ya kutujibu tu basi Serikali ya Oman na sisi tutakaa pamoja kutangaza zabuni, ili tuanze kulijenga lile jengo la hifadhi katika Mji Mkongwe na Uwasilia wake.

Mhe. Spika: Swali la mwisho la nyongeza kwa Wizara hii Mhe. Dimwa, sijakusikia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Spika, nikushukuru sana, pamoja na majibu marefu na mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala dogo sana la nyongeza.

Mhe. Waziri, kwa sababu tuna uzoefu mkubwa sana UNESCO kujibu majibu yoyote yanayopelekwa kwa kuuhifadhi Mji Mkongwe. Unauthibitishiaje umma wa Wazanzibari kuwa taarifa hizo zitakuja haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzo, Mawasiliano na Usafirishaji, napenda kumjibu Mhe. Mohammed Said Dimwa, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli tumekuwa makini katika kuhakikisha kwamba haya majibu yanakuja haraka na hivi sasa tumeituma timu yetu ya wataalamu Arusha kuna mkutano kule kuhusu UNESCO kwa nchi za Afrika ziliopo katika urithi wa duniani, ili kuhakikisha kwamba hili suala linafanyiwa kazi kwa haraka na UNESCO wametujibu kwamba watatupa jibu kipindi hiki na katika mkutano

utakaofanyika Uturuki Julai mwaka huu. Basi nina hakika kwamba itakuwa tayari tumeshapata jibu na matengenezo yake kwa kushirikiana na Serikali ya Oman yataanza mara moja ili Beit-el-ajaibu liendelee kutoa huduma kama kawaida.

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Utaratibu Ibara ya 56 ya kanuni, inazungumza kwamba kwa idhini ya Baraza yoyote kati ya kanuni hizi inaweza kuwekwa kando kwa madhumuni makhsusi baada ya Mjumbe yeyote atakayetoa hoja.

Hoja yangu inakwenda katika Kanuni Ibara ya 49 ambayo inasema kwamba:

"Bila kuathiri masharti ya Katiba au Kanuni hizi, Mjumbe yeyote anaweza kupendekeza jambo lolote lijadiliwe katika Baraza kwa kutoa hoja, yaani kwa kutoa pendekezo lililokamilika na liwe limewekwa katika hali inayoweza kueleza uamuzi wa Baraza".

Mhe. Spika, katika hayo jana katika mswada wetu lilikuja suala zima la nyaraka, lakini kwa bahati nzuri au mbaya likakataliwa kujadiliwa. Sasa kutokana na kanuni hizi zinatupa nguvu kuzungumzia hili suala kwa maana ya kuweza kuweka kanuni kando, ukitilia maanani kwamba Wajumbe waliokuwemo humu wengi wetu ni wapya na hilo suala liko *very sensitive* kwa ajili ya nchi yetu na hatujui mustakbali wake umefikia vipi, ndio zimetungwa Kamati teule lakini hatujapewa taarifa yoyote.

Mhe. Spika: Samahani sijakufahamu, hilo jambo ambalo unataka lijadiliwe ni jambo gani?

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ni juu ya suala la upotevu wa nyaraka za serikali, ukichukulia maanani kwamba sisi sote humu ni wapya na tuna hamu lile jambo lijadiliwe ili tujue. Kwa sababu sio tunakuja humu kama vibiriti, tunatupiana vitu halafu hatujui nchi imekuwa hivi. Sasa kupitia kanuni hizi ningetoa muongozo huo Mheshimiwa kwamba, tunaomba tuweke kanuni kando za Baraza lako la Wawakilishi ili tuweze kulijadili lile suala la upotevu wa nyaraka.

Mhe. Spika: Hizi nyaraka zimepotelea wapi hebu kuwa wazi kidogo Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Nyaraka zimepotea kutoka *archive* ambazo nafikiri mpaka Kamati Teule humu katika Baraza lililopita imeundwa lakini hatujapata majibu mpaka dakika hii, tumeambiwa kwamba yashapelekwa na jana katika maswali mmoja kuchangia wengi wetu tulikuwa na haja au hamu ya kuchangia suala lile. Lakini tukanyamazishwa kwamba tumeambiwa kuwa hili jambo tayari limeshazungumzwa. Kutokana na kanuni hizi zilizokuwemo za Baraza la Wawakilishi zinatupa uhuru kuyaulizia masuala yale.

Mhe. Spika: Ni sahihi unachokizungumza lakini sasa sijakufahamu hoja yako kwamba lilikuwa ni mjadala unaohusu hii wizara ambayo ipo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Waziri wa Miundombinu amemaliza ndio nimekuja kuchukua hayo kwa sababu....

Mhe. Spika: Waziri wa ...

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mheshimiwa nimesimama kwa ibara ya 63.

Mhe. Spika: Nimeshakufahamu kwa mujibu wa kanuni, kila kitu nimeshafahamu, lakini hoja yako sijaifahamu inahusiana na wizara gani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Hoja yangu inahusiana na Wizara ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tutaendelea nayo.

Mhe. Spika: Kwa hiyo ulikuwa unataka kuchangia nini.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mimi nilizungumza kwamba tuweke kanuni kando kwa sababu tumeambiwa jambo lile limeshajadiliwa katika Baraza lililopita kwa hiyo haliwezi tena kujadiliwa. Lakini kutokana na kanuni ya 156 ndio nikasema kwamba kwa idhini ya Baraza yoyote kati ya kanuni hizi inaweza kutengwa kando kwa madhumuni makhsusi baada ya Mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo. Kwa hiyo nilikuwa natumia kanuni ya 49.

Mhe. Spika: Nimekufahamu vizuri Mheshimiwa. Mimi ningekuomba jambo moja iweke vizuri kwa maandishi hiyo hoja yako halafu ilete kwa Spika tutaifanyia huo utaratibu, tutaitafutia nafasi tutaweza kulijadili hilo suala. Kwa sababu wizara yenyewe inayohusika bado ipo hapa na waziri yupo anasikia, nadhani vizuri tungesubiri hapo atakapokuja kujumuisha jioni ya leo tusikie kauli yake anasemaje waziri kuhusiana na suala hilo. Baada ya hapo kama tutakuwa hatukuridhika tutalileta tena humu, tutaweka kando kanuni, tutatafuta muda wa saa moja kwa mujibu wa kanuni, tutalizungumza kwa urefu wake.

Tatizo nililonalo Mheshimiwa idadi ya wachangiaji nilionao na wote nataka wamalizike hivi sasa, ni kubwa sana kwa sasa, nikiichukua saa moja nyengine kwa ajili ya kujadili hilo suala lako ambalo pia ni muhimu. Mimi nadhani liandike halafu lije kwa Mhe. Spika kama alivyofanya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa). Vile vile utaratibu tutaufuata nitakupatia saa moja kwa ajili ya huo mjadala wala haina tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, ni kweli kama ambavyo Mhe. Abdalla Diwani alivyosema kwa mujibu wa kanuni ambayo ameitumia, lakini ni vyema Mhe. Spika, Baraza hili likakumbuka kama kadhia ya nyaraka iliundiwa Kamati Teule. Kamati Teule ilifanya kazi yake na ripoti ile ikajadiliwa na Baraza, na maazimio yakatolewa na serikali ikayafanyia kazi. Kwa maana yake ule mjadala ulishamaliza, hatuwezi kurudia tena mijadala ambayo tayari ilishaamuliwa.

Sasa anachosema Mheshimiwa ni kama turudie kwenye mjadala ambao ulishajadiliwa kwenye Baraza la Nane na maamuzi kutolewa. Sasa kwenye hilo Mhe. Spika, nadhani ungetumia busara kama jambo hili limeshaamuliwa na sio tu kuamuliwa lakini liliundiwa Kamati Maalum Teule na Mwenyekiti wa Kamati ile akapata safari mpaka kwenda Oman kulishughulikia jambo hili, yeye na aliyekuwa waziri Dkt. Mwinyihaji Makame, nadhani wanakumbuka vizuri. Yote hayo ni katika kushughulikia kadhia hiyo na tulipofika nadhani tumefika pazuri na maamuzi yalitoka na Baraza likaridhika na utekelezaji ambao umefanywa na serikali.

Kwa hiyo, kimsingi hili jambo lilishamalizika Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nafahamu pia kwa mujibu wa kanuni kuwa suala ambalo litakuwa limeshatolewa maamuzi haliwezi tena kurudi mpaka kipite kipindi fulani hivi kwa mujibu wa kanuni. Sasa nadhani Mheshimiwa pamoja na majibu yako wewe atakwenda kuangalia halafu tutajaribu kuona tunafanya nini, kwa sababu mimi sikuwepo Barazani wala na yeye hakuwepo. Kwa hivyo, atakwenda kuangalia kwenye *hansard* kwa sababu lipo halafu kama utakuwa hukuridhika tutatafuta namna ya kulitafutia ufumbuzi suala lako Mheshimiwa. *(Makofi)*

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe ukweli kwamba bado tuna watu wengi sana ambao wanataka kuichangia hii wizara, naomba nitoe matangazo mafupi.

Kwanza kabisa naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na zoezi la upigaji picha kwa ajili ya kutayarisha *postal.* Zoezi hili linawahusu Waheshimiwa Wajumbe ambao hawakuridhika na picha walizopiga awali. Aidha, pahali patakapofanyikia zoezi hili ni *VIP Lounge* ya pili badala ya *reading room* na zoezi hilo litaanza saa nne na nusu asubuhi ya leo.

Waheshimiwa tangazo jengine linatoka kwa mafundi ambao walikuwa wanatutaka tunapokuwa tunatumia hizi *microphone* kwanza tuziwashe halafu tujitahidi muwe mnasikika kwa sababu ya kurikodi *hansard*. Kwa sababu inafika pahali hawasikii vizuri kwa hivyo *microphone* mziweke karibu yenu wakati mnapozungumza ili *hansard* iweze kurikodiwa kwa uzuri zaidi.

Baada ya hapo naomba sasa nitoe tangazo moja tu la wageni ambalo ninalo wageni wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ni watatu ambao ni masheha wa Jimbo la Amani na Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ambao hawakufika hapo jana. Karibuni sana muone namna ambavyo Mwakilishi mliyemchagua anavyochapa kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe huo ndio mwisho wa matangazo. Kuhusu utaratibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

UTARATIBU

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, kanuni ya 63(1) Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika, sisi ni Wajumbe wapya suala hili la upotevu na wizi wa nyaraka ni *hot cake* kwa Zanzibar, nchi hii tumerithi kwa wana Mapinduzi wametuachia nchi na nyaraka; nyaraka hizi zimeibiwa hili suala bado halijesha liko *hot cake.* Kwa sababu ripoti tumezisoma hamna kitu. Sasa tunaomba hili suala tuambiwe utaratibu gani, lakini tunataka tulijadili tena tuweze kuwaambia wananchi kama walivyotutuma. Nchi tunayo lakini nyaraka zao hazipo na kuna maneno mengi nje kwamba watu wamekula pesa kuhusu nyaraka hizi.

Mhe. Spika, naomba sana hili suala ni *hot cake*, naomba sana hili suala tusilivyuvyuze, naomba hili suala tusilidharau wala tusiliache na tusimlinde mtu kwa suala hili ni suala *very hot.* Mhe. Spika, naomba utaratibu wako.

Mhe. Spika: Ahsante, nadhani Mheshimiwa tulikuwa tumeshaelewana na maelewano yetu baada ya ule muongozo ambao alikwishautoa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba hili suala lishajadiliwa, sasa kama suala

limeshajadiliwa maana yake lipo kwenye *hansard* kwa hiyo tunapo pahali pa kwenda ku-*refer* kwanza. Kama hatukuridhika huko na tutaangalia na muda kwa mujibu wa kanuni basi linaruhusiwa kuja tena halijazuwiwa. Mimi sikuzuwia, yale ni mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu kwamba suala lisije tena kwa sababu lishawahi kujadiliwa. Limeshawahi kujadiliwa kweli, sisi wengine hatukuwepo Barazani lakini kumbukumbu zipo, kutokuwepo kwetu hakuzuwii kwenda kuangalia kumbukumbu za wakati ule, zimefikia wapi kuhusiana na suala hili na majibu.

Mhe. Waziri bahati nzuri anakuja hapa tukiwa hatukuridhika basi tufuate utaratibu, tulete muongozo kama vile alivyoleta Mhe. Mohammed Said Dimwa. Leteni kwa utaratibu ule mimi Spika nitaamua nini tutakifanya wakati huo. Mimi nadhani tufanye hivyo. Katibu tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana nami asubuhi hii kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia machache katika Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniamsha na pumzi zake na nikaweza kufika katika Baraza lako hili tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii pamoja na watendaji wake wote. Kama nilivyosema mimi mchango wangu utakuwa mdogo, kwa sababu naamini kwamba wenzangu wameshayazungumza mengi na mimi sitaki niyarudie hayo kwa hayo, isipokuwa niseme tu kwamba Mhe. Waziri namjua alikuwa ni bosi wangu, mimi nimetokea Wizara ya Elimu kwa hiyo sitaki nimuwekee mazito.

Mhe. Spika, Isipokuwa nataka nifahamu kwamba tunaamini kuwa nchi yetu inatawaliwa na utawala bora, kama ni hivyo nataka nimuulize Mhe. Waziri

swali langu ili atakapo kuja kutoa majumuisho anieleze kwa kina ili nifahamu na nafsi yangu iridhike.

Mhe. Spika, katika kisiwa cha Pemba kulikuwa na wahasibu wa wizara mbali mbali, katika mwaka 2006 wahasibu hawa walipata mitihani ya kufukuzwa kazi. Katika mwaka huo huo wa 2006 mwezi wa Aprili wahasibu hawa walipelekwa Mahakamani, lakini katika mwaka huo kesi ikaondoshwa na baadae mwezi wa Septemba kesi hii ilipelekwa tena Mahakamani, iliendelea mpaka mwaka 2013, Mahakama ikaamuru kwamba washtakiwa hawa hawana kosa la kujibu na warudishwe makazini.

Mhe. Spika, lakini mpaka nasimama hapa huu ni mwaka 2016 watu hawa hawakurudishwa kazini na hawakuambiwa chochote. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze nini hatima ya watu hawa, kwamba Mahakama iliamua warudishwe kazini na barua waliandika na wengine wakafika mpaka kuandika kwa Katibu Mkuu Kiongozi lakini hakuna majibu yaliyoendelea. Kwa hiyo, hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa naomba anieleze kwa kina kuhusu mustakabali wa watu wetu hawa ambao ni wanyonge wana familia zinawategemea na wengine ukiangalia bado ni vijana, damu inachemka wana uwezo wa kufanya kazi. Hivyo Mhe. Waziri atapokuja hapa anieleze vizuri.

Mhe. Spika, naomba pia nizungumzie jambo jengine kwa ufupi nalo ni suala zima la vyeti vya kuzaliwa. Nimpongeze kwanza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alivyokuwa akitoa majumuisho ya hotuba yake alisema kwamba, kwenye ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa vitu vyote viko sawa na hususan vyeti vya kuzaliwa vitapatikana. Tuiombe serikali kwamba jambo hili lifanywe haraka sana kwa sababu bado kuna watu wetu wameshafika watoto wao kwenda skuli vyeti havijapatikana. Kwa hiyo, tuiombe serikali jambo hili litiliwe mkazo na lichukuliwe hatua madhubuti.

Mhe. Spika, kama nilivyosema nimekuomba dakika tano tu, kwa hiyo naunga mkono hotuba hii, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa katika chombo hiki, lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipatia na mimi nafasi niweze kuchangia machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri.
Kwanza kabisa na mimi nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na

Utawala Bora, yeye pamoja na timu yake ya watendaji kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wamejitahidi wakaweza kutuletea hotuba hii.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 27 ambao unaelezea rushwa. Kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa kuliona hili kwa kukiweka hiki kitengo ambacho cha kuzuwia rushwa. Wenzangu wengi wamechangia hili suala na mimi naomba niongezee.

Mhe. Spika, rushwa ni adui wa haki ambayo lazima tupambane nayo ili haki za wananchi ziweze kupatikana. Kitengo hiki kina kazi kubwa na mimi nitumie fursa hii labda kuwaomba Waheshimiwa wenzangu au wananchi wote kwa ujumla kwamba kitengo hiki lazima tukisaidie kaz, vyenginevyo kitakuwa hakiwezi kupata hayo masuala. Kwa sababu rushwa ni jambo linalotendeka kwa siri, kwa hiyo ni lazima sisi tufanye huo ufichuaji wa kuwafichua wale ambao wanatoa na kupokea hiyo rushwa. Kwa hiyo, nisisitize niombe wananchi na sisi viongozi hapa kwa ujumla wetu lazima tukisaidie kitengo hiki kwa kuyafichua yale maovu na kuwapelekea ili wao waweze kufanya kazi zao kama kawaida.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu katika hii Tume ya Utumishi wa Umma. Tume hii imesema katika kazi zake ambazo imejipangia ni usimamizi wa uajiri na nidhamu kwa watumishi wa serikali. Nataka nimuulize Mhe. Waziri serikali imejipanga vipi kuna sasa ni wakati muwafaka wa kupambana na wafanyakazi wazembe, wachelewaji, wabadhirifu wa mali za umma, ili tuzingatie hotuba ya Mhe. Rais ambayo amekuja kuitoa hapa katika uzinduzi wa Baraza letu la Tisa kuona sasa serikali tunahitaji kujitegemea sisi wenyewe. Kama hatukusimamia vizuri masuala haya ya kuona wafanyakazi wanafanya kazi kwanza kwa muda unaopaswa wa kazi, lakini pia kufika kazini mapema ili wakaweza kufanya shughuli zao kwa wakati waliopangiwa. Sasa mimi niombe kujua serikali imejipanga vipi ili sasa kuona masuala haya yanakwenda kama kawaida, ili tuweze kufikia mahala pazuri.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya *PAC* kwa hotuba yao nzuri na ambayo imefafanua kwa kina kabisa kuonesha ripoti ile imeeleza mengi kabisa. Mimi napenda niungane nao na kwamba ripoti ile imebaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika kitengo kile na mimi naomba nisisitize au nimuulize Mhe. Waziri kwamba, panahitajika wafanyakazi wangapi pale kwa *CAG* ili aweze kufanya kazi zake ipasavyo na lini serikali itamruhusu mama huyu kuwaajiri wafanyakazi wa ofisi ile ili ofisi iweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, tunaelewa kazi kubwa ya ofisi hii na tunaelewa yule mama alivyo mahiri kabisa lazima tumsaidie ili aweze kufanya kazi zake ipasavyo.

Mhe. Spika, niende katika Chuo cha Utawala wa Umma. Kwanza nipongeze kwa kuwepo hivi vyuo ambavyo tayari vijana wetu wapata huduma mbali mbali. Lakini nataka kusema kwa sababu kule Bara juzi nilishituka nilipoona Tume ile ya Vyuo Vikuu uliparaganywa pale kwa kubainika vyeti feki ambavyo vinatumika katika kuwaendeleza watu.

Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri aende akalifanyie uchunguzi hili isijekuwa sisi tunasomesha watu lakini wale wenye sifa wanakosa kupata nafasi na tunachukuwa watu ambao hawana sifa tukijua serikali inategemea kupata watu muhimu ambao watakuwa na sifa na vigenzo vizuri vya kuweza kufanya kazi hizo, tukawa sasa tunabaki na tatizo lile lile. Kwa sababu mtu anakuja na cheti chake inabidi lazima umuajiri katika kazi. Lakini kumbe ukija katika utendaji anashindwa hicho cheti kilikuwa ni feki na tunaendelea kukosa watalamu.

Sasa Mhe. Spika, hili naomba ulifanyie kazi kabla ya kamati hizi hazijaenda kule katika mawizara kufanya ziara zile za kamati. Ili uone likoje uweze kujiridhisha wewe mwenyewe, lakini kamati zikienda kule tukija tukikuta uwoza huu upo Mhe. Waziri hatutakubali hii kwa sababu hichi si kitendo kizuri cha kuwa bado tunahitaji watumishi bora lakini bado tunaendelea kuajiri watu feki na kuwakosesha wenye haki.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchangu nije katika ukurasa wa 37 ambao unamuelezea Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, ripoti ya *PAC* wakati inawasilishwa ilieleza kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu inatakiwa kumalizia eneo lililobaki kama vile kibanda cha mlinzi kwa kutumia fedha za *OC*. Kitendo ambacho kinanyima shughuli zile za kawaid kufanyika. Je, Mhe. Waziri hadi hivi sasa Afisi hii imetumia kiasi gani cha fedha za *OC* kwa ajili ya kumalizia eneo hilo lililobakia wanalotakiwa kulijenga kwa fedha za *OC*. Mheshimiwa utakapokuja hapa naomba unipatie majibu hayo ili na wao waweze kuwa salama katika utendaji wa kazi zao.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangi niende katika ukurasa wa 35 ambao unaelezea masuala ya usimamiaji wa mambo ya dini. Mhe. Spika, hapa kuna suala zima la usajili wa misikiti na madrasa zetu hizi. Sasa mimi nilitaka kujua tu kitengo hiki cha Mufti kinajishughulisha vipi jinsi ya kuwahamasisha walimu wa madrasa kuja kusajili hizi madrasa zao na hawa maimamu kusajili misikiti yao ili vitambulike kisheria na ikiwa inatokezea misaada ya vijana wale ambao wanapatiwa elimu za kwenda kusoma nje, ili na wao hawa waweze

kutambulika kisheria. Tena mimi naomba sana hili Mhe. Waziri angalia sehemu za vijijini kuna wasomi wengi wa dini na wao wapatiwe nafasi hizi zinapojitokeza, ili na wao waweze kufaidika.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika kitengo cha Utawala Bora. Mhe. Spika, nakumbuka hapo nyuma wizara iliwahi kutwambia kwamba suala hili la Utawala Bora kuna wizara hizi ambazo zilipangiwa kama ni *pilot area* kwa ajili ya kuwa wao kama ni muonekano wa utangulizi wa kuweza kufanikisha katika zile wizara nyengine zitaweza kufanya vizuri. Mimi nilikuwa nataka kujua tangu imefanyika hiyo mpaka muda huu je, labda tuweza kupata mafanikio gani katika suala hili la Utawala Bora kuona sasa kazi zetu kiofisi zinafanyika vizuri kwa tangu tumelianzisha suala hili. Lakini je, pia tumekumbana na changamoto gani ambazo bado zinatakiwa ili tuweze kuihudumia jamii katika hali nzuri na tukielewa kuwa jambo lolote la kuhudumia jamii ni kazi, kwa sababu kunahitajika pia unyenyekevu mkubwa ili watu wetu tuweze kuwaridhisha katika huduma zetu.

Mhe. Spika, pia niseme katika suala la Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Spika, pia niumuombe Mhe. Waziri kufanya ziara ya makusudi kule kiswani Pemba kwa sababu kunaonekana kuna malalamiko ya wananchi wanasema kwamba pale wafanyakazi hawafiki kwa wakati muafaka kazini na wanashindwa kuwahudumia wananchi ipasavyo. Naomba hili wewe ulifanyie utafiti uende ufanye ziara za mshitukizo ili uweze kuona na kugundua hili.

Mhe. Spika, nije katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, niipongeze sana tume hii kwa kazi na nzuri ambayo wanaifanya kwa kutupatia elimu wananchi inayohusu mambo haya ya sheria, hasa kule kwetu vijijini ambapo kulikuwa na upungufu mkubwa wa kuelewa masuala haya ya kisheria. Nawapongeza sana kwa kazi hii ambayo wanaifanya ambayo elimu ile itaweza sasa kutusaidia na wao bado wasichoke, waendelee kutoa elimu ile ili elimu hii ya kisheria ikijulikana wananchi tunaweza kutatua matatizo yetu mengi kupitia wao. Mie nawapongeza sana kitengo hiki.

Mhe. Spika, mimi nilisema niseme tu machache kupitia wizara hii na kwa dhati kabisa naomba nichukuwe fursa hii kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu wote waweze kuipitisha kwa moyo mmoja, ili Mhe. Waziri aweze kufanya kazi zile ambazo kapangiwa katika kipindi hiki. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kunipa afya njema nikaweza kusimama hapa na mimi nikatoa mchango wangu kwa ajili ya mustakbali wa taifa letu.

Mhe. Spika, awali ya wote napenda kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba na Utawala Bora kwa uwasilishaji wake mzuri wa kitabu hiki. Mhe. Waziri ni mwalimu wetu, ni mtu wetu, ni kiongozi wetu wa siku nyingi kwenye skuli, katufundisha wengi. Kwa hiyo, hatuna budi kumpongeza, pazuri tutamsifu na penye kasoro tutamuelekeza kwamba mwalimu hapa kiodgo mambo si mazuri. Lakini kwa ujumla napenda kutoa shukurani za dhati kwake.

Pia nitakuwa mkosefu wa fadhila nikikosa kuwashukuru na kuwapongeza mawaziri waliopo chini ya kamati zangu, Waziri wa Nchi (OR) Baraza la Mapinduzi nampongeza kwa dhati na kwenye nafsi yangu naamini ni kiongozi bora mchapakazi na pia Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, sasa nataka niende kidogo katika mchango wangu kabla muda wangu haujapotea sana kwa sababu kuna mambo kidogo tutayagusia kidogo kidogo.

Mhe. Spika, kwanza mimi naomba nichukuwe fursa hii kuchangia kwenye mambo ya kisheria. Mhe. Spika, kwenye mambo ya sheria kuna jambo ambalo limekuwa ni kero na baadhi ya manung'uniko kwa wananchi wetu kutokana na mgongano wa kisheria uliokuwa upo kwenye taasisi mbili hizi. Kwa sababu Mhe. Spika, ukitizama katika sheria utakuta kwamba kuna sheria ile ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1992 na Sheria ya Wakfu ya mwaka 2007 ibara ya 16. Mhe. Spika, hata kwa mtu ambaye si mwanasheria akivisoma vipengele hivyo vya sheria atavikuta kwamba sheria hiyo au sheria hizo mbili zinakinzana.

Sasa mimi najiuliza au tujiulize sote sisi sote tuko kwenye gurudumu moja ni sababu gani inayopelekea kwamba tuwe na sheria mbili au taasisi mbili zinazokinzana ambao wote wana lengo moja. Ushauri wangu ni kwamba taasisi hizi zilete sheria au Wizara ya Sheria ikae pamoja na taasisi hizi ili kuzipatia ufumbuzi sheria hizo namba 2 ya mwaka 2007 ya Kamisheni wa Wakfu na Mali ya Amana na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1992, ili kuondoa sintofahamu na mivutano inayojitokeza ya kila wakati kuhusu usimamizi wa sheria hizi. Mfano utakuta katika mambo ya ardhi sheria inampa mamlaka waziri kutoa hati ya umiliki kwa ardhi au njia nyengne ya kuwea kumiliki ardhi ni mirathi au kununua au kupewa hiba.

Lakini ukija kwenye Sheria ya Wakfu ibara ya 16 ya mwaka 2007 sheria namba 2 inasema kwamba:-

" Mali yoyote ambayo ni ya Wakfu iwe ardhi iwe shamba, iwe nyumba mali hiyo iko chini ya Kamisheni ya Wakfu bila ya kujali muda au kitu chochote."

Mhe. Spika, jambo hili linaleta mvutano wa kiutendaji wa usimamizi, kati ya taasisi hizi mbili. Kwa hiyo, naiomba wizara ishughulikie kwa makini suala hili ili kuondoa sitafahamu. Tujue sasa nani ana haki ya kutumia kati ya Wizara ya Ardhi na Kamisheni ya Wakfu kwenye sheria hizi inapotokea mvutano kama huo.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho aniwekee bayana juu ya suala hili. Lakini pia hapo napita tu lakini lengo langu nakuja tena naangalia sasa kwenye madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, tatizo la Madawa ya kulevya limekuwa ni sugu, limekuwa ni donda ndugu katika nchi yetu na sisi kwenye kamati yetu ya wenyeviti tulipendekeza kwamba kamati hii ipewe meno ya kuweza kuwadhibiti waingizaji na wasambazaji wa madawa ya kulevya. Mhe. Spika, wezi wa mali ya umma wanaitwa mafisadi lakini mimi siwaiti mafisadi nawaita wezi wa mali ya umma. Hawa ni wezi wa mali ya umma kwa sababu wanatumia mali ya umma. Lakini mafisadi mie nataka kuitafsiri kidogo kama vile tulivyoelekezwa kwenye Qur-an kwamba *"Mufsiduna fil ardhi"* ni watu wanaofanya uharibifu kwenye nchi.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya waingizaji wasambazaji hawa ni waharibifu kwenye nchi. Kwa hiyo, pamoja na kuwa na sheria ya udhibiti ipo lakini inaonekana kutokusimamiwa kwa sababu sheria pia inawataka kwamba mtu mwenye kujihusisha na madawa ya kulevya anapokamatwa anatakiwa azuiliwe mpaka kesi yake ya msingi itakapomaliza. Lakini je, tujiulize ni wangapi watu waliokamatwa na madawa ya kulevya wanaofanyiwa hivi.

Sasa naishauri wizara itengeneze sheria ya kuwadhibiti watu wa madawa ya kulevya kikamilifu ikiwa pamoja na kuianzisha mahakama ya madawa ya kulevya, tunayo mahakama ya ardhi, tunayo mahakama ya wafanyabiashara, kwa nini tusiwe na mahakama maalum ya watu wanaojihusisha na madawa ya kulevya. (*Makofi*)

Wito wangu kwa serikali ni kwamba tufanye inavyowezekana lakini tuianzishe mahakama hii kwa ajili ya kuiokoa jamii yetu. Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba jamii inapotea sana kwa madawa ya kulevya, tutafika kipindi kizazi kinachokuja kitakuja kutulaumu kwa nini tumeiacha jamii imepotea na kwa kweli tutakuwa tunalaumika. Si dhani kwamba mpaka sasa wako watu waliokwisha kutiwa hatiani wakapata adhabu ya kufungwa kwa kesi za madawa ya kulevya. Kwa sababu kama tulivyosema miongoni mwa wanaojihusisha na madawa ya kulevya wengi wao ni vigogo wa serikali, wafanyabiashara wakubwa na wengine ni viongozi wa dini.

Mhe. Spika, jambo hili halitaki tochi, ni jambo ambalo lipo na ndio maana unakuta mtuhumiwa wa madawa ya kulevya anakamatwa na baada ya muda unamkuta yuko nje anadunda na anaendelea na kazi yake kama kawaida. Mhe. Spika, jambo hili ni chukizo na linatakiwa lipigwe vita kwa nguvu zote ili kuinusuru jamii yetu Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu haki za binaadamu na Utawala Bora. Mimi napenda kuipongeza serikali kwa nia yake nzuri juu ya kuanzisha azma hii ya Utawala Bora. Lakini Mhe. Spika, kila penye zuri hapakosi kasoro, tumeshuhudia mambo mengi yanayotokea hivi karibuni ya uvunjifu wa amani na mambo mengine kwa ajili ya kisingizo cha Utawala Bora.

Mhe. Spika, mimi nasema hakuna uhuru usio mipaka kila uhuru unatakiwa uwe na mpaka. Watu wanaovunja amani kwa kisingizio cha Utawala Bora Mhe. Spika, hapana budi serikali pamoja na kuwa limeshazungumzwa na naamini limeshatekelezwa lakini na mimi natia msisitizo kwamba ni wakati muafaka sasa wa kuliona hilo na kulichukulia hatua zinazofaa ikiwa kwenye mahakama tunatengeneza *certificate of agency* kwa ajili ya dharura ya jambo hili, nia ni nzuri ya serikali ya kuanzisha Utawala Bora. Lakini wenzetu waliokuwa hawaitakii wema nchi hii, wanakitumia kipengele hicho au wanapata chaka la kujificha kuendelea uhalifu wao.

Sambamba na hilo sasa nakuja kwenye ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, katika taarifa yake Mhe. Waziri aliyotuwasilishia kwenye kifungu cha 13 alikiri kwamba kwenye taarifa ya ukaguzi huo kwamba kuna baadhi ya wizara na Taasisi za Serikali hazikuopata hati nzuri. Baada ya ukaguzi ripoti inaonesha kwamba wametoa hati za aina tatu; hati inayoridhisha, hati isiyoridhisha na hati yenye shaka. Hati zenye shaka zimeanishwa kwenye ripoti hiyo na hati zenye kuridhisha.

Sasa mimi nataka waziri atakapokuja hapa aniambie ni hatua gani zimechukuliwa kwa wizara au kwa taasisi ambazo zimepata hati zisizo ridhisha na zile hati zenye shaka. Kwa sababu ukiangalia utakuta kuna matumizi mengi ya fedha za serikali ambayo hayakuiainishwa uhalisia wala hakuna hati zozote zinazoonesha matumizi ya fedha hizo za serikali.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi wakati Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho nitaomba anipe jibu kwamba hatua gani zimechukuliwa kwa zile taasisi au wizara ambazo hazikupata hati zinazoridhisha na zile hati zenye shaka. Kwa sababu nikiangalia kidogo utakuta kama Wizara ya Afya utaikuta kuna shilingi milioni mbili, milioni mia tisa thamanini, laki tatu thalathini na sita ukurasa wa 93 mpaka wa 95, Wizara ya Kilimo nayo mia moja hamsini na sita, mia nne na mbili, utakuta nyingi zipo.

Mhe. Spika, sisi tunapambana kutafuta fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. Tupo hapa kwa ajili ya kung'ang'ana kuiondoa serikali yetu na nchi yetu kutoka kwenye janga la bajeti tegemezi, twende katika bajeti ya kujitegemea. Sasa leo inapotokea kwamba kuna matumizi ya fedha yanakwenda kinyume na taratibu ya sheria ya fedha. Mhe. Spika, jambo hili ni la kusikitisha sana.

Kwa hivyo mimi nitaungana na wenzangu, nitamzuia shilingi kidogo Mhe. Waziri mpaka pale nitakapopata majibu ya kujiridhisha juu ya taasisi ambazo zina mapungufu ya ripoti yake kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Sina nia ya kukomoa wala sina nia ya kufanya kitu kibaya, lakini nia yangu ni kujiridhisha ili tuone kwamba sisi wananchi wametuchagua na tunawatetea. Kwa sababu hizi ni haki zao, ni nguvu zao wavuja jasho.

Kwa hivyo mimi kwanza ninamshukuru sana Waziri kupitia Idara yake hii Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuliona hili na kuliweka wazi. Waziri, ahsante sana na taasisi yako ninaipongeza sana. Lakini mimi pamoja na kuipongeza nitataka majibu na nione na utekelezaji na hatua zinazochukuliwa kwa watu waliopewa hati zenye shaka Mhe. Spika, ili haki itendeke ni lazima tulione hili linafanyika kwa uwazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu ajira kimekuwa ni kilio kwa vijana wetu.Vijana wanamaliza kusoma, wanamaliza vyuo lakini leo vijana wale wakimaliza wanaondoka vyuoni wanakwenda vijiweni. Matokeo yake ni nini. Athari yake vijana wale ndiyo wanaoingiza kwenye biashara haramu kama hizo tunazozipiga vita ya madawa ya kulevya na mambo mengine. Lakini tukitazama asili ni nini. Asili ni kwamba wao hawana kazi, mtu anafikiria nini

la kufanya baada ya kupoteza nusu ya umri wake kwenda kusoma, baadae Chuo Kikuu na College. *(Makofi)*

Sasa mimi ninaiomba wizara ichukue mkakati mahususi. Idara hii kwa kutumia wataalamu wake iliyonayo ione kwamba jambo hili ni la dharura. Na kwamba zile kazi ndogo ndogo zote za ndani zinazotokea hata za muda zilizokuwa zinaweza kufanywa na vijana wetu wa Kizanzibari wasipewe wageni.

Mhe. Spika: Mhe. Omar Seif Abeid una dakika moja.

Mhe. Omar Seif Abeid: Naam!

Mhe. Spika: Umebakiwa na dakika moja.

Mhe. Omar Seif Abeid: ...wasipewe wageni, wapewe wazawa. Kwa nini tufanye hivi. Leo ukenda mahotelini na ukenda sehemu nyengine utawakuta watu kutoka Kenya, Uganda na kwengine wanazichukua nafasi ambazo na vijana wetu tunao. Matokeo yake vijana wetu wanaanza upinzani, wanaiona serikali yao kama haiwatendei haki.

Kwa hivyo sisi hapa kama Wawakilishi wao waliotuchagua kimoja kilio chao ni hiki. Kwa hivyo Mhe. Spika, sitaki niende kinyume. Hivyo naunga mkono hoja hii kwa asilimia tisini na tano, tano ninaiweka mkononi mpaka nitakapopata majibu na maelezo mazuri kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid na kuhusu utaratibu Mhe. Suleiman Sarahan Said.

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, ninashukuru sana kwa kuniona. Mhe. Spika, ninatumia Kanuni ya 60(1):-

(a) Isipokuwa tu kwa idhini ya Spika Mjumbe yeyote hatoruhusiwa kusema zaidi ya mara moja juu ya hoja ila tu kama wakati huo Baraza lipo katika Kamati.
(b) Kama anatumia haki yake ya kujibu.

(c) Kama anatoa maelezo zaidi juu ya sehemu muhimu ya hotuba yake ambayo imeeleweka vibaya wakati wa maelezo hayo aliyoongeza kitu kipya.
(d) Kama unasema kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako. Kwanza jana nilisema kitu kimoja ambacho nina wasi wasi watu wengine walifahamu vizuri na wengine hawakufahamu vizuri. Baada ya kutoka hapa watu wengi walinipigia simu jana wakasema na wao nimewaona katika muongozo wa madereva na wale wapiga chapa, kwamba kitu kimoja sikuongeza kwamba kwa nini sikuwaombea mishahara mingi na kazi walizonazo. Lakini walifurahia sana kwa sababu nilivyoisema nilichokusudia nilizungumza wale ni watu hatari na wale ni watu muhimu. Tunahitaji sisi watu wale kuwa nao karibu na kuwa na watu wale tuwatizame kwa jicho la huruma sana. Wale watu ni watu muhimu sana. Nikasema tusiwafanye tu *simple simple* kwa kuwa ni mpiga chapa au ni dereva tu wakati anaendesha gari. Ni watu muhimu sana.

Kwa hivyo nieleweke kwamba wale walionipigia simu wakanifurahisha wakasema umetuona kumbe sisi ni watu muhimu, lakini kwa nini hukumwambia Waziri akatuongeza na mishahara. Kwa hivyo hilo lilikuwa ninalisemea na wale walioni-*quote* vibaya basi ninawaomba samahani kama hawakunifahamu malengo yangu. Ni watu wazuri sana, ni watu muhimu sana, ni neno nililokusudia, siyo watu wa kudharau. Mhe. Spika, la kwanza lilikuwa ni hilo.

La pili Mhe. Spika, niseme kwamba jana usiku baada ya kutoka hapa waliofika kwenye TV ya *Star TV* ambayo iliunga kipindi cha Dira ya Dunia. Mhe. Spika, kulikuwa na mdahalo wakimjadili Dkt. Ali Mohamed Shein hali halisi alivyoweza kuwahurumia wazee wale ambao anawalipa shilingi elfu ishirini ishirini. Kitu kile kwa dunia hakijafanyika. Walimsifia sana na waliibadilisha ikawekwa Dola tisa, wakaweka elfu ishirini lakini wakasema kwamba ina gharama karibuni bilioni kumi na nne ambazo Dkt. Shein anatumia kwa hali hiyo. Kwa kweli ni jambo la mfano kwa Marais na wanalisemea kuwa Marais wengine wachukue mfano kama ule. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa nimekuelewa na hasa hii kwamba unatoa maelezo zaidi juu ya sehemu muhimu ya hotuba yako ambayo imeeleweka vibaya. Ninafikiri nimepokea muongozo wake. Ahsante sana.

Tunaendelea mheshimiwa. Sasa ninaomba nimwite Mhe. Hamad Abdalla Rashid atafutiwa na Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ajiandae.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniona na kunipa ruhusa hii ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwanza mimi nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kukaa pamoja na kutunga kitabu hiki ambacho kwa kweli niwape hongera kwanza kwa kukipanga vizuri. Upangaji huu mzuri wa kitabu hiki unaonekana kabisa ni ukomavu wa Mhe. Waziri na umri wake. Pia napenda kumpongeza Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kumuweka kwenye wizara hii ambayo aliona kabisa kwamba ni mtu atakaekuwa wa busara, atakayeweza kuiendesha hii wizara kwa umakini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nije kwenye Tume ya Utumishi Serikalini. Tume hii Mhe. Rais aliiunda makusudi au mahususi kwa kuweza kutoa hizi huduma za utumishi na kusimamia ajira. Ninataka nimwambie Mhe. Spika, Mhe. Waziri muda wote ambao atakuwa na Tume hii. Hii Tume kule Pemba sisi inatupa matatizo.

Kwa sababu usimamizi ninaamini kwamba siyo mzuri na ninatoa mifano makusudi ili Mhe. Waziri aweze kufuatilia kwa karibu. Panapotokezea nafasi za ajira kule Pemba hususan sehemu ya usaili, ni vizuri unatangazwa usaili kwamba utafanyika tarehe fulani. Lakini jambo la ajabu wale watahiniwa wakitoka kule kufanya usaili wao, wanaambiwa wakatazame majibu. Mimi sijui unasahihishwa saa ngapi usaili. Yaani siku ile ile hawajafika hata majumbani mwao, wanaambiwa wakatazame majibu yameshapachikwa. Kwa kweli hii inatupa usumbufu mkubwa na ulalamishi, kwa sababu wananchi waliofanya usaili wanalalamika sana. Ni jambo la ajabu. Si kweli kwamba siku ile ile, wakati ule ule, wameweza kusahihisha usaili na wakapata majibu ya nani wanaofaa kuajiriwa.

Ni uonevu. Mfano hai nitatoa katika ile Tume ya Rushwa. Ilifanya usaili lakini amini Mhe. Spika, ule usaili wengine hawajamaliza mule kwenye chumba, majibu yameshapachikwa kwamba aliyefaulu ni huyu na huyu. Baya zaidi wote waliokuja kufanya usaili kutoka Unguja, yaani pale pa usaili waliuliza jamani wapi Chuo cha Amani tukafanye usaili, wanaoneshwa wanakwenda kufanya ule usaili. Lakini hawajatoka kule, kule majibu yameshapachikwa. Matokeo

yake usaili ule walifaulu wale vijana wa Unguja tu na Wapemba akafaulu mmoja. Ni jambo la kusikitisha. (*Makofi*)

Serikali inafanya kwa makini kabisa kujua hasa kwamba tunatoa nafasi kumi Pemba, nafasi kumi Unguja, nafasi mbili Wilaya ya Mkoani, nafasi mbili Wilaya ya Chake Chake, nafasi mbili ya Wilaya ya Magharibi. Kwa nini ile Wilaya husika zile nafasi zake isizipate. Huu ni uonevu ambao sisi kama Wawakilishi... Ninamthibitishia Mhe. Waziri kuwa tutakuwa pamoja naye kulisimamia hili, baada ya hilo lililokwishakutokea lisitokee tena. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kuendelea ninasogea sehemu ya Mahakama. Mimi kwanza niwapongeze Majaji wote wanaongoza kesi. Majaji wetu wanafanya kazi nzuri, wanaendesha kesi vizuri, ikabakia yale matatizo madogo madogo ambayo wenzangu sitaki niyataje wameshasema hapa, kwamba inashindikana kesi labda kwenda kwa wakati kwa sababu Majaji pengine wanashindwa kupelekwa kwa wakati sehemu yake ya kazi, malipo madogo n.k. Lakini haya yote isiwe sababu ya kuiangusha hii Wizara. Ninamuomba Mhe. Waziri ahakikishe analisimamia hili, Majaji wetu wanapelekwa maofisini kwa wakati. Yale magari ambayo Mhe.Naibu Waziri aliahidi hapa yatashulikiwa, yashughulikiwe kwa wakati haraka sana ili Majaji hawa waweze kufanya kazi na waweze kuhukumu kesi kwa wakati.

Mhe. Spika, niende katika sehemu mahususi sasa. Serikali hii au nchi yetu hii ya Zanzibar, roho kabisa ya serikali ni wizara mbili mimi naona; Wizara ya Afya ambayo inasimamia afya za wananchi wetu na Wizara ya Elimu. Kwa kweli wizara hizi tukiziachia tu tukaenda songombingo, tutachukua dhima kubwa kwa Mwenyezi Mungu na kwa wananchi wetu wa Unguja na Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wizara hizi namuomba Mhe. Waziri asimamie kwa kina kabisa na kinachoonekana hasa maadili ya uongozi na usimamizi wa kazi serikalini umeondoka katika nchi hii. Na umeondoka kwa sababu nina hakika labda ufuatiliaji ni mdogo au kuna usimamizi wa kulindana au kuogopana. Mimi ninafikiri mfanyakazi wa serikali ambaye hataki kufanya kazi zake vizuri, haendi kazini kwa wakati, huyu anastahiki kuchukuliwa hatua. (*Makofi*)

Ni jambo la ajabu Mhe. Spika, na mimi nitatoa mfano tena Waziri wa Afya kama yupo atanisikia hapa. Mimi ninakaa Vitongoji, tena ndani ya *campus* ile *Cottage Hospital* ya Vitongoji. Jambo zuri zaidi mimi nilikuwa mfanyakazi wa Wizara ya Afya. Hawawezi kunidanganya. Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza hapa swali la kipindupindu kwa nini kinaenea mpaka vijijini. Mimi kwanza

nataka nimthibitishie Mhe. Spika, na Mhe. Jaku asikie kabisa. Kipindupindu bwana tusidanganyane hakiwezi kuja bila ya muathirika kula kinyesi cha binadamu ambacho kina maambukizo. Siyo kinyesi cha mtoto kwenye *pampers*, hapana *pampers* haiwezi kuleta kipindupindu. Kinyesi ambacho kimeambukizwa na maradhi yale ya kipindupindu, kuna mdudu anaitwa *Vibrio Cholerae*. Huyo ukimla ndiyo tayari kipindupindu. (*Makofi*)

Sasa kipindupindu tunaelezana kila mwaka Zanzibar kinatokea. Mimi ninasema kwamba kipindupindu kinatokea na wala hakishi kwa sababu moja kubwa. Pale Vitongoji nilikwenda kwenye kambi ya kipindupindu, yaani mwananchi wa kawaida ndiyo anasaidia mgonjwa wake. Kitu ambacho hairuhusiwi, haiwezekani na hiyo inaitwa ni kambi na ina karantini. Na kwa kweli inatakiwa ifungwe mpaka kamba kwamba wananchi wa kawaida hawaruhusiwi kwenda kule kwenye wagonjwa. Leo inakujaje mtu ambaye anakaa na mgonjwa anaruhusiwa kukaa mule kambini, anaambiwa akaoshe zile nguo. Halafu tuseme kipindupindu kiondoke, kiende wapi.

Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi Hospitali ya Vitongoji kuna televisheni pale. Wizara na serikali imezipeleka televisheni zile kwa uhalali kabisa kuweza kutoa huduma ya afya katika zile sehemu za hospitali. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Afya au Naibu Waziri kama ananisikia asikilize neno hilo. Pale madaktari na wauguzi na ma-*orderlies* wamefungua TV wamechukua kanda, kuna kipindi cha karibuni kimepita cha Mhe. Mufti na Masheikh ambacho wanainyanyasa serikali ya nchi hii wale Masheikh. Wauguzi na ma-*orderlies* wanaacha wagonjwa wa kipindupindu, wagonjwa ambao wanahitaji msaada wao, wanahitaji huduma yao, wanahitaji *close observation* kutoka kwao waliosoma; bahati mbaya wanaangalia ile *CD* tena wanashangilia. Wagonjwa maskini za Mungu kule wanateseka. Wanatapika, wanahatarisha na wengine kupoteza maisha. Ni jambo la kusikitisha. (*Makofi*)

Na ninamuomba hasa yule daktari dhamana wa Vitongoji ile TV aikomelee ndani kama haina kazi ya kutoa huduma ya afya pale. Tunahitaji wananchi wetu washughulikiwe, wapewe huduma na watendaji ambao wameajiriwa na serikali hii. Lakini mtendaji ambaye serikali hii hawezi kufanya kazi na hawezi kufanya kazi chini ya ilani ya Chama cha Mapinduzi, hilo ni jipu aondolewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu. Wizara hii kuna walimu mimi ninataka nikwambie Mhe. Spika, wiki nzima madarasani hawapiti wala hawatoi elimu kwa wanafunzi. Inakujaje mtumishi huyo ambaye ana kiongozi pale anasimamiwa. Ndiyo nikasema yale maadili ya uongozi hayapo na

hayasimamiwi, sheria za kazi hazisimamiwi. Matokeo yake watendaji wetu wanafanya wanavyotaka, wanangoja tarehe ishirini wanaulizana vipi haujatoka mshahara huko. Utoke wapi na tena wana matusi. Na wanasema hasa kama serikali wanaikashifu, haina pesa, haina kitu lakini mwisho mwezi wakichukua pesa, kwa nini wasifanye zile kazi ambazo wamechukulia pesa pale. *(Makofi)*

Tukikosa huduma hizi Mhe. Spika, Mhe. Waziri tunawapeleka wananchi wetu kwenye matatizo makubwa. Tutawakosesha wanafunzi wetu elimu ya kutosha. Lakini naomba yale maadili ya kazi, sheria za kazi zisimamiwe ipasavyo ili mfanyakazi ambaye hastahiki kufanya kazi, asistahiki kulipwa mshahara na serikali hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninakwenda sehemu ya Usajili sasa, maana yake kuna usaili na usajili. Kuna wananchi wetu wanahitaji kusajiliwa vikundi, lakini ninarudi pale pale, wanapodai kusajiliwa katika vile vikundi mtendaji mkuu pale ni jipu hilo hilo ambalo halisimamii ilani ya Chama cha Mapinduzi, hataki. Hawapitishii, hawasajili anawapotezea muda, anawazungusha. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hayo ni mambo ya kusimamiwa ambayo naamini kama hayatekelezwi. Ninarudia tena naamini kama hayatotekelezwa, sikatai wananchi wote ni Wazanzibari, watu wa Pemba, watu wa Unguja ni Wazanzibari. Lakini serikali mbona imefanya uwiano mzuri tu na imetamka kwamba tunatoa nafasi hamsini za ajira kutoka serikali hii, kutoka ishirini na tano ziende Pemba na ishirini na tano ziende Unguja. Kwa nini zile za Pemba zimezwe tena na huku huku Unguja. *(Makofi)*

Watendaji wakuu kila mtu anakwenda na mtu wake kibindoni, nikisema kibindo nafikiri Mhe. Spika, unakijua. Anakwenda naye pale anasema hakikisha huyu unamchukua. Si hawa wameshafanya usaili kule kwao, kwa nini unampeleka tena na kule. Mjini/Magharibi wameshafanya *process* zao kumi wameshachukua. Unawatoa tena watu Mjini/Magharibi keshokutwa usaili wa Pemba unawapeleka Pemba na unatoa amri kwamba hawa lazima wapitishwe. Wale wa Pemba unawakusudia nini? Munatupa kazi ya kujibu maswali mengi ambayo kwa kweli si ya msingi. Haki ingetendeka basi uajiri ungekwenda vizuri. Vijana wetu wasingetulalamikia sana, tungemaliza kazi mara moja.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri la mwisho kabisa. Mimi naomba zile taasisi husika basi ndiyo zisimamie yale mamlaka. Mimi kama Mkuu wa Mkoa kuna ajira pale, niiachie taasisi husika isimamie utaratibu ule mpaka umalizike. Nisiende kutia mkono wangu kwamba lazima mimi vijana wangu hawa watatu

uwachukue. Hiyo siyo haki wala uongozi bora. Kwa sababu unatumia haki ya kuchukua unayemtaka yeye yule mwengine akose.

Mwisho naomba sisi viongizi hasa wa Chama cha Mapinduzi chama - tawala tuwache kutoa ripoti ambazo sio za kweli, na kwa sababu Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa ananisikia mimi nataka niseme kuna malalamiko mkubwa kuhusu Wizara ya Afya ambayo imeajiri watu wameambiwa wote ni kutoka upinzani, natamka bayana Mhe. Makamu wa Rais unanisikia na kwa sababu kuna chombo kile cha Serikali cha kurusha matangazo kinasikika, nasema kwamba si kweli kwamba wale walioajiriwa Wizara ya Afya wote ni *CUF*, katika wote walioajiriwa wale *CUF* ni wanne tu naomba wale vijana warudishwe kazini tena hata kwa majina nawafahamu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu hiki ni chombo cha kutunga sheria, chombo ambacho kinaongoza mambo ya kusimamia wananchi naomba nimpongeze Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na watendaji wake, nasema kwamba naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia ipite haraka twende tukatekeleze majukumu kwa wananchi wetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Kabla sijaanza kutoa michango yangu nakuomba sana tutumie kanuni ya 8(6) kwamba kama muda wangu utamalizika basi naomba zile dakika zako japo tano, ili niweze kumalizia yale ambayo nimekusudia kuyazungumza katika hotuba hii ninayochangia.

Pili Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba hii, lakini vile vile nimpongeze Naibu Waziri swahibu yangu, jirani yangu Mhe. Khamis pamoja na watendaji wa Wizara hii jinsi wanavyochapa kazi vizuri na kwa umahiri.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu leo nitaanzia kwenye dini; nianze kwenye ukurasa wa 18 kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, kwa mujibu wa kitabu hiki Mhe. Waziri ameeleza kwamba takriban kuna mizozo ya mirathi 35, sita imekamilika lakini 29 inaendelea kushughulikiwa. Hapa nilikuwa nataka Mhe. Waziri anipe darsa kidogo juu ya chanzo na kiini cha mizozo ya mirathi katika jamii yetu tukizingatia asilimia kubwa ni waislam. Sasa nini kinachosababisha mizozo hii ya mirathi na hatua ambazo Wizara inachukua kuweza kukabiliana na mizozo yetu.

Pia katika kipindi cha karibuni katika jamii yetu kumezuka talaka nyingi sana, sasa tuwaombe Wizara kupitia hii Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana wamegundua nini katika jamii yetu hata ikapelekea ongezeko la talaka, na wanaishauri nini jamii yetu ya kiislam kuhusiana na suala hili.

Vile vile nije kwenye suala la misikiti ukurasa wa 35, katika kitabu hiki imeelezwa kwamba kwa mwaka 2016/2017 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inakusudia kusajili misikiti 95 na madrasa 195. Hapa ilikuwa nataka nijue tu Mhe. Waziri, kuanzia huko nyuma mpaka sasa labda Kamisheni ya Wakfu imesajili misikiti mingapi na madrasa magapi. Lakini vile vile kuna mizozo katika misikiti na ile vile vile wamechukua hatua gani.

Mhe. Spika, nizungumzie kidogo suala la Katiba pendekezwa, tumeona kwamba Katiba pendekezwa imepitia katika hatua mbali mbali na hivi sasa ipo katika *final stage* ambayo inasubiriwa kupigiwa kura za maoni. Sasa nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri atakapokuja basi atueleze wamekutana na wameshafanya mazungumzo na Wizara ya Katiba na Sheria ya Serikali ya Muungano wa Tanzania ili kujua hatma ya katiba ile pendekezwa, basi atueleze atakapokuja kufanya majumuisho.

Mhe. Spika, niingie kwenye ukurasa wa 22 ambao unazungumzia Mahakama katika *paragraph* ya 79 na 78 utaona kuwa kuna mrundikano wa mashauri ya kesi, katika Mahakama kuu, kuna 355 yale ya awali na mapya lakini Mahakama ya wilaya kuna 4,616 na Mahakama za mwanzo takriban ni 9000 mashauri hayo. Kwa hivyo kila ukishuka chini kazi za Mahakama mashauri ya kesi yanakuwa mengi. Kwa hivyo tumuombe tu Mhe. Waziri sababu hasa ya kurundikana kwa mashauri haya na hatua gani zimechekuliwa za kuzipeleka hizi kesi ili zipate kutatuliwa kwa wakati. Lakini vile vile kuna changamoto katika Mahakama kuhusiana na utoaji wa ushahidi na mashahidi kwa kawaida wanakuwa wanalipwa. Sasa Wizara imejipanga vipi kuwalipa mashahidi wa kesi nauli zao kwa wakati ili kuzipelekea zile kesi ziende kama zilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 26 kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, nimpongeze tu *CAG* kwa kufanya kazi vizuri na tayari tumepokea ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2013/2014, lakini pia tumeambiwa kwamba ripoti za mwaka 2014/2015 za Ukaguzi nazo zimekamilika. Lakini hapa Mhe. Spika, nilitaka kujua tu nini kinafuata baada ya ripoti zile kutoka. Tumepokea kama ripoti nne, sasa nini kinafuatia baada ya pale kwa hivyo tunaziwacha hivi hivi au kuna hatua Serikali ambayo inachukua kwa sababu ukiangalia ripoti moja katika zile ripoti nne, ile ripoti ya ukaguzi yakinifu

Value For Money Auditing ambayo ukiangalia kwenye kile kitabu ukurasa 9 *Paragraph* ya 8.4 kuhusiana na viwango vya barabara kuna barabara mbili za Selemu na *Kilwa Road* hazikufikia kiwango kile ambacho kinachotakiwa na sijui kama huyo mkandarasi kama yupo aliyetengeneza barabara hiyo. Sasa utakuta ripoti zimeeleza hali halisi na kama alivyosema Mhe. Omar Yussuf Abeid ile ripoti ya hisabu za Serikali kuna wengine wamepata hati chafu, sasa tunataka tujue baada ya ripoti hizi kutoka nini kinafuata, zinabaki kwenye vitabu au kuna hatua ambazo zimechukuliwa.

Mhe. Spika, waswahili wanasema sheria ni msumeno, kwa kuwa mkaguzi *CAG* anafanya ukaguzi katika taasisi mbali mbali za Serikali ya SMZ lakini na yeye ofisi yake vile vile inakaguliwa na ripoti yake inatakiwa iwasilishwe katika Baraza hili la Wawakilishi, lakini tulipopokea zile ripoti sikuona ripoti ya *CAG* na hii imo katika hii sheria ya *Public Finance Act* Ibara ya 36 kifungu 4 inataka Waziri husika aiwasilishe barazani ripoti ya ukaguzi ya Ofisi ya *CAG*. Sasa nataka Mhe. Waziri atakapokuja basi anieleze ni lini ripoti hii itawasilishwa ili na sisi tuone ufanisi na utekelezaji wa Mkaguzi wetu wa hisabu, nafikiri mwenyewe yupo anasikia pale kwa hivyo Mhe. Waziri akija tunataka tulijue hilo.

Mhe. Spika, nije kwenye fungu katika kitabu kikubwa hiki Fungu G04 *page* ya G54 kuna changamoto ya tatu, ni kukosekana mtambo maalum wa kupimia vinasaba vya *DNA*, ipo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka. Moja katika changamoto ya Mkurugenzi wa Mashitaka anasema ni ukosefu wa *DNA* mashine. Sasa hapa mimi nilikuwa niiombe Serikali ilichukue suala hili kama ni dharura, kama ilivyofanya kwenye suala la Meli ya Mapinduzi II, basi lichukuliwe kama dharura kwa sababu mbele hapa Mkurugenzi wa Mashitaka anakiri kwamba kesi nyingi za udhalilishaji na mauaji zinakosa ushahidi mzuri wa kuthibitisha kwa kukosekana chombo hiki. Kwa hivyo tunaomba Serikali ilichukue hili kama ni suala la dharura, ili basi katika bajeti ya mwaka 2016/2017 chombo hiki kiweze kupatikana.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 37 kuhusiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nimpongeze *CAG* kwa kazi zake nzuri na Ofisi hii ni muhimu sana kwa sababu inatoa ushauri wa kisheria wa Taasisi za Serikali, sasa nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri je, ni taasisi ngapi za Serikali mpaka sasa hazina wanasheria tueleze kwa sababu taasisi nyengine wanao wanasheria lakini kuna nyengine hamna, kwa hivyo ni taasisi ngapi hawana.

Vile vile tunataka tujue kwamba Ofisi yake hii inafanya tathmini na ufuatiliaji wa wale wanasheria kwa sababu tumegundua kwamba taasisi zetu kipindi hiki

zinaburuzwa zinapelekwa Mahakamani na hao wanasheria wamewekwa kwa ajili ya kuzuia hali ile isitokezee, nashauri Wizara au taasisi hali ile isitokezee. Sasa tunataka tujue katika kipindi cha 2015/2016 ni taasisi ngapi za Serikali zimepelekwa Mahakamani, na katika kesi hizo zilizopelekwa Mahakamani ni kesi ngapi Serikali imeshinda na kesi ngapi Serikali haikushinda na tumepata hasara kiasi gani, kwa hivyo Mhe. Waziri akija naomba aje anipe ufafanuzi.

Jengine hili nilikuwa nataka kutoa ushauri kwa Ofisi ya Mwansheria Mkuu, kama tunavyojua kwamba Ofisi ya *CAG* wanafanya ukaguzi na wanapata ile ada ya ukaguzi yaani *Auditor fee*, lakini ukija kwa watu wa upimaji nao wana ada ile kwa taasisi zile zile za Serikali ambazo wanazifanyia kazi kuna ada ya upimaji taasisi zinalipa. Sasa ilikuwa niombe au nitoe ushauri kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwamba Taasisi za Serikali zinapopelekwa Mahakani au zinaposhitakiwa, yeye ndio anazisimamia kesi pale Mahakamani sasa ningeomba basi azitoze ada zile taasisi, ili iwe chanzo kikuu katika taasisi yake na hii itakuwa tumeongezea mapato Serikali. Kwa hivyo huo ni ushauri kama utaona unafaa sawa, lakini kama utaona haufai anawea akaniachia mwenyewe.

Mhe. Spika, kwa vile muda si rafiki sana nimalizie kuhusiana na asasi za kiraia pamoja na jumuiya. Zanzibar sasa hivi tuna asasi nyingi za kiraia pamoja na jumuiya mbali mbali zimeundwa na baadhi ya asasi hizo nyengine hata ofisi hazina ofisi zao ziko kwenye *briefcase*, lakini vile vile baadhi ya asasi zinakwenda kinyume na yale matakwa ya sheria yalivyo, tuseme taasisi au hizi jumuiya zimeanzishwa kwa ajili ya jambo fulani lakini badala yake wao wanafanya jambo jengine kinyume na lile ambalo wamedhamiria. Sasa nataka nielewe tu Serikali inachukua hatua gani kwa asasi hizi au jumuiya hizi maana yake jumuiya ziko nyingi na nyengine zimeleta athari hapa. Ukiangalia ukenda *deep* sana utakuta kwamba lile lengo lao walilolikusudia silo ambalo wanalifanyia kazi na Serikali ipo kimya….

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Haya nashukuru, kwa hivyo nilitaka nijue Serikali inachukua hatua gani kwa jumuiya na hizi asasi za kiraia ambazo hazifuati sheria iliyopo, kwa vile muda sina baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono hoja kwa asilimia tisini, asilimia kumi baada ya kupata maelezo kwa kina. Ahsante sana. *(Makofi*)

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hotuba hii nzuri sana ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na zote ziliopo. Kwa kweli hii ni Wizara kubwa

sana wizara ambayo karibu kila Wizara inaigusa, ni Wizara ya mfano kama vile Wizara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais , Wizara ya Fedha na nyengine.

Mimi leo Mhe. Spika, nitazungumzia mambo ya bajeti kwa sababu mengi yameshazungumzwa, nitazungumzia mambo yanayohusiana na bajeti tuliyonayo ambayo ndio imepata hiki kitabu cha bajeti kwamba ni ile bajeti ambayo *PBB* yaani *Program Base Budget* kwa maana nyengine *Program Base Budget* ni bajeti ambayo ni shirikishi, kwa hivyo inashirikisha *Sector Holders* wote na kushirikisha *Sector Holders* wote si lazima kwamba uende ukawashirikishe wote mfanye bajeti pamoja itakuwa ni watu wengi sana. Kushirikisha watu kwa njia ya kutafuta maelezo kufanya *Criminal Assessment* au kwa njia ya kufanya *Appraisals* mbali mbali au kwa njia ya kufanya utafiti kamili.

Katika kuiangalia hii bajeti nimeona pamoja na madhumuni yake ya kuwa shirikishi hii bajeti kidogo, inawezekana ikawa haikushirikisha zile *Sector Holders* au watu wote ipasavyo. Mhe. Spika, lengo kuu la bajeti hasa hii *PBB* ni kuwezesha shughuli za maendeleo ziendelee kwa ufanisi. Lakini pamoja na dhamira hii nzuri kabisa baadhi ya shughuli zilizokusudiwa haziwagusi walengwa, hivyo kusababisha wasipate maendeleo yanayokusudiwa hali ambayo inachangiwa sana na mambo mengi yakiwemo ya kisiasa, kiuchumi, kimiundo mbinu na hata kijamii.

Mhe. Spika, nitatoa mfano wa matatizo ya kutokutumia *Program Based Budget* yaliyotokezea katika Mji wa Ho Hi Min Hage katika mji wa Henchman miaka kama ya 1980 mpaka 1990 kulikuwa na matatizo makubwa kwamba familia masikini zilikuwa hazipati huduma zinazotakiwa. Magonjwa yalikuwa mengi na vifo vilikuwa vingi, hata makaazi yao wanasema kwamba asilimia 100 ya makaazi katika ule Mji wa *Ho Chi Minh* ilikuwa ni majumba ambayo hayastahiki kukaa binadamu. Asilimia 70 walikuwa hawana elimu hata ile ya msingi.

Asilimia 100 tena nyengine walikuwa hawashiriki kwenye shughuli za maendeleo, hivyo kukawa na vifo vingi mpaka Umoja wa Mataifa ikaingilia kati ikaenda ikafanya *study* katika maeneo hayo na ikagundua kwamba hawashirikishwi katika bajeti. Ukafanywa mpango maalum, ukashirikishwa katika bajeti matokeo yake tatizo hilo sasa hivi kule *Ho Chi Minh* hakuna na ni moja katika nchi zinazoendelea sana duniani.

Mhe. Spika, nikienda moja kwa moja kwenye hii Ofisi ya Hati Miliki, hapa kuna takwimu zimeelezwa, takwimu hizi zimetaja vikundi mbali mbali, vikundi

vya taarabu, vikundi vya *Zenji Flavour*, kaswida, injili, filamu na kadhalika. Sasa idadi iliyoorodheshwa hapa, ukitizama na watu walioko majimboni wanaohitaji kusajiliwa hailingani. Nikitoa mfano kwenye Jimbo langu tu la Mtopepo. Kuna miradi ambayo ni zaidi ya hii iliyoainishwa. Miradi mitano iliyosajiliwa mwaka mzima wakati kuna miradi mingi. Siku hizi watu wamehamasika na wana miradi mingi wanayoifanya. Sasa nashangaa kwamba ni miradi mitano tu iliyosajiliwa kwenye Hati Miliki na wakati kuna miradi mingi ambayo haikusajiliwa. Sasa labda tungeelezwa ni utaratibu gani unaofuatwa katika kusajili hivi vikundi.

Mhe. Spika, halafu pia nijuwe hivi vikundi vilivyo orodheshwa kuna vingine vimewekewa zero, kuna vingine viko vitatu. Sasa ni kwamba hivi ndivo vikundi vinavyotarajiwa kusajiliwa au viko vingine zaidi. Kwa maana kwamba kama kuna orodha ya vikundi hivi ndio vitakavyosajiliwa basi ndio hivyo vitawekwa zero, lakini kama kuna vikundi vitakavyokuja vyovyote kinakuwa hakiingizwi tu katika vile vilivyosajiliwa badala ya kuwekwa hapa vikapewa.

Mhe. Spika, nasema kwa kweli kuna vikundi vingi sana ambavyo vinahitaji kusajiliwa. Kwa mfano, nikichukua hapa mwaka huu wamesajili vikundi 120, halafu kwenye malengo yao ya mwakani wanataka kusajili vikundi 1,576 nafikiri iko hapa. Sasa ninachotaka kuuliza mwaka mzima huu wa 2015/2016 wamesajili vikundi 200, sasa hii 1,576 wameipataje hii, imepatikana vipi na kwa vigezo gani ambavyo wamevifanya watoke 120 hadi kufikia 1,576. Nasema hivi kama kuna utaratibu huu utakwenda bila ya kufanya bajeti shirikishi inawezekana wakaanguka na pale pale 120, kwa sababu hawajawashirikisha wale wahusika kwa kufanya *study* na mambo mengine, wakaweza kuingia na wao wakahamasika kuja kujisajili.

Mhe. Spika, nikiingia kwenye ukurasa wa 8 wa bajeti, kidogo nimepata mshtuko, fedha zilizokubaliwa nadhani zilizoidhinishwa ni milioni 18,662,000/- kati ya hizo 11,000,000/- ni mishahara, lakini kinachonishangaza ni kwamba milioni 9 tu ndizo zilizopatikana kwa mishahara. Sasa hii bajeti imefanywa vipi mpaka ziidhinishwe kwa mujibu wa idadi ya mahitaji milioni 18,000,000/- zikaidhinishwa, zikaja zikatumika milioni 9 tu, kwa nini walipungua watu au walifanya nini, hapa kidogo nataka nipate maelezo.

Jengine Mhe.Spika, ni ajira. Mhe. Waziri kuna tatizo kubwa sana la ajira, na tatizo la ajira sio hapa Zanzibar tu, bali ni dunia nzima. Katika majimbo yetu huko kuna vijana wengi hawana ajira. Sasa mimi napendekeza kwamba tuanzishe utaratibu wa kuwa na *National Insurance Number*, ambayo itawawezesha Wazanzibari kupata ajira, hii itapunguza ile kuajiri wageni. Kwa

sababu ukienda unaonesha *International Insurance Number* ya Zanzibar unayo unapata ajira. Najua zinatumika ID za Zanzibar, lakini bora iwepo *International Insurance Number*. Hapo hapo nadhani kuna umuhimu wa kuwa na *job centres*, najua kuweka *job centres* ni gharama sana, lakini pia itapunguza makali ya ajira, kwa sababu ukifungua *job centres* zikiwa chini ya usimamizi wa wizara husika, pale ilipo *job centres* patakuwa na ajira za watu na halafu tena wananchi watapata pahala pa kwenda kutafuta kazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo napenda niishauri sana serikali, nadhani wakati umefika sasa, tumewasaidia wazee wapate shilingi 20,000/- kwa mwezi Alhamdulillah, hiyo ni ajira moja niseme itasaidia kuendesha maisha yao. Pia nadhani iko haja kwa vijana wenye umri unaopindukia miaka 18 kupatiwa msaada wa kimaisha. Kwa sababu vijana ambao hawana kazi wako mitaani hawana la kufanya, wameshavunjika moyo na wameshakata tamaa hata ya maisha, na ukikata tamaa ya maisha huko mbeleni nadhani utakuwa huna tamaa hata ya kufanya lolote, matokeo yake utaangukia umaskini mpaka unakufa. Kwa hivyo, naomba sana hawa vijana wanaopindukia miaka 18, uwepo utaratibu na wao wa kuwasaidia chochote hadi hapo watakapopata ajira. Haya hayatokuwa yanafanyika hapa Zanzibar tu, dunia nzima mambo haya yanafanyika ya kuwasaidia vijana ambao hawana kazi ili waendeleze maisha yao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nataka nisipindukie wakati niliopewa. Napenda niipongeze sana hii bajeti ambayo imeandaliwa vizuri sana na imewasilishwa vizuri sana, na kwa kuzingatia kwamba hakuna zuri lisilokuwa na kasoro hata ndogo, ndio maana tumeona tutowe hayo na wenzangu wamechangia hayo. Nitawashauri sana wajumbe wenzangu tuiunge mkono hii hotuba ili waende wakayatekeleze haya waliyoyaomba.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Dk. Makame Ali Ussi, naomba naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa, atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajiandae.

Mhe. Mohammed Said Mohammed(Dimwa): Mhe. Spika, nikushukuru sana nikushukuru sana kwa imani yako ya kunipa nafasi muda huu. Mhe. Spika, kwanza kabisa nimsifu Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini nikiri na ni-*declare interest* zangu kuwa Mhe. Waziri ni mwalimu wangu na nitachangia kadiri ya uwezo wangu na kwa sababu leo nataka niseme maneno mazito sana.

Mhe. Spika, kama kanuni ingekuwa inaniruhusu basi leo ningevaa ninja ili nisiwaone wengine, niseme maneno mazito sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kwanza nichukuwe fursa hii sana kuwapongeza watendaji wote wa Mdhibiti Mkuu pamoja na yeye mwenyewe. Lakini nichukuwe fursa hii kuwapongeza Kamati yetu ya PAC kwa ripoti yao nzuri sana akiwemo Mwenyekiti wao.

Mhe. Spika, tume au chombo hiki cha Mdhibiti Mkuu ni chombo muhimu sana na ambacho kinaibua mambo mengi sana, kinafanyakazi kubwa na wanatoka jasho jingi. Lakini mimi nataka nidhubutu kusema hakina maana yoyote kuwepo. Nina sababu zangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sababu moja ya msingi chombo hiki kinatuletea mambo mazito sana, lakini serikali haiyafanyii kazi. Wanajihatarishia maisha yao, mshahara wanaolipwa mdogo, lakini bado wanaibua mambo mazito sana. Mimi nadhani niishauri serikali sana kutilia mkazo mambo yote yanayoletwa na Mdhibiti Mkuu. Wafanyakazi wale wanafanyakazi ngumu sana katika mazingira magumu, sisi sote ni mashuhuda wa hili. Lakini ikiwa wanaibua ufisadi mkubwa, mambo mazito na serikali haichukulii hatua zozote. Mhe. Spika, mimi ningeomba ofisi hii ifutwe kabisa itakuwa haina maana. Tunapoteza fedha za wananchi nyingi, wavuja jasho katika kutekeleza wajibu wa Mdhibiti Mkuu. Lakini leo serikali bado inafanya mzaha na chombo hiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba sana na ninamshauri Mhe. Waziri, nakufahamu sana tangu unanisomesha, hujawahi kuwekwa pahala pakaenda vibaya. Ni hakika kila unapowekwa Maalim Haroun basi wizara inakwenda vizuri, na ninakuamini. Suala hili uje uniambie utafanya vipi ili kuona basi Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu inachukuliwa hatua ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niende tena kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma. Chuo hiki ni chombo ambacho ni msingi mzuri sana kwetu sisi na nina hakika kama tutakiendeleza vizuri basi kinaweza kujiendesha kuliko kupokea ruzuku. Lakini vile vile chombo hiki nacho kinahitaji kusimamia ili uwe usimamizi bora zaidi.

Mhe. Waziri nakuamini umetoka kwenye taaluma hii na unaweza kukisimamia na chombo hiki kikaweza kujiendesha wenyewe hata bila ya kuchukua ruzuku kutoka popote. Mhe. Spika, chombo hiki muhimu nataka leo niishauri serikali sana kufanya hata *refresher course* kwa wale watumishi wa umma ambao

wamesoma zamani, ili tuone basi wanarudia katika msingi wa maadili ya kazi na hii ndio taaluma ambayo tumewekewa pale. Lakini hiki chombo ni kizuri na uzuri wake haukosi kasoro, kuna kasoro ambazo zipo. Kuna mitaala mingi sasa, kuna *faculty* nyingi zimeanzishwa, lakini zimeanzishwa kwa utashi. Kuna wanafunzi wanalalamika hawana walimu pale, sasa sio jambo zuri, tunaweza tukatoa wanafunzi wamepasi pale lakini hatutowi wanafunzi wazuri, wamepata elimu bora lakini bora elimu. Sasa nikishauri sana chombo hiki muhimu tuweze kwenda kwa uhakika na tusimamie vizuri.

Mhe. Spika, kwanza niende kwenye Tume hii ya Utumishi Serikalini. Juzi katika michango yangu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nilikuwa nikisikitika na kuoneshwa kukerwa kwangu sana na miundombinu duni inayofanywa kwa walemavu. Lakini hapa kwenye Tume hii ya Utumishi lipo hili hili, na kwa hivyo leo Maalim Haroun hili nitavaa kabisa ninja nisikuone, kama suala hili sikupata majibu mazuri, kwa sababu kuna wataalamu wengi walemavu na wanajikusanya pamoja kuweza kuona wanapeleka vyeti vyao pale kwa walemavu ili kupatiwa ajira, lakini kila tunapoajiri na wataalamu hawa walemavu wanakuwa kidogo sana au hakuna kabisa. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri utakapokuja uniambie kwa miaka hii mitano walemavu wameajiriwa sehemu gani na wangapi na katika maidara ni maidara gani au mawizara gani ambayo wameajiriwa.

Mhe. Spika, niende tena kwenye Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki. Kwanza niipongeze sana kwa hatua kubwa sana, wasanii wenzangu wa maigizo na nyimbo mbali mbali wameanza kufaidika hata imeweza kupelekwa katika Wizara ya Habari, Utalii na Michezo kuweza kupata mirabaha mbali mbali na wanafanyakazi kubwa tu sana, na hata nimeshuhudia maduka mingine ya kurikodi kaseti kule na CD wameanza kuyafungia ili kuona hawa wasanii wetu wanafaidika na kazi zao ambazo zinafanywa.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii niwape hongera sana na waendelee na kazi yao hii. Lakini Mhe. Spika, kwenye ofisi hii kuna bodi hapa, lakini bodi hii imekwisha muda sasa tunaanza kwenda kibabe, sijui Mhe. Waziri kama unajua hilo au hujui, hebu ukija uniambie bodi hii imekwisha muda lini na una mpango gani wa kuunda bodi hii nyengine hapa ili twende kisheria. Tukiweza kwenda hivi hivi hatwendi na sheria, bodi hii muhimu sana na nimeisifu huku kutokana na ubora wake kwa wasanii wenzangu hawa. Sasa ikiendelea tu bodi imekwisha muda na chombo hiki kinaweza kushtaki na kushtakiwa. Sasa tusije tukaingia hasara zisizokuwa na mpango. Ningeomba tu nipate ufafanuzi kwa jambo hili linakuwaje au bodi hii inaundwa lini.

Mhe. Spika, nirudi tena kwenye *E-Government*, mimi mpaka leo hii miaka yangu sita katika utumishi huu wa siasa sijaijua hasa iko wizara gani, maana naanza kuona inapigwa danadana tu. Leo Wizara ya Fedha na Mipango, inasema *E-Government*, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji *E-Government*, Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora *E-Government*, hebu niambiwe hasa iko wizara gani, ili tuone basi mafanikio gani tutayapata, au kama tutaishika basi tujuwe tunaishika wizara gani. Nadhani Mhe. Waziri atanipa ufafanuzi wa kutosha ili basi na mimi niweze kujiridhisha kuona nijuwe *E-Government* iko wapi.

Mhe. Spika, niende kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, dhana ya serikali ni nzuri sana, chombo chochote ambacho serikali inakikusudia kukiunda kinakuwa kizuri sana. Nimewasikia wajumbe wenzangu chombo hiki kinakwenda kufanya semina mbali mbali vijijini na mambo mengine.

Mhe. Spika, sio kila kitu siasa, wao hawataki *legitimacy* kuwa kubwa kwa wananchi kule kupata sera, hiki chombo cha kisheria watunge sheria, warekebishe sheria hizi za zamani zilizopitwa na wakati. Mhe. Waziri utakapokuja uniambie ni sheria ngapi mpaka sasa zimeweza kufanyiwa *amendment*, marekebisho hayo ili tuweza kujua basi na sisi sheria gani ya zamani imefanyiwa hivi na sheria hii imeiona kasoro gani, tusiende tukafanya semina tu vijijini utafikiri sisi wana siasa tukapige mdomo tu kule.

Mhe. Spika, nije kwenye sheria ya usajili wa vyama vya siasa sheria namba 5. Juzi wakati naleta hoja yangu hapa ya kuitakia nchi hii amani, sheria namba 5 ya usajili wa vyama vya siasa inasema;

"Chama chochote kitakachokwenda na maadili yaliyopotoka kifutwe"

Mhe. Spika, na ninayo sheria nilijaribu kui-*search* kwenye mitandao nimeipata, lakini nataka wizara iniambie ni hatua gani, baada ya kuwashtua kwa ile hoja yangu imechukua ili kuzungumza na Msajili wa Vyama vya Siasa, ili kujua Msajili wa Vyama vya Siasa amepelekewa nini au anatoa tamko gani kuhusu ukiukwaji huu mkubwa wa haki za binadamu.

Mhe. Spika, nadhubutu kusema ukiukwaji wa haki za binadamu, kwa sababu leo wenzetu Pemba sala zinasaliwa jamaa mbili, jamaa ya CCM na jamaa ya CUF tunaanza kusahau Uislamu wetu. Mhe. Spika, lakini wengine isitoshe wanaanza kutolewa Misikitini wanafungwa kamba kabisa wasiingie. Sasa hii inasikitisha sana kusikia habari hizi zinakera na zinasikitisha sana kwa waumini dini ya Kiislamu kuwa hivi…

Mhe. Spika: Una dakika tano mheshimiwa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nakushukuru Mhe. Spika, zitanitosha sana.

Mhe. Spika, vile vile ningeomba ufafanuzi kwenye hiki kitabu kikubwa hapa Mhe. Waziri anisikilize vizuri sana na watendaji wake. Kifungu PG 0402 ningeomba ufafanuzi wake nitatoa kwa kifupi tu, lakini kifungu PG 0401 naomba ufafanuzi. Vile vile kwenye Tume ya Utumishi Serikalini, kifungu SG 090101 ningeomba ufafanuzi wake. Vile vile na kifungu HG 09010101 kwa nini mwaka 2015/2016 bajeti hiyo hakikutengewa pesa, lakini 2016/2017 kimetengewa pesa. Kwa hiyo, ningeomba ufafanuzi kwa nini vitu hivyo havikutengewa pesa.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana sasa nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia 98, asilimia 2 naomba nizichukue ili mpaka nikapata ufafanuzi nitaweza kuunga mkono. Nakushukuru sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi hii ya kuweza kuichangia hotuba hii na kwa kuwa michango yangu mingi niliyoiandaa kwa ajili ya kuchangia leo, baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza. Lakini kwa kuwa nimeleta jina na mimi niweze kuchangia basi nitaomba kuna mambo tu ambayo nitaomba ufafanuzi wake.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hotuba yake hii nzuri ambayo imebeba mambo mengi ya kuonesha kwamba sekta zote na taasisi zote zilizomo ndani ya nchi yetu hii basi zimo ndani yake. Mhe. Spika, mimi nitaomba mambo haya yafuatayo ili nipewe ufafanuzi.

Namuomba Mhe. Waziri katika hotuba hii kuna mambo ambayo ya utawala bora na haki za binadamu, kuna kipengele ambacho kipo ukurasa wa 13 kuna elimu ya uraia ambayo imetolewa katika vijiji saba kwa mwaka 2016 ikiwemo Unguja na Pemba. Naomba anipe ufafanuzi ni vijiji gani ambavyo vimepewa elimu hiyo katika kamati za ushauri za shehia. Lakini pia Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze kwamba kuna Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika ukurasa wa 19, kamisheni hii ina jukumu la kusimamia mali za wakfu, mali za amana, mirathi ya Waislamu, zakka, sadaka na misaada ya kheri.

Jumla ya shilingi milioni 277,272,000/- zilikusanywa hadi kufikia mwaka Machi, 2016. Misaada yenye thamani ya shilingi milioni 273,312,500/- imegaiwa kwa wahitaji Unguja na Pemba watu 20 kutoka Wilaya saba za Unguja. Naomba Mhe. Waziri atapokuja kutoa majumuisho anieleze kwamba ni watu wa Wilaya gani katika hizo Wilaya saba, ni Wilaya ipi ambayo watu hao wamepatiwa misaada hiyo. Hapa nimeeleza ni Wilaya saba za Unguja je, Wilaya za Pemba hakuna mtu aliyepatiwa misaada hiyo?

Mhe. Spika, lakini pia kuna kesi nyingi za watoto ambazo kwa Mkoa wetu wa Kaskazini zinaripotiwa katika Mahakama ya Mfenesini, kesi hizo ambazo zinahusu udhalilishaji na unyanyasaji kwa wanawake na watoto. Lakini sasa katika Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Kaskazini "B" kumejengwa Mahakama ya Watoto. Naomba Mhe. Waziri anifafanulie kwamba Mahakama ile imejengwa itakuwa inawahudumia kwa kusikiliza kesi za watoto ambao wananyanyaswa na kudhalilishwa au watoto wale ambao wanafanya makosa chini ya umri ya miaka 18. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kuleta majumuisho basi anitolee ufafanuzi.

Mhe. Spika, lakini pia katika usimamizi wa masuala ya dini katika ukurasa wa 35, katika masuala haya ya dini tunafahamu kwamba kuna madrasa na misikiti, lakini kuna walimu wa madrasa baadhi yao ikifika wakati wa kipindi cha uchaguzi wanakuwa wanatoa elimu ya kuhamasisha vibaya, au wanapotosha watu wetu badala ya kufundisha masuala ya dini wanafundishwa masuala ya siasa. Haoni kwamba siasa na dini ni vitu tofauti na wanaipotosha jamii yetu wasiiunge mkono serikali yao. Je, ofisi hii itasimamia vipi kuwachukulia hatua watu kama hawa?

Mhe. Spika, kuna baadhi ya watumishi wa serikali katika sekta zao na wao pia wanajihusisha na masuala ya siasa katika hizo sekta zao, hususan walimu wa shule za msingi na sekondari badala ya kufundisha masomo ambayo wao wanatakiwa wawape elimu lakini wao wanawasomesha masuala ya siasa, masuala haya yapo. Je, wizara hii inawachukulia walimu hawa hatua gani pindipo wakifanya makosa haya?

Mhe. Spika, nitazungumzia la mwisho suala la rushwa. Rushwa ni adui wa haki lakini pia wajumbe wenzangu wamezungumzia kwa kina, ninachokiomba na kushauri bila ya sisi wenyewe viongozi kwanza kubadilika basi nadhani rushwa hii haiwezi ikaondoka. Kwa sababu sisi viongozi katika maeneo mbali mbali tunatumia hizi kutoa au kupokea kwa sababu sasa hivi umefika wakati sasa mtu yeyote anapokwenda katika sekta yoyote hawezi kufanikiwa jambo lake mpaka atoe rushwa, na hususan sisi wanawake, wanawake wengine wanashindwa

kwenda kuomba ajira sehemu kwa sababu ya rushwa ya ngono. Mhe. Spika, naomba wizara hii itoe elimu kuhusu suala hili na likomeshwe suala la rushwa ya ngono katika maofisi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba watumishi wengine wa serikali na taasisi mbali mbali wanapofanya makosa, wawe wanapewa adhabu ya kuhamishwa katika eneo husika na kupelekwa eneo jengine. Kwa hiyo, ningeishauri wizara kwamba mtumishi yeyote atakapofanya kosa basi afukuzwe kabisa kwa sababu atakapohamishwa hapa kafanya kosa fulani akienda katika sekta nyengine ataenda kulifanya kuliko lile.

Mhe. Spika, na mwisho kabisa nasema na mimi niungane mkono na wenzangu katika kuiunga hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi mchana huu kuweza kuichangia hotuba hii.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora hotuba yake ni nzuri ambayo ina hekima, busara na uadilifu mkubwa ndani yake, na pia hotuba hii imetupa changamoto mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi kwanza nianzie kwenye Mahakama. Mhe. Spika, kama tunavyojua kwamba kuna wananchi wengine wakipelekwa Mahakamani kwao ni aibu, lakini pia imetokea kuwa wananchi hao hao wanapelekwa Mahakamani wakifika Mahakamani wanawekwa rumande si chini ya miezi mitatu au minne.

Mhe. Spika, inapokuja kesi yao huangaliwa kwa kina na huonekana kwamba hawana tatizo. Mtu yule yule anaambiwa aende tena Mahakamani na atachukuliwa dhamana, kwani wananchi wengine huwa hawana uwezo mtu ana akiba yake ya ng'ombe au mbuzi anakwenda kuiuza kwa ajili ya kwenda pale kudhaminiwa na hatma yake akaonekana hana hatia. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kwamba huu si udhalilishaji?

Mhe. Spika, pia kuna baadhi ya askari wetu wanapokwenda kupekua kwenye nyumba za wananchi basi tunakosa utaratibu. Mhe. Spika, niseme hili ndani ya wiki mbili zilizopita tumemshuhudia mama mmoja kwa kweli alisikitika vibaya sana na alitwambia kwamba linalonisikitisha zaidi nimekwenda kupekuliwa ndani ya nyumba yangu nikiwa mimi mwenyewe ni mwanamke, simo ndani ya

nyumba na aliyekuwepo nyumbani ni mtoto wangu ana miaka 15 waliokwenda kunipekua ni sheha pamoja na askari wa kiume. Mhe. Spika, anasema sio tatizo kwake yeye kupekuliwa na sioni tabu lakini naona aibu kupekuliwa na wanaume. Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba utakapofanya majumuisho utueleze kwa kina je hii ni sheria?

Mhe. Spika, vile vile niseme kwamba hapa Mhe. Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 18 (63) unasema.

"Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazo taasisi tatu zinazopokea ruzuku ambazo ni: Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Chuo cha Utawala wa Umma na Afisi ya Hakimiliki".

Mhe. Waziri tunao wanawake ambao wamefikia miaka 10 ni wajane hawana waume, hali zao ni ngumu, wanashindwa hata kuingia katika vile vikundi vya *SACCOS* ambavyo tunavyo ndani ya mitaa yetu.

Mhe. Spika, hapa namwambia Mhe. Waziri tayari wazee wameshasaidiwa waliofikia umri wa miaka 70. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba hawa wanawake ambao wamekaa ujane kwa umri wa miaka 10 hawajaolewa, je wao hawa atawasaidia vipi kwani na wao wana haki, na wao ni wananchi wake kama inavyosema Ofisi yake ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, leo ingelikuwa kama Mhe. Shadya tuko nyumba moja basi lile alilolizungumza mwanzo lingeonekana kama tumelipanga pamoja. Lakini niseme lile alilolizungumza Mhe. Shadya nimpongeze sana, sana kwa sababu lile limo ndani ya shehia yangu na mmoja aliye na tatizo lile ambaye ninae hata asubuhi ya leo alinikumbusha kwamba yeye alikuwa ni mtumishi wa umma, lakini pia alifukuzwa kazini na mpaka hii leo hajarejeshwa na taratibu zote kamaliza.

Mhe. Spika, na mimi niongeze kwamba nalitilia mkazo watu wa aina hii Mhe. Waziri awaangalie kwa kina sana hawa ni wananchi wetu, na wao ni wapiga kura wetu tusiwaweke nyuma lazima yanapotokea kama haya wasimamiwe na wao wajisikie kama ni wananchi kama wenzao.

Kwa sababu kuna wengine waliofanya matatizo kama haya wamesharejeshwa kazini, lakini huyu kwa nini mpaka leo hajapata jibu lolote. Mhe. Waziri naomba utakapokuja kutoa majumuisho ya hotuba yake atupe majibu, kwa nini mtu huyu mpaka leo hajarejeshwa kazini au kuna ugumu gani uliofikia

kwamba mpaka leo bado hajamaliza tatizo hili na yeye ni binadamu kama binadamu wengine.

Mhe. Spika, kwa kumalizia hayo naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja kwa Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Spika, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi hii adhimu na mimi kuwa mchangiaji katika wizara hii.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia kuamka tukiwa wazima wa afya na hatimae kuweza kukutana katika chombo hiki muhimu. Lakini Mhe. Spika, nianze kwa shukurani zangu za dhati nampongeza kwa dhati kabisa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa imani kubwa aliyopewa na Wazanzibari yakuweza kuongoza kwa awamu ya pili. (*Makofi*)

Pia nimpongeze Mhe. Makamu wetu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kuweza kuaminiwa tena kwa mara ya pili kushika nafasi hii na kuweza kushirikiana nae Rais wetu katika majukumu yake, nimpongeze sana, sana, sana.

Mhe. Spika, pongezi zangu nizilete kwako wewe, kwa Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wetu wote wawili wa Baraza hili kwa kuaminiwa na wajumbe wenzao kwa kuweza kuwaongoza katika kipindi hiki.

Mhe. Spika, nilipongeze pia Baraza lake la Mawaziri Mhe. Rais, kwa pamoja nalipongeza kwa vile lina sura ya vijana. Mimi naamini sana kwamba vijana hawa watatuvusha kwa salama na amani kuona nchi yetu inasonga mbele. Nawapongeza na naamini vijana tunaweza. Kipekee kabisa niishukuru sana familia yangu kwa kunipenda, kunishauri, kuniunga mkono katika harakati zangu zote za siasa tangu nimeanza mpaka hapa nilipofika.

Vile vile nawashukuru na niwapongeze kwa dhati kabisa vijana wenzangu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kuniunga mkono, kwa kuniamini na kunichagua kwamba mimi nije hapa kuwawakilisha katika mambo yetu ya vijana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwanza kabisa niende kwenye hotuba hii moja kwa moja. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii nzuri, mlezi wangu, baba yangu kwa kweli hotuba hii ameipamba kwa mambo mazuri sana. Nimpongeze kwa muundo mzuri ambao ametuwekea lakini kidogo na mimi niseme nigusie

katika baadhi ya mambo. Nianze kwenye kesi ya Tume ya Marekebisho ya Sheria.

Mhe. Spika, kwenye tume hii tumeona kwamba ina-*deal* sana na mwenendo mzima wa kesi za jinai, na bahati nzuri katika kesi hizi zikiwemo kesi za udhalilishaji na katika kesi hizi tumekuwa tunaona kwamba kuna kipengele cha ushahidi, na kipengele hiki kimekuwa kikituadhibu sana. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nakasema kwamba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleweshe na atujuulishe kesi hizi au sheria hii ama kipengele hiki amekichukuliaje na wamefikia wapi katika kesi hizi hasa hasa hizi za udhalilishaji. Kwa sababu mtu yeyote ambaye anafanya udhalilishaji hatokubali na wala hatoridhia kwamba jambo hilo alifanye akiwa anaonekana.

Mhe. Spika, pia niende kwenye kesi ya mamlaka ya kuzuia rushwa. Mhe. Spika, rushwa ni adui wa haki sio Tanzania tu peke yake ama Zanzibar, lakini dunia nzima wanaimba wimbo huu na hii rushwa tunaona imegawika katika sehemu mbali mbali kama wenzangu walivyoanza kutangulia kusema kwamba kuna rushwa ya ngono, rushwa ya pesa lakini pia kuna rushwa ya maneno Mhe. Spika.

Mhe, Spika, Mimi nizungumzie sana kwasababu mimi ni mwanamke, kwenye kesi ya rushwa ya ngono napo ni tatizo. Na Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake hii ametuambia kwamba kuna semina kumi na nne ambazo zimetolewa kuhusiana na hawa kesi zetu hii ya rushwa, na mamlaka hii mimi naamini kwamba katika semina hizi sijui Mhe. Waziri, wamejumuisha makundi gani au tabaka gani. Kwa hivyo mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atueleweshe, atufahamishe katika semina hizi amegusa makundi gani na je, kama sisi kama mabosi maofisini na sehemu nyengine wamegusia kuwaelewesha katika kesi hii.

Mhe. spika, lakini vile vile sote ni mashahidi tunatembea njiani kuna hawa ndugu zetu Askari wa Polisi barabarani, hawa wao wenzetu rushwa yao sijui niseme wanaiomba vipi, kwasababu rushwa yao hii wanakuomba wakiwa macho meupe, hawaoni aibu tena iko wazi wazi. Kwa hiyo Mhe. Waziri, atakapokuja hapa na katika maelezo yake ametuambia kuna kesi 51 ambazo zimefunguliwa kuhusiana na kesi hii ya rushwa basi atueleze, kuna baadhi ya kesi ambazo zimewagusa hawa Askari polisi? Kwasababu nao ndio walalamikiwaji wakubwa katika kesi hii na hasa ukizingatia wananchi wetu wanawaona moja kwa moja.

Mhe. Spika, naomba kugusia kwenye Tume ya Utumishi Serikalini. Katika kitu ambacho kinatusumbuwa sana vijana na kitu ambacho tunakilalamikia sana vijana ni Tume ya Utumishi Serikalini, kwa sababu hapa ndipo kwenye mategemeo yetu kama vijana tunapohangaika baadaye mwisho wa siku tunategemea ajira kutoka Serikalini, tunaamini ni nafasi chache.

Kwa sababu Mhe. Spika, Mhe. Waziri, katika hotuba yake ametuambia katika mwaka uliopita kuna nafasi za ajira 225. Sasa sijui Mhe. Waziri, kwenye Tume hii ameangalia angaliaje haya makundi maalumu, wakiwemo ndugu zetu walemavu; kwa sababu najua kuna sheria ambayo inazingatia makundi haya maalumu wakiwemo walemavu lakini pia na nafasi za wanawake.

Kwa hivyo sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa mimi ningeomba kidogo atufanyie upelelezi na pia atutolee ufafanuzi kwamba nafasi hizi zimewekwa kutokana na mahitaji haya maalumu, lakini pia atueleze kwamba hii Tume hii inayoshughulikia huu uajiri haiendani na urasimu. Kwa sababu watu wengi sana wanalalamika huko nje kwamba Tume hii inakwenda na urasimu. Kwa hiyo Mhe. Waziri, atakapokuja hapa tungemuomba sana sana aje kututolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka nizungumzie kesi ya Chuo cha Utawala wa Umma. Chuo hiki kipo katika Wizara hii, kipo vizuri tunashukuru, tunapata mafunzo mazuri, kinazalisha watu wazuri nikiwemo na mimi. lakini Mhe. Spika, cha kusikitisha sana kwamba Chuo kile mpaka sasa hivi bado kinamalizia kwenye ngazi ya Diploma na ukizingatia malengo sana ya Chuo hiki ni kuwasomesha na kuwaendelea wafanyakazi wetu.

Sasa Mhe. Waziri, mimi ningemshauri tu kwanza ili kwenda sambamba na elimu yetu sasa hivi hiki Chuo akiendeleze. Elimu ya Diploma kwa sasa hivi kwa mfanyakazi wa Serikali kidogo naona ipo chini sana, kwa hiyo mimi ningeomba wakieongeze, si kukiengeza jengo tu bali ni huduma ambayo inatolewa pale, wanafunzi wake wazalishe *Degree* ya Kwanza na hata ikiwezekana na madaraja mengine yote yatolewe pale.

Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri, akiangalie vizuri, kwa sababu mimi naamini kwamba Chuo hiki kama kitafanya vizuri au kitaendelezwa vizuri wafanyakazi wetu hawatatapa shida tena kwenda kwenye vyuo vya mbali, wakati chuo chetu kipo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache Mhe. Spika, niungane na wenzangu kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia zilizokuwepo baada ya kupewa majibu mazuri na Mhe. Waziri, Ahsante.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kufika hapa katika Baraza lako Tukufu leo hii. Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nimpongeze Mhe. Waziri, kwa jinsi alivyowasilisha hotuba hii mwanana kabisa. Pia niwapongeze wote walioshiriki ili kumrahisishia Mhe. Waziri kuweza kuwasilisha kitaalamu. Nimuombe Mwenyezi Mungu aiwezeshe bajeti hii kutekeleza yote yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, iweze kutekeleza kwa sababu bajeti hii ya Safina, bajeti hii ndio chombo kitakachovusha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini chombo hiki ambacho ndio tegemeo kimetiwa mafuta kidogo ambayo sijui kwamba yatafikisha safari, kwamba tukiangalia fedha zilizoingizwa katika Wizara hii hazitoshelezi na hii ndiyo Wizara ya Sheria na Serikali lazima ifuate sheria na ndipo inapokuwa Serikali. Sasa ikiwa kuna upungufu mambo mengi yatachupwa, mambo mengi yatakuwa hayatekelezeki, kwa hivyo itakuwa sheria inakiukwa. Kwa hivyo ningeshauri tu kwamba bajeti hii iongezewe ruzuku kwamba hii ndio muhimili wetu.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mrefu, lakini ninataka nianze na suala zima la rushwa. Mara nyingi tunaitaka Serikali iondowe rushwa, lakini rushwa haiwezi ikaondolewa kama malaria, malaria yanaweza yakaondoka na kupulizwa dawa majumbani na kwenye mazalio ya mbu halas, lakini rushwa haina dawa, rushwa haiondolewi na Jeshi la Polisi, haiondolewi na dawa ya aina yoyote, isipokuwa rushwa itaondoka kwa kukubali sisi kama jamii kushirikiana kikamilifu tukaiondowa rushwa, si vyenginevyo vyovyote.

Kama tutasema tu Serikali iondowe rushwa, miaka mia rushwa itakuwa ipo, kwa sababu gani; kwa sababu rushwa Mhe. Spika, ni haja za watu, ile rushwa ni haja za watu. Sasa hapa ningewaomba sana wenzangu, ningewaomba sana wananchi wa Zanzibar, ili tuondowe hii rushwa tuwe na subra. Tufanye subra katika kuhitaji mambo yetu. Kwa sababu yule mhitaji, kila mhitaji wa jambo lolote au nafasi yoyote anataka mambo yake yawe kama anavyotaka yeye leo leo, Kesho kesho, hapo ndipo inapoanza rushwa. Sasa tuwe na subira na tujiamini kabisa tumuelekee Mwenyezi Mungu ambaye ndiye mtoaji rizki, tukifanya hivyo itaondoka rushwa yenyewe.

Mhe. Spika, kama abiria yupo kwenye gari, gari ambayo ikisimamishwa njiani na Jeshi la Polisi ikawa honi haifanyi kazi, *indicator* hazifanyi kazi, mipira ni vipara, abiria wote wakamngangania pale Askari lazima umshitaki huyu kama hukumshitaki tutakushitaki wewe kwa sababu ukimuachia huyu ni hatari yetu sisi na vizazi vyetu. Sasa tukenda namna hiyo kwa nini isiondoke rushwa au popote inapoonekana rushwa, kwa sababu rushwa kama wanavyosema wenzangu inakuja kisiri siri. Sasa pale ambapo mtu amebahatika kuiona ile rushwa basi itangazwe. Fulani ameonekana pahali fulani akitoa jambo fulani kwa ajili ya kutaka jambo fulani. Sasa rushwa itangazwe kwa sababu mwanadamu hapendi kutangaziwa uovu wake, kwa hivyo itakapotumika njia hiyo ya kuwatangaza wale wanaokula rushwa huenda ikapungua kasi.

Mhe. Spika, tuangalie suala moja, kesho kutwa ni Ramadhan tukijaaliwa, Waislamu wote watafunga, lakini hao hao watakaofunga hawasali, sasa tupime hapo ibada ya funga na ibada ya sala nzito ni ipi, suala linachukuwa dakika saba tu kama utakwenda inavyotakiwa au pengine tano au wengine tatu basi ushamaliza, lakini ibada ya funga ni kutwa nzima, lakini na binaadamu anaogopa njaa, ataona bora akae na njaa mpaka jioni, lakini kwa nini hasali, na suala lililo rahisi kuliko funga.

Sababu yenyewe ni kwamba kama mtu atamuona Mhe. Said mwezi wa Ramadhani ndio anywa chai, Pemba nzima itaenea kule ah! Mhe. Said unamuona anakunywa chai. Kama ni Unguja Mheshimiwa yule ameonekana anakunywa chai pale Lukmani, sasa hii ndiyo inayoogopwa tu, lakini sala aliyekuwa haswali watu husikii kuwa yule hasali yule. Sasa hiyo haimshughulishi. Kwa hivyo endapo sisi tutawatangaza wale wakosa wa rushwa Unguja na Pemba hiyo ni njia moja ya kuondoa rushwa.

Mhe. Spika, niende katika Tume ya Utumishi Serikalini. Mhe. Spika, tuna tatizo kubwa la ajira, mara nyingi tunapiga kelele, tuna vijana wetu hawana ajira na ajira zilizoko ni chache ambazo haziwatoshelezi walengwa, kama ajira za mwaka kama ni elfu mbili na tano kwa mfano, watu wetu ni elfu sita na kila mwaka wanatokea watu ambao wanahitaji ajira na wenye sifa za kuajiriwa, lakini nafasi hazipo za kuajiriwa, mimi naona zipo nafasi zimejificha tu. Mhe. Spika, Mzee wangu mmoja alinambia hivi yule yule wa sadaka ndiye yule yule wa kuchinja.

Mhe. Spika, sababu iliyopelekea kukakosekana ajira ni wale wafanyakazi ambao wameshafika muda wa kustaafu wakakaa miaka mitatu, miaka minne ndio wakapewa kiinua chao mgongo. Endapo wafanyakazi kazi wale waliostaafu watapewa kiinua mgongo *within six month* na walionyuma huku

ambao bado miaka mitatu wote wataomba kustaafu, wakiomba kustaafu hao tayari kundi kubwa la ajira za vijana wetu, na hata siku moja baada ya mtu kushastaafu hatopeleka tena barua ya ombi kuwa nachukua tena mkataba wa miaka miwili. Kama mtu kashafikia muda wake wa kustaafu halafu akapeleka tena ombi la miaka miwili si kwamba hajachoka kazi eti, miaka arubaini ndio kashachoka kazi hii, lakini anaogopa nini miaka mitatu sijapata kiinua changu mgongo. Kwa hiyo bora nichukuwe miaka miwili huwenda miaka miwili ikawa mambo yasharekebishwa. Sasa namuomba Mhe. Waziri, hii aiangalie kwa kina ili tuweze kuwapatia vijana wetu ajira.

Mhe. Spika, nije katika Ofisi ya Mufti. Ukurasa wa 14 kuna maelezo yafuatayo naomba kunukuu.

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana nashukuru. Hadi kufikia Machi 2016 madarasa 85 na Misikiti 35 imesajiliwa Unguja na Pembana, Vyuo vya Qur-an 52 na misikiti 35 imetembelewa kwa lengo la kushauriana na kutoa nasaha na ushauri juu ya maendeleo ya Taasisi hizo.

Mhe. Spika, nilivyokuwa nachangia hotuba ya Wizara ya Fedha nilisema kwamba Zanzibar tumebarikiwa kwamba kila hatua ishirini tuna Msikiti, lakini ninashangaa kwamba katika kitabu hiki misikiti 35 tu iliyosajiliwa ambayo hayo ni kama majimbo mawili tu ya Zanzibar, sasa ina maana zinapokuja sadaka za Waisilamu hapa Zanzibar itakuwa kundi kubwa haziwafikii kwa sababu Misikiti hiyo haina usajili. Ningemumba Mhe. Waziri aendelee kuisajili misikiti ya Zanzibar ambayo ni mingi mno ili itakapokuja sadaka wafaidike Waisilamu wote.

Pia imesema kwamba Vyuo vya Qur-ani 52 vimetembelewa. Hii sentensi ingesomeka hivi: "Vyuo 52 vimewezeshwa" ingependeza zaidi hapa.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Spika, tungemuomba sana Mhe. Waziri vyuo hivi japo hivi 52 wapewe msukumo walimu wa vyuo hivi angalau kwa shilingi 50,000 na tutamuomba Mhe. Waziri atuhakikishie kwamba atatoa msimamo gani angalau hivi 52.

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Wingwi basi nipongeze na kuipitisha bajeti hii bila ya buti yoyote.

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika hapa nikiwa mzima wa afya na pia nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuweza kuchaguliwa kwa kipindi cha pili kuweza kutuongoza.

Vile vile nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Gando kwa kuweza kuniunga mkono na mpaka sasa kufika katika Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi nielekee katika kifungu cha Tume ya Utumishi Serikalini. Katika kifungu hiki kuna programu ya usimamizi wa uajiri, haki na nidhamu ya watumishi serikalini na utawala na uendeshaji. Kwenye eneo hili imeoneshwa moja ya majukumu ya Tume ya Utumishi ni kusimamia uajiri na kuimarisha maadili na haki za watumishi serikalini.

Mhe. Spika, lakini Tume hii haifanyi kazi kwa uadilifu na kupelekea kuleta malalamiko mengi hasa kutokana na mabadiliko ya mishahara. Kuna wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu, wafanyakazi hao ni kama wale wasafishaji mitaro, wazoa taka majaani, wasafishaji mabarabara. Watu hao Tume hii ni ya kuwaonea huruma kwa kweli mazingira yao ya kazi huwa ni magumu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile kuna wafanyakazi ambao huhama kutoka wizara hii kwenda wizara nyengine, wafanyakazi hawa hucheleweshwa mishahara yao kuhamishwa mpaka kufikia kulalamika. Mishahara yao hawabadilishiwi kwa haraka ili kupata kujikidhi kutokana na sehemu hii waliyotoka kwenda sehemu nyengine, hucheleweshewa na kubakia kulalamika kupeleka barua na kuzungushwa huku na huku mpaka wakakata tamaa. Kwa kweli naiomba tume hii ijitahidi kuwaona wafanyakazi hao.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze utaratibu gani anaotumia katika mabadiliko ya wafanyakazi kubadilishwa mishahara yao.

Mhe. Spika, kwa kweli katika nchi nyingi duniani ajira ni tatizo kubwa. Kwa hivyo, naiomba tume hii au wizara kuna vijana ambao walipitia JKU kule Msaani zinapotokea ajira katika sehemu za vikosi naomba wizara hii vijana wale waliopita JKU kujitolea na vijana hawa tunao. Katika jimbo langu ninao

ambao wana vyeti vyao bado zikija ajira watu hawa naiomba serikali iwaone kwanza kuliko hali nyengine.

Mhe. Spika, nielekee katika kipengele cha Programu ya Usimamizi na Masuala ya Dini. Kipengele hiki kimetugusa sana kwa sababu asilimia kubwa ya Wazanzibari ni Waisilamu. Hivyo basi, naiomba wizara hii kutokana na serikali hii kuwa ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio iliyopindua ikaondosha ubaguzi, ikaondosha watumwa. Kwa hivyo, naiomba iwaone watu ambao wanabagua wenzao kule kisiwani Pemba na hasa sisi Waisilamu na kesho kutwa tunaingia katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Sasa wizara hii iwaone watu ambao wanafanya mambo haya yaliyokuwa si mazuri, Mwenyezi Mungu anaweza kutuletea nakama yoyote ikisha baadae wasingizie serikali hii haiwasaidii. Serikali hii ndiyo iliyoleta ufukara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nina ushahidi ambao watu wanaodhalilishwa na waume zao kwa ajili ya kuichagua serikali hii. Watu hao wanasema sisi hatuwapi chejio kwa sababu mmeichagua serikali hii ndiyo itakayowapa chejio, wamenilalamikia mpaka jana wamenipigia simu. Kwa hivyo, naomba serikali kupitia wizara hii ya masuala ya usimamizi wa masuala ya dini isimamie ipasavyo kutokana na sisi Zanzibar tuna Mufti wetu afuatilie kwa kina masuala haya ili wananchi wapate haki zao kama ipasavyo.

Mhe. Spika, walimu wetu wa Madrasa hapa nimeona kwenye kipengele cha 128, Misikiti 95 na Madrasa 195 ambayo imesajiliwa. Mheshimiwa kutokana na hawa walimu wa Madrasa ambao wanatusomeshea watoto wetu na watoto wakipitia kwenye madrasa ndio wanapopata ufahamu zaidi wa kuanzia masomo yao ya skuli. Mwenyezi Mungu alitwambia kwamba tutafute elimu mpaka China, kwa hiyo elimu hii sio elimu ya duniani tu bali na elimu ya Akhera. Naomba Mufti huyu ashughulikie suala hili la walimu wa Madrasa angalau kuwapa posho tu, ili kuwatia motisha ya kutusomeshea watoto wetu.

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kusema ndio hayo tu, naiunga mkono hoja hii kutokana na kwamba hakuna mkamilifu basi naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako na mimi napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo nikaweza kupata fursa hii na mimi pia nikawa miongoni mwa wale ambao wataichangia hotuba hii muhimu ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kabla ya hapo nigependa nichukue fursa hii pia kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili tukufu katika misingi mizuri ya usawa na haki na kuzingatia mambo mbali mbali ambayo inatuwezesha mpaka sasa hivi tunakweda vizuri. Ni imani yangu kwamba kazi hii itaweza kuleta tija katika nchi yetu nakuweza kuleta mafanikio kwa yale majukumu ambayo sisi yanatuhusu kama Waheshimiwa Wawakilishi.

Vile vile ningeomba nichukue fursa hii adhimu na maalumu kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameanza kuifanya mapema. Ni dhahiri kwamba wizara hii zilikuwa ni wizara mbili na sasa imekuwa wizara moja, kuunganishwa kwa wizara hizi mbili nyeti ni kazi moja ngumu sana. Lakini pamoja na hayo kutokana na ukomavu na uzoefu wa Mhe. Waziri naona imeonesha kwamba kuna kazi nzuri ambayo baadae itaweza kuonekana muda si mrefu.

Mhe. Spika, vile vile niseme kwamba imenipa matumaini na faraja kubwa wizara hii kwa mara ya mwanzo. Watu wanasema ukiona sehemu ambayo watu wanaweza kukosoa na kuchangia mambo mengi ni dhahiri kwamba utekelezaji hapo unaonekana, kwamba watu wanafanya kazi. Kwa fursa hii vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana wafanyakazi wa wizara hizi mbili ambazo zimeunganishwa imekuwa wizara moja, kwa kazi nzuri ya awali ambayo wameshaanza kutuonesha sisi Baraza hili na kuweza kuona malengo na mafanikio yanaweza kuonekana muda sio mrefu.

Mhe. Spika, vile vile napenda nichukue fursa hii adhimu kuwapongeza sana wapiga kura wa Jimbo la Micheweni kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na imani yao kubwa waliyoweza kunionesha mimi hadi leo nikasimama hapa kuendelea kuwasemea yale ya kwao ambayo wanahitaji au ni kero juu yao.

Mhe. Spika, mimi pia kwa mara ya mwisho katika pongezi niombe tu nipongeze sana Wizara hii ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ripoti nzuri yenye umakini, ambayo imeweza kuwasilishwa hapo mbele na ikatoa mwanga katika kuona kuwa imeanza kufanya kazi nzuri na inahitaji kupongezwa. Vile vile kujipongeza na mimi binafsi kwa sababu na mimi nikiwa miongoni nimefanya kazi nzuri.

Mhe. Spika, mimi sitochukua muda mwingi kwa sababu tumeshaanza kuona kuwa haya yote ambayo nataka kuyazungumza kila mtu tayari wameshaanza kuyachangia. Lakini hata hivyo, na mimi kwa vile nimepata fursa lazima niitumie katika kuchangia mambo matatu yafuatayo.

Kwanza nitagusa katika kuzungumzia masuala ya Utawala Bora na Haki za Binadamu ukurasa wa 13, lakini vile vile nitazungumza katika usimamizi wa masuala ya Dini ukurasa wa 35 na Chuo cha Utawala wa Umma ukurasawa 43.

Mhe. Spika, naomba nichangia katika Programu ya GO103 ya Utawala Bora na Haki za Binadamu. Katika programu hii imesemwa kwamba, moja kati ya majukumu ya programu hii ni kuimarisha misingi ya utawala bora katika utendaji wa taasisi za umma, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 imejieleza kuwa katika hotuba hii elimu ya uraia imetolewa vijijini kwa kuendesha mikutano sita. Vile vile imeweza kufanya vipindi 22 vya redio kwa upande wa Pemba vipindi tisa ambavyo vimerushwa kupitia redio jamii ya Mkanyageni.

Mhe. Spika, suala la elimu ya uraia pamoja na haki za binadamu ni jambo la msingi sana katika nchi yetu na ni jambo ambalo linaweza likaleta faraja, lakini bado napata mashaka kidogo katika taaluma ambayo imetolewa. Niombe na nitahadharishe wizara hii kwamba tuweze sasa yale ambayo tumeji-*commit* na zile fedha ambazo tumeomba na *Inshaallah* anatarajia Mhe. Waziri zitapitishwa hizi fedha ziweze kutekeleza majukumu ambayo yamepangwa.

Ningeomba kuishauri wizara hii kupitia wewe mwenyewe Mhe. Spika, kwamba ni vyema sasa tukaweza kufanya tathmini au tafiti ndogo juu ya zile huduma ambazo tunazitoa katika maeneo yetu hususan maeneo ya vijijini. Kwa sababu baadhi ya taasisi zinaweza zikachukua fursa hii ikawa ni simulizi tu, hatimaye ikawa utendaji unaweza ukawa tofauti kwa baadhi ya watendaji ambao sio waaminifu.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba Jimbo la Micheweni ni jimbo ambalo linaonekana liko nyuma na nashukuru kwamba hata makadirio ya mapato alipokuwa akiwasilisha Waziri wa Fedha na Mipango ilionekana hivyo katika viashiria vya umasikini vinaonekana bado viko juu. Moja katika suala zima la kupambana na umasikini ni suala la taaluma au elimu na ni jambo ambalo linaweza likasaidia zaidi katika kufikia malengo au kuweza kuongeza ufanisi katika kupunguza umasikini.

Jimbo langu la Micheweni bado hali hiyo ipo na hili pia limetokana na uelewa au taaluma kuwa bado ni ndogo. Hivyo, pamoja na juhudi mbali mbali za serikali hii kuonekana kwamba inaelekeza nguvu katika jimbo langu hili, bado kuna kazi nyengine ya kufanya kwa kufanya tathmini kwa zile taaluma ambazo zinatolewa. Tunawapitia wale wale ama tunapitia makundi yote kwa mfano kama watu wenye ulemavu na watu wengine.

Mhe. Spika, ningeomba katika hivi vipindi vya redio ambavyo vimerushwa kwa sasa hivi ningeshauri kwa mara nyengine inayofuata basi tutafute namna ya kuona kuwa na Micheweni pia kumeanzishwa redio, ambayo lengo lake ni kuweza kuwaelimisha watu wa Jimbo au Wilaya ya Micheweni na wananchi wengine wanaosikiliza katika kusaidia kupunguza umasikini, sambamba na kutoa taaluma. Sasa ningeomba hii elimu ya uraia basi ni vyema katika vipindi vyengine vingetumika kuangalia kwa upande mwengine katika Jimbo la Micheweni, kule kuna redio inaweza ikatusaidia katika kufikia malengo haya.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba nisogee kidogo katika usimamizi wa masuala ya dini. Mwaka wa fedha 2016/2017 katika masuala haya ni kwamba programu hii imepanga kufanya yafuatayo;

Mapitio ya Sheria ya Mufti, Kutembelea Misikiti 95, Madrasa 195 na Kuendesha Mikutano Miwili ya Baraza la Maulamaa na Vikao sita vya Kamati ya Kudumu kwa mwezi. Vile vile kuuza mahusiano kwa jumuiya za Kidini, za Kitaifa na Kimataifa.

Pia naomba nizungumzie kuwa hotuba imesema katika kipindi cha 2016/2017 ofisi hii au katika masuala ya dini katika Baraza lako tukufu limeombwa kuidhinisha fedha ambazo wameziomba katika kutekeleza jukumu hilo. Hii fedha ambayo wameizungumza hapa sina haja ya kuinukuu, lakini fedha hii ningeshauri kwamba ni vyema wapatiwe yote na kwa muda ambao wameshauri wao wenyewe katika kutekeleza jukumu hili. Lakini bado niendelee kutahadharisha kwa wizara au kwa taasisi hii, kwamba sasa hivi katika nchi yetu kuna changamoto nyingi ambazo kama ni taasisi ya dini, wao wanaweza wakahusika kwa njia moja au nyengine.

Katika mapitio ya sheria ningeomba basi ni vyema tuzipitie sheria zetu hizi pale itakapofika muda wake na kuangalia mazingira tuliyonayo sasa katika nchi yetu. Hili tumeangalia kwamba wizara imepanga kutembelea Misikiti 95 ni Misikiti michache mno katika nchi yetu, lakini pamoja na hayo bado katika Misikiti hiyo waweze kufanya tathmini kuona *out put* ambayo inaweza ikapatikana katika kufanya kazi hii na isiwe ni kutembelea tu. Nadhani wamepanga vizuri sio kutembelea tu, wafanye kazi nyengine zaidi ya kuweza kuelimisha kutoa taaluma zaidi katika Misikiti ambayo wameitaja. Kwani sasa hivi ukiangalia taasisi hii ya dini imekumbwa na changamoto nyingi, inapandikizwa mambo mengine ambayo hayahusiani moja kwa moja na katika kuupeleka mustakabali mwema katika masuala mazima ya dini kama vile ambavyo kwa kweli wameshaanza kuzungumzia Waheshimiwa wengine.

Tumeweza kushuhudia misikiti mbali mbali katika nchi yetu, kuna migogoro kuna mifarakano na ukifatilia kwa karibu utaona bado afisi hii mengine haijaweza kuyafikia. Sasa ni vyema ningeshauri Baraza hili tuidhinishe hiyo fedha na baadae kuwepo na mkakati na ufuatiliaji wa kina kuona kwamba shughuli hii inafanyika vizuri na yale malengo ambayo taasisi hii imeyapanga basi iweze kuyafanya na kuweza kuleta tija katika nchi yetu katika kupunguza haya ambayo sasa dunia au nchi yetu inaweza kuyazungumzia kwamba inaonekana ni kero katika jamii yetu.

Lakini vile vile programu hii imepanga kuendelea na usimamizi wa kuendeleza watumishi wa kuwapata fursa ya kujenga uwezo wao kitaalamu na kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa afisi, ni jambo moja ambalo kwa kweli ningeshauri kwamba hili pia ni jambo linahitajika kwa sasa hivi na ni vyema kwamba tuweze kuunga mkono hili na kuweza kusaidia katika kufikia malengo hayo ambayo yamekusudiwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba niende moja kwa moja katika Chuo cha Utawala wa Umma katika ukurasa wa 43 ambayo tayari walioendelea na walioanza wameanza kuchangia vizuri na kuweza kutoa ghofu zao na mambo mengine ya kuweza kuonesha kwamba kunaletwa maboresho.

Mhe. Spika: Una dakika tatu, Mheshimiwa.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kimepanga katika mipango yake kuimarisha mafunzo ya kujenga uwezo kwa watumishi wa umma kutoka serikali taasisi binafsi ikiwemo mafunzo elekezi, yaani kozi ya muda mrefu kwa watumshi wa ngazi za msingi, cheti, stashahada na shahada ya kwanza.

Mimi nilikuwa niombe tu kwamba Chuo hichi ni chuo ambacho kwa kweli kwa sasa hivi ni muhimu sana katika nchi yetu, ningeomba fedha ambayo wameiomba waweze kuidhinishiwa yote na kwa wakati. Lakini sambamba na hilo pia na ufuatiliaji kama vile wengine walivyoonesha ghofu basi tuweze kufuatilia kuona kwamba hizo fedha zilizopangwa zinatekelezwa kwa malengo mahususi ambayo yamekusudiwa. Kwani chuo hichi ninaposema kuwa ni muhimu sasa hivi watu wengi wanalalamika na Waheshimiwa wengi tumewasikia wakilalamika kuhusu masuala mazima ya kushuka kwa nizamu kazini ni jambo ambalo la msingi na tumeweza kulibaini.

Kwa hiyo, nadhani chuo hichi sasa kifundishe mambo ambayo kwa kweli ni ya msingi yenye maadili ya utumishi, sambamba na hilo kuutanguliza uzalendo

mbele ya nchi yetu. Basi na kuwepo hapa hichi chuo kikitumika vyenginevyo tunaweza tukafika sehemu ambayo tukaja kujiuliza.

Kwa hiyo, fursa hii ya chuo ningeiomba sana Mhe. Waziri, naamini Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman ni mtu mmoja ambaye anaweza kuifanya kazi hii kama vile Mhe. Rais amemuamini na imani yangu kwamba mabadiliko yataweza kupatikana kuona kwamba, chuo sasa kizalishe watumishi ambao wanasifa na wale ambao wanaweza kuisaidia nchi hii katika kusonga mbele katika kutatua kero hizi. Kwa sababu kama nidhamu ya utumishi ikishuka chini, tunaweza mambo tukaweza kuzalisha vitu ambavyo vinaweza kuwa hatarishi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo ningependa niseme kwamba nashukuru sana Mhe. Waziri, naunga mkono hotuba hii ambayo imewasilishwa kwetu kwa asilimia mia moja na sina shaka kabisa Mhe. Waziri, anaweza kuifanya kazi hii na mwisho wa siku tunaweza kukuta matokeo mengine, anaanza na nadhani ataendelea vizuri na atamaliza vizuri. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa sasa zamu ya Mhe. Zaina Abdalla Salum, kwanza kabla hajaendelea naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa.Nimeletewa ujumbe hapa kwamba mnapokuwa mnachangia na kutaja watu wenye ulemavu msiwataje kama walemavu, kwa sababu ni kosa kwa mujibu wa *terminology* yenyewe. Wenyewe wanataka waitwe 'watu wenye ulemavu' baada ya kuitwa 'walemavu', utu kwanza ulemavu baadae. Hii nimeletewa na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis ambaye ni Mwakilishi wa Viti Maalum kundi la watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Kwa vile hayupo Waheshimiwa Wajumbe, mchangiaji huyo sasa anakuwa ni wa mwisho, lakini hivi sasa nitaanza kuwapa baadhi ya Mawaziri, kwa sasa hivi nitawapa wawili halafu jioni nitawapa wengine. Lakini labda niwataje kabisa ili wajifahamu. Nitamuanza Mhe. Juma Ali Khatib, Waziri asiyekuwa na wizara ambaye atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Kilimo na baadae atafuatiwa na Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said, halafu baadae atakuja Mwanasheria Mkuu kabla ya kumpa Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii yenye hoja ili waweze kuzihitimisha.

Kwa hiyo, kwa sababu muda tunao wa watu wawili naomba sasa nimwite Mhe. Juma Ali Khatib, ili aweze kutoa mchango wake.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Juma Ali Khatib): Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi

hii. Lakini vile vile nataka kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri, ukiangalia historia yake huyu ni kiongozi katika wizara zote yeye akiwa kama waziri amefanya vizuri sana. Na nayasema haya kwa sababu kuna baadhi ya Wawakilishi wenzetu wamekuwa wakitoa malalamiko kwake au pengine fikra au ushauri. Lakini nataka kuwakumbusha huyu kwanza ni Waziri mpya katika wizara hii na tukumbuke kwamba wizara hii katika Serikali ya Awamu ya Sita iliyopita ikiongozwa na Chama chengine ambacho kwa sasa hakimo katika serikali hii. (*Makofi*)

Kwa hivyo, yale baadhi ya mapungufu ambayo leo tunayaona Waheshimiwa Wawakilishi, labda ni kwa namna mmoja au nyengine ni kutokana na kwamba huyo waziri aliyekuwepo hakutekeleza wajibu wake. Kwa hiyo, sasa ni juu yetu sisi Waheshimiwa Wawakilishi, tumpe mashirikiano Mhe. Waziri, kwa yale ambayo tunayaona, tuna uwezo wa kwenda kuzungumza nae wizarani kama waziri au kumfata moja kwa moja.

Lakini nataka kusema kwamba hata mimi nayaona haya lakini sasa tusilaumu tunatakiwa tujenge. Kwa mfano wale Waheshimiwa Wawakilishi walomsifia Mdhibiti Mkuu wa Serikali hii ndio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hili ndilo lengo la serikali la kuwataka watendaji wawe mfano kama Mdhibiti Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Namshukuru Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wa wizara hii bi Asha na wasaidizi wake wote wanafanya kazi kubwa na nzuri, na vile vile tukumbuke kwamba wizara hii imeunganishwa na imekuwa kubwa zaidi. Sasa nataka kusema kuna baadhi ya wengine walizungumzia kuhusu mahakimu kwamba stahiki zao au majaji haziko sawa.

Mimi nataka kuwaambia ndugu zangu serikali inajitahidi pale inapokuwa na nafasi basi wafanyakazi wanakuwa wanapewa stahiki kubwa zaidi na kuongeza mishahara. Tunashuhudia juzi tu Dkt. Ali Moh'd Shein katika kampeni zake za urais aliahidi kuongeza mshahara asilimia mia moja. Wakati ukiangalia katika nchi kadhaa hakuna katika nchi kuongeza mshahara asilimia mia moja. Lakini kutokana na mapenzi makubwa ya serikali yetu kwa wananchi na wafanyakazi wa serikali.

Kwa hiyo, mimi kitu ninachotaka kusema ni kwamba, sasa hivi tunatakiwa sisi Waheshimiwa Wawakilishi kwanza tujijue na tujitambie na hasa ukiangalia

kwamba serikali hii inaongozwa na kiongozi mwenye kujali Utawala Bora na Demokrasia. (*Makofi*)

Mimi nasema kwamba ni kiongozi mwenye kujali Demokrasia kwa sababu ni Chama cha Mapinduzi ndicho kilichoshinda kwa asilimia 91% katika uchaguzi uliopita. Lakini kwa hekima na burasa ya Dkt. Ali Moh'd Shein ameona kwamba serikali yake ashirikishe, humu ndani tuko Vyama vitatu. Sasa ukiangalia serikali hii inaongozwa na vyama vinne lakini kuna na Vyama viwili viko kwenye Tume ya Uchaguzi.

Kwa hivyo, ukiangalia utakutia vyama sita, kimoja ni Chama Tawala cha CCM na vyama vitano tunatoka kwenye vyama vya Upinzani kuna Chama cha *ADA Tadea* ndio mimi hapa, kuna chama *ASP* Mhe. Said Soud, kuna chama cha *ADC* Mhe. Hamad Rashid. Kwenye Tume ya Uchaguzi kuna Chama cha *CUF*, Tume ya Uchaguzi hiyo hiyo kuna chama cha *SAU*, Sauti ya Umma. Sasa hii ndio Demokrasia kubwa waliotuonesha ndugu zetu wa CCM pamoja na Mhe. Dkt. Ali Moh'd Shein. (*Makofi*)

Mhe. Spika, walikuwa na uwezo CCM na Rais Dkt. Ali Moh'd Shein kuunda serikali hii peke yao. Wala isingelikuwa kavunja Katiba au Sheria au Kanuni. Lakini kutokana na kwamba Utawala Bora pamoja na kuonesha uzalendo na Demokrasia ndio maana ameamua sasa kuvishirikisha vyama vengine. (*Makofi*)

Sasa mimi kitu ninachotaka kusema Mhe. Spika, ni kwamba uchumi wetu wa Zanzibar pale unapokuwa basi serikali kwa namna mmoja au nyengine inawahudumia wale wananchi na wale wafanyakazi na serikali ipo kwa ajili ya wananchi wote wa Unguja na Pemba. Kwa mfano tuangalie Mhe. Spika, ni juzi tu hapa alipotokezea mafuriko serikali ilichukuwa hatua za haraka zaidi za kwenda kuwahamisha wale watu na kuwaweka maeneo ambayo ni mazuri na kuwapatia chakula na malazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hata inalipotokezea ajali ya meli kuzama ni serikali ambapo ilichukuwa hatua za haraka kwenda kutoa misaada ya hali na mali kwa wale wahanga. Kwa hivyo, nawakumbusha Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, serikali yetu inafanyakazi kwa pale inapojipata. Hata katika familia sisi mababa kwenye nyumba yako unatamani uwe na vitu vizuri lakini kutokana na hali ya uwezo unakwenda kwa wakati na ule uwezo uliokuwa nayo kwa wakati ule.

Tutizame leo kuna msemaji mmoja alisema jana kaona *Star TV*, mimi nimeona kwenye *CNN* na *BBC* wakieka kipindi maalum cha kujadili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya jambo jema la kutoa posho kwa wale

wazee wastaafu. Kuna nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea mpango huu haupo. (*Makofi*)

Sasa wale wanaosema kwamba kima ni kidogo lakini serikali hii imeanza. Kuna serikali nyengine wana vima vikubwa na mapato yao ni makubwa lakini hawana mpango huu Mhe. Spika. Kwa hivyo, nataka kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi, tuipitishe bajeti hii ili Mhe. Waziri, apatiwe mafungu aende akafanye kazi. Naamini kutokana na uwezo wa Mhe. Waziri na wafanyakazi wenzake wanaomsaidia tukipitisha bajeti hii, basi hata hayo malalamiko tunayoyatoa atayatekeleza kwa sababu hana historia ya kuboronga wala kufanya vibaya akiwa kama waziri. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawaomba kwa unyenyekevu mkubwa tushirikiane sote kwa pamoja Wawakilishi tuipitishe bajeti hii ili malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yaweze kutimia. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Samahani Mhe. Waziri wa Kilimo kabla sijakupa Mhe. Zaina Salum Abdalla, kumbe alikuwepo. Lakini ni mwenzetu ambaye ana tatizo hilo la kutokusikia vizuri.

Kwa hivyo, sasa hivi naomba kwa heshima nimpe ili na yeye aweze kutoa mchango wake. Mhe. Zaina Abdalla Salum, karibu. (*Makofi*)

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi kuweza kuchangia machache katika hii hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye aliyetuwezesha kufika hapa sote tukiwa wazima na salama.

Pili, napenda kukupongeza sana wewe Mhe. Spika, kwa kutuendeshea Baraza letu hii la Tisa na vikao vyetu vyote ambavyo ulivyokuwa unatuendeshea. Mwenyezi Mungu akujaalie akupe uwezo mkubwa ili tuweze kuendesha mikutano yetu katika Baraza letu hili la tisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa haraka haraka kutokana na muda kama unavyojua jina langu *alphabet* ya mwisho, kwa hiyo, na mimi nitakuwa wa mwisho. Lakini wa mwisho aghlabu huwa ni wa mwazo.

Mhe. Spika, mimi mchangu wangu utakuja kwa upande wa watu wenye ulemavu hasa katika sheria ambayo ya ushahidi ambayo uliokwisha kupitiwa.

Lakini sheria hii mimi naomba watu wenye ulemavu watizamwe kwa ukaribu sana kwa sababu tu kutokana na ulemavu na vigezo na viwango; kuna wengine wanaweza kujieleza wengine hawawezi kujieleza.

Mhe. Spika, kuna changamoto nyengine ambazo zinzowapata watu wenye ulemavu hasa pale wanapokwenda katika vituo vya polisi. Wanasheria hawa huwa wanapokwenda kuripoti kutoa matatizo basi huwa wanawatolewa maneno ambayo ya kuwavunja moyo watu hawa au wazazi hawa wenye watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, changamoto nyengine ambayo inayowakabili watu wenye ulemavu ni umasikini mkubwa waliokuwa nao pale ambapo wanapotakiwa kufuatilia kesi zao inakuwa *file* liko polisi, basi anakwambia kuwa tunasuburi kipimo kutoka kwa daktari. Inakuwa mlemavu yule ni masikini au familia yake ni masikini, kwa hiyo, wanashindwa kulipia gharama zile na kesi ile huishia hapo hapo.

Mhe. Spika, hasa kwa sasa tukiangalia kesi nyingi ni za watoto na watu wenye ulemavu. Hii inasababishwa na upungufu uliokuwemo ndani ya sheria zetu. Kwa sababu mtuhumiwa anapofanya basi huona hata kama akishitakiwa hakuna hatia yoyote ambayo itapatikana kuona kwa vile yule aliekwenda kumshitaki hawezi kujieleza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, natoa ushauri kwamba wapewe taaluma wale wote wanasheria waweze kusimamia kazi zao vizuri na waweze kuwasaidia watu wenye ulemavu ili wawapatie haki zao. Kwa upande wa familia Mhe. Spika, naomba wanafamilia nao wasimalize kesi hizi ndani ya familia zao kwa kulipwa faini au kutolewa mahari kwani hili linaongeza sana katika vitendo kushindwa kutoa ushahidi au kushirikina na vyombo husika ili kupata kumaliza matatizo haya.

Wito natoa vyombo vya sheria au vyombo husika vichukuwe hatua kali kwa yeyote yule ambaye watakaemuona anamaliza kesi kwa kinyume na sheria ili iwe funzo kwa wengine wote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kumshukuru Mhe. Waziri kwa mpango wake mzuri na uwasilishaji wake mzuri kwa hotuba hii na mimi naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu.

Namshukuru sana Mhe. Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri sana waliotuletea na naamini kabisa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kwanza wataheshimu mambo mawili wazungu wanasema *"old is gold"* heshima ya Mwalimu Haroun Ali Suleiman ni kubwa sana. Mimi naamini kabisa tutaheshimu hiyo na kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa wanafunzi wengi waliomo humu ndani na waliko nje, mimi naamini kabisa tutaipitisha bajeti yake bila ya matatizo yoyote. (*Makofi*)

Lakini la pili Mhe. Spika, ilikuwepo dhana kwamba labda Mhe. Rais Ali Moh'd Shein aliekuwa hapendi kushirikiana na watu hawapi watu misaada. Mimi nimejifunza wakati nilipoingia kwenye Baraza la Mapinduzi na hasa kwenye Baraza la Mawaziri kwamba kama kuna Rais anatoa ushirikiano wa hali ya juu sana katika kuhakikisha kila aliyempa dhamana anatekeleza dhamana yake ni Rais Ali Moh'd Shein. (*Makofi*)

La pili ambalo amelifanya na analifanya ni utu aliojaaliwa nao katika maisha yake ana utu ndani yake. Ukifanya kazi na kiongozi ambaye ana utu unauona ule utu, kazi yako ni wajibu wako wewe kutekeleza. Sasa kuna baadhi ya watu wana-*take advantage* ya yule mtu wake. Ule utu wake unamfanya kama ana *weakness* fulani, lakini ndiyo utu. Kumbe ni wewe ambaye hutimizi wajibu wako ndiyo usiwe mtu, yeye ndiye mtu. Sasa hilo ndiyo tatizo ambalo ninaliona lipo na mimi ningeomba tushirikiane naye kumpatia kila msaada ili tuweze kutimiza wajibu wetu kikamilifu.(*Makofi*)

Sasa kwa kufuatilia hilo Mhe. Spika, ningeomba niseme tu kwamba tumejitahidi sana kuomba kwamba sheria zitungwe, zipitishwe. Lakini kutungwa na kupitisha sheria ni jambo moja. Kazi kubwa ni kusimamia sheria yenyewe utekelezaji wake. Ilikuwa asubuhi Mwakilishi alinipa niangalie *website* ya Serikali ya Mauritius. Mauritius ni katika nchi tano *top* zenye utawala bora, zenye rushwa ya chini kabisa, zenye *crime rate* ya chini kabisa. (*Makofi*)

Hawa hawatokani na serikali, wanatokana na wananchi wenyewe kuheshimu sheria. Sasa kama hatuheshimu sheria, hata sheria ngapi tukipitisha kwenye Baraza hili, kama sisi, kama *individuals* hatuheshimu sheria bado tutakuwa tatizo la kutekeleza sheria zenyewe. Kwa hivyo, la kwanza kabisa *crime*. Tulisema sisi tulijitahidi sana kuheshimu misingi ya sheria. Tukiwa wenyewe hatuvunji sheria, ndiyo hawa Mahakama hatutopiga kelele, jela hakutojaa watu, askari hawatokuwa hawana kazi. Ukenda hapo Mauritius na nchi nyingi ambazo zinaheshimu, kazi yao kubwa kabisa ni kuangalia wachache sana ambao wanavunja sheria. (*Makofi*)

Na rekodi ya Zanzibar hii hapa. Mimi ninakumbuka mwaka 1982 nipo Wizara ya Mambo ya Ndani, tulikuwa na askari mia nne tu hapa Zanzibar. Hakukuwa na *crime* kabisa. Nenda *archieve* ukajue *crime rate* ya Zanzibar ilikuwa chini kabisa. Leo *crime rate* imepanda juu kabisa. Kwa hivyo, unaweza kulaumu taasisi hazifanyi kazi lakini na sisi wenyewe je, tunasimamia tunaziheshimu sheria. Hatuheshimu Sheria ya Mwenyezi Mungu. Hata hizi wenyewe tulizojitungia sisi wenyewe. Sasa hilo ninasema ni jambo moja ambalo kama viongozi ni vizuri tukalielewa. Kama sisi wenyewe tunahitaji kuona hilo.(*Makofi*)

Lakini la tatu, Mhe. Spika, kuna Mwakilishi mmoja Mhe. Zulfa Mmaka Omar, alizungumzia sana la kupitishwa sheria kwa ajili ya kudhibiti uvunaji wa madafu. Mhe. Spika, nchi yetu inasikitisha sana. Mwaka 1996 Zanzibar tulikuwa na minazi milioni tano na laki tatu. Sensa ya mwaka 1912 tuna minazi milioni mbili na laki tatu. Milioni tatu na laki moja imekatwa minazi. Kwa hivyo, hata tukipitisha sheria ya kukata madafu, yaani ya kutaka madafu yasitolewe bado ukataji wa minazi ni mkubwa sana. Minazi haipo. Unguja peke yake minazi milioni moja na laki tatu imeshakatwa. Hiyo hatuwezi kuendelea katika maisha. Ninasema kule kule katika kuheshimu sheria na sheria ilipopitishwa kwamba misumeno ile tunayoita *sea sow* ni haramu. Nenda kaangalie huko Newburg.

Kwa hivyo, sisi wenyewe hatutii sheria na tutapiga kelele kila siku, lakini lazima tutii sheria. Misumeno ile ya *sea sow* inakata minazi, inakata kila mti. Leo Zanzibar hii tuko katika hatari kubwa sana. Ningeomba sana suala la kutii sheria, sheria tunazozipitisha lakini hatuzitii sheria zenyewe, tutaendelea kulaumiana kila wakati. Kwa hivyo, ninakubaliana na Mheshimiwa kwamba ni vizuri tukapitisha ya kuzuia madafu, lakini sheria kubwa kwanza ni kudhibiti ule mti wenyewe usikatwe. Miti ikatwe na minazi haipo.

Nimekwenda kuonana na yule mwenye kiwanda cha kutengeneza fanicha za minazi. Akasema sheria inasema; 'minazi angalau imeshapita miaka thamanini na kuendelea ndiyo ukatwe'. Lakini nenda kaangalie minazi inayokatwa leo na yeye ndiyo mnunuzi mkubwa. Anasema michanga ya miaka kumi na tano, ishirini minazi imekatwa. Kwa hivyo, tuna tatizo kubwa sana la msingi kabisa.

Leo kama Waheshimiwa Wawakilishi munataka muelewe mnazi katika *product* ambayo duniani ina bei kubwa ni mafuta ya nazi. Na pembejeo zote zinazotokana na nazi. Kenya wameanzisha kiwanda kikubwa sana cha ku-*process* nazi. Kina-*play* kubwa sana. Leo Zanzibar hapa hatuna minazi hata

kidogo. Kesho Ramadhani inaingia hali tutaiona. Hivyo, suala la kuheshimu sheria ni jambo moja la msingi sana.

La pili, Mhe. Spika, ambalo lilizungumzwa vile vile ni suala la *deep sea* na Waziri hapa katakiwa aeleze juu ya Sheria ya Muungano ikoje. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya Baraza la Wawakilishi mpaka leo haijaridhia Sheria ya *deep sea fishing*. Bahati nzuri Mwanasheria Mkuu ninamshukuru sana alitukumbusha juzi kwamba tuzipitie sheria zote zinazosimamia ili tuone namna gani zinaweza kutekelezwa.

Naomba sana, hili tushalifanyia kazi wizarani ametuletea wataalam wapo wawili wazuri wanafanya kazi nzuri sana, tunashukuru sana na waendelee kufanya kazi na tunakuletea *draft* yetu ili kuonana sasa na Mwanasheria Mkuu wa Bara. Kwa sababu hili ni la Sheria ya Muungano, tumefanye *amendments*.

Moja katika maeneo mawili muhimu sana. La kwanza, sheria yetu haishirikishi wazalendo kushiriki katika *sea side*. Unamuachia mgeni anavuna anaondoka. Hilo la kwanza ambalo limo ndani ya sheria.

La pili, haiwalazimishi wenye vyombo kuja kwenye gati zetu kuwekeza halafu tukapata faida ya kuingia watu wetu kuajiriwa, kupata samaki wenyewe na kuuza mafuta na bidhaa nyengine. Hizi ni kasoro ambazo baadhi yake tumeziona, tutaomba azirekebishe ili ziweze kuzisimamia vizuri. Lakini hata sheria zetu za uvuvi ziliopo hapa, tumezipitia tumeona kuna mapungufu makubwa sana. Kuna watu huko wanakusanya pesa hawakuajiriwa na serikali, hakuna risiti lakini wanakusanya mazao ya baharini. Hizi ni sheria tutaziangalia na ninakuhakikishieni Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutajitahidi sana kwa upande wa serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili mambo haya yaende haraka. (*Makofi*)

Mhe. Spika, la tatu, ni suala zima umoja wetu. Tunatikiswa sana. Wapo watu waliamini kwamba Firauni ni Mwenyezi Mungu na Hamana alikuwa ndiyo mshawishi mkubwa sana wa kusema Firauni ni Mwenyezi Mungu. Lakini Firauni mwenyewe alijua kama yeye si Mwenyezi Mungu na Hamana mshawishi alijua kwamba Firauni si Mwenyezi Mungu. Na kuna baadhi ya watu waliokuwa pamoja na Firauni na Hamana walijua kama Firauni si Mwenyezi Mungu. Ndiyo Mwenyezi Mungu akafika pahala akamuangamiza kwa sababu alikuwa mpaka Bilisi alimwambia wewe ulifika mbali, mimi sijafika kusema mimi ni Mungu, wewe umefika kusema huko, utapata adabu yako, alipata adabu yake.

Naomba wenzangu watuamini, uchaguzi tumemaliza usalama usalimini. Tunahitaji kusimamia maendeleo yetu sasa hivi, tumejipanga katika serikali kusimamia maendeleo. Mhe. Spika, asubuhi hii nimekwenda kukagua sehemu ya soko la samaki. Wajapani wanakuja kesho asubuhi tunazungumza mazungumzo na tunaanza kujenga.(*Makofi*)

Ondokeni hapa tulipo tuzungumzieni maendeleo. Nchi yetu itabaki maskini kwa sababu siasa tumeziweka mbele, tumeacha Dini, tumeacha kila kitu, tunashughulikia siasa. Mhe. Spika, juzi tumekwenda Pemba na Rais. Ukiona mpunga, mtu kenda kaukata kama hana habari, kama majani hivi unakata. Mpunga una miezi sita keshokutwa anavuna, umekatwa mpunga. Halafu huyo anasema ni Muislamu, anakwenda Msikitini. Msikitini gani unaokwenda, unamuabudu nani. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ninasema hata hizi *ethics* za Kidini hatuna, tumefika hapo. Halafu unazungumzia nchi ipate maendeleo. Maendeleo yatapatikana wapi. Kwa hivyo, naomba sana kabisa, naomba ndugu zangu wa Zanzibar tutaendelea na umaskini kama tumefanya siasa ndiyo Dini, tutaendelea na umaskini kama tumeifanya siasa ndiyo ajira, tutaendelea na umaskini kama tumeifanya siasa ndiyo Mungu. Ndipo tumefika hapo. Unamuachaje maiti nje humsalii. Tumekwenda pale maskini za Mungu tumemuona mama amekatia migomba yake, amekatiwa kila kitu chote. Tunaanza upya kumsaidia. Hata visiki vya muhogo havijaota unakwenda kuving'oa, lakini nikamwambia kina dhambi gani kisiki cha muhogo. Ninasema ubinadamu umetoka kabisa. (*Makofi*)

Sasa mimi ninasema ni vizuri na ninamkumbuka Mwanasheria Mkuu hebu tukazae hiyo sheria. Leo *law enforcement reshuffle* sasa ifanyike. Huwezi kuendesha nchi kama hakuna *law enforcement*, Hamad kakosa apelekwe Mahakamani, ashitakiwe na watu wanaoshtaki wanaonekana. Hilo la kwanza.(*Makofi*)

Lakini la pili, lazima na vile vyombo vinavyosimamia sheria na wao wawe safi. Tunakwenda tunakuta watu ati wana-*negotiate* ma-*files*. Una-*negotiate* vipi na *criminal*. Tumekuta ati tumezungumza naye, amekuja hapa ame-*organize* watu, hujamkamata kwa nini na ushahidi unao? Huwezi kuendesha nchi namna hiyo. Ninasema lazima nchi iende kwa *principles*, anayetaka aendelee hataki aondoke. *That can not run the government this way.* Ninasema lazima anayebaki kwenye serikali atimize wajibu wake, aliyekuwepo nje abaki nje tuendeshe serikali. Watu wanataka maendeleo. (*Makofi*)

Tumeshazungumza na *donors* chungu nzima wanataka kutusaidia. Kwa nini watu wanakwenda Mauritius kwa sababu kuna *peace and stability*. Sasa kuna watu wanatuchokozachokoza hapa katikati na sisi tuwaachie macho. Mimi naomba sana suala la *law enforcement* tusi-*compromise* hata kidogo. Anayetaka aheshimu sheria, aliyekuwa hataki atafute pahala akae aingie nyumbani mwake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hamad Rashid Mohamed ambaye ni Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Waheshimiwa Wajumbe, muda tulionao haumtoshi Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) kwa ajili ya mchango wake. Hata yeye tungependa tumsikie lakini naona tutafanya hivyo atakuwa ni mtu wa mwanzo jioni tutakaporudi kuchangia. Na baada ya mchango wako tutamsikiliza Mhe. Mwanasheria Mkuu, kabla sijamkaribisha Naibu Waziri kwa ajili ya kuanza mchango wake kwa ajili ya *winding up* ya wizara yake.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba pia nitoe tangazo moja. Mulipewa barua kujuulishwa kuhusiana na semina ile ambayo iliyokuwa imeahirishwa. Ilikuwa ifanyike Jumamosi kwenye barua zenu mumeandikiwa kwamba itafanyika Jumamosi ijayo tarehe 04 Juni. Kwa bahati mbaya tulisahau kuwajuulisha Wajumbe kuthibitisha ushiriki wao katika semina. Kwa hivyo, munaombwa kuthibitisha ushiriki wenu katika Ofisi ya sekretari wa Katibu wa Baraza. Ahsanteni.

Baada ya hayo machache naomba kusitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 6:47 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyoondokea asubuhi, naomba sasa nimwite Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum), ili aweze kutoa mchango wake. Karibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii katika nyakazi hizi za jioni kwa ajili ya uchangia hoja ya Mhe. Haroun Ali, akiwa ni Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, awali ya yote ningependa nichukuwe nafasi hii kuwaambia Wazanzibari wenzangu pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba Zanzibar ilifanya Mapinduzi yake mwaka 1964, lakini Katiba ya kwanza ilitayarishwa mwaka 1984, kwa vile Zanzibar iliweza kukaa miaka 20 haina Katiba, lakini mwaka 1984 Zanzibar ilifanikiwa kupata Katiba. Kwa hivyo, anapotokea mtu akasema kwamba hatuna Katiba au hatuna sheria, arudi kwenye historia ya nchi hii. Katiba ipo, sheria zipo na ndizo zilizotufikisha hapa kuwa na chombo adhimu cha kutunga sheria kwa Zanzibar na Wazanzibari, sheria ambazo zinaifanya nchi yetu kuthaminiwa kitaifa na kimataifa, kutokana na kuendeleza utawala bora.

Mhe. Spika, inashangaza sana kuona kwamba watu wanasahau hata kilichofanyika jana, wanakisahau. Nataka ifahamike kwamba wizara hii ilikuwa na mtu ambaye kakaa humu ndani ya miaka mitano na ndani ya miaka mitano hiyo anasema hajapata serikali. Kwa vile yote hayo yanayodaiwa, maposho, marupurupu na ongezeko la mishahara lilikwamishwa na watu hawa, hakukuwa na sababu ya kuwa mishahara iongezeke na marupurupu yaongezeke wakati watu hawajapata serikali. Kwani nyinyi mlikuwa hamsikii wanasema kwamba hawajapata serikali wale. *(Makofi)*

Wale sio sisi. Mhe. Spika, sisi tumeshapata serikali. *AFP* imepata serikali, *TADEA* imepata serikali, *ADC* imepata serikali. Tunachofanya hapa ni kuhakikisha kwamba tunamsaidia Mhe. Rais kwa mujibu wa viapo vyetu, ili kuhakikisha kwamba anaiongoza nchi hii kwa miaka mitano kama vile ambavyo inatakiwa kikatiba. Ninachosema ni kwamba ni wakati wetu muafaka kama Wazanzibari kuangalia historia ambayo imepita juzi na sasa hapa tunapoelekea, ni wajibu wetu kuipitisha bajeti hii kwa misingi ya kumtaka Mhe. Waziri, ayatekeleze yale ambayo wenzetu walioyawekea pazia wakasema hawajapata serikali wao. Maana yale yalikuwa wazi yatekelezwe lakini wenzetu walisema hawajapata serikali, kwa hivyo, wakaendeleza utaratibu wa kuyaziba na kuzuwia haki za watu, maposho ya watu, ongezeko la mishahara na leo tunalaumiana wenyewe.*(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba utawala bora uliopo hivi sasa Zanzibar, ni utawala wa aina yake na tunalazimika kuhakikisha kwamba utawala huu unaendelea kuwepo. Sisi kama Mawaziri tunawahakikishia

wawakilishi pamoja na wananchi wote kwamba tutatumbua majipu kwa namna yoyote ile. Tutatumbua majipu kwa sababu tunatekeleza Sera ya Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi ndicho kinachotawala katika nchi hii na kila anachokifanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kutekeleza Sera ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa sisi kama tumekula kiapo kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Tunawahakikishia tutapasua majipu kwa *chain-saw*. Tunachokiomba ni kwamba kila mfanyakazi na kila mtu mwenye dhamana katika serikali hii, ahakikishe anafanyakazi yake kwa uhalisia wa mambo, vyenginevyo, mikasi tunatembea nayo, majipu tutayapasua hadharani na hatumuonei mtu huruma, hatutomuonea mtu haya, tumekubali kuisaidia Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kiapo na tutafanya hivyo usiku na mchana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Zanzibar ina historia kubwa sana, Baraza la Wawakilishi limeanza mwaka 1980 na limeanza na wajumbe 20 kutoka wilaya 10 za Zanzibar na nataka niseme hivyo, wajumbe wawili wawili walitoka kila wilaya Unguja na Pemba. Wajumbe wawili wawili walitoka kila mkoa Unguja na Pemba na baadae Rais akateuwa wajumbe wake anaowataka yeye. Nataka nikuthibitishie Mhe. Spika, mimi mwenyewe nilikua mgombea katika mwaka 1980.

Lakini kwa bahati utaratibu ule ulioanzia ulikuwa ni utaratibu wa kutoka kwenye Kamati za Mapinduzi za Wilaya na Kamati za Mapinduzi za Mkoa, ndio watu walikuwa wakitoa wajumbe wawili na hatimaye kupigiwa kura. Wajumbe wanne; wawili wanapatikana wanakuja kwenye Baraza, hivyo ndivyo Baraza lilivyoanza kwa wajumbe 20. Leo kuna wajumbe zaidi ya 80 hakuna utawala bora. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niwaambieni, mimi nilikuwa mgombea wa kwanza wilaya ya Chake Chake, mimi niligombea kwa mara ya kwanza linaundwa hili Baraza la Wawakilishi. Lakini angalia historia yangu mwaka 1980 mpaka nimeingia juzi katika Baraza la Wawakilishi. Ni uvumilivu wa kisiasa. Yaani wanasiasa wanasema *tolerance*, ni uvumilivu wa kisiasa ambao umejengeka nikiwa na imani kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iko siku itanipa nafasi ya kuwawakilisha Wazanzibari wenzangu.

Sasa hilo ukiwa umejengeka nalo na ukawa na imani na wenzako ambao wanaongoza basi utafika pahala pazuri. Tumekuwa na utaratibu wa kupokezana vijiti tokea tulipoanza Baraza la Wawakilishi mpaka tumefika leo. Sasa juzi juzi wenzetu wamekataa kupokezana vijiti wakaviangusha wakafikiria

hatutoviona tukavidaka. Tunawathibitishia kwamba tutatembea navyo vijiti hivi kwa miaka mitano hii, chini ya uongozi wa Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na msaidizi wake Mhe. Seif Ali Iddi na Spika wetu Mhe Zubeir Ali Maulid yule pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, huu ndio utaratibu wa demokrasia unavyokwenda dunia nzima. Sasa leo tusijisahau kwamba tulikuwa tumeinamiwa na jinamizi lililochukua miaka 20 katika Baraza hili, wakakorofisha mambo mbali mbali kwa malengo yao na hatimaye mpaka tumefika pahala leo tunajiuliza kwa nini mishahara imekimbiana kiasi hiki chote, kwa nini rushwa imetawala namna hii yote, kwa nini nchi imefikia hatua hii hakuna sheria, hakuna kanuni na kadhalika. Wenzetu waliokuwemo kwa miaka 20, angalieni kule Pemba wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi walikuwa wanatoka Pemba kwa miaka 20. Lakini la kusikitisha hakuna hata banda la mbuzi walilojenga, wakasema kuwa huu ni msaada tuliokuwa tunautoa kwa wananchi wa Pemba kwa muda wa miaka 20 tumekaa katika Baraza tunawajengea banda la mbuzi, hakuna. *(Makofi)*

Mhe. Spika, watu hao kila siku walikuwa wana *demote* serikali isipate nguvu kwa malengo ya kwamba wao iko siku watatawala. Mimi nasema hawatawali ng'oo. Hicho kitu kifahamike na kieleweke kwamba tutapokezana vijiti kwa utaratibu unaokubalika katika Katiba yetu na sheria zetu na kwa misingi hii tunayokwenda nayo ya kuwa sisi Wapinzani tumeshindwa kujipanga na kuheshimu Katiba ya nchi na taratibu za demokrasia, bado naendelea kusema CCM Zanzibar itaendelea kushinda tena kwa miaka 20 ijayo, hata kama mimi nimekufa mtanikumbuka.

Kwa sababu serikali haiwezi kupatikana kwa njia mbadala zaidi ya wananchi kwenda kupiga kura wakachagu kiongozi wanayemtaka, na utaratibu huo wenzetu hawautaki, utaratibu huo wenzetu wameupinga pamoja na sala zinazosaliwa, kuombwa dua ya Rais, Mwenyezi Mungu atuletee Rais, lakini sala hizo pia bado huwekwa nyuma baada ya yule Rais anayetakiwa hajapatikana. Ina maana Mwenyezi Mungu wamemfanya rafiki yao, wanalotaka wao ni lazima Mwenyezi Mungu awakubalie na hicho kitu hakuna bwana, hakuna hiyo. Analotaka Mwenyezi Mungu ndilo litakalokuwa na leo hii Mwenyezi Mungu ametaka demokrasia ya Zanzibar, serikali yake iongozwe na vyama vinne na tayari, serikali sasa hivi inaongozwa na vyama vinne chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa leo inakuwaje kuwa wenzetu ambao tayari tunaendesha gurudumu hili, halafu tunajua kwamba wenzetu waliochukua nafasi wamezuwia mambo yote kwa muda wote, wamekorofisha kila aina,

wamesababisha kila mitafaruku, vijana wengi wamekosa kusoma, watu wengi wamekosa ajira, uhasama wanauendeleza, matatizo wameyaingiza, wanasusia mpaka maiti. Halafu sisi tunakuja humu tunamwambia Maalim Haroun kwa nini wewe wizara yako hukulipa mishahara. Mwambieni Abubakar Khamis, sio mnamuambia Maalim Haroun, mtafuteni Abubakar Khamis mumwambie, yeye ndiye alikuwa miaka mitano yumo humu na hizo sheria zote za kulipa marupurupu yeye ndio zilikuwa zinamuhusu.

Nyinyi kama hamuwezi nileteeni mimi nitamwambia. Sio mnafika pahala leo mnawabana mawaziri wafanye mambo ambayo yalikwisha kwama. Yamekwama kwa sababu gani, yamekwamishwa na watu miaka mitano. Malengo yao, haja yao walikuwa wanataka wafute kabisa utaratibu wa hali zote za kidemokrasia hapa. Kwa sababu mtu akiwa dalali siku zote anafanyakazi ya bwana wake. Sasa mazingira yale chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi...*(Makofi)*

Mhe. Spika: Mheshimiwa, una dakika mbili.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said): Ahsante Mhe. Spika. Wameweza kufanikiwa hadharani, serikali hii imeletwa tena hadharani, ni kazi yetu kuilinda sote kwa kuwatumikia wananchi waliotutuma humu, sio kuja kukorofishana humu. Sisi tuwatumikie wananchi, miaka 20 wamekosa kutumikiwa wananchi wa Zanzibar. Watu wanawasubiri watu walete mabwana zao waje wawatumikie hapa, hicho hakikuwezekana. Tunasema CCM ndio chama pekee kwa sasa kilicho na dira ya kuongoza nchi hii, na sisi kama watu wenye vyama vya siasa tunapaswa kujifunza elimu ya CCM, CCM hawachukiani, CCM hawakerani, CCM ugomvi wao kama nyuki, wanafumuka mara moja wanaungana mara moja, ni tofauti na sisi tunapelekana Mahakamani kila siku, tunatafuta madaraka. Sijapata kusikia CCM wanapelekana Mahakamani na baada ya kushindwa sasa kupelekana Mahakamani wanaanza kuwapitia watu wagome. Atagoma mtu aliyekuwa mpumbavu mwenye akili hagomi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, yeyote mwenye akili nchi hii hatogoma, hata ukimuona mtu anagoma hana akili. Sasa jihesabu wewe unamgomea kaka yako, baba yako au jirani yako kwa mazingira gani, kwa mazingira ya kwamba CCM imeshinda ndio. CCM imeshinda ndio na wewe kama unataka kushinda jitayarishe uje ushinde mara nyengine. Lakini haimaanishi kwamba wewe umeshindwa leo umgomee mtu aliyeshinda. Nasema hivi, wawakilishi sote tuliomo humu tunawajibu wa kusimama na viapo vyetu kuilinda na kuitetea Katiba ya

Zanzibar kwa misingi ya kuifanya serikali iende zake moja kwa moja isisite pahali. Baada ya kumaliza hayo Mhe. Spika, naomba nikae ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Said Soud Said, najua nilikuwa nalazimika nikusimamishe, lakini hiyo shangwe ndio nilikuwa nashindwa niingie vipi hapo. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangie hoja hii ya makadirio ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na hasa baada ya mchango mzuri wa MBM Mhe. Said Soud Said. Nadhani ingekuwa vizuri tungemuita Mhe. Waziri tu akafanya majumuisho. Lakini kwa vile na sisi tuna dhamana ya kumsaidia basi wacha na sisi tuchukuwe fursa hii ya kumsaidia Mhe. Waziri katika baadhi ya zile hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe, wamezizungumza. *(Makofi)*

Kwanza kabisa naomba nichukuwe fursa ya kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. La pili, Mhe. Spika, kwa dhati kabisa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe na wao waipitishe hoja hii ya Mhe. Waziri, kwa asilimia zote mia moja. Wana kila sababu ya kupiga mabuti kwa sababu hiyo ndio kazi yenyewe. Lakini baada ya hayo basi wamuidhinishie haya mafungu Mhe. Waziri ili akaendeleze yale mazuri ambayo yameanzwa na Mhe. Rais. Kwa sababu kama tunavyojua tunajadili Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa mengi yamefanywa Mhe. Spika, na mwenye ofisi hii kwa kipindi cha miaka mitano au sita iliyopita.

Kwenye Utumishi wa Umma Mhe. Spika, Mhe. Rais amerudisha nidhamu kwenye utumishi wa umma. Sote tunajua utumishi wa umma huu ambao ulikuwepo kabla ya hapo ulikuwa uko *ICU*, lakini kwa kuja kwake yeye Mhe. Rais, amerudisha nidhamu. Nidhamu aliyoirudisha sio ile ya kijeshi tuliyoizowea ya mabavu. Amerudisha nidhamu kwa kuweka utaratibu wa kisheria. Katika sheria za mwanzo zilizotungwa na Baraza hili katika uongozi wa miaka mitano iliyopita ya Mhe. Rais ni kupitisha Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011, nayo ni Sheria ya Utumishi wa Umma, pamoja na mengi ambayo yamezungumzwa lakini kwa kiasi kikubwa Mhe. Spika, imeweka nidhamu, imeweka misingi ya utumishi wa umma, maadili ya utumishi wa umma na imeweka kanuni za utumishi wa umma ambazo sasa zinatakiwa kufuatwa kwa kila mtumishi wa umma.

Pia, Mhe Spika, kwenye Sekta ya Sheria, Mhe. Rais hakuwa nyuma, nayo pia amewainua wanasheria kwa kiasi kikubwa katika kipindi chake hiki cha miaka mitano kilichopita. Sekta ya Sheria ya leo sio Sekta ya Sheria ya miaka mitano

iliyopita, sisi tuliokuwa katika sekta hii kwa muda mrefu tunatambua hilo na kwa dhati kabisa tunamshukuru Mhe. Rais kwa kazi kubwa aliyofanya katika sekta hizi.

Lakini pia Mhe. Spika, kwenye utawala bora katika sheria ambazo zilikuwa zina ukakasi kupitishwa Mhe. Rais amezisimamia Sheria ya Maadili na Sheria ya Rushwa amezileta katika kipindi chake cha miaka mitano kilichopita, hayo yote kuonyesha jinsi gani Mhe. Rais yuko makini na imara katika kusimamia sekta ya utumishi wa umma, sekta ya sheria na pia sekta ya utawala bora.

Sasa kwa haya yote mazuri ambayo Mhe. Rais ameyafanya na mengi ambayo anakusudia kuyafanya katika kipindi chake hichi cha miaka mitano au minne na nusu iliyobaki, naamini kabisa Waheshimiwa wengi humu watakubaliana na hoja ya Mhe. Waziri ya kumpitishia Makadirio ya Ofisi yake kwa asilimia mia moja, kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, wafanye hilo.

Lakini la pili Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumsaidia Mhe. Waziri katika baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe, wamezisema. Sitokwenda kwenye hoja zote, lakini nitazungumza zile chache ambazo nitamsaidia Mhe. Waziri.

Moja, nikianza na Mhe. Nadir, ameuliza katika kipaumbele cha ajira na hasa hizi ajira zilizokuwa kwenye mahoteli na hizi sekta binafsi. Mimi nimkumbushe tu Mhe. Nadir, kama atambue tofauti ya utumishi wa umma na sekta binafsi, kinachozungumzwa hapa ni utumishi wa umma. Lakini sekta hii ambayo amezungumza nayo pia ni muhimu ina waziri wake ambaye nae anaisimamia, lakini kwenye sekta ya umma nimuhakikishie Mhe. Nadir, kwenye yale yote ambayo ameyazungumza yakupewa kipaumbele Wazanzibari akisoma Sheria ya Utumishi wa Umma, kifungu nadhani cha 59 ataona kwenye ajira ambazo zinatangazwa Zanzibar basi kipaumbele cha kwanza ni cha Wazanzibari, na sheria imeeleza hivyo wazi kabisa.

Haina maana kama wale wengine ambao si Wazanzibari hawaajiriwi, lakini hawaajiriwi kwenye mkataba ambao una mafao ya uzeeni. Kwa hiyo, Wazanzibari ndio wanaopewa kipaumbele cha kwanza cha kuajiriwa katika utumishi wa umma kwa mkataba wa kudumu ambao baada ya hapo akistaafu anastahiki kupewa mafao. Lakini wale wenzetu na ndugu zetu wa Tanzania Bara na wageni wengine wote ambao watataka kuajiriwa kwenye sekta ya umma, wao inabidi sasa waajiriwe kwa mkataba maalum. Kwa hiyo, hili nilitaka nimfahamishe vizuri ili atapokuja Mhe. Waziri, husika wa ajira awe tayari ameweza kupambanua baina ya sekta hizi mbili. Lakini aliyoyasema ni

ya msingi, sasa wakubaliane tu na Mhe. Waziri husika atapokuja jinsi ya kuisaidia na hiyo sekta binafsi.

Lakini pia amezungumzia masuala ya leseni na usajili wa bunduki nadhani. Mhe. Spika, eneo hili linasimamiwa na sheria ya Muungano, Sheria sura Nam. 223 inaitwa '*Aims and Ammunition Act'* ndio inayosimamia eneo hili. na ukiisoma sheria ile Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 5 imetoa mamlaka kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar kusimamia eneo la usajili kwa upande wa Zanzibar. Amepewa madaraka makubwa kabisa ya kusimamia eneo la usajili wa vyombo hivi kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, lakini pia na Waheshimiwa Wajumbe, tukumbuke kama hili ni eneo moja ambalo ni hatari, vyombo hivi nje viko vingi na hivi vyengine ndio ambavyo vinatumiwa na wahalifu katika kufanya uhalifu wake. Sasa ni vyema ikaratibiwa pahala pamoja sasa kama kuna tatizo ambalo Mhe. Nadir, analiona kwenye sheria hii basi ni vyema atueleze ni kifungu kipi ambacho anaona kina tabu ili na sisi tuweze kushirikiana na wenzetu ili tuweze kufanya hayo marekebisho, lakini kwa ilivyo sasa hivi sheria hii sura Nam. 223 ni Sheria ya Muungano lakini akisoma kifungu cha sita na cha tano ataona utaratibu mzima wa usajili ambao amekabidhiwa Kamishna wa Polisi kwa upande wa Zanzibar.

Lakini pili niende kwa Mhe. Suleiman Sarahan Said, yeye pamoja na mengi ambayo ameyazungumza lakini ameyazungumzia huu utaratibu ambao upo sasa hivi wa Majaji kukaa pale na kutumia muda mwingi kuandika, wanasikiliza lakini pia wana-*take note* kwa kile ambacho wanakisema, ni kweli na sisi ambao tunakwenda Mahakamani mara zote tunaambizana tizama peni ya jaji, ukiona jaji haandiki basi ujue unachokisema ni 'pumba' usipoteze muda wako, ukiona jaji yuko *busy* anaandika basi ujue kile unachokisema kina maana na jaji ana-*take note*. Sasa ni kweli, lakini mara nyengine na hawa majaji wanatumia muda mrefu kwanza katika kusikiliza, inabidi wasikilize na u-*analyze* halafu pia waandike halafu pia waje kuandika hukumu zenyewe.

Sasa ushauri ambao wameutoa ni ushauri sahihi kabisa, kama sasa ifike pahala Mahakama zetu sasa hivi tuondoke katika utaratibu huu tuliouzowea *Conventional way*, tuende sasa kwenye *Modern way of doing things*, yaani tuende kwenye utaratibu mpya wa kiteknolojia, kama ambavyo tumo humu Barazani, unazungumza kwenye *mic*, lakini unavyotaka *Hansard* unakwenda kuchukua tayari imeshapishwa, ndio utaratibu wenyewe wa kileo ulivyo. Sasa na hili nadhani kwa Mahakama nalo sio baya lakini nalo linakwenda na uwezo, linakwenda na bajeti, linakwenda na nyezo nyingi ambazo inabidi zishughulikiwe. Kwa hivyo, hili ni wazo zuri ambalo amelieleza.

Lakini pia amezungumzia kuhusiana na kuwatunza wajane, nimhakikishie kuwa kuna Sheria Nam. 4 ya mwaka 1985 inaitwa 'Sheria ya Wari na Wajane', akiisoma sheria ile vizuri ataona utaratibu mzuri ulioelezwa kule kwa watu hawa wawili kuweza kudai matunzo, kwa yule ambaye anastahiki kuwalipa matunzo. Sasa sheria ipo, *of course*, ni ya zamani tokea mwaka 1985 inawezekana mambo yame-*advanced*, inawezekana inabidi tuitizame upya mambo mengi yamebadilika, sasa kimsingi sheria ipo, aitizame tu Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwenye yale maeneo anayoona tume-*improve* basi sisi tuko tayari kushirikiana nae katika ku-*improve* sheria hiyo.

Jengine ambalo amelizungunza naye Mhe. Suleiman Sarahan Said na wajumbe wengi ni muda wa kustaafu umezungumzwa kwa mapana kabisa na Waheshimiwa Wajumbe, hasa zaidi kile kipindi cha mkataba wa nyongeza au kwa Kiingereza kinaitwa '*Extended Service'*. Mhe. Spika, muda wa kustaafu Serikalini kwa utumishi wa umma bado umebaki ni miaka sitini kwa lazima na miaka 55 kwa hiyari huo ndio muda wa kisheria ambao upo, lakini sheria hii ambayo tumeipitisha hapa Nam. 2 ya mwaka 2011 imetoa fursa kwa muajiri pale ambapo anaona mtumishi wa umma amefika umri wa kustaafu, kumuomba, maana wala haombi muajiri mwenyewe ila anaombwa na Ofisi yake kuendelea kwa miaka mingine miwili ya kuitumikia Ofisi aliyokuwepo.

Lakini kiujumla napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe, kama wakitizama tungekuwa tuna-*narrate* wale ambao wanatoka na wale ambao wanabaki basi wanaotoka ni wengi zaidi kuliko wanaobaki. Kwanza ukibaki na haki zako nyengine zote zinakuwa *free*, kama ulistahiki kwenda kuchukua pencheni yako *ZSSF*, pencheni hiyo huichukui. Sasa wengi wenye akili zao timamu wanaona aa, maisha yenyewe haya mafupi, keshastaafu miaka sitini, anachukua chake na anakwenda zake kuhiji au anakwenda kuoa mke mwengine. Lakini utaratibu wa kisheria uko hivyo, Mhe. Spika, kama huu ni utaratibu ambao tumeupitisha na si wengi ambao wanachukua *extended service* kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wengi wanadhani.

Lakini niende kwa Mhe. Simai, nae kwanza amezungumzia sare za watumishi wa umma, nimwambie tu hakuna sare maalum ya utumishi wa umma, hakuna toleo lililotoka kama watumishi wa umma sasa wote wawe wanavaa sare fulani, lakini nimuhakikishie Mhe. Simai, akisoma Kanuni ya Utumishi wa Umma, kifungu cha 34, kuna utaratibu mzima umeelezwa wa kivazi ambacho mtumishi wa umma anatakiwa avae. Na kama itatokea idara yake ambayo anaitumikia ina haja ya kuvaa sare maalum, basi sare hizo zitakuwa ni gharama za Serikali.

Kwa hivyo, utaratibu wa kisheri upo tu ni mzuri, ni kuhimizana tu kwenye taasisi zetu hizi nyingi kama Mahakama, Wanasheria hawa wanavaa makoti na mashati meupe, basi inatolewa ndani ya mfuko wa Serikali, lakini hakuna vazi maalum ambalo limewekwa kwa ajili ya watumishi wote wa umma. Lakini kama kuna Ofisi moja inahitaji hivyo basi ni wao kuamua ni sare gani ambayo wanahitaji na sare hiyo itaingia kwenye mafungu ya Serikali na italipiwa kwa wafanyakazi wote.

Lakini amezungumzia Mahakama ya Biashara, najua yeye anaelewa fika kama Mahakama hii imeanzishwa kutokana namaamuzi ambayo yametokea kwenye Baraza la Biashara la Zanzibar linaitwa *Zanzibar Business Council*, wafanyabiashara wengi walikuwa wakizungumza utaratibu huu mzima wa kesi hizi hasa za kibiashara kwenda kwenye msururu huu wa kesi za kawaida za Mahakama, mara nyingi zinakuwa zinachelewa na mara nyingi hawa wafanyabiashara wanataka *Quick and Fast Decision*, sasa wengi wa wafanyabiashara waka-*propose* kama tuanzishe Mahakama hii ya Biashara. Mhe. Spika, Mahakama hii kama ambavyo anavyojua Mhe. Simai, imeanzishwa kisheria kwa Sheria Nam. 9 ya mwaka 2013 na taratibu nyingi tayari zimeshaanza, sina hakika na sijui kwa nini haikuanza kufanya kazi.

Lakini nadhani katika kikao cha mwisho tulichukua Ikulu Mhe. Rais yeye mwenyewe aliagiza kwamba kwa nini mpaka leo Mahakama hii bado haikuanza kazi, lakini *of course*, sio kesi zote zinazopelekwa, kuna kesi ambazo zina viwango maalum ambazo zinatakiwa kupelekwa huko, lakini utaratibu mzima ule wa kusikiliza uwe tofauti na ule ambao tumeuzoweya kwenye Mahakama zetu hizi ambazo tunakwenda. Sasa nimuhakikishie tu tutashirikiana na Mahakama kuangalia nini kikwazo ambacho kinakwamisha Mahakama hii ya Biashara isi-*take off three years* baada ya sheria hii kupitishwa na Baraza na Mheshimiwa Rais kuitia saini.

Lakini jengine ambalo amelizungumza ni suala la ulinzi viongozi nadhani hili nitawaachia Mhe. Waziri na Naibu Waziri, hili wala sio jambo kubwa, hili ni jambo la kawaida na ambalo linajulikana kwa viongozi wakuu wote wanastahiki zao za kupewa ulinzi, Mhe. Spika, anastahiki kupewa ulinzi, Mhe. Jaji Mkuu ana stahiki ya kupewa ulinzi na viongizi wakuu hawa wa kitaifa Mhe. Rais mwenyewe na Mhe. Makamu wa Rais, wote hawa wanastahiki, Majaji, Mawaziri, sasa ni jambo tu hili unajua sisi wengine huku ukiambiwa ufuatane na mtu kila wakati inakuwa tabu kidogo, lakini ndio utaratibu ulivyo. Ukishakuwa umefika kwenye nafasi maalum basi ndio nafasi hiyo inakuja na mambo yake na yale mengine ambayo tumezoea inabidi pia tuache, maana

hawa wanakufuata kila pahala, lakini ni utaratibu upo nadhani Mhe. Jaji Mkuu, mwenyewe hana tatizo na hili.

Lakini kubwa ambalo amelizungumza ni kwenye Mahakama ya Rufaa, wamezunguma kama Mahakama ya Rufaa mpaka sasa kuna Mzanzibari mmoja kwenye *list* ya majaji wengi wa rufaa ambao wapo, ni kweli alilosema ni sahihi mpaka sasa hivi kuna Mzanzibari mmoja Mhe. Mbarouk ambaye ndie ana-*sound* katika Mahakama ya Rufaa. Lakini nimwambie kama akisoma Katiba, Ibara ya 118, hakuna mgao ambao umewekwa wa kwamba nafasi fulani ziende Zanzibar na nafasi fulani ziende Tanzania Bara, lakini pia Katiba hiyo hiyo imeweka sifa kama ili uende uka-*serve* kwenye Mahakama ya Rufaa basi uwe ume-*serve* angalau kwa miaka isiyopungua15.

Sasa sekta yetu hii ya sheria pamoja na kwamba ipo muda mrefu lakini sasa hivi ndio imeanza kuchuchuka vizuri, ukitizama wale ambao wana-*serve* Mahakamani ukiwacha Jaji Mkuu mwenyewe, wengi ambao wana-*serve* miaka 12, 13 na wengi ambao tuko kwenye hizi sekta za sheria muda ni huo. Sasa alilosema ni kweli lakini najua hivi karibuni walileta barua na kuomba sasa Zanzibar iteue na ipeleke *list* ya majina ili wapate fursa na wao kuteuliwa kwenye Mahakama ya Rufaa.

Sasa naamini hili wenzetu wa Mahakama wanalifanyia kazi, lakini hakuna mgao ambao umewekwa, ukasema kwenye Mahakama ya Rufaa kuna nafasi 20 basi 10 zitoke Zanzibar, hakuna mgao ambao umewekwa kisheria, ni maamuzi ambayo mwenyewe mteule anafanya lakini kwa kutimiza sifa ambazo zimewekwa, sasa hili ametukumbusha vizuri na sisi tutalifuatilia kuhakikisha angalau tunazidisha watu wawili watatu.

Lakini pia Dkt. Mwinyihaji, amezungumzia kwa mapana kabisa ucheleweshaji wa kesi na wajumbe wengi wamelizungumzia hili ucheleweshaji wa kesi, wanasema; '*Justice delayed is justice denied*' yaani 'haki inayochelewa ni haki iliyonyimwa', hiyo ndio lugha ambayo tunaitumia muda mrefu. Mhe. Spika, ucheleweshaji wa kesi una mambo mengi na hasa hizi kesi ambazo zinaanzia Mahakama ya Mikoa na Mahakama Kuu, *of course*, huku sasa ndio wanaanza kuingia Mawakili, tofauti na hizi Mahakama za chini ambazo Mawakili hawaingii, lakini unapoanza kujumuisha sasa Mawakili ambao kila upande unakuja na wakili wake mara nyengine na hawa wana mawakili wanakuwa na mambo yao mengi, sasa ni mambo mengi ambayo yanachelewesha usikilizaji wa kesi mpaka utolewaji wa hukumu.

Sasa sisemi hili kama ni *Excuse* ya kusema kwamba kama kesi ziendelee kusikilizwa, lakini naamini Mahakama imeanzisha sasa utaratibu mzuri unaoitwa *Case Flow Management*, kuhakikisha kwamba sasa kila yule ambae anapangiwa kazi zake basi huwa wanamuwekea muda wa kuzisikiliza na kutoa hukumu inayostahiki, sasa hili wenzetu wa Mahakama wanalishughulikia na nadhani walipofika ni pazuri.

Lakini niende haraka haraka kwa Mhe. Hamza. namshukuru amerudi kwa kasi ambayo amemaliza nayo ya sheria yake ya mswada binafsi, amemaliza kwa kasi na amerudi kwa kasi kukumbusha mswada huu binafsi, kama alivyosema ni kweli kuna aina mbili za mswada kwa mujibu wa kanuni, kifungu cha 78, Miswada ambayo inaletwa na Serikali na ile ambayo inaletwa na Wajumbe maarufu ni miswada binafsi.

Mhe. Spika, na yeye anajua tulipofika kwenye ule Mswada wa Baraza hatukufika pabaya, umefika pazuri, mimi nilipoingia humu katika kazi ambayo wamenikaribisha ni ile na walikuwa *hot* kidogo, sasa na mimi wakaona huyu ni mpya huyu lazima tumuweke sawa, nashukuru tulielewana na tukaenda vizuri, nadhani hapa tulipofika si pabaya, maagizo ya Mhe. Rais yako wazi, sasa ni utekelezaji tu uliobaki Mhe. Hamza, jinsi gani sasa Baraza na taasisi za Serikali tunaweza kulitekeleza lile agizo la Mhe. Rais.

Lakini niende haraka haraka Mhe. Spika, kwa Mhe. Hassan Hamis Hafidh, suala la *External Service* nimeshalizungumza utaratibu wake, lakini alizungumzia mshahara wa mashirika na mishahara ya mawizara, nimuhakikishie ni kweli katika eneo ambalo lilikuwa lina tatizo moja ni hili, lakini kama nilivyosema katika nidhamu ambayo Mhe. Rais amerudisha moja ni hii ya kuhakikisha sasa kwenye utumishi wa umma kunakuwa kuna nidhamu, moja ya nidhamu yenyewe ni malipo yalingane; dereva anayefanya kazi kwenye shirika fulani la Serikali hatafautiani kwenye udereva wake na wanaofanya kazi kwenye Wizara fulani za Serikali, lakini malipo yamekuwa ni tofauti. Ni kweli kwa sababu mengi ya mashirika haya ambayo yanajitegemea mambo yao mengi yalikuwa yanamalizwa na bodi zao, bodi zile zikikaa zinaamua hakuna pengine pa kwenda, kwa hivyo, wanaamua na wanapanga wanavyoona wao inafaa na wanatekeleza wanavyoona wao inafaa.

Sasa kwa kuja sheria hii ya utumishi wa umma, moja jambo ambalo limewekwa ni kwamba hakuna maamuzi yanayofanywa bila ya kuanza kwenda kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma, wanakwenda wanajenga hoja wanakubaliana na Kamisheni inatizama hali halisi ya uchumi ilivyo na baadae wanakubaliana, sasa hili moja ya eneo ambalo Serikali inalifanyia kazi. Lakini

pia najua Serikali ipo katika *process* ya kuandaa *pay policy* ambayo sasa itaongoza utaratibu mzima wa malipo katika utumishi wa umma, kwa hivyo, hili ni jambo ambalo linafanyiwa kazi na Serikali.

Lakini pia amezungumza sheria ambazo za udhalilishaji zilizoletwa na bado zimeganda *AG* na hazijafanyiwa kazi. Sidhani kama hili ni sahihi, sisi Mhe. Spika, sheria zote ambazo zinakuja tunapewa idhini na Baraza la Mapinduzi kuzitayarisha na kuzileta ndani ya Baraza la Wawakilishi. Sasa kwenye hizi sina hakika kama tumepata maelekezo hayo, lakini nimuhakikishie kama tunaleta *Miscellaneous Amendment,* Sheria ya Mabadiliko ya Sheria mbali mbali. Sasa kama kuna maeneo ambayo yeye anahisi yanahitaji kufanyiwa marekebisho, basi awasiliane na wizara husika ili tusaidiane katika kufanya yale marekebisho kupitia sheria hii ya marekebisho ya sheria mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka Mhe. Bi Panya, amezungumzia kibanda cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kiasi gani kimetumia. Sina hakika kama Mhe. Bi. Panya, amepita hivi karibuni kwenye kibanda kile, nadhani akipitia ataona sasa ile hali ambayo iliyokuwepo imebadilika, sasa Mhe. Waziri, hapa anasema kuna mbanda. Ni kweli mwanzo kilikuwa hali yake sio nzuri lakini sasa tumekifanyia kazi kinapendeza, kimetiwa rangi, milango, simu, mafeni, tumejitahidi kukifanya kile kibanda kiende na hadhi ya lile jengo ambalo lipo. Sasa gharama imekaribia shilingi milioni 10 au 12 ambazo tumetumia.

Mhe. Spika, Mhe. Yussuf Hassan, yeye alitaka kujua idadi ya wanasheria, *of course,* sasa wanasheria wa serikali kwa ujumla tunakaribia 35 au 36, na wengi hao wengine tumewa-*deploy* kwenye taasisi na wizara za serikali. Baraza la Mapinduzi lilitoa agizo kama wale Maafisa wa Sheria ambao wapo kwenye mawizara sasa tuwape *title* ya kuwa wanasheria wa serikali, maana yake nini? Maana yake sasa wasaidie kwenye zile kazi za kisheria zinazotoka kwenye wizara zao, wao wawe ndio wa kwanza kuzishughulikia kazi hizi kabla hazijaja Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, hili tunalifanya vizuri na tunaendelea kulifanya, *of course,* tunafanya tathmini ya kazi zao, sasa hivi uwanasheria wa Serikali tofauti na ule ambao tuliuwahi sisi, sasa hivi uwanasheria wa serikali ni dhamana.

Kwa hiyo, unaweza ukapewa ile dhamana, lakini unaweza pia ukavuliwa ile dhamana ya uwanasheria wa serikali. Sasa tunafanya tathmini, usimamizi wa kesi katika taasisi za umma, *of course,* ni kweli tunawasaidia lakini hatuwasaidii bure, kuna muongozo ambao umetoka wizarani na sisi tunauita pale kuna kitu tunakiita *'bill of cost'* kwenye mashirika haya ambayo yanajitegemea mara nyingi yanatakiwa yajisimamie wenyewe na watafute

Mawakili wao, lakini wanakuja kwetu kwa sababu kwetu ni rahisi, lakini tunawasaidia na watupa *a token* kidogo yakuweza kuwapa motisha wale wafanyakazi.

Mhe. Spika, kesi ambazo tunazo ni 60 mpaka sasa hivi; kesi 9 zimemalizika zimeshatolewa uamuzi na tumeshinda, nane tumeshinda, moja tumeshindwa na nyengine hizi zinaendelea. Sasa kiujumla Mhe. Spika, haya ni yale ambayo nimeona nimsaidie Mhe. Waziri katika majumuisho yake, lakini kwa dhati kabisa niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe, kama pamoja na yote yale ambayo watayafanya lakini baadae niwaombe wampitishie Mhe. Waziri, makadirio yake haya ili sasa ashirikiane na wenzake wote katika kueleza yale mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe, wameyaeleza. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa majumuisho ya hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi zilizotolewa katika uwasilishwaji wa hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima, na kumuomba pia awajaalie wale wote walio wagonjwa awaponyeshe ili waweze kuendelea na majukumu yao ya kulijenga taifa letu. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ili kutoa maelezo na kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yake ambayo ililenga kutoa ushauri na maelekezo kwa Idara na Taasisi zote za ofisi hii. Michango yao imeonesha ni kwa kiasi gani Kamati inavyotekeleza kazi zake kwa umahiri na umakini mkubwa katika kuhakikisha Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inawahudumia wananchi ipasavyo.

Mhe. Spika, pia, nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi hususan wale waliopata fursa ya kuchangia hotuba yangu kwa maelekezo yao waliyotupa, hoja na maswali mbali mbali waliyoniuliza na wale waliochangia kwa maandishi. Michango yao itaijengea uwezo zaidi wa kiutendaji ofisi yangu ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa

rasilimali za umma, utoaji wa haki, utawala bora na utoaji wa huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, hotuba yangu ya bajeti imechangiwa na wajumbe mbali mbali, kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba waziri wangu atakapokuja hapa mbele aweze kuwataja wajumbe hao waliochangia bajeti hii.

Mhe. Spika, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kuzitolea ufafanuzi hoja mbali mbali za wajumbe na maswali waliyouliza, na maelezo yangu yatalenga moja kwa moja katika hoja za wajumbe badala ya kujibu hoja za mheshimiwa mmoja mmoja. Katika kujibu hoja hizo, ikiwa itajitokeza hoja ya mjumbe kutojibiwa isionekane kwamba ni swali lililofanywa kwa makusudi, bali hoja hiyo itakuwa imetolewa ufafanuzi katika maelezo yangu ya jumla.

Mhe. Spika, miongoni mwa hoja za wajumbe ambao zilijitokeza katika kuchangia bajeti hii ni suala zima la kutaka kujua hoja kuhusu wafanyakazi waliofukuzwa mwaka 2006, na kwamba uwamuzi wa Mahakama ulikuwa ni kuwarudisha kazini lakini hadi leo wengine hawajareshwa.

Mhe. Spika, tukio limetokea miaka mingi iliyopita. Kwa taarifa tulizonazo kati yao wengine walirudi na wengine walikataa wenyewe kurudi. Kama wapo ambao hawajaridhika na maamuzi, wawasiliane na ofisi yetu na hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa inalenga kujua maslahi ya watumishi wa *CAG* na *DDP* kuwa ni madogo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2014/2015 ilifanya marekebisho ya mishahara kwa baadhi ya kada katika utumishi wa umma. Miongoni mwa kada hizo ni watumishi wa Ofisi za *CAG, DPP* pamoja na Mwanasheria Mkuu. Serikali itaendelea kuzingatia maslahi yao kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni kuhusiana na Ofisi ya *DPP* ina utaratibu gani ya kupeleka huduma zake katika Wilaya zote za Zanzibar. Pia, kuhama kwa wafanyakazi wa *DPP* na kuelekea Tanzania Bara.

Mhe. Spika, ofisi inatoa huduma zake katika ofisi zilizopo Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Kati. Vile vile, ofisi za Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja zinategemea kuanza kazi katika mwaka wa

fedha 2016/2017. Aidha, hatua za uendeshaji wa mashtaka kwa Wilaya za Pemba zimekamilika.

Mhe. Spika, ni kweli Ofisi ya *DPP* inakabiliwa na tatizo la wafanyakazi wake wazoefu kuhama ofisi na kutafuta kazi nyengine Tanzania Bara. Hata hivyo, ofisi imeshatayarisha muundo mpya wa kiutumishi ambao umezingatia maslahi ya wafanyakazi wa Ofisi ya *DPP*. Muundo huo umeshawasilishwa na kupitishwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kwa sasa uko katika ngazi za juu kwa hatua za mwisho.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni kuwa suala la Sheria ya Ushahidi imefikia hatua gani. Mhe. Spika, mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Ushahidi yako katika hatua nzuri. Yameshawasilishwa kwenye kikao cha Makatibu Wakuu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa Sheria ya Kugawana Mali. Mhe. Spika, sheria zote isipokuwa za Mahakama ya Kadhi zina uwezo wa kusikiliza mashauri ya mgawanyo wa mali ya wanandoa walioachana. Katika kushugulikia mashauri hayo Mahakama hufuata misingi ya *Common Law* kwa kuzingatia mchango wa kiuchumi kwa wanandoa walioutoa katika kipindi cha ndoa yao.

Mhe. Spika, suala jengine liloulizwa na wajumbe ni kwamba je, serikali imechukua hatua gani kuhusu vyama vya kisiasa. Mhe. Spika, naomba kuwajuulisha Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba kutokana na Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa Namb. 258(19), Mambo ya Vyama vya Siasa ni suala la Muungano, hivyo, serikali itawasiliana na taasisi husika ili kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Mhe. Spika, suala jengine ilikuwa idadi ya kesi Ofisi ya *CAG*. Mhe. Spika, kesi zote ni 60, ambapo kesi 9 zimeamuliwa, nane kati ya hizo serikali imeshinda na kesi moja serikali imeshindwa. Mhe. Spika, hili suala lilikuwa tayari limeshaelezewa na Mwanasheria Mkuu, kwa hivyo, sina haja kuendelea nalo.

Mhe. Spika, suala jengine lilotaka kujuulikana na wajumbe ni kwamba ucheleweshwaji wa kesi Mahakamani. Mhe. Spika, ili kutatua tatizo hilo, ofisi imechukua hatua zifuatazo:-

i. Kuanzisha vikao vya kusukuma kesi (*Case Flow Management Committee*);
ii. Kukutana na polisi wapelelezi kwa ajili ya kutafuta njia sahihi za kufikisha mashahidi wa kesi kwa wakati;

iii. Kuwahimiza Mahakimu kushugulikia kesi hizo kwa uharaka na kwa mujibu wa sheria; na
iv. Kuhimiza jamii kutoa ushahidi na kuondoa muhali.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa linahusiana na madeni ya mashahidi na wazee wa Baraza (*accessors*). Mhe. Spika, hadi sasa fedha za mashahidi zinazodaiwa na mashahidi ni shilingi 90,000,000/=. Aidha, Mahakama inahitaji kila mwezi kiasi cha shilingi 25,000,000/= kwa ajili ya kuwalipa mashahidi, wazee wa Baraza na maulamaa wanaohusika katika kesi. Utaratibu unafanywa wa kulipa madeni hayo.

Mhe. Spika, suala jengine lililoulizwa au wajumbe walitaka kujua Maslahi ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Mhe. Spika, Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wanalipwa kulingana na elimu zao na tayari serikali imekwisha chukua juhudi za kuongeza maslahi yao kwa kuwalipa posho maalum la shilingi 250,000/= kila mwezi. Jitihada nyengine zinazofanyika ni kufanya mapitio ya Sheria ya Kuanzisha Mahakama za Mahakimu ambayo pamoja na mambo mengine italiangalia suala la kuongeza sifa za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kuaandaa muundo mpya wa Utumishi wa Mahakama ambao utaangalia maslahi yao. Aidha, zoezi la tathmini ya kazi na madaraja litakuwa na nafasi nzuri ya kuliangali suala hili.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo liliulizwa na wajumbe walitaka kujua wanaofanya makosa ya ubakaji kwa watoto na madawa ya kulevya wanyongwe. Hili ni wazo ambalo lilitoka kwa mjumbe. Mhe. Spika, Sheria ya Adhabu ya Nam. 6 ya mwaka 2004, imeweka adhabu kali kwa wale wote watakaotiwa hatiani kwa makosa ya udhalilishaji wa watoto na wanaohusika na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni takwimu za kesi za udhalilishaji, Mahakama ya Watoto ya Mahonda itashughulikia watoto wa aina gani. Hizi ni miongoni mwa hoja ambazo ziliibuka katika michango ya wajumbe.

Mhe. Spika, Mahakama hupokea aina mbali mbali za makosa ya udhalilishaji. Makosa hayo ni kama vile; kubaka, kutorosha, kukashifu, na kadhalika. Takwimu zinaonesha kwamba kuanzia mwaka 2013 hadi mwishoni wa mwaka 2015 Mahakama imepokea kesi 106 za makosa hayo. Kesi 73 kati ya hizo zimetolewa uamuzi ambapo kesi 7 washtakiwa wake wamepatikana na hatia na kupewa adhabu ya kifungo cha kuanzia miaka 2 hadi 11. Kesi 33 bado zinaendelea. Mhe. Spika, Mahakama hii itashughulikia watoto waliofanya

vitendo vya kihalifu walio chini ya miaka 18. Hii inahusiana na ile Mahakama ya Mahonda.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa wajumbe wanataka kujua idadi ya kesi za madawa ya kulevya zilizopokelewa na kutolewa uamuzi. Mhe. Spika, takwimu inaonesha kama ifuatavyo:-

Mwaka 2013 kesi zilizofunguliwa ni 24 na zilizotolewa uamuzi ni 20 na zinazoendelea ni 4. Katika mwaka 2014 kesi zilizofunguliwa ni 16, zilizotolewa uamuzi ni 11 na zinazoendelea ni 5. Mhe. Spika, katika mwaka 2015 kesi zilizofunguliwa ni 10, zilizotolewa uamuzi ni 4 na zinazoendela ni 6. Kwa maana hiyo, jumla ya kesi zilizofunguliwa ni 50, zilizotolewa uamuzi ni 35 na zinazoendelea ni 15.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo wajumbe walitaka kujua kuhusiana na mgongano wa sheria baina ya Kamisheni ya Wakfu na Wizara ya Ardhi na Kilimo. Mhe. Spika, suala hili limeonekana na tayari wizara imepeleka waraka Baraza la Mapinduzi. Baraza limeunda kamati ya Mawaziri wa Wizara za Katiba na Sheria, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi na Wizara inayohusiana na Tawala za Mikoa. Tunatarajia kamati ikimaliza kazi yake mgongano huu utaondoka.

Mhe. Spika, suala jengine liloulizwa na Wajumbe walitaka kujua je, Tume ya Kurekebisha Sheria imerekebisha sheria ngapi na ngapi zimekwishaanza kutumika. Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria tayari imezifanyia marekebisho sheria 17 na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika kwa hatua nyengine.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni mjumbe alikuwa anataka kujua polisi wangapi wamefikishwa Mahakamani kwa makosa ya rushwa. Mhe. Spika, jumla ya malalamiko matatu (3) yanayowahusisha askari watano yalichunguzwa. Kati ya hayo, taarifa mbili zimekamilika na majalada yake yamewasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Mbali ya hatua hizo, Kamishna wa Polisi Zanzibar amekuwa akichukua hatua za ndani za jeshi hilo kwa watumishi wanaohusishwa na vitendo vya rushwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo wajumbe walitaka kulijua linahusiana na faida ya kuwepo kwa mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi wanasema kwamba haijaonekana. Mhe. Spika, kumekuwa na faida mbali mbali za kuanzishwa kwa Mamlaka hii ya rushwa zikiwemo:-

(i) Uelewa wa wananchi umeongezeka, hivyo basi idadi ya tuhuma zinazoripotiwa katika Mamlaka zimeongezeka pia;

(ii) Tahadhari imeongezeka ya watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa;

(iii) Faida nyengine Mhe. Spika, ni taasisi mbali mbali zimefaidika na ushauri unaotokana na hatua za udhibiti. Miongoni mwa ofisi hizo ni Ofisi ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi na Hoteli ya Bwawani;

(iv) Mafanikio ya uchunguzi yamewekwa wazi katika Ibara ya 102. Taarifa ya nyongeza ni kwamba, katika wiki iliyopita Ofisi ya *DPP* imeidhinisha majalada mengine mawili kesi zake kufikishwa Mahakamani.

Mhe. Spika, hoja nyengine kutoka kwa wajumbe ilikuwa semina za Mamlaka ya Rushwa je, zilihusisha watu wa aina gani.

Mhe. Spika, semina za Mamlaka ya Rushwa ziliwahusisha watu mbali mbali na taasisi mbali mbali; Masheha wa Wilaya zote za Unguja, Wilaya za Mkoa wa Kusini Pemba, Mahakimu na Waendesha Mashtaka na baadhi ya makundi ya vijana, Wagombea wa nafasi za Ubunge na Uwakilishi wa vyama vyote, vikundi mbali mbali vya wajasiriamali (vinne Unguja na vinne Pemba). Pamoja na hayo wanawake kwa Unguja, Jeshi la Polisi, Wilaya zote za kipolisi Unguja na tunatarajia kumalizia za Pemba Maafisa wanaokusanya Kodi wa *TRA* nao pia watapata mafunzo kutoka taasisi hii.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo wajumbe walikuwa wanataka kujua ni utaratibu na vigezo vya usajili wa kazi za Hati Miliki.

Mhe. Spika, utaratibu unaotumika ni kwa mwenye kazi inayolindwa kwa mujibu wa sheria ya Hati Miliki Nam. 14 ya mwaka 2003, ni kuwasilisha nakala halisi ya kazi anayokusudia kuisajili, hivyo, niwaombe Wawakilishi wenye vikundi vya sanaa kuwashajihisha wananchi wafike Ofisi ya Hati Miliki kwa ajili ya kufanya usajili kwa wale watakaotumiza vigezo na masharti ya usajili. Mhe. Spika, sambamba na hilo, Wajumbe walitaka kujuwa idadi ya kazi zilizosajiliwa zinapatikana vipi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/2017 ofisi ilitarajia kusajili kazi 1576 za Hati Miliki na sio vikundi baada ya kushajihisha wenye hati miliki katika maeneo yao mbali mbali hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Wajumbe pia walitaka kujuwa Bodi ya Hati Miliki imemaliza lini muda wake. Mhe. Spika, Bodi ya Hati imemaliza muda wake mwaka 2014 na utaratibu wa kuchagua Bodi nyengine umeanza na Bodi hiyo itachaguliwa muda wowote kuanzia sasa kwa mujibu wa sheria hiyo ya Hati Miliki.

Mhe. Spika, baada ya kuchambua hoja mbali mbali za Wajumbe, kwa ruhusa yako naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Jimbo la Pangawe kwa kuniamini na hatimaye kunichagua kuwa muwakilishi wao ili niweze kuwawakilisha katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, naomba pia kuwaambia wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe tuzidi kushirikiana na kupenda ili tuweze kuzidisha mshikamano wetu katika kuleta maendeleo kwa vitendo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe na mimi ni vyema na sina budi kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa asilimia mia moja.Ahsante naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni ya leo kupata nafasi hii kwa mara ya pili kuanzia jana ili kujaribu kujibu hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa walizitoa. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na *alhamdullillahi* niko tayari kujibu hoja zote za Waheshimiwa. Lakini ninataka nitangulize kitu kimoja kabla sijajibu.

Mhe. Spika, kama ni mtoto hivi sasa aliyezaliwa basi ana umri wa mwezi mmoja na nusu au miezi miwili kasoro siku kumi. Sasa Waheshimiwa humu Barazani kama kuna watu wakongwe na mimi mkongwe, nishavuka miaka 55 naingia 60 na ushei. Lakini pia ninataka niwaombe sana kama mwalimu wenu munisikilize, muniulize pale ambapo hamtofahamu kwa sababu ni wajibu wangu masuala kujibu tokea darasani na nawaomba sana Waheshimiwa, wataridhika nina hakika na majibu ambayo nitayatoa hapa, na wale ambao hawatoridhika sio kwamba nimewadharau, naomba tuje tutafute wakati tuje tufahamishane zaidi, kwa yote ambayo nimeyaeleza hapa ninawahakikishia kwamba nitawapa majawabu baadae.

Mhe. Spika, pia, ninataka niseme kwamba kuna mambo yaliulizwa kwa mapenzi yao Waheshimiwa hawa wakaniuliza mimi ingawa yalikuwa

hayanihusu mimi lakini maadam yameulizwa katika Serikali ndiyo yamenihusu vile vile. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna suala limeulizwa kuhusu ufungaji wa barabara ya Mkunazini kuelekea kule *CRDB*, suala hili liko chini ya Mamlaka ya Mji Mkongwe. Kutokana na heshima tuliyopewa na *UNESCO* kwamba ni moja katika miji ya urithi, kwa hivyo, imebidi tufuate taratibu fulani ambazo zimetuachia na hatuwezi kuzikiuka, kwa hivyo, ni kwa muda huo, sio kwa sababu nyengine yoyote. Lakini Waziri muhusika atakapokuja atazidi kutoa maelezo na muekeeni masuala kama haya nayeye ataweza kuyajibu.

Mhe. Spika, suala la *pension* za wazee zimeulizwa, lakini hili liko Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake, Vijana, Watoto na wengineo. Kwa hivyo, tumsubiti Bi. Castico atakaporudi kenda kuchukua ukali Geneva akirudi ana visu vyake vizuri kaviweka. Mhe. Spika, hati za nyumba, Wizara yetu ya Ujenzi inahusika na masuala hayo, kuna Shirika zima la Nyumba limeanzishwa wataendelea kujibu.

Mhe. Spika, sekta binafsi au ajira za watu binafsi au sekta binafsi kwa ujumla, hizi Waheshimiwa mmeniuliza mimi, nilikuwa Waziri wa Kazi kweli lakini nimeshahama, sasa niko kwenye utumishi wa umma. Mhe. Mwanasheria Mkuu, kanisaidia vizuri sana suala hili, tupembue kati ya utumishi wa umma na sekta binafsi, kwa sababu hizi sio kazi zangu. Kwa mfano Mhe. Hassan, aliposema na hili ninataka nimuombe sana, mwaka juzi palipotokea suala suala fulani hapa kuna Mheshimiwa mmoja akasema; 'yule muhindi wa kule anawatesa wenzake', sikilizeni vizuri, hayo hakusema Hassan, ila huyo wa siku hiyo alisema; 'kuna muhindi kule katika kituo fulani shirika fulani la mafuta anatesa Watanzania na wazalendo wa Zanzibar'.

Mimi nikamjibu, kwani si ungesema tu kuna raia wa kigeni, lazima utaje na kabila. Sasa na huyu wa Uwanja wa Ndege ambaye anatayarisha chai katajwa huyu kwamba kuna mhindi mmoja pale anatayarisha chai, kwani kazi ile Wazanzibar hawawezi kuifanya? Wanaweza kuifanya, lakini ungesema kuna raia wa kigeni ambaye anatayarisha chai ndio tungefahamu, si Mzanzibari.

Mhe. Spika, Mhe. Hassan mimi ni mwalimu wako na nazidi kukufahamisha na hata Mhe. Hamza vile vile ni mwalimu wake, namwambia kwa leo bado aendelee kuheshimu kile kibali maalumu nilichompa ambacho anaendelea kukitumia mpaka leo hapa. Kuna mambo kayaeleza Mhe. Hamza, anasema pamoja na mwalimu wangu lakini leo... Kama Mhe. Dimwa, alivyosema kwamba leo anavaa ninja ananambia.(*Makofi*/*Kicheko*)

Sasa kwa bahati nzuri keshazivua hizo na sasa hivi kawa raia wa kawaida. Kwa hivyo, ajira binafsi tumngoje Waziri wa Kazi tukijaaliwa atajibu majibu mazuri na sisi tutakuja kumsaidia Waziri mwenzetu.

Mhe. Spika, jengine kuna suala zima la vyeti vya kuzaliwa, hivi haviko kwangu sasa tusubiri na bahati nzuri kesho tukijaaliwa Wizara hii ya Tawala za Mikoa, Idara Maalum, Serikali za Mitaa iko tayari kabisa kuja kuwasilisha bajeti yake na mambo haya yote yamo na jawabu anazo kabisa.

Mhe. Spika, Chuo cha *CCK* kikowapi, yaani Chuo cha Kiislamu kikowapi. Mimi niliwahi kuwa Waziri wa Elimu kilikuwa chini ya Wizara ya Elimu na bado kiko chini ya Wizara ya Elimu na Bi. Riziki yule pale keshasikia atakuja kusaidia.

Mhe. Spika, sasa naomba uniruhusu baada ya jumla niwataje wajumbe wote waliochangia. Kwanza kabisa ni:

1. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
2. Mhe. Salma Mussa Bilal
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
4. Mhe. Suleiman Sarahan Said
5. Mhe. Simai Mohammed Said
6. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
7. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
8. Mhe. Abdalla Ali Kombo
9. Mhe. Suleiman Makame Ali
10. Mhe. Hamza Hassan Juma
11. Mhe. Hidaya Ali makame
12. Mhe. Miraji Khamis Mussa, lile jina lako la utani mimi silijui
13. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
14. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
15. Mhe. Mussa Foum Mussa
16. Mhe. Shehe Hamad Mattar
17. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
18. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
19. Mhe. Shadya Muhammed Suleiman
20. Mhe. Panya Ali Abdalla
21. Mhe. Omar Seif Abeid
22. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
23. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
24. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti

25. Mhe. Mohammed Said Dimwa
26. Mhe. Asha Abdalla Mussa
27. Mhe. Bahati Khamis Kombo
28. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma
29. Mhe. Said Omar Said
30. Mhe. Maryam Thani Juma
31. Mhe. Shamata Shaame Khamis
32. Mhe. Juma Ali Khatib
33. Mhe. Hamad Rashid Mohammed
34. Mhe. Said Soud Said
35. Mhe. Said Hassan Said
36. Mhe. Khamis Juma Maalim na
37. Mhe. Zainab Abdalla Salum

Mhe. Spika, jumla yao waliochangia kwa kusema ni 37 na wafuatao wamechangia kwa maandishi.

1. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
3. Mhe. Masoud Abdurahman Masoud
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
   na mzee wangu
6. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), nimemwita mzee wangu Mhe. Spika, kwa sababu mimi ni Haroun Ali Suleiman na huyu kazaa mtoto kamwita Haroun, kwa hiyo, mapenzi yake juu yangu.

Mhe. Spika, nimepokea maombi, nimepokea maelezo, nimepokea hoja za Waheshimiwa. Bahati nzuri nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu, amenisaidia sana mambo ya kisheria, mimi ndio kwanza nimeingia safari kwa mwezi mmoja na nusu yalikuwa mikononi kwa Waziri mwengine, simtaji jina, mambo ya Katiba na sheria yalikuwa hayapo kwetu, mambo mengi yamechelewa chelewa mmesema wenyewe, sasa mimi nina mwezi mmoja na nusu sasa hivi na kidogo, msiwe na wasi wasi, sina historia ya kushindwa kazi, *alhamdullillahi*, na nawaahidi kabisa kwa masuala yote yanayohusiana na Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora yaliyokuwa yamekaa pembeni pembeni tutayaweka kwenye laini tutakwenda nayo *inshallah* na ikifika 2020 ushindi wa kishindo upo pale pale.

Mhe. Spika, suala la Mahakama limezungumzwa kwa ujumla Mhe. Hamza, Mhe. Jaku na wengineo, nipeni muda mimi nakuhakikishieni nina uchungu

sana wa suala hili, nimekwenda nimefanya ziara, mimi bahati nzuri nimeshatembelea taasisi zote zilizokuwa chini ya Wizara yangu sasa hivi, ninazijua na bado nitazitembelea zile zilikuwa kwenye Wilaya na Mikoa ili nipate kuzijua zaidi, nimejifunza mengi Mahakamani, Jaji Mkuu kanipokea vizuri sana, Majaji wamenipokea vizuri, Mwanasheria wangu nimekwenda ofisini kwake kanipokea vizuri, Mkurugenzi wa Mashtaka kanipokea vizuri, Mkurugenzi wa Rushwa kanipokea vizuri na wengine wote wamenipokea vizuri, *CAG* kanipokea vizuri sana na wengine wote ambao nimewatembelea. Niliyekuwa sikumtaja haina maana kwamba hakunipokea vizuri, maana wananitazama sana kule juu, nyote mmenipokea vizuri.

Mhe. Spika, kwa hivyo, napenda niwahakikishie, wamenambia tatizo lao na tayari tunafanya utaratibu tukijaaliwa. Katika bajeti ijayo tutahakikisha bajeti yao waliyoiyomba tunaifuatilia, wao watafatilia kwa utaratibu wao kwa sababu ni muhimili ambao unajitegemea wenyewe na sisi tutatia nguvu zetu kuhakikisha kwamba wanapata fedha za kutosha ili kazi zao zisichelewe na ziende kwa wakati *inshallah.*

Mhe. Spika, suala la ulinzi wa jadi, Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshalitolea ufafanuzi, msiwe na mashaka nalo tukijaaliwa, walinzi kuna wa aina mbili; viongozi wakuu wa kitaifa wana ulinzi wao kwa mujibu wa sheria, Rais, Makamo wa Pili wa Rais na wengine wako wawili watatu ambao wana jukumu hilo, Spika, Jaji Mkuu na wengineo. Mawaziri walinzi wao tumepewa masaa ishirini na nne wa kutulinda majumbani, sio wale wa kutufuata fuata nyuma wale, wale wanaotufuata fuata nyuma wakati mwengine ndio tunao kwa baadhi yetu.

Mhe. Spika, ilitokea dharura mwaka fulani Katibu Mkuu Wizara ya Fedha alipewa mlinzi Omar Sheha, kulikuwa na sababu maalum akapewa mlinzi na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ikitokea haja kama hiyo wanatusaidia sana, lakini mpaka sasa walinzi ambao tumepewa kisheria kwa mujibu wa taratibu zote za kisheria za utumishi ni wale walinzi wa masaa 24 majumbani, *alhamdullillahi,* tunalindwa na polisi na kama kuna Waziri bado hajalindwa na Polisi au Askari yeyote wa vikosi vyetu basi atujuilishe ili tufanye utaratibu tushirikiane na Wizara husika ili apate ulinzi. Mhe. Spika, ulinzi ni kitu muhimu sana.

Mhe. Spika, Ofisi ya *AG* kaizungumza mwenyewe, sina haja ya kuirejea.

Mhe. Spika, suala la *IPA*, Chuo cha *IPA* kimezungumzwa na wengi, na kusema kweli waliyoyazungumza yote ni sahihi, hakuna hata moja ambalo

wamedanganya na ninakuhakikishieni kwamba mmenifurahisha sana, kwa sababu juzi mimi nilikwenda huko huko *IPA*, yale mliyazungumza nyinyi ndio niliyoyazungumza mimi, nikazungumza na Wakurugenzi na Bodi iliyokuwepo pale, na mimi tunajuwa na mnaendelea kufahamu kwamba chuo cha *IPA* kinatoa mpaka Stashahada (*Diploma*), lengo letu tunataka na tayari mipango imeshakamilika mwaka huu tutaanza Shahada ya Kwanza tukijaaliwa pale, ili kukipandisha daraja chuo chetu cha *IPA*.

Mhe. Spika, mafunzo ya utumishi na nidhamu za wafanyakazi na mambo yote yanayohusiana na mambo ya utumishi pale kuna dozi maalum inatolewa. Haya mambo ya uvujaji wa siri mulioyazungumza ni kweli zinavuja siri, kuna Mheshimiwa, alisema hapa nyie mnawachukuwa hawa madereva na nini, wenyewe wanakasirika huko wanasema siye madereva hatuaminiwi.

Lakini wakati mwengine siri tunazitoa sisi wenyewe viongozi, tunalaumiana tu, kaeni kwenye vikao, kwenye mikutano yenu huko Wilayani, Mikoani, asubuhi siku ya pili unayasikia yote yaliyozungumzwa. Kwa hivyo, utoaji wa siri ni kosa kubwa, ukitoa siri ile hasa ya Serikali ya vikao vyote ni kosa, sasa kule kwenye Chuo cha Utumishi wa Umma kuna mafunzo maalum yanatolewa kwa ajili ya watumishi wa umma katika suala zima la ulindaji au pengine utunzaji wa siri.

Mhe. Spika, kulikuwa na upotevu wa pesa wala si uongo ni kweli, pesa nyingi zilipotea pale mamilioni ya pesa, muhusika katakiwa azilipe zote na yeye akaondoshwa pale kabisa asiwepo pale, kachukuliwa hatua na nadhani amesimamishwa kama sikosei, na hivi karibuni kumetokea matatizo ya malipo fulani, mshika fedha yule ambaye tuliazima kutoka Wizara ya Fedha akaja akafanya kazi pale kwa muda, ikawa fedha zile badala ya kuzipeleka Benki akawa anakaa nazo, unajua pesa raha eeh! Sasa habari ya pesa mnajuwa nyinyi upate noti mpya zile za elfu tano tano, elfu kumi kumi ziko kwenye *rubber band* zinakunjwa vizuri unasema hizi sizitumii kwanza, lakini kila ukiwa na haja unakwenda kuchungulia unatoa moja, unatoa moja mpaka kile kibunda chako kinakaa kama ngarawa hivi kishakwisha, ina maana hiyo *rubber band* ukikunja pesa zako, ukisha unatoa *rubber band* unaitupa na pesa unaitia mfukoni kazi imekwisha.

Sasa pesa ndio kazi yake kutumiwa, lakini kosa limetendeka huyu afisa akawa anatumia kwa maslahi yake, tayari tumeshamrejesha Wizara ya Fedha wanajua wenyewe Wizara ya Fedha na Waziri ananisikia huyo kijana ninamuomba kwa sababu ni muajiriwa wake achukuwe hatua za kufaa na kama hana taarifa za

ziada *inshaallah* mimi naahidi kwa niaba ya Waheshimiwa walioulizia suala hili nitakuletea jina lake ili uchukuwe hatua za kufaa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika suala la upotevu wa mali za Serikali, fedha za Serikali hatuna sumile nalo, mimi nakuambieni na nakuahidini hilo litafanyika tutakwenda nalo bega kwa bega ili kuhakikisha kwamba suala linamalizika vizuri *inshaallah.*

Mhe. Spika, suala la ajira kwa walimu, tuajirini walimu, ninakubali, mimi mwenyewe mwalimu na nimeshamuhakikishia Waziri kama kuna mwalimu wa sayansi ana *Degree* au Diploma wa sayansi yupo tayari watuletee majina tutafanya kila njia katika bajeti hii tuwachukuwe walimu hao watusaidie kutusomeshea, na wale wengine wote ambao tutawahitajia kwa mazingira maalum tutawaajiri.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mufti. Mheshimiwa, Waheshimiwa wengi wamezungumza kwamba tutafute sabuni tuwagaiye wale walimu. Sabuni ina njia mbili; wakati mwengine unafua nguo inatoka mapovu, wakati mwengine inachuna mikononi, ndio sababu, inategemea *quality* ya sabuni yenyewe. Waheshimiwa, walimu wetu wanapata tabu hivi sasa hawana sabuni, sabuni waliyoipata inawachuna mikono, sasa ombi kwamba tuwapatie maposho, hili sitaki kujifunga sasa hivi, isipokuwa tutafanya juhudi kushirikiana na Ofisi ya Mufti kutafuta nchi rafiki ambazo zina *interest* ya mambo ya dini ya kiislamu ili watusaidie kutupatia chochote kusaidia walimu, hilo tutalifanya.

Lakini kama Serikali hatuwezi kujifunga jambo hilo hivi sasa. Isipokuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge ndio wakati wenyewe wa kufanya kazi huko vyuoni na nyinyi wenyewe mtoe mifukoni mkawagaie hao walimu kidogo kidogo msione tabu, thawabu hizi zitakusaidia, unatengeneza hatima yako ya duniani na kesho akhera, lakini pia ishirini, ishirini ndio hatima yenyewe, ndio hiyo hiyo, dua za walimu wale wa chuoni hazirudi zile nakwambieni.

Mhe. Spika, kumbukeni mlipokuwa wanafunzi chuoni, kila mwalimu wa chuoni ukimtukana ndio anangara tu siku ya pili, unamwombea afe ili chuoni usende, matokeo yake asubuhi mapema keshafika na bakora yake tayari na bakora za mwalimu wa chuoni hazina sheria zinapokuangukia ndio hapo hapo. Kwa hivyo, sabuni tuwasaidie kadri itavyowezekana sisi viongozi pamoja na wananchi wengine wote waliokuwa na uwezo tuwasaidie walimu wetu, tutatizama njia ya kuwasaidia kwa njia ya kuwatafutia wafadhili hao wengine *inshaallah.*

Mhe. Spika, Mufti wetu huyu amefanya ziada maalumu Unguja na Pemba na anaendelea kutoa taaluma kwa Maimamu wa Misikiti ili kuleta amani katika nchi yetu anaendelea, na ataendelea kuhubiri dini, ni wajibu wake, anafanya kazi kwenye Misikiti yote ametembelea, kuwaita Maimamu kuzungumza nao na kwenye vyuo na madrasa zote anakwenda, anafanya kazi nzuri, tumshukuru sana na tumpongeze Mufti wetu anafanya kazi nzuri.

Mhe. Spika, suala la Wakfu. Ndugu yangu Mhe. Abdalla Ali Kombo, kazungumza kwa dakika tatu. kaweka rikodi humu, muda mfupi lakini kazungumza mambo mazito. Kazungumza suala la nyaraka na suala la pesa za Zakka. Hili la nyaraka nataka niwaombe sana nimeshazungumza kwa mujibu wa Kanuni ya 37(2). jambo ambalo lishatolewa uamuzi siwezi kulirejea tena, lakini kwa heshima yao Waheshimiwa hawa naomba wanipe muda mimi mwenyewe nitawatafuta, nitawaita na nitawapa taaluma ili wafahamu na ikihitajika Mhe. Spika, niwaletee taarifa kamili, lakini tutapanga kikao chengine sio hiki ili niwaletee taarifa na niwakabidhi mkononi waitizame na waisome. Kwa sababu ni maamuzi yaliyotolewa hapa Barazani na yako kwenye *Hansard*. Kwa hivyo, ni kuyachukua tukasaidiana na tukawaeleza kwa kutoa taaluma, lakini hatua mbali mbali zilichukuliwa, kwa hivyo, msiwe na wasiwasi.

Serikali ilichukua hatua kubwa kweli kweli mpaka kupeleka ujumbe Omani. Kwa hiyo, nawaomba watulie, mimi mwalimu wao nipo hapa nitalishughulikia na nitawapa taaluma ili wafahamu.

Kuhusu pesa za Zakka. Pesa za Zakka sio mkopo, mimi bahati nzuri wakati ule nilikuwa Waziri wa Uwezeshaji na pesa za Zakka zililetwa pale lakini hatukupewa sisi wizarani. Watu wa Zakaa wenyewe wa Wakfu na Mali ya Amana walilisimamia, tukazigawa wilaya zote 10. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walikuwemo humo kila mmoja na mimi niletee na mimi niletee, tukawapelekea na utaratibu ulikuwa vipi? Pesa zile ukishapewa wewe unazifanyia biashara au kazi yoyote ya maana ukipata faida unampa na jirani yako au mtu mwengine aliyepo pale ili na yeye zimsaidie.

Sasa zimekuwa zikizunguka huko, wako ambao waliripoti wakenda kunakohusika, wakaja wizarani pale tukawaambia hapana, zipelekeni Wakfu kule watakupeni maelekezo. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba hilo wamelifanya. Lakini zile hazikutolewa kama mkopo au kugaiwa, zilitolewa kwa ajili ya kufanya shughuli za kibiashara na huyo aliyetoa Zakka ndivyo alivyofanya. Hata zile wilaya saba ambazo zilitolewa Zakka safari hii zikasemwa mbona Unguja tu, Pemba hakuna, mwenyewe alisema hivyo zipewe

wilaya saba za Unguja, inawezekana kataka mwenyewe tufanyiwe hivyo na tukafanyiwa hivyo.

Mhe. Spika, Idara ya Nyaraka. Idara yetu ya Nyaraka kule sasa hivi nakuombeni nendeni, tumetia kamera za *CCTV*, kumebadilika sana sasa hivi na *Alhamdulillah* tumepata Mkurugenzi mpya yule keshastaafu kapumzika na mitihani aliyopata keshapumzika. Sasa kumebadilika na kazi inakwenda vizuri. Kazi iliyopo sasa hivi ndani ya eneo la nyaraka kuna nyumba ya mtu binafsi, hatuwezi kukubali nyumba ya binafsi kuwemo ndani ya eneo lile la nyaraka, kwa sababu ukifunga geti ndani inabidi akija na yeye ana ufunguo wake afungue anaingia ndani. Tutakachofanya ni nini, tutafanya kwamba tumeshazungumza naye, nimemuita amenambia yuko tayari apewe chake aondoke na aache nyumba itumike kwa shughuli zote ambazo serikali itaamua. Kwa hivyo, sasa hivi tunawasiliana na wenzetu wanaotia thamani ya mali za serikali na nyumba kama zile watupigie thamani apewe chake atuachie nyumba, sisi tukafanye shughuli zetu.

Mhe. Spika, suala la *E-Government*. Hili Waheshimiwa nataka nikuhakikishieni kwamba tunajiandaa kukuandalieni mafunzo maalum, tutajitahidi ikiwezekana mapema iwezekanavyo kwa sababu taaluma hii ya serikali mtandao watu wengi hawaijui, yaani hawajaifahamu, wanaisikia tu. Kwa hivyo, *Inshaallah* tutaandaa programu maalum tukusaidieni mpate taaluma hiyo. Lakini tumeunganisha taasisi sasa hivi 53 kwa Unguja na Pemba, tayari zimeshaunganishwa wizara mbali mbali za serikali, orodha ninayo pale atakayeihitaji Mhe. Spika, mimi nitakupa kopi ili baadae tuweze kuwapa Waheshimiwa waone wapi na wapi tumeunganisha katika suala zima hili.

Mhe. Spika, pale taarifa zote za serikali tunataka ziwepo na kuna vyombo vya kisasa ukienda utashangaa, kwanza pana kamera inakuchukua kila unachokifanya kinaonekana kama kule maeneo ya nyaraka sasa hivi. Mitambo iliyokuweko pale ni ya kisasa kabisa inawashwa saa 24, pale hapazimwi kwa sababu inarikodi kila kitu, mambo yanayotokea Pemba, yanayotokea Nungwi, Makunduchi, Kizimkazi yote pale inakuwa *recorded* taarifa zipo. Nimemuomba waziri mwenzangu wa Miundombinu ambaye ndiye dhama wa mambo ya ufundi tufanye siku twende pale tukalione lile eneo ili tufanye kazi hiyo. Kwa hivyo, tutafanya hivyo tukijaaliwa.

Mhe. Spika, suala la *CAG*. Jamani nyote mmempongeza *CAG* kwa kazi nzuri anayoifanya na mimi naunga na nyinyi kumpongeza. Mmesema apatiwe ulinzi kwa sababu anafanya kazi nyeti. Nakumbuka mimi hata mwaka jana au mwaka

juzi lilizungumzwa suala la ulinzi wa *CAG*. Tutalizingatia na kuona taratibu gani za kisheria tuzitumie ili kulitekeleza hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la Wizara au taasisi zilizopata hati chafu tunachukua hatua gani au ndio yamekwisha? Waheshimiwa, ninajitahidi kujibu maswali yenu yote nisikilizeni vizuri. Hati chafu ikitolewa katika wizara ile wizara au taasisi ina kiongozi wake atakuwepo waziri, naibu waziri, katibu mkuu au mkurugenzi na wengineo. Kwa hivyo, kila mmoja atizame ripoti ile na zimetolewa hapa kila mmoja akapewa na maofisini tutaletewa ili mtizame palipokuwa na udhaifu turekebishe.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alitoa taarifa habari ya Mfuko wa Jimbo, mambo ya Mfuko yaliyotokezea ni hatari, watu pesa wamechukua na kazi hazikufanyika. Sasa yeye mwenyewe kasema atachukua hatua kwa sababu ndiye dhamana wa Mfuko ule na sisi ni wajibu wetu kumsaidia. Sisi tukiletewa mtu Mahakama tunazo na wanasheria tunao, tutawapeleka kunakohusika tuletewe tu.

Sasa nakuombeni na nyinyi Waheshimiwa tuziangalie zile ripoti tuzisome vizuri, lakini viongozi mawaziri, makatibu wakuu na watendaji wote waangalie zile ripoti halafu wafuatilie na mashirika mbali mbali, wakurugenzi, mameneja halafu watajua hatua za kuchukua, hawakuchukua wao hatua kuna utaraibu mzima wa kiserikali na hili litazungumzwa katika ngazi za juu serikalini ili tuone sasa hatua zinazochukuliwa, tutazijadili na baadae hatua zitachukuliwa.

Mhe. Spika, kweli limezungumzwa suala la mashirika haya, lakini *CAG* anayo haki hiyo na sheria inamruhusu kama kuna taasisi kwa mfano za mashirika kama *ZRB, PBZ* na nyenginezo kama anahitaji ukaguzi wa kina wa kitaalamu zaidi anaweza akawachukua *service* kutoka nje wala hakuna matatizo. Bora upate *service* kutoka nje kuliko sisi wenyewe kwa wenyewe wakati mwengine tunaaminiana. lakini kuna masuala mengine ya kitaaluma tunahitaji wataalamu zaidi ambao wamebobea. Kwa hivyo, wanafanya kwa mujibu wa sheria sio kama anavyotaka yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, Suala la ajira limezungumzwa sana na mimi namshukuru sana *AG* kalitolea ufafanuzi, hivyo, sina haja ya kulirejea tena.

Nawashukuru sana *DPP* kazi nzuri wanazozifanya lakini tuna lawama nyingi za *DPP*, lakini *DPP* anafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Huwezi kumpeleka mtu Mahakamani kama huna ushahidi na sio ushahidi wa kusikia, *'hears say evidence'* huwezi kuichukua kama ni ushahidi na mimi naanza kuwa

mwanasheria kidogo kidogo. Ushahidi wa kusikia, yaani *'hears say evidence'* huwezi kuuchukulia kama ni ushahidi kwamba, mimi nimesikia, mimi niliambiwa na nani, huo si ushahidi, uthibitishe. Hata katika Dini ya Kiisilamu kuna mambo ambayo lazima uyashuhudie na uyaone tena usiwe mmoja, wawili au watatu, muwe wanne pengine na uone hasa. Basi nadhani inatosha.

Mhe. Spika, Masuala ya rushwa. namshukuru sana Mkurugenzi Mussa kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya na aendelee kufanya, lakini suala hili hatuna sumile nalo. Limeelezwa Mhe. Naibu Waziri, namshukuru ametoa ufafanuzi mzuri kesi ngapi za rushwa zilizoshughulikiwa na umetoa jawabu.

Mhe. Spika, nakaribia kumaliza, wala sichukui muda wako mrefu kwa sababu *AG* na Naibu Waziri, wamenisaidia sana. Nimalize mimi kwa kutoa wasio mmoja, Waheshimiwa, tuliokuwemo humu ndani sote ni wamoja, tupendane, tujenge umoja wetu kwa maslahi ya nchi yetu, nyote dhamira zenu ndio hizo hizo tunajenga umoja, tunajenga mshikamano kwa lengo la kuleta maendeleo katika nchi yetu, kwa hivyo, tushirikiane. Tukifanya hivyo tutasaidia wananchi wetu na Rais wetu pia tutakuwa tumemsaidia vile vile. Kwa hiyo, tuendelee kushirikiana, tupendane kwa hali na mali ili kuhakikisha kwamba tunapambana na tabia zote chafu ambazo hazipendezi katika nchi yetu kutendeka. Masuala ya rushwa na mambo mengine.

Mwisho kabisa, tumesema tutatoa fomu zile zitatolewa karibu za maadili ya viongozi kwa viongozi wote, watumishi wa umma na wanasiasa. Zile ni fomu muhimu sana, tunajipanga sasa hivi karibu mtaletewa na kila kiongozi atawajibika kujaza na kueleza mali alizokuwanazo kama ana madini, au kama ana nini, yote ataeleza halafu Tume ya Maadili itashughulikia ipasavyo, pale ambapo patakuwa na maswali tushirikiane nao wenzetu hawa watakapokuwa wanapita kutuuliza.

Mhe. Spika, baada ya hayo niendelee kuwaomba tena Waheshimiwa, nadhani kwa juhudi niliyochukua leo na Mwanasheria Mkuu na Naibu Waziri, nadhani wamefahamu, hawa hawachelewi kufahamu wanafahamu haraka sana. Kwa hivyo, Mheshimiwa, naomba nikushukuru tena, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Makunduchi tena kwa kuendelea kuniamini lakini na humu mniamini kwa niaba yao nasema hotuba hii tunaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba hoja iamuliwe, wale wote wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ulipowauliza Waheshimiwa Wajumbe, hoja iungwe mkono, wamenyanyua mikono na wako watatu ambao hawakunyanyua, sio kwa sababu hawataki, isipokuwa ni baridi kidogo imekuwa kali humu ndani.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili nakuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri, kabla sijamwita katibu nina wasi wasi tunaweza tukapindukia ule muda wa kawaida. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu ili tutengue kabisa ile kanuni ya wakati ikitokezea hivyo tutakuwa tuko salama tutaendelea bila ya kuwa na haja ya kurudi. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nikushukuru kwa busara ambayo umeitumia nakuomba tutenge kando kanuni ya muda ili tutoe fursa nzuri kwa Waheshimiwa Wajumbe, kupitisha mafungu kwa utulivu. Sasa naomba nitoe hoja Mhe. Spika, ya kutenga kando Kanuni ya 23(4) ya muda ili tuongeze muda badala ya kumaliza saa mbili kama muda unavyoelekeza na tumalize pale ambapo tutamaliza kupitisha bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba kuwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja iliyotolewa wanyanyue mikono. Wanaokata, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU G01 - OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu G0103	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	85,604,000
	Jumla Kuu:	**85,604,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PG0103	Programu kuu ya Utawala Bora, Haki za Binadamu na Usalama wa Watumishi wa Umma.	
Kifungu SG010301	Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala Bora, Haki za Binadamu na Usalama wa Watumishi wa Umma	268,620,000
Kifungu SG010302	Programu ndogo ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma	120,000,000
	Jumla ya Kifungu:	**348,620,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mimi katika maelezo yangu nilizungumza kumuomba Mhe. Waziri, kuna kadhia zilitokea kwa upande wa Haki za Binadamu kuhusu juu ya kutekwa, Kanuni au Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 13, watu kuteswa na kutiwa nguvuni bila ya sababu. Vile vile, nikazungumzia juu ya suala zima la mwanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kupigwa msumari hadi kupelekea maradhi na mauti, nafikiri sikupata jibu, kwanza. Sasa na nikamwambia wakati natoa maelezo yangu sitokuwa tayari kupitisha fungu lake kama hajanitosheleza na maelezo mazuri ili wapiga kura wangu waliokutwa na hiyo kadhia wasikie nini nilichokifanya.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hicho kifungu kilikuwa tayari tushakipitisha, lakini kwa busara tu nitamruhusu Mhe. Waziri kama ana majibu aweze kukujibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ni suala lake la mwanzo sio kama nimesahau ni masuala ambayo yanahusu polisi na polisi ni suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa vyovyote waziri pengine angetusaidia hapa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni Makamu wa Pili wa Rais.

Na hili suala jengine hatuna taarifa nalo atuletee kimaandishi tutalifuatilia tukijaaliwa.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Sawa pamoja na kwamba polisi iko ndani ya Jamhuri ya Muungano Tanzania. Lakini hapa vile vile imezungumziwa juu ya kusimamia Katiba na Sheria, wala hawezi kufanya kazi bila ya vitu hivyo viwili. Vile vile, hususan kwamba ile inaonyesha japo inaonesha katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu wapo Zanzibar na wanatumika Zanzibar.

Sasa sidhani kama kuna sababu kusubiri kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati hapa tuko katika masuala la Katiba na Sheria. Wamekiuka Sheria au wanaendelea kukiuka Katiba ya Zanzibar, kwa nini hili tusilizungumze hili suala.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani Mheshimiwa ameshauri kwamba umuandikie hilo swali ili aweze kulifanyia kazi kama nitakuwa nimemuelewa vizuri, yaani umpelekee rasmi tu hilo swali halafu atalifanyia kazi, unasemaje Mheshimiwa?

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Alosema nimuandikie juu ya yule mwanafunzi wa Chuo cha Mafunzo aliyefariki. Lakini suala hili la polisi kalizungumza kwamba hili suala liko nje ya mamlaka yake. Kwa sababu liko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa alivyosema hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mwache atuletee yote hayo tutashirikiana hatuna matatizo. Sisi hatupendelei wananchi wetu kipigwa kwanza, hilo tunalikemea sote tunalilaani, si jambo zuri. Na kama linatendeka hilo tunaomba wenzetu wasifanye hivyo. Lakini nasema suala hili lina sheria wanafata Katiba ya Jamhuri ya Muungamo. Kama ingeikiwa vikosi vyetu jibu ungelipata hapa

hapa. Sasa lakini na hilo jengine hatuna taarifa nalo, tuletee taarifa usiwe na wasi wasi tutashirikiana tu. Wewe unanielewa vizuri sana kama ninavyokuelewa wewe.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Kifungu PG 0104 Programu Kuu ya usimamizi wa masuala ya dini...

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nataka nimthibitishie mwalimu wangu kipenzi Mwalimu Haroun Waziri wa Katiba na Sheria kwamba, nia ya kuzuia mafungu sio kumkomoa Mhe. Waziri, wala kuwa na chuki na waziri. Lakini ni kutaka ufafanuzi wa ziada lakini vile vile kuishauri serikali na tusikilize serikali inatusikiliza vipi.

Nilizungumza katika suala zima ambalo na wenzangu pia wamelilizungumza suala la walimu wa vyuo vya qur-ani na Mhe. Waziri tumemsikiliza vizuri sana alivyokuwa akieleza na alitutaka sisi tuwasaidie walimu hao. Na nataka nimthibitishe Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe tunawasaidia sana walimu wetu wa madrasa na tuna mashirikiano makubwa sana.

Mimi leo ukiniuliza jimbo langu lina madrasa ngapi nakutajia kwa ghibu. Kwa hiyo, ujuwe kwamba tunashirikiana nao kwa karibu. Lakini kama tulivyosema kwamba nchi yetu asilimia karibu 99% waisilamu na walimu wetu hawa wanaisaidia sana jamii yetu ya Zanzibar kuwaweka vijana wetu katika maadili ya kiutu lakini vile vile ya kibinaadamu ndio maana Zanzibar inaendelea kuwa na amani na utulivu wa msaada ya walimu wetu.

Sasa tulipendekeza kwamba tumeishauri serikali kwamba walimu hawa waandaliwe utaratibu maalum ili kuweza alau kupatiwa posho la sabuni. Mhe. Mwenyekiti, alijaribu kuzungumza kwamba tuwasaidie, sisi tunawasaidia katika utaratibu wa sisi kama sisi. Lakini labda tungeishauri zaidi serikali sisi tuna mfuko wa jimbo.

Kwa hivyo, kama humu kwenye mfuko wa jimbo, mimi nafikiri tungeongezewa *amount* fulani. Sasa hivi tumepata milioni 20 tuongezewe milioni 25 ili ile milioni tano alau tupate kifungu cha kuanzia. (*Makofi*)

Halafu baadae hayo mashirika mengine ya taasisi za kiislamu yataongezea, kwa sababu tunataka tuweke mfumo wa utaratibu wa kuwalinda na kuwahifadhi, haiwezekani walimu wetu hawa wanaotengeneza utamaduni wa vijana wetu tukawaachia wafadhili tu kila siku tutegemee wafadhili mpaka lini.

Tutengeneze utaratibu wa serikali yetu iandae mazingira mazuri kuwahudumia walimu wetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, radhi atapata tu asiwe na wasi wasi ata akisimama mara kumi. Mimi nafurahi kila akisimama, nasema bado mwanafunzi wangu ana nguvu.

Nataka nimfahamishe kidogo kwamba suala hili analolipendekesa sasa hivi ninahitajia bajeti. Bajeti ya Serikali tumepitisha sisi humu ndani na imeshapita. Sasa aweke suala lake mwakani tutizame tupendekeze mapema ili tuliingize kwenye bajeti. Lakini bado nasisitiza Mhe. Mwenyekiti, na mfuko wa jimbo ule anaosema ni sisi Waheshimiwa Wawakilishi, tunaosema pesa zile tuzitumie kwa hivi na vile, kuna sheria zake na utaratibu wake na kuna mambo yameelekezwa kwamba haya yanafanyiwe kwa pesa hizi na haya yasifanywe kwa pesa hizi.

Sasa tuangalie vizuri hizi sheria za mfuko wa jimbo. Mhe. Hamza Hassan Juma na wenzako wote na tuliokuwepo humu ndani tuendelee kuchangia ni sehemu ya sadaka ambayo unaitoa wewe hapa duniani kesho akhera itakusaidia. Tusione tabu kutoa shilingi ishirini kumgaia mwalimu wa chuoni. Najua mnatoa sana mnasaidia kujenga; mnapeleka saruji, mabati na kila kitu. Lakini si vibaya kusaidia na pesa.

Lakini kwa sasa hivi mimi nilichosema tutajitahidi kama wizara kusaidiana na Afisi ya Mufti ili kutafuta njia mbali mbali za nchi mbali mbali za Kiislamu ambazo zinaweza kutusaidia katika kuendeleza suala zima la Vyuo vya Qur-ani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri, na kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wetu ndio Waziri wa Katiba na Sheria. Sheria ya Mfuko wa Jimbo tumeipitisha, lakini sisi tulipendekeza sana tuingize na masuala ya dini. Lakini tukaambiwa tusijiingize kwenye masuala ya dini. Lakini sisi ndio tunaotunga sheria lakini vile vile tunayo nafasi ya kuweza kurekebisha hizi sheria zetu. Na suala la kusema kwamba tuendelee kuwasaidia sisi bado itakuwa ni utashi wa mtu binafsi. Sisi tutaka tutengeneze utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia kuna matukio mengi ya uzalilishaji watoto, kwa hiyo, ina maana hawa walimu tukiwatengeneza uzuri tukiwaekea mfumo mzuri wa kaserikali, mimi nadhani tutakuwa tumewapa nguvu hawa.

Sasa mimi simlazimishi lazima tupitishe katika bajeti hii, lakini Mhe. Waziri, hili aondoke nalo na sisi tutaendelea kulifanyia kazi. Sisi nchi yetu kila siku tunaengeza mapato tutajaribu kuangalia tumeanzisha mfuko wa Miundombinu hapa na mfuko ule tumeusema kwamba fedha zake zinagawanywa katika maeneo mbali mbali. Kwa hiyo, hata katika zile fedha za mfuko wa Miundombinu, mfuko ukijaa tunaweza tukapendekeza, basi hii bilioni moja kwa mwaka huu ianze kuwasaidia walimu wa madrasa hata kama shilingi na nusu.

Leo nafikiri alizungumza mwenzangu, toka jana kwa kweli watu wengi duniani hata mimi nimefurahi *BBC, CNN* wamemsifu sana Rais wa Zanzibar kutokana na namna gani alivyoweza kuwajali wazee, yaani nchi masikini lakini imeweza kuwajali wazee. Sasa hebu tuengeze na hichi kitu chengine, mimi naamini Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman, ni mtu ambaye ni mzuri sana, ambaye anaweza kubuni mipango na programu akaishauri serikali mwakani tukaanza japo kidogo kuwasaidia walimu wetu. Anikubalie tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kanambia mtu mzuri na mimi nafurahi kwamba mzuri.

Sasa Mhe. Hamza Hassan Juma, tuendelee kadri tunavyokwenda, lakini msimamo wangu tutafute msaada kwa njia nyengine kwanza sasa hivi. Kwa sababu tukifanya marekebisho ya sheria kuna suala zima la Katiba linasemaje. Itabidi turekebishe mambo mengi sana. Sasa hebu tusifanye haraka, tufanye subira. Lakini tuachie tukatafute njia mbali mbali za msaada, mimi ni mmoja mwenye uchungu sana wa dini ya kiislamu kwa sababu ni muislamu na naipenda dini yangu ya kiislamu na *alhamdulillah* hamniti tu lakini nimeshakuwa *Alhajj* sasa hivi. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, napenda nimuhakikishe Mhe. Hamza Hassan na Waheshimiwa wote kwa jambo hili, tutashirikiana kwa hali na mali kuhakikisha kwamba walimu wetu wa vyuo vya qur-ani *inshaalla* wanapata fursa nzuri. Mafunzo tunawapatia kwa njia mbali mbali, semina tunawasaidia kuwapatia vile vile na haya mambo mengine tutatafuta njia ya kuwasaidia. Lakini si kwa utaratibu wa kiserikali, sasa hivi hatuwezi kujifunza kwa sababu bajeti tayari, wasubiri bajeti ijayo wapendekeze ili tufanye utaratibu na wale ni wananchi wetu wale.

Mhe. Abdalla Mauli Diwani: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia juu ya masuala ya Afisi ya Wakfu au Mufti kwa sababu masuala ya dini haya mimi

niliingia sana katika suala zima la kuratibu safari za Hijja, kuna mashirika zaidi ya 16 yanapeleka mahujaji wetu kule kwenda kuhiji Makka, tukazungumza gharama zile ni biashara imekuwa zaidi sasa kuanzia dola elfu nne mpaka elfu nne mia tano na nikamuomba Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya michanganuo basi anijibu hili saula. Nafikiri kashindwa kunitolea maelezo. Sasa labda kupitia nafasi hii anipe yale majibu yangu yamekuwa vipi na tukitoka hapo tutakuja na maswali mengine.

Mhe. Mwenyekiti: Una swali jengine kwenye kifungu hichi hichi. Uliza kabisa kwa sababu sitakupa tena nafasi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekuiti, zile nyumba za Wakfu zinazouzwa zina utaratibu gani mpaka zinauzwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hili la Hijja ni bahati mbaya nimelisahau lakini ninalo na kwa ruhusa yako nilisome.

Kwanza Hijja ni ibada inayowahusu waislamu wenye uwezo. Kwa vile uwezo wa watu na mahitaji yanatafautiana hata gharama za Hijja zinatafautina. Kwa sababu inategemea ndege unayoingia ukiingia *Qatar*, Oman, Ethiopian bei tafauti Mhe. Mwenyekiti. Halafu ukifika kule Makka nyumba iliyo karibu na msikiti bei yake tofauti na iliyokuwa mbali na msikiti. Kuna wengine wanakaa meli mbili, tatu huko ndio wanapata tabu kweli hata ukifika jamaa zote zimeshamalizika, unakuta mengine tena.

Kwa hivyo, bei zinatafautina hakuna *formula* ya kusema kwamba hii ni bei ya Hijja kwa kila mtu. Inategemea lile shirika lenyewe na ile kampuni yenyewe ambayo inashughulika, ni biashara hii. Halafu ukifika kule kuna *services* kuna wengine wanahudumia milo mitatu; asubuhi, mchana na usiku. Kuna wengine wanahudumiwa mchana tu asubuhi na usiku wanajitegemea. Kwa hivyo, hakuna *formula* maalum ya kuweka kiasi gani.

Kwa hivyo, kama unataka zaidi *detail* nitakuomba uwe mstahamilivu *inshaalla* tutalifatilia zaidi katika afisi zetu zinazohusika ili tukuletee *detail* za kila shirika wana-*charge* kiasi gani na kila taasisi wana-*charge* kiasi gani tukuletee na wala hatuna matatizo lipo kabisa, Wakfu juzi wameshaniletea taarifa zote ninazo. Sikujua tu kama utaniuliza, ungeniuliza toka juzi ningelikuwa nimeshakupa jibu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi wakati wa kuchangia Bajeti niliuliza kuhusu suala la Wakfu na Mali ya Amana. Nilisema Mhe. Mwenyekiti, kuna mali za Wakfu lakini mali hizi nataka kujua ni mali ngapi na za aina gani? Pia, kuna maneno ambayo sina ushahidi nayo lakini hizi mali namnukuu mtumishi mmoja kutoka taasisi hiyo akisema kwamba, hizi mali zikikaa zina mtihani. Kuna wanjanja wanataka kuzidhulumu na wengine wameshazidhulumu mali hizi.

Sasa hoja yangu ilikuwa mali ngapi zinachangamoto hizi nilizomnukuu mtumishi mmoja kwamba hali hizi kuna wajanja nyengine wameshazidhulumu na nyengine wanataka kuzidhulumu ambazo zina changamoto za kutoka kudhulumiwa au zimeshadhulumiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria,Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, idadi ya mali za Wakfu nisikilize Mhe. Hassan Khamis, aina za nyumba za Wakfu; Unguja kuna nne na Pemba kuna kumi na mbili na jumla yake ni kumi na sita katika nyumba hizi.

Kwa mujibu wa sheria kuna kitu kinaitwa 'Wakfu' halafu kuna kitu kinaitwa 'Amana' kwa hivyo, kuna moja Unguja na Pemba tisa jumla ni tano na huku 21. Halafu kuna aina nyengine ya Wakfu na Amana jumla ya Unguja ni 254 na Pemba nane Amana 37 na Pemba mbili jumla 301.

Hakuna mali zilizotumika visivyo kwa vile mali zote hutumika kwa mujibu wa wasio uliowekwa na mwenye mali. Yaani hizi nyumba za Wakfu yule anaetoa Wakfu anasema kabisa nyumba hii ifanyike moja mbili tatu na Wakfu hawezi kwenda kinyume na maagizo ya yule mwenyewe anaetoa mali, ndio zake na anatoa Wakfu, sadaka anayotoa kwa wale watakayoitumia. Kwa hivyo, utaratibu ni huo, nadhani maelezo yanatosha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ni nyumba tu Wakfu wanazo lakini mimi najua mashamba yapo ya Wakfu nayajua ambayo ndio miongoni mwao mwa changamoto, mali hizi ni nyumba tu?

Mhe. Mwenyekiti: Ngojea Mhe. Waziri, nafikiri ana *reference* hapa ngoja aangalie.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumtosheleza Mhe. Hassan Khamis Mwakilishi wa Jimbo la Welezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri, anazungumzia idadi ya mali zote, kwa hivyo, ametoa kwa jumla mashamba na nyumba. Sasa naomba nirejee kidogo ili tuweze kufahamiana.

Idadi ya mashamba ni 16 kwa maana kwamba Unguja kuna 4 na Pemba 12. Sasa ukija idadi ya nyumba kuna za Wakfu Unguja 254 na Pemba 8, sasa kwa jumla hizi aina hii utapata 262. Halkadhalika, Amana kwa Unguja kuna 37 na Pemba 2 na jumla ni 39. Sasa kwa jumla zote za Unguja tutapata 291 ambao Pemba kuna 10, jumla kuu itakuwa 301. Ahsante Mhe. Naibu Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PG 010401	Programu Kuu ya usimamizi wa masuala ya dini	
Kifungu SG 010401	Programu mdogo ya usimamizi wa masuala ya dini	Shs. 333,707,000/-
Kifungu PG 0105	Programu kuu wa mipango na Utawala...	

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akitoa majuisho alijibu suala langu. Akasema kwamba baadhi wamerudishwa lakini wengine walikataa. Lakini mimi nasema si kweli kwa sababu kuna kijana anaitwa Moh'd Abrahaman Mwinyi alikuwa ni Muhasibu Afisi ya Mkoa wa Kusini Pemba na huyu alifika hata kuandika barua hakuna kilichoendelea. Je, Mhe. Waziri, uko tayari nikukutanishe na mtu huyu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shadya Mohamed Suleimani, ni binaadamu kazungumza vizuri Naibu Waziri, mimi nampongeza sana kajibu vizuri suala hili.

Kwatwambia kama kuna mtu yeyote, yaani mfanyakazi yeyote ambaye hajaridhika na lile ambalo limetendeka na bado anahisi yuko nje basi aje tuliangalie kwa mujibu wa sheria.

Kifungu PG 010501	Programu ndogo ya uongozi na utawala	Shs. 1,730.644,000/-
Kifungu SG 010502	Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	Shs. 507,325,000/-
Kifungu SG010503	Programu ndogo ya kuratibu shughuli za (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba	Shs. 680,688,000/-
	Jumla	**Shs. 578,456,000/-**

Kifungu PG 0106	Programu kuu ya usimamizi wa rasilimali watu mifumo na miundo ya taasisi	Shs. 236,475,000/-
Kifungu SG 010602	Programu ndogo ya maendeleo ya Miundo na mifumo ya taasisi	Shs. 270,850,000/-
	Jumla Kuu	**Shs. 507,325,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

PG 0107 Programu Kuu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimpongeze Mhe.Waziri na Naibu Waziri, kwa majibu mazuri yaliyozungumzwa na nikiri kwamba Mhe. Waziri, ni baba yangu, rafiki yangu, kiongozi wangu pia wa Mkoa.

Lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sisi tupo hapa ili tupate majibu yenye kuturidhisha kabisa, kwa sababu watu wa kupewa matumaini ni wananchi. Hivyo, mimi kuna majibu bado sijaridhika vya kutosha na hasa katika hili suala la *e-government* ambalo lipo hapa.

Majibu niliyopata ni kwamba, yalivyozungumzwa na Mhe. Waziri suala la *e-government* limeanza miaka mitatu. Majibu tuliyopata hapa ni kwamba kuna mawasiliano tutachukuliwa, tutapelekwa kwenye semina. Masuala niliyouliza hayapo kabisa. Nimetaka kujua ni jinsi gani hizi milioni kumi na nane Dola ambazo sawa sawa na bilioni zaidi ya thalathini sita za Tanzania, kitu ambacho huwa tunajigamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba tutakuwa *connected* na suala la *e-government*. Lakini hata leo kuna taasisi za serikali bado zinatumia *e-mail* kutoka kampuni binafsi *Internal Service Provider(ISP)*. Lakini mbali na hilo Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kabisa ni kwamba hili suala la *e-government* wame-*connect* na *Fiber Optic* kupitia hii *Submarine Cable* ambayo inapita kutoka Zanzibar inakwenda Tanzania Bara, inaunganishwa hii moja kwa moja kwenda zake mpaka Tanga, tunatumia *Fibre Optic* yetu ya Pemba kwa mzunguko wote kuhakikisha kwamba tunapata huduma za kutosha *Internal Service Provider*.

Lakini pia hawa wameingia mkataba na *ZANTEL* na kuna fedha zinatakiwa serikali idadi au tayari tunataka tujue serikali imepata kiasi gani katika hizo

kwenye muda hichi kipindi ambacho tangu huu mkataba umefungwa. Na nimesema moja kwa moja ninahitaji maelezo mazuri kwenye suala la *e-government*, kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amezungumza katika hotuba yake, amesema kwamba tunakwenda kwenye mpango wa pili sasa wa *e-government*.

Sasa angalau huu mpango wa kwanza wa *e-government*, sisi kama Wajumbe tunaambiwa tutakwenda kwenye semina. Hivi kweli itakuwa ni haki tunawatendea wananchi, miaka mitatu. Hebu naomba kidogo tupate maelezo mazuri tujiridhishe kabla hii hapa halijatoka. Mimi sihitaji matumaini, ninahitaji majibu mazuri. Matumaini mpaka niwape wananchi.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa. Eeh! Mhe. Waziri wa Afya, atasaidia.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kama ilivyokuwa kawaida na Kanuni pia, serikali yote iliyokuwepo hapa inawajibika kwa pamoja. Na tuna wajibu mkubwa kuwa panapotokezea jambo kama hili kutoa maelezo na mimi nitaomba nitoe maelezo kwa sababu mradi huu ninaufahamu kwa kina kidogo.(*Makofi*)

Mradi huu Mhe. Mwenyekiti, unagusa wizara tatu na ndiyo maana Mhe. Waziri alikuwa anasisitiza itolewe semina, kwa sababu hata Baraza lililopita Wajumbe wengi walikuwa wakiuliza maswali hapa na mimi pia niliwahi kuchangia na kutoa maelezo ya ziada. Nikatoa mfano kwamba huyu ni mke mmoja mwenye waume watatu na nikatoa pia ufafanuzi kwamba Wizara ya Mhe. Maalim Haroun, Wizara ya Mhe. Ali Karume inahusika pia na Wizara ya Fedha inahusika.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani, ni mke mmoja mwenye waume watatu au mume mmoja mwenye wake watatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Hapana, 'mke mmoja, waume watatu' kwenye kitabu cha Bwana Msa, nanukuu; 'Mke Mmoja, Waume Watatu'.(*Makofi*)

Sasa mimi ninahisi tungemuomba akubali itolewe semina, kwa sababu mradi huu katika maelezo *phase I* ni kutandika ile barabara ya lami, yaani hii *Fiber Optic* ndiyo barabara yenyewe. Hiyo *phase* ya pili ndiyo kupitisha hayo magari

kwenye barabara ya lami, ninatoa kwa lugha hii ya *layman* ili iweze kufahamika vizuri zaidi.

Sasa katika hii *phase II*, hata sisi Wizara ya Afya tumo na sisi ndiyo wa mwanzo kabisa. Tupo *e-health*, kuna *e-tax* na *e-tourism* eneo la Mhe. Simai Mohammed Said. Eneo la Mhe. Simai *e-tourism* pia ipo. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana Mhe. Simai, akubali tufanyiwe semina, Wajumbe wote na sisi tutashiriki pia, serikali nzima ninaamini itashiriki katika semina hiyo.

Tufanyiwe semina na baada ya semina, tuulize pia maswali ya *phase II* patakuwa nini na nini. Kwa sababu hata sisi katika *phase II* vituo vyetu vya afya vyote vinatakiwa viunganishwe na hivi leo tumeupokea na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, tumempokea *governor* wa Jimbo la Jiangsu. Na katika mazungumzo yao sehemu kubwa aliyozungumzia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye mwenyewe ni mradi huu wa *e-health* na *e-government*.

Kwa hivyo, naomba sana tupate hiyo semina kwa sababu Wajumbe wengi ni wapya, watapata taaluma kubwa. Kuna kitengo pale kizuri, jengo zuri ambalo watatoa taalum hii ya kutosha, halafu tutapata kuzungumzia hii *phase II* na siyo *phase II* tu, itakuja na *phase III*, *phase IV* mpaka Mhe. Mwenyekiti, wewe ukikaa pale kwako juu, wewe huna kompyuta pale, utakuwa moja kwa moja unajua ni watu wangapi wameuliza maswali mangapi, *at click of finger*, unabonyeza tu pale, unabonyeza tu pale juu na unapata kila kitu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kajibu kitaalamu, mimi ninataka nimuhakikishie kwamba jibu lilikuwepo lakini niliona muda ni mdogo na kwa taarifa yako ukiniruhusu ninaweza nikaisoma yote hii *page* moja, halafu baadae nikamuachia akaisoma zaidi Mhe. Simai Mohammed Said, kwa sababu serikali hii haijibu majibu kwamba kwa kuondosha njiani, na nimesikitika sana na anavyosema kwamba tujibu maswali ambayo wananchi wanayasubiri, tusijibu tukaondosha njiani. Mhe. Mwenyekiti, majibu yapo na kwa ruhusa yako ama nisome au nimkabidhi moja kwa moja, nipo tayari.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ninadhani umkabidhi kwa sababu tunajaribu kuuwokoa na wakati.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningependa kuyajibu yale, si ninaruhusiwa kujibu na mimi? Mimi ninakubaliana na hilo suala la semina na ninaunga mkono, lakini ijapokuwa nina upya wangu, lakini pia nina maarifa. Kitu nilichokiuliza kwa muda wa miaka mitatu kwa manufaa tuliyopata, tutaendelea mimi hichi nitapita nacho.

Lakini ninachokiomba kitu kimoja. Suala la kwanza juu ya hii *Fiber Optic*, Kampuni ya *ZANTEL*, tunataka kujua ili tuletewe maelezo mazuri huko mbele, ni kiasi cha fedha serikali imeshapoteza, kwa sababu hawa wanatoa huduma kwa wanafanya biashara. Pengine Mhe. Waziri, inawezekana yeye hili halijui.

Suala la pili, Kabla hatujaenda katika hiyo semina kwa ajili sote sisi Wajumbe juu ya suala la *e-government*, haya ambayo tutakuja kuzungumziwa yote kwa pamoja, *e-health*, *e-tax* basi angalau katika kipindi cha mwaka huu katika masuala ambayo tayari yalikuwa yanafanyika muda wa miaka mitatu na katika taasisi hii, inaelekea kuna uzembe paingiliwe kwa undani. Kwa sababu huu mradi unaelekea kama hauna mwenyewe. Hamna mtu ambaye anasimamia lakini inaelekea wale walioanza nao, ndiyo waufuatilie ili hatimaye yake serikali iweze kufaidika, kwa sababu hizi fedha ni nyingi mno.

Na kwa muda miaka mitatu hivi *internet* kuunganisha ndani ya serikali tunahitaji utaalamu gani wakati tayari hii *Fiber Optic*, wenzetu wapo mbali sana wanaendelea sasa hivi. Kweli masuala ya *archieve*, masuala ya *communication*, masuala ya *storage*, haya katika mwaka huu yaanze kufanyika ili Rais wetu atakapokuja kuzindua masuala ya *e-government* angalau ang'are.

Mimi siyo Mpinzani, mimi ni mwana-CCM, ninasema kitu cha ukweli. Mimi ninakubali hichi kifungu kipite. Naomba maelezo yangu na mimi na haya niliyozungumza yachukuliwe na Mhe. Waziri, mimi ninamuamini na wote waliozungumza pamoja na rafiki Mhe. Waziri wa Afya, nao pia wanahusika, basi suala hili lianze kufanyiwa kazi, 'hapa kazi tu'. (*Makofi*)

Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia ingawa jawabu nilipata lakini ilikuwa *verse vesa*, nilitaka kujua huu mradi wa *e-government* umechukuliwa na wizara gani? Kwa sababu ya Wizara ya Fedha

na Mipango anasema *e-government*, Wizara ya Miundimbinu *e-government*, Wizara ya Utumishi *e-government*. Ningeomba hapa ufafanuzi kidogo.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Afya, kaeleza vizuri sana hapa, katoa kitabu cha Bwana Msa. Kasema 'Mke Mmoja, Waume Watatu'. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Mwakilishi, *e-government*, *management* ipo Wizara yetu ya Utumishi, *technical side* ipo Wizara ya Miundombinu na *financial* ipo Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, ukiendelea utakuwa bado unaninyima utamu mkubwa sana niliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti: Hujaridhika bado? Eeh! Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Kitu chochote kile kina kwao, mimi kwetu Donge, wengine kwao Kizimkazi Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Sasa huwezi tu kuniambia kama hichi kipo hapa na hapa, lazima kutakuwa na *source* ilikotokea ni wapi, *root* ile ilikotokea na nani anahodhi?

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nina hamu ya kumjibu. Nilisimama kabla hujaniita.

E-government ipo chini ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hata huyu Mkurugenzi wa e-*government* tunaye sisi. Sisi ndiyo dhamana, lakini mambo mengine yote ya kitaalamu yapo huko kwenye wizara nyengine. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe.Mwenyekiti, tuendelee.

PG 0107	Programu Kuu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali	Shs.526,034,000/-
SG 010702	Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa	

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, jana niliuliza sana habari ya nyaraka za serikali. Nimejibiwa sana, Mwanasheria Mkuu kajitahidi, Waziri kajitahidi lakini bado sijafahamu. Kwa hivyo, naomba tena maelezo ya juu ya kina ya nyaraka za serikali zilizoibiwa na wasaliti wa Mapinduzi ya 1964 ya wakwezi na wakulima.

Kwanza, lilijuulishwa Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi wa Unguja na Pemba, nani aliziiba nyaraka hizi na wamepewa adhabu gani na pia, hivi sasa hizi nyaraka zipo wapi nchini kwetu au bado zipo nje ya nchi?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na tokea asubuhi kama ambavyo tulivyokuwa tumelizungumzia jambo hili na tumekuwa tukitoa ufafanuzi baada ya ufafanuzi. Nilidhani tulifika pahali tulielewana. Tulifika pahali nadhani tulielewana kama jambo hili halikuanza kwenye Baraza hili. Jambo hili lilianza kwenye Baraza la Nane ambalo limemalizika.

Na liliundiwa Kamati Teule, kama wao inavyowauma na wale walioondoka iliwauma hivyo hivyo na ndiyo maana likaundiwa Kamati Teule. Kamati Teule ikafanya kazi yake, ikatoa ripoti yake, Baraza likaijadili na Baraza ikaridhia maazimio ambayo serikali inatakiwa iyafanyie kazi. Sasa kwenye taarifa ambayo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, ameleta hakuna taarifa hiyo ambayo ameleta. Na Waheshimiwa Wajumbe, wamekuwa na hamu sana ya jambo hili kuliendeleza na wametoa kanuni nyingi za kuzungumzia jambo hili na tumefika pahali tumekubaliana, basi warudi kwenye yale maazimio wayatazame na kama kuna jambo ambalo inahisi serikali halikufanyia kazi, walete tu hizo hoja na serikali itajibu. (*Makofi*)

Mimi ninadhani tulifikia pazuri Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Naam! Mheshimiwa, hapana wewe unaendelea, nipo na wewe mpaka tumalize.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, na ugeni wetu kama tulivyoambizana tunahitaji mafunzo. Lakini Kanuni ya 59(4) inasema; "Suala lolote ambalo lilijadiliwa katika Baraza, si vizuri tena kujadili tena". Lakini hii ilikuwa iwe mwezi wa Machi na Machi hakukuwa na Baraza ambayo Kamati Teule ilitakiwa ilete ripoti hapa.

Kwa maana hiyo, Kamati Teule haikuja na hakuna ripoti iliyoambiwa Baraza. Kwa hivyo, bado ninasisitiza Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji taarifa za *documents* za nyaraka tupewe.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, Mheshimiwa, ninadhani Kamati Teule ilileta ripoti. Nadhani kitu kinachohitajika ni serikali sasa kuleta taarifa juu ya ile ripoti. Serikali ije itoe maelezo juu ya ile ripoti ya Kamati Teule. Kwa sababu Kamati ilifanya kazi ikawasilisha ripoti yake kwenye Baraza, lakini sasa serikali bado haijaleta maelezo. (*Makofi*)

Sasa labda ndiyo tuwape nafasi serikali waje watupe maelezo kuhusiana na ile ripoti, maelezo ya hiyo ya Kamati Teule kwa hiyo kazi waliyoifanya, serikali waje waeleze hapa. Ninadhani kama nipo sahihi. Mhe. Mwanasheria Mkuu, hebu saidia.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ulivyo na ambao Mhe. Abdalla Ali Kombo, anauzungumzia ni kwamba yale yote serikali inatakiwa kutoa taarifa. Kwa mfano tumejadili ripoti ya *CAG*, haijajadiliwa kwenye kikao hichi. Sababu yake kikao cha Machi, serikali inabidi ije itoe taarifa ya utekelezaji kwa yale ambayo yameelezwa kwenye ripoti ya *CAG*. Sasa tulikotoka hatukukuwa na kikao kile cha Machi ambacho serikali ingeweza kuleta taarifa.

Tumeanza Machi lakini *of course* Baraza limeanza tarehe 30. Kwa hivyo, yale ambayo yalikuwa tuyafanye kwenye kipindi kile hatukuweza kuyafanya na baadae tumeingia kwenye Baraza la Bajeti. Sasa mambo mengi haya yamepangana nadhani Waheshimiwa Wajumbe wanaelewa, sina haja ya kuyazungumzia kwa nini tumefika hapa. Sasa hili tumeshalizungumza kama Kamati hiyo iliteuliwa, ni kweli, taarifa ililetwa, maazimio yametolewa, serikali imefanyia kazi, waliosafiri wamesafiri na taarifa wakaleta.

Sasa kama kuna jambo, ninadhani asubuhi Mhe. Mwenyekiti, umelielezea vizuri katika Kanuni na Kanuni zinaeleza vizuri. Kama kuna jambo halikatazwi kuletwa tena ili likatolewa tena taarifa. Halikatazwi na wala sisi serikali hatuna haja ya kuzuia ya kutoa taarifa, liletwe na taarifa zitaletwa kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa bado.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, sijawahi kuwa Mwakilishi, lakini huwa nina uzoefu wa kusikiliza Baraza la Wawakilishi. Majibu kama haya ni majibu ya kawaida, tutafuatilia, tutaleta. Mwaka jana iliahidiwa kwamba mambo yote yatakuwa tayari. Mwaka umekwisha na leo wananchi wetu wanatungojea hakuna jibu.
Labda serikali sasa inatuahidi nini itatuletea mambo haya katika bajeti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ninadhani Mhe. Mwakilishi Mhe. Abdalla Ali Kombo, hoja yake serikali imeisikia na Mwanasheria Mkuu amejitahidi sana kutoa maelezo juu ya utaratibu wa hii hoja ilipoanzia.

Hoja hii ilianza kwa michango ya Wajumbe kwenye Baraza lililopita. Baadae Mjumbe akaleta Hoja Binafsi. Mhe.Mjumbe, alipoleta Hoja Binafsi ikajadiliwa ndani ya Baraza hili Tukufu. Serikali ikapokea maazimio ambayo yalitolewa na Baraza kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Serikali ikenda ikayafanyia kazi. Serikali ikarudi ikaja ikato taarifa ndani ya Baraza lako Tukufu Mhe. Mwenyekiti. Kilichofuata baada ya serikali kutoa taarifa, Baraza likatoa ushauri na maagizo ya kutekelezwa.

Moja, lilikuwa ni kuhakikisha nyaraka zetu zinarudishwa. La pili lilikuwa ni kuhakikisha waliohusika wanachukuliwa hatua, wale wanaostahiki kupelekwa kwenye vyombo vya dola vya kisheria wapelekwe. Wafanyakazi ambao walikuwa wanahusika walishafukuzwa kazi. Moja kati ya hatua ambayo serikali imeichukua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala lililobakia ni kwamba shutma zilikuwa zinaonekana ni kati ya nchi na nchi. Hapa kuna masuala ya kidiplomansia, ikabidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iiarifu rasmi *Foreign Affairs* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iwasiliane na *Foreign Affairs* ya Serikali ya Watu wa Oman, ukaondoka Ujumbe mzito ukiongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje, pamoja na Waziri ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Dk. Mwinyihaji Makame na Mwenyekiti aliyekuwa wa Baraza la Wawakilishi Mwakilishi wa Kikwajuni. Ijapokuwa Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame anawakonyeza baadhi ya *backbenchers*, lakini yeye anayajua mazungumzo yaliyofanyika kwenye Serikali ya Oman.

Kwa hivyo, kinachotakiwa Serikali ya Oman...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, usimshtumu Mhe. Mjumbe, wewe endelea kujibu tu. *(Makofi)*

Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame nakulinda kwenye hili naomba ukae. Nakulinda Mhe. Dkt. Mwinyihaji nakuomba ukae, nakulinda. Usimshtumu Mhe. Mjumbe. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Naomba radhi kwa hili. Kinachotakiwa kati ya mazungumzo yale ya Serikali ya Oman kama ilivyo... *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, unaninyima fursa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ngojea amalize, ngojea amalize. Subiri Mheshimiwa amalize halafu nitakupa wewe *(Makofi)*

Basi Mhe. Waziri, nakuomba kaa wewe tumpe yeye. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame umeombwa radhi, amekuomba radhi Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti...

(Mhe. Mjumbe hapa alizungumza bila ya kuwasha kipaza sauti huku wajumbe wakimshangiria kwa kupiga Makofi)

Mhe. Mwenyekiti: Haya ok. Sawa nimesikia *(Makofi)*

Tuendelee Mhe. Waziri. Ondosha hayo maneno Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nilitangulia kumuomba radhi kama nimemkwaza. Kwa hivyo namuomba radhi..

Mhe. Mwenyekiti: Ondosha eeh, Futa na hiyo kauli Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Kwa hivyo, namuomba radhi na nafuta hiyo kauli.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Sasa endelea Mhe. Waziri *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Lakini, nikiwa kama serikali, natoa maelezo ya serikali. Hatua iliyobaki ni Serikali ya Oman kuturejeshea nyaraka zetu kama ilivyotuahidi. Sasa kwa nini taarifa haijaja Barazani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu ameeleza vya kutosha, kwamba tuna utaratibu kwa mujibu wa kanuni, kwamba mambo tunayoyajadili ndani ya bajeti na kwenye taarifa nyingi, Kikao cha Machi/Aprili serikali inakuja na taarifa. Sasa dharura hiyo ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wakalielewa, kwa sababu sote tunaumwa na hizo nyaraka. Ni nyaraka zetu na ni haki yetu Wazanzibari, na ndio maana ukapita utaratibu wa kidiplomasia kwenda kuzungumza na wenzetu na kusingekuwa na njia nyengine zaidi ya hiyo kwanza. Bahati nzuri Serikali ya Oman kwa mujibu wa taarifa tulizonazo serikalini walikubali kwamba watarejesha.*(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nadhani Waheshimiwa Wajumbe, wakubali kwamba serikali ilete mrejesho wa hatua zilizokubaliana kati ya Serikali ya Oman na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema hayo. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, lakini tukubaliane kwamba nyaraka zitarejeshwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla Ali. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, na mimi suala hilo hilo napiga buti kwa vikali sana na nina sababu.

Mhe. Mwenyekiti: Suala lipi tena Mhe. Hassan lako wewe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hilo hilo na mimi nililichangia.

Mhe. Mwenyekiti: Hili hili?

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Heeh! ninayo haki. Yeye kamaliza mimi bado.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, hapana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Aaah! Mhe. Mwenyekiti, utanionea.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mheshimiwa, twendeni kwenye Kanuni. Twende kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, utanionea.

Mhe. Mwenyekiti: Sikuonei Mhe. Mjumbe. Kanuni ndio inayokuonea. Suala hili hili limeshakamilishwa, sasa wewe unataka kulianza tena upya.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hapana, Mhe. Mwenyekiti, hili suala kila mtu tulilichangia, na ninatoa maelezo. Mhe. Mwenyekiti, tusilindane dhidi ya hili suala.

Mhe. Mwenyekiti: Simlindi mtu Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Usimlinde mtu dhidi ya hili suala.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, Mheshimiwa usikionee Kiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: TV za Zanzibar zinatuona, umma unatuona. Nyaraka za wana Mapinduzi zimeibiwa na watu wa hapa ndio waliozitoa, na wengine wanasadikiwa wamekula pesa.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba ukae Mheshimiwa. Mhe. Mjumbe kiti hakimlindi mtu, kwanza lazima ufahamu hivyo. Unapewa nafasi unauliza, halafu hoja zinajibiwa na serikali. Mimi kazi yangu ni hiyo, ni kama *referee* tu, siko upande wowote niko katikati na ndio maana nimekaa huku.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nisubiri kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

(Hapa Mhe. Waziri alizungumza nje ya kipaza sauti)

Mhe. Mwenyekiti: Ndio nitakupa nafasi. Hii hoja Mhe. Abdalla Ali Kombo, vipengele vyote ambavyo alikuwa ameuliza vimetolewa majibu, yeye mwenyewe anasema hakuridhika lakini tuendelee. Sasa wewe unataka turudi tena kwenye jambo ambalo tayari limeshazungumzwa na serikali, uwaulize tena maswali yale yale na mwengine na yeye atataka hivyo hivyo. Enhee nakusikiliza sasa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaendeshwa na Kanuni. Najua wewe ni mzoefu sana umeshafanya kazi mpaka Bungeni. Sasa kanuni gani ungeniambia inanizuia, kwa sababu hapa vipengele vyote mtu

anasimama anauliza kile kile. Wakfu na Mali ya Amana hapa wajumbe wamechangia watatu. Kwa hivyo, hii yule kamaliza mimi bado, vyenginevyo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una kitu kipya zaidi ya hicho. Yaani hoja yangu ni kwamba kuna jambo jipya zaidi ya hilo. Kama unalo jambo jengine Mhe. Mjumbe. Unalo jipya zaidi ya hili analouliza Mhe. Abdalla Ali Kombo. Kama unalo jipya ndio nakuruhusu sasa ulizungumze hilo jipya.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ninalo jipya.

Mhe. Mwenyekiti: Haya twende tulisikie. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kuchangia hii hoja kwa sababu nilisema mwanzo. Kwanza nataka ieleweke wazi wazi Mhe. Mwenyekiti. Hoja ya nyaraka ni nzito kwa taifa letu na sababu mbili kuu natoa.

Mhe. Mwenyekiti, sababu hizo ni kwamba nyaraka hizo hazijaibiwa wamepewa Oman, cha kushangaza na kusikitisha Mhe. Mwinyihaji Makame alikuwa kweli anatukonyeza akisema kwamba ...

Mhe. Mwenyekiti: Usiende huko.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sendi huko nanyamaza. Hoja yangu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: *Order* kidogo Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Narekebisha kauli yangu. Nafuta kauli yangu ya kumtaja Mhe. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba tukae Waheshimiwa Wajumbe,

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hoja yangu suala hili Mhe. Mwenyekiti, ni zito, ni gumu. Kwa hivyo, bado serikali haijaja na msimamo dhidi ya suala hili. Kwa vile serikali haijaja na msimamo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, serikali imeshasema wataleta maelezo kama mtakuwa hamkuridhika utafuata utaratibu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tunaiomba serikali itwambie maneno dhidi ya suala hili, kwa sababu ni *hot issue* kwa jamii ya Zanzibar, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Bado nyanyuka.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Lete hayo maelezo ili serikali isikie ikujibu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ombi langu ni kwamba kikao cha mwezi Septemba serikali ituletee ripoti, kwa sababu mimi binafsi ilikuwa kesho asubuhi nataka kuwasilisha hoja binafsi hapa kwa suala hili. Lakini naomba kikao kijacho serikali ije na majawabu dhidi ya suala hili. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Maalim Haroun, yaani anataka maelezo wakati wa mwezi Septemba yawe yamepatikana, sijui serikali inasemaje.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, tunafanya kazi kwa mujibu wa kanuni, hatuwezi kufanya kazi kwa *pressure*, wala hatufanyi kazi kwa sababu ya kumuona mtu au kumuonea mtu, taratibu ziko.

Kanuni kama zinasema ripoti kama zile na shughuli kama zile ripoti zake na maelezo yake yataletwa kwenye vikao vya Machi basi tusubiri mpaka Machi tukijaaliwa, hujaambiwa kwamba lazima mwezi Septemba, itakuwa tunavunja kanuni ambayo tumeitunga sisi wenyewe.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri nimekuelewa. Waheshimiwa Wajumbe, suala la kuharibika uchaguzi sote tunafahamu lilivyoikumba nchi. Hizi ripoti kumbe zilitakiwa mwezi Machi ziwe zimewasilishwa na wakati wake wa kufanya hivyo ni Machi. Kwa hivyo, mnatakiwa mstahamili mpaka wakati huo taarifa hizi zitaletwa kwa ukamilifu wake. Au vipi?

Waheshimiwa Wajumbe: Sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, *chapter* ile ya mwanzo ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imepita. Lakini naisemea hii...

Mhe. Mwenyekiti: Ya pili sasa.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Naona Mhe. Hassan Khamis hakumaliza, watu wamemdakia. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Enhee nakusikiliza bado.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Ndio nikasema bora tungemuachia mwenyewe angemaliza. Lakini sasa namsoma ile aliyotaka kusema. Kweli kwa sababu mimi nilikuwa mdau mkubwa wa suala hili. Katika watu waliokwenda hiyo safari waliyosema Mhe. Waziri mimi ni mmojawapo. Kwa hivyo, naijua *A to Z* mpaka yale ambayo ile ripoti tumeipeleka kwa Mhe. Rais aliyotutuma, ripoti yetu hii. *(Makofi)*

Sasa mimi sio mjinga kama alivyofikiria Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mimi sio mjinga, ripoti nimempelekea Rais na maamuzi yetu, halafu nije niwaambie watu. Mimi sio mjinga kiasi hicho. Wao waliponijia, kwa sababu mimi ni mdau, nikawaambia jamani hili suala limeshafika kwa Mhe. Rais na maelekezo yapo na Barazani imeshaundwa kamati na kila kitu, hivyo liacheni...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hata mimi ni shahidi. Sio kwa hili, lakini kwa mambo kama haya serikali mara nyingi imekuwa kama unaibeba badala ya kuikandamiza. Kwa hivyo, siamini kama unaweza kufanya kitu kinyume chake. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa mimi kwa heshima yangu, na kama ninavyosema na kiapo nilichokula humu na nilikuwa waziri, *15 years* niko mbele huko, siwezi kufanya mambo kama hayo hata siku moja. Kwa hivyo, naomba sana, *being a backbencher is not being a fool! (Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ni kweli. Sawa Mheshimiwa tumekuelewa.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Sote tuheshimiane, tuelekezane, tukosoane. Lakini nitawaomba sana Mhe. Mwenyekiti, tusiwadharau watu, tusiwadharau Waheshimiwa, *they are intelligent, they can think.* Wao wanafikiri, wanazungumza na wananijia kwa mengi sana. Ndio maana nimenyamaza kimya, kwa sababu nawaambia jamani nyie mimi ndio kwanza nimetoka huko. Ndio kwanza nimetoka juzi kama waziri huko, sasa haya mengine mmh! bora ulizeni huko huko. Sasa shutuma kama zile ni mbaya sana Mheshimiwa, tena ni mbaya sana na inauma sana. Tena hasa mwana CCM mwenzio, Waziri mwenzio tokea majuzi. Umetumikia juzi tu umeshakuwa unamshtumu hivyo. Aahh! *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nilivyoanza kulisikia mwanzo nimekukingia kifua. Mimi ni mtu wa mwanzo kutoa kauli ya kukukingia kifua lilipotokea hili. Kwa hivyo, nakuomba utuachie tuendelee, tunafahamu. *(Makofi)*

Nadhani Waheshimiwa sasa tuendelee, maana yake wajumbe watatu tayari kwenye hoja moja. Samahani Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kaa. Mhe. Waziri kuna...

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, tumeacha Baraza lifanye kazi yake na badala yake tumeingia porini. Sisi tunaongozwa na hii Kanuni na huu ndio msahafu wa Baraza hili. Kama Waislamu wana msahafu wao na Wawakilishi wote msahafu wao huu hapa. Msahafu huu kifungu namba 59(4) na (5) nataka kukisoma ili kuzuia hili wimbi humu ndani. Inasema hivi;

> 59(4) "Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote ambalo langojea uamuzi wa Mahakama, au ambalo lilijadiliwa na Mkutano wowote uliopita na ambalo halikuletwa rasmi kwa ajili ya mjadala unaoendelea na vile vile ni marufuku kwa Mjumbe kusema kwa kutaka kupinga au vyenginevyo, uamuzi wowote uliofanywa na Baraza, isipokuwa tu kwa kutoa hoja halisi inayopendekeza kuwa uamuzi huo ufutiliwe mbali".
>
> (5) "Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kuzungumzia shughuli yoyote ya Kamati ya Baraza mpaka shughuli hiyo iwe imewasilishwa katika Baraza kama taarifa au ripoti ya Kamati juu ya shughuli hiyo".

Leo sisi tunajifanyia tu humu ndani. Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kusema kwamba lazima kanuni zifuatwe halafu watu ndio wasimamishe hoja zao. Bila ya kufuata kanuni hatutoweza kujadiliana na tukaweza kuifanyia haki serikali kama vile inavyotakiwa. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tumeshakufahamu. Naomba ukae. Mheshimiwa naomba tuendelee.

Mhe. Mjumbe Fulani: *(Alizungumza nje ya kipaza sauti.)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae tuendelee.

Kifungu SG 010702 Programu ndogo ya Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Shs.387,253,000

Jumla Kifungu Shs. 913,287,000
Jumla Kuu Shs.7,891,395,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu G02 Mahakama Kuu

Kifungu PG0201 *Administration* Unguja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi na laini kabisa, na uzoefu unaonesha mwaka 2014/2015 mahakama ilipata 1.5 bilioni. Mwaka 2015/2016 1.3 bilioni, 2016/2017 1.1 bilioni na hivi sasa Maalim kajibu namshukuru sana. Kasema atajitahidi katika bajeti inayokuja.

Nilimsikiliza sana Mhe. Waziri na nimsifu sana kwa jitihada anazochukua. Lakini kila kukicha badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma. Kuna Majaji sita sasa hivi wanataka kuongezwa, baada ya sita wanatakiwa 11. Kuna matumizi ya ofisi, umeme unakatwa. Mwakani tutakapokuja nina wasi wasi itapungua zaidi, uzoefu unaonesha na kama hapatoshi hivi sasa mashahidi hawaji mahakamani wanadai pesa, kwa hivyo kesi haziwezi kwenda, tutawalaumu Majaji wetu na Mahakimu wetu hawafanyi haki siku zote wanapiga kelele matumizi yanaongezeka, kwa hivyo wangelifikiria hili suala kwa kila mwaka inazidi kupungua baada ya kwenda mbele tunarudi nyuma. Kuna Jaji sita wanataka kuongezwa sasa hivi, kwa hivyo mufikirie tu kwa heshima kabisa hili suala alifikirie, na kuna mashahidi wanadai pesa na hivi sasa wameshagoma kuja Mahakamani, wafikiriwe hawa watu ni muhimili mzito, Mahakama ni kimbilio la wanyonge.

Mimi nimuombe Mhe. Waziri kwa heshima kabisa alifikirie hili suala ili tupitishe fungu tuweze kuendelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Jaku ni mtaalamu wa kusoma kanuni, na akisoma kanuni ya 98 (5) wakati Baraza lipo kwenye Kamati hakuna Mjumbe ambaye atatoa hoja ya kuongeza fungu, kanuni inaruhusu kupunguza fungu ndio maana watu wanazuia shilingi wanafanyaje lakini hakuna hoja ya kuongeza fungu lolote.

Sasa anachosema ni kama kanuni tayari inamzuia kama hatuwezi tukataka kuongeza fungu la Mahakama kwenye bajeti ambayo tayari imeshapita, lakini kanuni inamruhusu kama anataka kupunguza basi apunguze tu hilo fungu lipelekwe pahali pengine, nashkuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kumekucha Mhe. Waziri, hivi unavyotaka wewe hawa wanaodai haki zao mnawaambia kauli gani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti suala la kuwalipa *assessors* sisi tunalifahamu kama ambavyo analifahamu Mhe. Jaku, na mimi nimshukuru kwa jitihada zake ambazo anachukua za kutetea Mahakimu, lakini nimhakikishie kwenye jambo ambalo linazungumzwa na linatakiwa lifanyiwe malipo kila siku na Serikali ni jambo hilo, sasa Serikali inalijua na inawalipa pale kadri hali inavyokuwa. *Of Course* ni wengi na madeni haya ni ya zamani, yako tu muda mrefu lakini sio kama hayashughulikiwi. Kwa hivyo nimuahidi kwamba yatashughulikiwa, na kwenye bajeti hii hii ambayo inapitishwa basi nayo itatumika katika kuwalipa hao watu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nitumie lugha ya kuwa mkaidi, hawa wananchi wana haki zao na Mhe. Rais kiongozi wetu mkuu anajua.

Katika sherehe za sheria alikuwepo wakadai suala hili Mhe. Rais anajua huu muda unakwenda, wale watu wanataka haki zao tushapunguza fungu basi wapeni haki zao shilingi ngapi kwani wanazodai, ni pesa kidogo tu wanazodai, huku punguza fungu tu taratibu sawa wapeni haki zao watu wapate kuja Mahakamani halafu mtakuja kuwalaumu watu kesi zinashindikana, msivutie kwenu kama maandishi ya kiarabu tu. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa swali lake. Mahakama tayari wameshapeleka maombi yao Wizara ya Fedha, tuvute subira hapa hatuwezi kuzitoa kwa sababu hazipo, Wizara ya Fedha tumeshawaandikia barua watatuletea, kwa hivyo wavute subira tutazilipa tu, haki yao haipotei, Serikali hii haiwezi kumdhulumu mtu, haimnyang'anyi mtu, wavute subira watapewa chao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina uzoefu wa lugha nyepesi tena laini, hichi chombo kimeshaahidi humu ndani kipindi kilichopita Mwenyezi Mungu alinijaalia kuwepo, waandishi wa habari hawa waliahidiwa pesa zao za maposho mpaka leo hawajapewa, Waziri wa Fedha aliinuka kwa

niaba ya Serikali, ndio utaratibu jamani kuwanyima wanyonge haki zao, hichi chombo tupo kwa niaba ya wananchi na kuwatetea wananchi, ni milioni ngapi kwani niambiwe shilingi ngapi zinadaiwa Serikali inashindwa kulipa, hili halina mjadala Waheshimiwa natoa hoja mnisaidie kwa hili, shilingi ngapi zinadaiwa Serikali zinashindwa kulipa.

Serikali imejibu juzi hapa Serikali haiogopi hasara kwa wananchi wake, juzi Naibu Waziri leo mnatujibu nini milioni ngapi zinadaiwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Jaku anaskia vizuri, Serikali ilichosema kama hayo madeni ya ma-*assessors* yanajulikana na *commitment* ambayo imetoka ni kama Serikali itawalipa, sasa zaidi ya *commitment* hii ambayo imetoa Serikali mimi sidhani kama kuna mwengine atakayesimama hapa atazungumza zaidi ya haya ambayo tumeyasema, hao ma-*assessors* watalipwa, asubiri mwaka huo ujao wa fedha uje halafu aseme kuna watu ambao walikuwa wakidai na madeni yao hayakumalizika kulipwa, watalipwa tu!

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa tupo kwa mujibu wa Kanuni hapa. Mimi kwanza nataka nikueleze Mheshimiwa, kwa mujibu wa Kanuni na Katiba ya Zanzibar humu sote ni Waheshimiwa hakuna mkubwa hakuna mdogo ukifika pahala tukadharauliana hafufanyiani haki.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakufahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa mujibu wa Katiba hakuna mkubwa hakuna mdogo sote ni Waheshimiwa humu ndani, tukatoka huko tena munidharau waziri au nini, Mheshimiwa baada ya maelezo hayo nimemsikia sana Mwanaheria Mkuu na namheshimu sana naomba tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake aje anambie ni kesi ngapi za udhalilishaji ambazo zilipelekwa Mahakamani na zikatolewa maamuzi kwa kipindi cha Mwaka 2015 mpaka kufikia tarehe ya jana, lakini Mhe. Mwenyekiti cha kusikitisha sikusikia kesi hizi za udhalilishaji nilisikia kesi za rushwa pamoja na nyenginezo, namuomba Mhe. Waziri anipatie majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, tatizo tunalo mimi nalisema wazi kwa sababu tupo kwenye chombo kikubwa, tatizo tunapotoa majumuisho

Waheshimiwa wanatoka hawamo humu ndani, sasa itakuwa tunaendelea kutoa taratibu majawabu yale kwa yale suala hili tulilitolea maelezo Mhe. Naibu Waziri kalieleza vizuri.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa tunamuomba Mhe. Waziri unajua ni mrefu sana, kwa hivyo anaposema ainamiye hii *mic* ili tupate kusikia vizuri. (*Kicheko*)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa endelea labda nimruhusu awe anajibu kitako.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Yeye haja yake niiname.

Mhe. Mwenyekiti, kesi za udhalilishaji lakini na hilo tulifahamu waheshimiwa ni vizuri waheshimiwa tunapotoa majumuisho wawemo humu ndani kwa sababu itakuwa tunajibu yale kwa yale. Mahakama hupokea aina mbali mbali ya makosa ya udhalilishaji; makosa hayo ni kama vile kubaka, kutorosha, kukashifu na kadhalika. Takwimu zinaonesha kwamba kuanzia mwaka 2013 hadi mwishoni 2015 Mahakama imepokea kesi 106 za makosa hayo, kesi 73 kati ya hizo zimetolewa uamuzi ambapo kesi 7 washitakiwa wake wamepatikana na hatia na kupewa adhabu ya kifungo cha kuanzia miaka miwili hadi kumi na moja. Kesi 33 bado zinaendelea. Mahakama hii itashughulikia watoto waliofanya vitendo vya uhalifu walio chini ya miaka 18.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, majibu niliyokuwa ninayataka ni kesi za udhalilishaji ni kesi za watoto, kwa sababu watoto kuna makosa tofauti ya watoto na sio kesi za ujumla, nilitaka kesi za udhalilishaji.
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri hebu msaidie.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Viwe naona bado hajatufahamu lakini ni kazi yetu kufahamishana humu naamini kwamba atafahamu.

Mhe. Viwe ametaka kujua takwimu za kesi za udhalilishaji, Mhe. Waziri amezungumza vizuri tu na mimi naomba kusoma tena, tena nitakwenda kidogo kidogo ili uweze kunifahamu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kusema kama alivyozungumza Mhe. Waziri, Mahakama hupokea aina mbali mbali za makosa ya udhalilishaji, makosa hayo ni kama vile kubaka kwa hivyo kubaka ni sehemu ya udhalilishaji nafikiria Mhe. Viwe utakuwa upo pamoja na sisi, kutorosha vile vile unapomtorosha mtoto wa mtu hiyo ni kumdhalilisha, vile vile na kukashifu unapomkashifu mtu ni udhalilishaji vile vile Mhe. Viwe na kadhalika.

Sasa takwimu zinaonesha kwamba kuanzia mwaka 2013 kama Mhe. Waziri alivyozungumza hadi mwishoni mwa mwaka 2015 Mahakama imepokea kesi 106 za makosa hayo. Makosa gani hayo Mhe. Viwe, makosa ya udhalilishaji ambayo ulikuwa ukiyaulizia nafikiria Mhe. Mwenyekiti amenifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Viwe umesharidhika.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee lakini kesi hizi zipewe kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai mtu wa mwisho.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nitapita juu juu tu kidogo na ningekuwa nimepata maelezo mazuri mapema wala hapa nisingekuwa na tabu, kuna vitu viwili au vitatu nataka kuvitolea taarifa kutokana na maelezo niliyoyatoa mwanzo.

La kwanza Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumzia kuhusu Mahakama ya biashara. Najua sheria lakini ninavyofahamu mimi ndani ya Mahakama tayari wao wenyewe kama wafanyakazi ni watu wa kushughulikia wameshajipanga vya kutosha, lakini tatizo ni pesa ili uweze kujipanga vizuri.

Suala la pili nilizungumzia suala la Mahakama ya *Industrial Court* ambalo jengo lile liko Mwanakwerekwe zaidi ya miaka saba hivi sasa hakuna majibu niliyoyapata katika maelezo ya mwanzo.

Suala la tatu, ilikuwa juu ya Mahakama ambayo Mhe. Rais amezungumza katika hotuba yake alipokuja hapa Barazani, na katika hotuba aliyoizungumza Mhe. Waziri wa Fedha alizungumzia nafikiri katika ukurasa wa 64 katika mpango mzima juu ya mpango wa Serikali.

Sasa haya yote nafikiria ingekuwa vizuri tukiyapata, lakini suala jengine pia nitakalozungumza ambalo Mwanasheria Mkuu ameligusia kwa juu juu na kwa undani kidogo juu ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa ambayo Jaji mmoja kwa

kumi na sita, akasema kwamba kunahitajika uzoefu wa miaka 15 ili sisi Wazanzibari tuwe tunafuata watu huko. Lakini hakusema kwa kweli nikaridhika kwamba sisi kama Zanzibar hatuna watu wazoefu wenye miaka 15 kama ni kigezo kwenda kuwa huko tukapata Majaji ndani ya Mahakama huko wakaeleza watu wanao, sasa hilo ningependa nilifahamu vizuri kama hawapo basi tupewe taarifa kwamba mwaka ujao huyo mtu kutoka mmoja kwa sababu hakuna uwiano tutapata watu zaidi ya hao watatu au watano au sita lakini idadi itaongezeka, hapo kidogo anipe matumaini kwenye suala hilo.

Lakini kwenye Mahakama ya Tunguu ambayo imezungumziwa ningeweza kujua kwamba hii Mahakama itajengwa lini huko Tunguu, na hasa kwa mimi ni mwakilishi wa wananchi katika Jimbo la Tunguu, nafurahia mambo kama haya, na mji mzima unaelekezwa kuja kujengwa katika Jimbo langu na umetajwa katika hotuba ya Rais.

Mhe. Naibu Waziri kwa sababu alizungumzia suala la madawa ya kulevya na katika kesi ambazo ulizitaja nilimsikiliza kwa umakini amesema kachukua miaka mitatu tokea 2013 kesi 23, 2014 kesi 16 na 2015 ni kesi 10, lakini jumla ni kesi 50 za madawa ya kulevya ambazo zilizotolewa majibu ni 35 na 15 bado ziko Mahakamani. Lakini kiundani nilitaka kujua, niliuliza hili katika hizi kesi ni watu wangapi wamehukumiwa kwa sababu hili dude ni janga la kitaifa, vijana wanaangamia, waheshimiwa kibao wamezungumza humu ndani kwa hisia na uchungu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa usihutubie tena nafikiri ungejaribu kujenga zile hoja ili aweze kujibu.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Sasa ningejibiwa maana yake hiyo hotuba nikiondoka katika G 02 siwapati tena hawa niko kwenye Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti: Jaribu kuzifupisha basi.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Hayo ndio maswali yangu niliyouliza mapema sikujibiwa, na haya nimezungumza tokea jana palikuwa pana muda wa kutosha kujibiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hamjaomba muda wa kuongeza kibali muda umekwisha.

Mhe. Mwenyekiti: Tumeomba Mheshimiwa wacha tumalizie.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Jaku kwamba wewe uliona haya mambo zamani, na ukatumia busara ya kutuomba tutenge kando kanuni ya muda ili tuongeze muda, hoja ilitolewa na Baraza likaridhia hoja hiyo, kwa hivyo hakuna haja ya kuahirisha kwa sababu hoja ya kuongeza muda tayari imeshatolewa na Baraza limeridhia.

La pili nadhani Mhe. Simai nilivyozungumzia kuhusiana na kwanza Mahakama ya Rufaa nilichosema akisoma Ibara ya 118 sifa zilizowekwa wala sio tu za upande wa Zanzibar, sifa za wale wote ambao wanatakiwa kuteuliwa kwenda kwenye Mahakama ya rufaa wanaotoka kwenye Mahakama ya Tanzania Bara na wanaotoka kwenye Mahakama za Zanzibar wanatakiwa wawe na sifa zisizopungua miaka 15 hilo ndio sharti la kwanza. Wacha na zile sifa nyengine ambazo zimeelezwa na Katiba.

Lakini la pili, nikamueleza kama hakuna mgao ambao umeelezwa ndani ya Katiba kama ukasema kwenye majaji 20 basi majaji 9 watoke upande fulani, nadhani kwenye Katiba waliopendekeza mgao huo angalau wameuweka vizuri, lakini kwenye hii ya mwaka 1977 hakuna huo mgao. Lakini nikamueleza pia kama historia yetu ya sheria pamoja na kwamba tulikuwa wanasheria wengi lakini hawa wa sasa hivi ndio tumekuwa wengi zaidi ambao sasa ndio tumo kwenye kutimiza hiyo miaka, kwa hivyo haina maana kama sasa hatutokuwa na fursa za kuteuliwa.

Nikamueleza pia yalishaletwa maombi na nadhani majina yamepelekwa lakini yalirudishwa kwa sababu tu za hapa na pale, lakini unapotimiza hizi sifa nadhani hili litapelekwa na wala hakuna hoja ya kwamba kwa nini watu wasiteuliwe kama kutakuwa na nafasi ambayo inahitaji watu kuteuliwa, juzi ameteuliwa mmoja, sasa kama kuna nafasi nadhani hilo ni jambo tu la kawaida.

Lakini haya ameyaeleza kuhusiana na nafasi, mimi nimueleze nafasi za Mahakama ni finyu, nadhani yeye hili analijua na ndio maana Mahakama inataka kuhamia Tunguu. Sasa hii ndio bajeti tunayoipitisha, apitishe hii bajeti halafu hizo harakati nyengine zianze, sasa akipiga buti kwenye bajeti hii sidhani sasa kama hiyo Mahakama itaanza kuanzishwa huko Tunguu, sasa aipitishe hii bajeti halafu hizo hatua za kutaka kuanza ujenzi wa Mahakama huko Tunguu zianze Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza vitu vingi nimepata jibu moja.

Mhe. Mwenyekiti: Majibu mawili.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Nimeuliza kuhusu Mahakama ya Tunguu ambayo imetajwa kwenye hotuba ya Rais, nimeongelea kuhusu *Industrial Court* ambayo jengo lake miaka saba wanasubiri mpaka leo hawajatimiza.

Mimi ningependa Mahakama Kuu ya Tunguu ambayo Rais ameitaja basi itajengwa lakini humu katika bajeti hata haijatajwa wala haimo, lakini kwenye Hotuba ya Rais imezungumziwa. Lakini tuendelee mimi nazungumza tu nifahamike lakini Mhe. Waziri namjua na namuamini, na viongozi wote wako hapa Baraza la Mawaziri watakuwa wananisikia.

La pili katika hawa majaji 16 na maelezo yote mazuri aliyonipa mimi nakubali ninachokiomba nataka matumaini katika hili kwamba mwaka ujao angalau patakuwa na *improvement*, kweli hakuna uwiano uliotajwa kwa mujibu wa Katiba zetu zote mbili, lakini angalau binadamu tuishi kwa matumaini kwa suala hili 16 kwa mmoja ni kidogo mno, basi tungeomba angalau tupate watu 5 au 4 na vigezo vitakuja kuruhusu huko mbele, basi tupate maneno mazuri hilo moja.

Lakini pia kwenye madawa ya kulevya katika kesi ambazo watu wamehukumiwa hizo 35 zishatolewa majibu nataka kujua wangapi wamefungwa, kwa sababu nilizungumza kwa hisia kwa sababu ndani ya Mahakama na ofisi ya *DPP* pamoja na Polisi kuna suala la rushwa. Sasa hapo tunataka tujue sisi kama Wajumbe tupo hapa tunataka tujue ni wangapi wamehukumiwa katika hao 35 tupate kujua, halafu ndio tutajua tunakwendaje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hapa mbele yangu naomba ruhusa yako ninukuu kitabu hiki cha Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohammed alipowasiliha hali ya uchumi kwa mwaka 2015 na mipango ya Maendeleo mwaka 2016/2017, nanukuu Mheshimiwa kwa ruhusa yako,

"Kuimarisha misingi ya utawala bora na kisheria" .

Mhe. Spika, utawala bora ni msingi muhimu katika kufika malengo yaliyopangwa katika nyanja zote ikiwemo uwajibikaji, utii wa Sheria pamoja na upatikanaji wa haki.Katika mwaka 2016/2017 serikali itaandaa mfumo wa kielektroniki na usimamizi wa kesi Zanzibar, kuanza ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu. Hilo jibu la kwanza.

Kwa hivyo, ina maana kwenye bajeti ya serikali, tayari hilo suala lipo kwenye mpango wa serikali.

Na kuhusu madawa ya kulevya kesi zilizotolewa uamuzi ni 35. Mheshimiwa anasema ingawa tutaandikiwa kwa maandishi hawa waliofungwa na walioachiwa huru au waliochukuliwa hatua nyengine, lakini amesema jambo hapa zito katika kikao hiki, kwamba anasema kuna rushwa, atuletee kimaandishi ushahidi kwamba kuna watu wametoa rushwa ili tuchukue hatua za kisheria, na bahati nzuri rushwa iko kwetu. Kwa hivyo, atuletee na sisi tutachukua hatua.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, mimi hilo suala la maandishi naliridhia kwa hapa, lakini kutokana na maelezo niliyouliza tangu jana nilistahiki kupata majibu mazuri palikuwa pana muda wa kutosha, hivi ni kuonewa kuambiwa kwamba nikubali kwa maandishi, lakini tangu jana kuna wataalamu wa kutosha ndani ya serikali yetu na Mahakama zetu, kupewa tu katika watu 35 ni wangapi wamefungwa nashindwa kupata majibu hayo jamani.

Lakini pia katika hotuba ya Rais aliyosoma mimi nasoma hapa anasema katika ukurasa wa 64

"Mhe. Spika, demokrasia na Utawala Bora ni nguzo na nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii yenye umoja, mshikamano, uadilifu na uwajibikaji. Kwa lengo la kuimarisha utawala wa sheria, serikali imefanya jitihada kubwa za kuziimarisha taasisi zinazosimamia utawala bora watendaji wake pamoja na mazingira ya kufanyia kazi. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo serikali itaongeza kasi katika kuziendeleza juhudi hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi, pamoja na mambo mengine, serikali ina mpango wa kujenga jengo jipya la Mahakama Kuu huko Tunguu, kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Watoto Mahonda na kuyafanyia matengenezo makubwa majengo ya Mahakama ya Mfenesini, Mwanakwerekwe na Wete na kuzisogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi".

Sasa katika miaka mitano kuna mwaka 2016, 2017, 2018, 2019 na 2020, jengo la Mwanakwerekwe ambalo ni *Industrial Court* lina miaka zaidi ya saba liko hivi na sehemu ile sasa panaegeshwa magari. Sasa haya majengo yote miaka mitano katika bajeti hii hakuna eneo linaloonesha kwamba hizi Mahakama zitaanza utaratibu gani. Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu anazungumza na anasema kwamba nikubali kupitisha hapa halafu huko mbele yatatokezea hayo, lakini kutokana na hiki kiwango kilichotajwa hapa ni kidogo mno hata kwa huo

utekelezaji wao wa kazi, bilioni 1.1 ni kidogo sana. Kwa hiyo, kama tukubali tupitishe mimi nikae bora niambiwe kaa subiri mwaka ujao.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nitakuomba hivyo, mheshimiwa hili suala la upungufu wa bajeti ni serikali nzima sio wao tu, hata sisi Baraza la Wawakilishi tumeathirika kwenye hilo. Kwa hiyo, nafikiri utakuwa unamuonea, kwa sababu hana pa kuzipata hizo nyengine za kufanya shughuli yako.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, basi nilikuwa naomba kitu kimoja katika madawa ya kulevya aniahidi hapa kwamba tutaona juhudi za serikali, *commitment* na maendeleo juu ya hali ya juu na hasa kuwasaidia vijana wetu, kuliporomosha na hao waliomtaja jana Mhe. Nadir kawataja hapa kuna hao alitumia jina sijui "mapapa". Tusikie sasa mambo yanafanyika, na hili jambo kwa sababu vijana wanaangamia, wazee wanakufa, wanapata kama *pressure* kabla ya hata muda wao, majumbani sabuni inatiliwa *lock* mpaka TV kwa ajili ya madawa ya kulevya. Leo tumekaa hapa tunasema kwa fedha hizi, kwa hiyo mimi ningependa nione kauli yake, atuahidi kwamba jambo hili, hayo mengine mimi niko tayari kustahamili lakini juhudi zionekane katika maeneo hayo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe Mwenyekiti, shughuli za ujenzi zinaelezwa kwenye ukurasa wa G 23 ndio kwenye miradi, ukisoma G 23 ndio kwenye miradi ya Mahakama ambayo inatakiwa kutekeleza kwa mwaka wa 2016/2017. Sasa Mhe. Simai angesoma G 246, G 239 angeona kama kuna fedha ambazo zimetengwa, na zilizotengwa ni kuanza taratibu za ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu, zimetengwa karibu shilingi milioni 100, kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu zimetengwa fedha. Sasa kuanza ujenzi sio kupeleka matofali, tunaanza kutafuta kwanza ramani, kuweka miundombinu mizuri. Sasa inawezekana kwa mwaka huu wa fedha na mimi nakubaliana naye kama inawezekana fedha hizi hazitoshi, lakini kwa maandalizi ya awali ndio fedha ambazo zimetengwa.

Sasa wakimaliza kazi ya matayarisho ya awali mimi naamini fungu hili mwakani halitokuwa na fedha kama ambazo zimewekwa hapa. Kwa hiyo, akitizama hii G 23 mengi ya maelezo ambayo ameyatoa Mhe Simai ya Mahakama na ujenzi wa Mahakama yameelezwa vizuri kwenye utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, hili la madawa ya kulevya nadhani hili tumelizungumza muda mrefu, na sisi tunakubaliana naye, serikali tutaendeleza juhudi za kupambana na wanaoleta madawa ya kulevya na wanaotumia madawa ya

kulevya, na kila inapobidi kukamatwa watakamatwa na watapelekwa kwenye vyombo vya sheria. Hili tumemfahamu na hili tunalifanya kila siku Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, nazidi kuheshimu kwa vile unanipa muda wa kuweza kujieleza nikafahamika. Naomba basi kutokana na hiyo *spirit* ambayo ya kuaminiana, na maelezo mazuri anayotoa Mwanasheria Mkuu mbele ya serikali na wajumbe wenzetu pamoja na waziri husika. Naomba basi kutokana na kwamba serikali ina mpango mkubwa sana, kwa sababu kuna mambo mengi yatafanyika kibiashara, kuna mpango wa *real estate* uko Kaskazini upande wa Fumba, migogoro itajitokeza, kuna barabara zinazojengwa. Kwa hiyo, *issue* ya Mahakama ya Biashara inabidi iangaliwe kwa jicho la huruma, kwa haraka sana katika mwaka huu wa fedha hapo watapozipata. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PG 0201 Programu Kuu ya Usimamizi ya Upatikanaji wa Haki
Kifungu SG 020101 Programu Ndogo ya Usimamizi ya
Upatikanaji wa Haki Shs. 2,832,923,000
Kifungu PG 0202

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa tena nafasi hii nikaweza kuzungumzia muhimili mwenzetu wa Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, katika Baraza lilopita niliwatetea Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo, na niliwatetea kuhusu suala zima la stahiki zao, na ilikuwa sio tu Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo lakini Mahakimu wote, kwa bahati nzuri walioweza kuzingatiwa maslahi yao walikuwa ni Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mikoa. Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo walisahauliwa, lakini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kipindi kile Abubakar Khamis Bakary aliniahidi kwamba hilo suala wanalichukua na wanalifanyia kazi na katika masuala na majibu akaja akanijibu tayari mishahara yao itarekebishwa.

Vile vile aliahidi watalipwa mpaka na *arrears* zao. Kwa bahati mbaya sana Mhe. Abubakar sasa hivi hayupo, lakini sasa hivi yupo Maalim wangu Haroun. Sasa kwa kuwa pamoja alisema yeye ni mchanga ndio kwanza ana mwezi mmoja na nusu, lakini bado watendaji wapo, Ofisi ya Mahakama ipo, basi nataka niambiwe, je, lile suala zima la haki hasa za mishahara na marupurupu mengine ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo limefikia hatua gani, na sasa hivi leo ndio tunapitisha bajeti. Je, katika bajeti hii suala la marekebisho ya mishahara yao limo?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hili Mhe. Naibu Waziri alizungumza maslahi ya Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo kama ni hilo. Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wanalipwa kulingana na elimu zao na tayari serikali imekwishachukua juhudi za kuongeza maslahi yao na kuwalipa posho maalum la shilingi 250,000 kila mwezi. Sasa Mheshimiwa tumeshachukua hatua hizo, sasa kama kulikuwa na tatizo jengine Mhe. Hamza basi aliseme tulichukulie hatua.

Na jitihada nyengine zilizofanywa ni kufanya mapitio ya sheria, kuanzisha Mahakama ya Mahakimu ambayo pamoja na mambo mengine itaangalia suala la kuongeza sifa za Mahakimu wa Mahakama za mwanzo na kuandaa muundo mpya wa utumishi wa Mahakama ambao utaangalia maslahi yao.

Aidha, zoezi la tathmini ya kazi ya madaraja litakuwa na nafasi nzuri ya kuliangalia suala hili. Kwa hivyo, juhudi zimechukuliwa na tunaendelea, na ni kama nilivyomwambia kama liliahidiwa na waziri aliyeondoka serikali ipo yeye hayupo, lakini serikali ipo na tumeshasema sisi tumetoa mwezi mmoja na nusu au miezi miwili sasa hivi ndio inaingia. Kwa hivyo, tuvute subra haya masuala tushayaeleza haya, kwamba yanashughulikiwa na tutachukua hatua kuhakikisha kwamba hili jambo linatendeka.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, leo tutapiga kura, kwa sababu inaonesha serikali inaleta jawabu halafu inasahau.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kubadilika mawaziri wanabadilika watu lakini ofisi zipo, suala la Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo Mhe. Mwenyekiti Mahakimu wa Mahakama za mwanzo wametambuliwa katika sheria hiyo hiyo ya Mahakama. Na Mheshimiwa moja katika kitu ambacho Mahakimu wametambuliwa katika tafsiri kuanzia Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo, na kama alivyosema na inaonesha hakufanya utafiti wa kutosha. Hawa Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo yeye amesema wametajwa kwa mujibu wa sifa zao na elimu zao. Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wametakiwa kwanza wawe na ngazi ya *certificate*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuthibitishie kutokana na uwajibikaji na kupenda kazi kwao Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wako 21. Katika hao 21 ni wawili tu waliokuwa hawana ngazi ya *degree*, lakini wapo ambao wana *masters* na hivi sasa wengine wanajisomesha wenyewe katika vyuo mbali mbali bila ya msaada wa serikali, bila kitu chochote. Sasa unaposema kwamba inatakiwa sifa, sifa wameshazipita basi wapandishwe Mahakimu wa Mahakama

za Mikoa. Kwa hiyo, sifa walizokuwa nazo hao Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wapo sasa hivi wanaanzia *degree*, nakutajia katika Mahakimu 21 ni wawili tu ambao wana *certificates*, lakini waliobakia wote kuanzia *degree* mpaka *masters*. Sasa leo kusema kwamba itakuja sijui kuangalia, ina maana hili suala linaanza upya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nipatiwe jawabu makhususi, ni lini Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo wataweza kuzingatiwa mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, sipendi sana kutaja mishahara ngazi ya Mahakimu ya Mahakama ya mwanzo na ngazi ya Mahakimu wa Mahakama ya Mikoa naogopa tu kusema…

Mhe. Mwenyekiti: Usiseme mishahara yao Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Lakini kwa kweli ni aibu, na hii mishahara yao na hizi posho zao wanazopewa sasa hivi tumewatengenezea utaratibu wa kuchukua rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aniahidi, kwamba Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo waweze kulipwa mishahara yao vizuri na stahiki zao nyengine, ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Suala la sifa sasa hivi kama nilivyomwambia Mheshimiwa hili akalifanyie utafiti tena, katika Mahakimu 21 ni wawili tu ndio wana *certificate* wengine waliobakia wote wameshazidi zile sifa zinazotakiwa Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza vizuri na nazidi kueleza, nimesema serikali tayari imeshachukua juhudi ya kurekebisha na kuwalipa posho maalum ya 250,000/-, kinachofanyika sasa hivi tunatayarisha muundo mpya wa utumishi ili kila mmoja tumuweke kwa mujibu wa *level* yake na kiwango chake cha mshahara anachostahiki. Tumeshafanya hivyo, haya mambo yanakwenda, elimu zao hapa tumesema tunawalipa kwa mujibu wa viwango vya elimu yao, tumeshaweka tayari na sasa hivi tunachofanya tunatayarisha muundo wa utumishi ili kuhakikisha kwamba maslahi yao yote wanayapata kwa mujibu wa haki zao na elimu zao. Kwa hivyo, tuvute subra, tutalifanyia kazi hili, tutashirikiana na wenzetu wa Mahakama, ili kuona jambo hilli na Wizara yetu ya Fedha tutakaa nao ili kuhakikisha jambo hili tutalitekeleza haraka iwezekanavyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe Mwenyekiti, nilipokuja kujenga hoja yangu hii Mahakimu hawa wa Mahakama ya Mwanzo walikuwa wanalipwa hiyo hiyo posho ya 250,000/-. Posho hiyo ya 250,000/- aliyoitaja yeye nilipokuwa najenga hoja yangu ilikuwa ndio posho yenyewe hiyo, wenzao wamewazidi mara tano Mahakimu wa Mahakama ya Wilaya, na hawa hizo kesi zote nyingi hawa ndio wanaozishughulikia.

Mimi nafikiri labda Mhe. Waziri anaposema watalipwa kulingana na elimu zao ndio kabisa analikoroga, hizo elimu zao mimi nataka niseme kuna Mahakimu wa Mahakama za mwanzo sasa hivi wana sifa kubwa kuliko Mahakimu wa Mahakama za Wilaya kielimu. Sasa kama anasema wanalipwa stahiki zao kwa mujibu wa elimu zao, ina maana hilo sio kweli, wako Mahakimu wa Mahakama za Wilaya elimu zao ndogo mara mbili ya Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo, lakini wao wanalipwa vizuri zaidi kuliko Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri akiri kwamba hili suala hawakulifanyia kazi niachie kifungu, na niachie kifungu ili ndani ya kipindi hiki warekebishiwe mishahara yao.

Na sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tulipopitisha bajeti hii na mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti moja katika tulichopitisha ni marekebisho ya mishahara, liko fungu katika mfuko mkuu wa serikali. Kwa hiyo, uwezekano Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo kufanyiwa marekebisho yao upo ndani ya bajeti hii, na nihakikishiwe kwamba Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo watarekebishiwa mishahara yao, *otherwise* Mhe. Mwenyekiti, tutapiga kura hapa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tungeelewana ngazi hizi za Mahakama zina utaratibu wake, hilo la kwanza. Lakini la pili sasa hivi kinachotizamwa wala hakitizamwi nani ana *degree* ngapi, nani ana *degree* ngapi apate kulipwa mshahara. Sasa hivi ile *post* ya Mahakama ni *duty post*, maana yake mtu anawekwa anapokuwa utumishi huu marekebisho yake yalipokuja ni kama sasa hizi ni dhamana, mtu anapopewa dhamana ya Mkoa maana yake hatizamwi yeye kama huyu Hakimu wa Mkoa ana *degree* moja kwa hiyo tumlipe kwa *degree* yake moja, au ana *degree* mbili alipwe kwa *degree* zake mbili. Ni kwamba analipwa kutokana na ile dhamana ambayo amepewa, kama Hakimu wa Mahakama ya Mkoa analipwa mshahara kutokana na ile dhamana yake ya Uhakimu wa Mkoa. Halipwi kutokana ana *degree* tatu kwa hiyo mshahara wake u-*reflect degree* tatu, ni sawa sawa na tuliokuwemo humu ndani. Kuna wenye *degree* na kuna ambao hawana *degree*, lakini

mishahara sote ni sawa sawa. Sasa kigezo hiki Mhe. Hamza anachosema mimi nadhani akitafakari vizuri, mengi yamebadilika kutokana na muundo ambao upo.

Lakini mimi nikubaliane naye kama hoja hii ya Mahakama hawa wa mwanzo imezungumzwa muda mrefu, sina hakika imefikia wapi, lakini najua kama imezungumzwa muda mrefu. Ahadi ambayo tunaitoa ni kama Mhe. Waziri amesema wacha arudi atizame limefika wapi, halafu alishughulikie ahadi ndio ambayo tunaitoa. Lakini pia kufahamu kama na haya mambo yamebadilika wala hayatizamwi sasa hivi una *degree* ngapi ili ulipwe kwa *degree* ngapi. Sasa inakwenda ni ile *post* ambayo inatizamwa, hata hapo ukiwa una *degree* tatu wewe utalipwa kama Mahmoud mwenye *degree* moja, natoa mfano. Ndio muundo ambao upo na Mahakama ni hivyo hivyo, kama miundo hii imebadilika kwa sababu sasa imekuwa ni *post rather than* yale ambayo ilikuwa tukitumia mwanzo. Sasa nimuombe Mhe. Hamza ili atuachie, nadhani Mhe. Waziri ametoa ahadi kama atalifuatilia bajeti hii ndio kwanza inaanza wana nafasi kubwa tu ya kuuliza maswali kuanzia sasa mpaka bajeti ya mwakani. Kwa hiyo, litashughulikiwa na litatolewa maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba serikali iwe na majibu *constant*, majibu yasiwe *very easy*, jawabu aliyonijibu waziri…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza nitazame mimi usimtazame Mhe. Hassan.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, jawabu aliyonijibu Mhe. Waziri wanalipwa Mahakimu vile vile ukizingatia na sifa zao za elimu. Mhe. Mwanasheria Mkuu ananiambia bila ya kujali *degree* zao na *masters* zao wanalipwa kwa mujibu wa *post*. Kwa hiyo, ina maana hizi kauli zinagongana, kama kauli zinagongana ina maana hapa sijapata jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaposema hivi suala la kusema kwamba uzito wa kazi hatutaki kuzungumzia na taasisi nyengine, lakini kuna kipindi tuliwahi kuzungumza Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ukiangalia uzito wa kazi zinatafautiana, lakini wale wenye kazi nzito ndio wanalipwa maslahi mazuri zaidi kuliko wale wenye kazi nzito, yaani wale wenye kazi nyepesi wanalipwa maslahi mazuri zaidi kuliko wenye kazi nzito. Sasa bado mimi narejea Mhe. Mwenyekiti, unajua kama ingelikuwa ni busara kuzungumzia maslahi ya watu kwenye kadamnasi ya watu ningelitaja, lakini si vizuri sana, hailingani Mhe. Mwenyekiti, *gap* Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na Mahakimu wa Ngazi ya Wilaya na ukiangalia kesi zenyewe wanazozihukumu utofauti wake, Mheshimiwa hawa tunawapeleka kwenye kushawishiwa

kuchukua rushwa, na tumeunda Tume ya Kudhibiti Rushwa kwa makusudi, sasa hawa mazingira yao tumewapelekea kuwashawishi kuchukua rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kitu kimoja, kama nilivyosema katika bajeti hii katika mfuko mkuu wa Serikali tumetenga fedha kwa ajili ya marekebisho ya mishahara. Mimi nataka Mhe. Mwenyekiti, kama sitosema tupige kura baada ya kujibu majibu ya mwisho, basi tukae na Waziri na Mwanasheria tuangalie hii mishahara wanayolipwa Mahakimu kuanzia ngazi ya Mahakama ya Wilaya na Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, halafu tuangalie *difference* gani, lakini sitaki kusema lazima, lakini *possibility* ya kuweza kurekebisha ndani ya bajeti hii iwepo, kwa sababu bajeti tumeipitisha maalum, tumeweka fungu maalum la kufanya marekebisho ya mishahara na hili kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, niliahidiwa na Serikali.

Abubakar yeye alikuwa ni mtu ndio maana hayupo, lakini Serikali bado ipo; na yeye aliahidi kwamba katika mwaka huu wangeliweza kutengenezewa maslahi Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, leo suala linaanza upya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado sijaruhusu kuzuia kifungu hichi mpaka nihakikishiwe kwamba ndani ya bajeti ya mwaka huu Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wanafanyiwa marekebisho ya stahiki zao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri mwalimu Haroun.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kweli Waziri wa Katiba na Sheria hayupo, Serikali ipo na *inshallah* itakuwepo tukijaaliwa.

Mimi sina tatizo, mimi Mwanasheria Mkuu na yeye tutakaa pamoja kuona njia gani tufanye, lakini siwezi kuahidi moja kwa moja sasa hivi kwamba tutafanya moja mbili tatu, tujadiliane tuone huo uwezekano wa kurekebisha, cha kurekebisha na cha kutengeneza tutengeneze, lakini hizi taarifa ambazo nimezisoma mimi zimeandikwa na watu wa Mahakama wenyewe, ina maana wanalielewa suala lao na Mwanasheria alipozungumza ni kweli, sawa sawa hakuna matatizo, lugha hizo hizo labda tumekosea katika kuelezena tu.

Kwa hivyo ninachoomba Mhe. Hamza na wenzake wote ambao wana maelezo kama hayo atulie tukae tukutane, na Kamati yetu ya Sheria ipo tunaweza tukakutana au na chombo chochote ambacho tunahisi kitatusaidia tukae pamoja tulijadili jambo hili na tulitatue tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza ukae nao.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi si Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, lakini naomba suala hili tulifanyie kazi nje ya kazi za kawaida za Kamati za Baraza, zile ambazo Kamati unazipangia wewe shughuli zao. Kwa sababu hii hoja mimi mpaka sasa hivi sijaiachia nakusudia tupige kura, kwa hivyo ili tusipige kura, ina maana hii kazi tuifanye mimi pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri mwenyewe ili tuweze kuliweka sawa.

Na hii Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kumsaidia yeye Waziri, watendaji wake wakiweza kulipwa maslahi mazuri ndio watafanya kazi vizuri, na wewe Mhe. Waziri utakuja kumsifu baadae hapa.

Mhe. Mwenyekiti: nadhani ndio alilolizungumza hilo kwamba mkae naye yeye pamoja na Mwanasheria Mkuu, hilo ndilo alilosema yeye.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hili Baraza unaliongoza wewe, ina maana hiyo kazi itabidi uje uiagize wewe, kwa sababu hapa ndio tunapitisha mafungu, kwa sababu Waziri anaweza akasema hivyo anaweza akafanya asifanye, lakini sasa ndio maana nikasema hili suala lisije likafanywa kwenye kazi za kawaida za kamati, tulifanye ni zoezi maalum Kamati ya Katiba, kwa sababu mimi si Mjumbe, na mimi niwepo mwenye hoja ili niweze kujenga hoja na tuangalie katika fungu la bajeti tuweze kulisaidia hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi sina tatizo Mheshimiwa, mimi ninachokitaka mutafute namna kwa sababu fedha ya kukulipeni Kamati kwa ajili ya kazi hii hiyo sina, pesa hiyo sina. Lakini tafuteni namna ambayo mnaweza, kwa sababu sio suala kubwa, mimi nadhani ni suala wala halihitaji siku nzima, kwa sababu ile misingi yote wewe unaifahamu, ni kitu ambacho unaweza ukawaeleza tu yaani ukawaekea ule utaratibu zile tafauti unazijua za mishahara na hayo maposho wewe unafahamu kila kitu, pamoja na kwamba tumesema usizitaje hapa hadharani, ni vitu ambavyo mnaweza na Mhe. Waziri na Mwanasheria Mkuu, na hata Kamati ikitaka halafu mkaweka *guidelines* halafu mkaona namna gani mnakubaliana. Nadhani hata saa moja haliwezi kuchukua, wakikubali ndio itakuwa lishakuwa limekaa sawa hilo Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nina uzoefu wa kufanya kazi bila ya posho, kwa hilo mimi wala Mhe. Mwenyekiti usiwe na wasi wasi sina tatizo na hilo, lakini kama nilivyosema kwamba hili suala, kwa sababu unajua Mheshimiwa…

Mhe. Mwenyekiti: Wao washakubali, wao washakubali hawana tatizo

Mhe. Hamza Hassan Juma: Unajua Mhe. Mwenyekiti, unajua kuna suala moja hapa. Kuna suala unajua tunaitana sana, sisi tunaitana sana, sisi tunakaa na Waziri na wengine, lakini suala linataka liwe *official* kwa sababu ina maana hili

Mhe. Mwenyekiti: Ngojea basi Mhe. Waziri wa Fedha akusaidie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Eh basi labda anisaidie Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nataka kutoa ufafanuzi kuhusiana na hoja ya Mhe. Hamza na hasa pale alipokuwa akigusia Mfuko Mkuu.

Ninachotaka kuongeza Mhe. Mwenyekiti, kwanza bajeti ya Serikali tayari tumeshaipitisha, bajeti kuu tayari na kitabu hichi hapa, lakini pia kilielezea mfumo mzima wa bajeti kwa mwaka 2016/2017, na katika matumizi ya kawaida liko fungu la mishahara ambapo kwa mwaka 2016/2017 ni jumla ya shilingi bilioni mia mbili ishirini na tatu nukta tatu (223.3 Bilioni), lakini pia ruzuku ya mishahara pia imeshaelezwa ni shilingi bilioni ishirini na saba nukta nne (27.4 Bilioni) na tumeshaipitisha.

Sasa Mfuko Mkuu nao una matumizi yake, na tumeshapitisha hapa ambapo Mfuko Mkuu huo kwa mwaka 2016/2017 ni bilioni thamanini na mbili nukta tatu(82.3 Bilioni). Sasa nilikuwa ninaomba kama kuna mazingatio yoyote ni vyema yakazingatiwa lakini tukayafikiria kwa bajeti ijayo. Kwa bajeti hii tayari tumeshaipitisha na sioni *room* ya kuwa na *flexibility* ya kutoa mafungu mengine kuongezea mafungu ya mishahara. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kutoa ufafanuzi huo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Hamza

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nitakaa na Wizara lakini nitarudi kwenye Hansard za Serikali, kuhusu suala la marekebisho ya mishahara ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Tukienda kwenye Hansard za kipindi kilichopita za Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hizo ndio tutakazokuja na fat-wa ya kumaliza suala la Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

Kifungu SG020201	Programu ndogo ya Usimamizi wa Shughuli za Uendeshaji na Utawala Unguja	1,119,355,000
Kifungu SG020202	Programu ndogo ya Usimamizi wa Shughuli za Uendeshaji na Utawala Pemba	1,280,122,000
	Jumla ya Kifungu	**2,399,487,000**
	Jumla Kuu	**5,232,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PG0301 Programu Kuu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria
Kifungu SG
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini vile vile kwa ufafanuzi wake mzuri lakini sikuufahamu kwenye suala langu la silaha, na nitaomba aninukuu kwenye mchangio wangu niliozungumza jana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu nilichokizungumza mimi naamini Serikali inataka pesa, na kwa maana ya kwamba inataka pesa tunakusanya mapato hapa ya wauza tungule kwa maana ya kwamba iingize *income*; sasa kwa *project* yangu mimi niliyoipendekeza nairejea tena ili uifahamu vizuri, inawezekana binadamu jana hujaisikia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nili-*propose project* ya *fire arms* ambayo nilimaanisha *short gun* ni bunduki ya Wasasi wanaotumia Zanzibar pamoja na *air gun* ambayo inatumika kupigia kama Kunguru au mdugu yoyote ambaye anakusumbua katika maeneo yako; hizi silaha mbili hizi Zanzibar zinaruhusiwa na zinatoa leseni *official* kabisa. Silaha hizi zinapatikana wanaenda kununua Dar es Salaam lakini hapa Zanzibar kwa mwaka uliopita wa nyuma kuna watu wanamiliki silaha hizi za kulindia na *air gun* watu zaidi ya mia nne kwa mwaka uliopita 2014/2015 mimi mwenyewe binafsi nimeona buku.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kazungumza katika hoja yake kwamba kuleta silaha ni moja ya jambo hatari ndani ya Zanzibar, lakini je, hizi bunduki zinazotumika kwa nini zimeruhusiwa na watu wanatumia, hilo suala langu moja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ningeweza kumuelewesha zaidi kwamba Zanzibar ni nchi, na yeye kama Mwanasheria Mkuu nataka hivyo alivyo kama anavyoonekana anajiamini nataka ajiamini zaidi kwenye kutengeneza sheria ya kutengeneza pesa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kusema kwamba Zanzibar inatoa leseni kila kitu, kwa maana kwamba Zanzibar inakukabidhi kila kitu wewe unaenda kununua tu, unarudi nayo kutoka Dar es Salaam kuja nayo Zanzibar. Kwa nini nilizungumza ofisi kama ile, kwa sababu kule Dar es Salaam iko moja inamilikiwa na Jeshi na moja inamilikiwa na mtu binafsi lakini kwa ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; nafikiri tumefahamiana.

Sasa mimi nikasema kwamba kitengo kama kile mimi ni mtu binafsi na mimi niko tayari kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watu wa Zanzibar na wa Pemba badala ya kwenda kununua Dar es Salaam, *income* ile iwepo Zanzibar zaidi, kuliko pesa yetu tukaenda tukaipeleka kule kwenye vikundi vingine ambavyo vinafaidika wakati suala lile uwezo wa kulifanya Zanzibar upo.

Mhe. Mwenyekiti, nina uhakika nalo

Mhe. Mwenyekiti: suala lako likoje.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Suala langu nataka anihakikishie kwanza, kwa sababu mimi nimerudia nilichokizungumza sijamaliza nilikuwa, lakini ninataka kujua.

Mhe. Mwenyekiti, nakwambia uende kwenye swali ili najaribu kupunguza hiyo hotuba tu.

Mimi nataka nieleze tu kwa nini Zanzibar imeweza kutoa leseni kila kitu halafu tunaenda kuchukua Dara es Salaam tunakuja kutumia, wakati yeye kazungumza kwamba hilo suala kuleta silaha ni suala la hatari, kwa nini Zanzibar watu wanamiliki zile silaha na wanazo zaidi ya watu mia nne, hilo ndio suala langu mimi. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nilipomjibu Mheshimiwa Nadir suala lake nilifafanua kwa uwazi kidogo, kwamba kwanza eneo hili la ulinzi na usalama ni eneo ambalo ni moja katika mambo ya muungano, eneo la ulinzi na usalama ni moja katika mambo ya muungano.

Na huko Marekani wanakouza silaha madukani tabu yake tunaiona sasa hivi kwenye TV, kila wakiamka asubuhi unasikia watu wanauana kama wanavyouana kuku, na ni moja ya *issue* ambayo wanaizungumza, wanataka kufanya *amendment* kwenye *second amendment* ya katiba ya Marekani kwa sababu ya jambo hili, kama uratibu wa jambo hili la silaha sio jambo dogo na wala halitaki kutunishana mfuko, kusema nani ana mfuko mkubwa aweze kufungua duka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuhakikishie, hakuna mtu mwenye mfuko mkubwa kama mfuko mkuu wa Serikali, kwa maana hili lingekuwa lina manufaa kwa Serikali wala asingehitaji Mhe. Nadir kusema hili lishughulikiwe na Serikali, lingeshughulikiwa tu zamani. Lakini nikamwambia sheria inayoratibu mambo haya ni sheria Sura 223, akisoma sheria ile kifungu cha 5 na 6 kuna utaratibu mzima ambao wamepewa Kamishna wa Polisi Zanzibar uratibu wa usajili wa silaha, uratibu mzima na hili wala hatutoweza kutunga sheria ya Baraza la Wawakilishi kwa kuratibu mambo haya.

Mimi ninaomba nilieleze wazi kwa sababu hili ni moja ya mambo ambayo inaratibiwa kimuungano. Kwa hivyo aisome ile sheria vizuri, kama kuna jambo ambalo anaona tulirekebishe tushirikiane na wenzetu tuliofanya hivyo. Lakini kwa sasa Kamishna wa Polisi Zanzibar amepewa mamlaka kamili ya kuyashughulikia mambo haya.

Mimi nadhani karibuni alipita na kuna watu alipita kutaka kusajili rekodi zao, wengine wako Mahakamani kesi zao zinaendelea, wengine wamenyang'anywa, kwa hiyo linaratibiwa tu vizuri jambo hili Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo sidhani kama kuna hoja ambayo Mhe. Nadir, sikumjibu inayohusiana na sheria hii sura namba 223.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mimi Mhe. Mwenyekiti, kama sikuridhika tabia yangu nakuwa sikubali, na kama nimeridhika huwa nakubali. Mimi suala langu liko moja tu. Unajua anapozungumza Mwanasheria Mkuu namuheshimu sana, lakini kwenye suala la *investment*, hili Baraza tukufu tunalolizungumza Baraza la Wawakilishi limejengwa na nani, ni mtu binafsi kushirikiana na Serikali, kusema kwamba mimi nataka kufanya kushirikiana na Serikali si kwamba nasema Serikali haina pesa; Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ina pesa kuliko Serikali ya Zanzibar, lakini imempa binafsi kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu ninalotaka kulizungumza, lazima tujiamini, tusikae tu tukasema vitu haviwezekani.

Mimi nina suala langu jengine ninataka kumuuliza hawa wote wanaomiliki silaha Zanzibar zaidi ya watu 400, hizo *short gun* ninazomaanisha na *air gun*, kwa nini wanatumia mpaka sasa hivi wakati yeye anasema hatari.

Na isitoshe kuna mfano kautoa Marekani ina watu milioni mia nne thamanini (480) watu wanaokaa Marekani ni nchi kubwa sana, huwezi kufananisha na Zanzibar yenye watu milioni moja *point* sita, isiweze ku-*control* mambo ya silaha wakati watu wanaomiliki hawatofika elfu moja elfu moja mia mbili ni suala ambalo mimi sikubaliani nalo. Lakini vile vile kama ni Serikali ya Zanzibar haitaki silaha kwa nini inaruhusu kutoa leseni na tunakwenda kununua na tunatumia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa suala hili nafikiri nitamfuata Mhe. Hamza kwamba kutapigwa kura, lakini kwa maana ya kwamba tusikubaliwe kufungua suala kama lile basi tusiruhusiwe tusitowe leseni, na tusiende kununua, na waliokuwa na silaha wote wanyang'anywe, hilo ndio suala langu anijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa sijui unamsaidiaje, maana silaha anazozungumza huyu ni *air pistols.*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Sio *pistol* ya moto wala sio *machine gun*, afahamu kuna kitu kinaitwa *short gun* wanaotumia Wasasi mimi mwenyewe binafsi sitaki kujitaja lakini nawajua watu wenye nayo, rafiki zangu wanaenda kusasia Bwejuu na sehemu nyengine, ushanifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Basi kaa Mheshimiwa, mpe Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu kuna watu wana silaha za usasi, wasasi wale wanamiliki silaha *short guns*, halafu watu wanazo zile *air guns* ambazo zinatumia *pellets* nafikiri ndio suala lake hilo, yeye hayupo kwenye *machine guns* na *pistols*.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, zote hizo ni silaha *whatever name you call it*, inabaki kuwa silaha. Ndio maana nikasema, ile sheria ya Kiingereza inayoitwa *arms and ammunition act*, akiisoma atajua nini kimeandikwa ndani ya sheria ile, na ninaposema hizi silaha *whether* magobole, *whether* kitu gani, hatuwezi kwa hapa, kwanza inakatazwa.

Lakini la pili hatuwezi tukafungua maduka tukayauza kama tunavyouza tungule. Kwa hiyo Mhe. Nadir kama yeye kuna rafiki zake ambao wanamiliki

hizi basi afuate utaratibu ulioelezwa na sheria ya *arms and amuninition* sura ya 223 na watasajiliwa kwa mujibu wa taratibu ulioelezwa na sheria, tena wala hana haja ya kwenda Dar es Salaam, Kamishna wa Polisi hapo Kilimani aende akamueleze na atamsajili na atampa ruhusa ya kutumia sheria hizo ambazo wanazo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti, ahsante Mwanasheria Mkuu, Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri bado hatujafahamiana. Kwa nini turuhusiwe kupewa leseni, turuhusiwe kupewa mamlaka ya kumiliki lakini tukainunue Dar es Salaam wakati ile inaruhusika kutumika Zanzibar? Sijui ushanifahamu *point* yangu. Silaha, tunapewa leseni Zanzibar, kule *authorization* inatoka Zanzibar halafu tunakwenda kuinunua tu Dar es Salaam, tunaitumia Zanzibar, isiweje lile duka tukalifungua wenyewe Zanzibar. Mbona hili suala linachukuliwa uzito kuna kitu gani?

Halafu mimi nili-*propose* kama alisikia mchango wangu, nili-*propose* ifunguliwe katika sehemu ya serikali ikiwa Madema, ikiwa kwa Kamishna ijengwe mle, sija-*propose* lifunguliwe kama duka la tungule.

Kwanza hizi silaha nataka niseme kuwa nchi zote zilizoendelea hazitoi kwa leseni *airgun* wala *shotgun* hazina leseni, masuala ya leseni hayo yako Zanzibar, ukienda kununua Uturuki, Marekani silaha zile hupewi leseni.

Mimi nimeinunua moja nchi naijua, mimi nimekuja nayo mpaka Dar es Salaam sijapewa leseni na nimefika nayo, lakini kwa leseni ya Zanzibar najitaja kwa sababu nampa kitu kwa uhakika. Nimenunua nje sijapewa leseni, na nimepita nayo kwenye ndege kakabidhiwa *pilot* imekuja mpaka Dar es Salaam, Dar es Salaam nimefanya *process* imetoka Zanzibar imekwenda kuchukuliwa na Polisi imeletwa. Sasa akiniambia masuala ya kwamba kama tungule mimi nitakuwa simfahamu mfano kama huo.

Ninachotaka kuzungumza ofisi ile ifunguliwe Zanzibar kwa kujiamini kama sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nini tupeleke pesa Dar es Salaam, silaha ya Rais inauzwa shilingi laki nane na nusu au milioni moja kuna *shotgun* mpaka shilingi milioni tatu, kwa nini tusifungue wenyewe hapa tukapata pesa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hili anavyonifahamisha yeye mpaka sasa naona sijamfahamu wala silifahamu mpaka nijue kinachofahamika nitalikubali.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi nakuomba kitu kimoja, tusiende kwenye kura, ukakae na Waheshimiwa uzungumze nao uwafuate ofisini uwaelekeze.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mimi nilizungumza sana lakini kuna mifano hawezi mtu kuzungumza sijui kama tungule, sijui kama maana yake ina pesa. Katika serikali mimi sijaidharau kusema hivyo, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, nimembana nikampa mifano kwa nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina *share* kwenye *Zantel*? Kwa nini kuna miradi serikali inaingia *shares* na watu binafsi, kwa nini isifanye wenyewe basi kama hawataki kuingia na watu *private*.

Mimi ninachozungumza kwenye suala la biashara hili suala linawezekana kwa akili yangu, sio mwanasheria, lakini linawezekana, la sio hivyo akafutishe leseni zote Zanzibar zinazotoka na watu wenye silaha zote wanyang'anywe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nadhani Waheshimiwa Wajumbe majibu ambayo yamejibiwa na serikali kupitia Mwanasheria Mkuu nadhani yangetosha kabisa kutoa maelekezo na hoja ya Mhe. Nadir. Lakini mimi nadhani tunapokuwa hapa Barazani kuna mambo mengine tukiyazungumza *hansard* zipo kwa mfano, mfano ambao ameutoa Mhe. Nadir Abdul-latif kama hivyo ndivyo, na kama itakuwa hakufuata ule utaratibu ambao Mhe. Mwanasheria Mkuu ameufanya maana yake hilo ni kosa kisheria. Kwanza aelewe hivyo kama ndivyo.

Sasa mimi nadhani nimuombe Mhe. Nadir kwa sasa hivi sheria ambayo tunayo ni ile ambayo ameisema Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na huyo Kamishna wa Polisi ambaye anatoa ruhusa ya kumiliki hayo magobore anafuata sheria hiyo hiyo, yeye amepewa mamlaka kwa hapa Zanzibar kama Kamishna wa Polisi ambaye anaifanyia kazi hiyo sheria.

Kwa hivyo, mimi niombe Mhe. Nadir akubali kwamba hili jambo kwa sasa hivi tuendelee na utaratibu tulionao mpaka hapo baadae, Serikali ya Zanzibar kama wazo alilolitoa tutakaposhauriana na wenzetu, kwa sababu hili jambo linamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatuna mamlaka sisi hapa kama Zanzibar kwa sababu hili ni jambo la ulinzi na usalama, na suala la ulinzi na usalama ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, yale mengine ambayo yatakuwa wamepishana kilugha na Mwanasheria Mkuu ni mambo ya kawaida, na nadhani wakubali kwamba pengine hiyo inawezekana itakuwa amezungumza kitu Mwanasheria Mkuu pengine na yeye kimemkwaza tuvumiliane.

Kwa hiyo, mimi nadhani tukubaliane kwamba hili jambo tuliachie, sheria iliyopo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kutoa mamlaka kwa umiliki wa silaha mpaka hapo baadae serikali itakavyoamua vyenginevyo, lakini kwa sasa hii sheria ndio iliyopo. Nimuombe sana Mhe. Nadir Mwakilishi wa wananchi wa Chaani akubaliane na hoja za Mhe. Mwanasheria Mkuu ambazo amezitoa. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana unajua sisi sote binadamu mimi nilichokifanya hapa sikukosea nimeishauri serikali, nimetoa mawazo na nimemshauri yeye Mwanasheria Mkuu kwa uwezo aliokuwanao ailete sheria sisi sehemu ya silaha, isipokuwa kibinadamu mimi kama Mheshimiwa wa Jimbo la Chaani namuomba radhi kama nimemkosea, kitu *openly* sina tatizo ndio mambo ya Bunge. Kuna Mabunge mengine mpaka wanapigana kwa masuala ya kutetea haki na pesa za serikali.

Mimi namuomba radhi yeye kibinadamu kabisa, lakini kwenye suala la kutengeneza pesa katika serikali yetu nitakuwa mkali kweli kweli, kwa sababu haiwezekani, kuna vitu vyengine uwezo wa kufanya sisi wenyewe tunao halafu tusivifanye hata kama tuko chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mimi hili nitaliachilia kibinadamu kwa kuwa sisi sote ni Waislamu sitaki kugombana na mtu nimeshamuomba radhi, na yeye hana haja hata ya kunirejeshea kuniomba radhi, namuheshimu kama mkubwa wangu. Na hii hoja naridhika nayo naipitisha kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu juu ya sheria nilimuomba Mhe. Waziri atapokuja kufanya majumuisho anambie ni lini serikali italeta mswada wa kurekebisha sheria ya udhalilishaji, ambayo ile ya zamani sasa hivi ina karibu miaka 100, iliundwa mwaka 1807.

Vile vile katika suala la sheria kuna sheria moja ya mwaka 2011 juu ya kuongeza umri wa kustaafu baada ya miaka 60 mtu unamuongezea mkataba miaka miwili (*contract)*. Nafikiri hii imepitwa na wakati, kwa sababu kuna kundi kubwa sana la vijana wenzetu ambao wanamaliza skuli wanakuwa hawana kazi ambapo nafasi zinachukuliwa na wazee ambao tayari wameshafanya kazi miaka 40 na wameshafika miaka 60, wanapewa tena nafasi

wanazidi kutubania zile nafasi ambapo hatuwezi kupata. Nafikiri vile vile serikali inambie lini itakuja na sheria hii hapa angalau tuweze kuiondoa ile sheria kandamizi kwa vijana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mhe. Abdalla Maulid Diwani na amelisema hili nilipokuwa nikimsaidia Mhe. Waziri wa Uwezeshaji kama sheiria ya ushahidi *evidence decree* ni ya tarehe 17 Januari, 1917 na nikasema mwakani inatimia umri wa miaka mia moja na mambo mengi yanatukwaza kuyatekeleza kwa sababu ya sheria ile kuwa ya zamani.

Sasa nimuahidi tu Mheshimiwa kwamba tayari sheria ile imeshafanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria na ni miongoi mwa sheria ambazo tayari ziko wizarani ambazo zinasubiri tu kupelekwa kwenye Baraza la Mapinduzi ili zije kwenye Baraza la Wawakilishi. Sasa nimhakikishie kabla ya kumaliza muda wa Baraza hili la Tisa basi sheria ile italetwa ya ushahidi na itapitishwa na Baraza hili.

La pili lilikuwa *extended service. Extended Service* imeelezwa kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011. Ukisoma kwenye kifungu cha 60(1), (2), (3), (4) imeelezwa utaratibu mzima wa jinsi ya ajira.

Na nilisema wakati nikimsaidia Mhe. Waziri kujibu baadhi ya hoja kama umri wa kustaafu bado umebaki ni miaka 60 kwa lazima na kwa hiari ni miaka 55. Lakini sheria ikaongeza muda wa miaka miwili mpaka mitatu kwa mtumishi wa umma kuweza kuongezwa utumishi, inaitwa *extended service*, na unapoongezwa ule muda unakuwa haki zako pia hupati.

Pia nikasema sio mtumishi mwenyewe anayeomba kuongeza muda, ile taasisi yake ndiyo inamuomba, lakini ile taasisi yake ikimuomba haimalizikii pale inabidi pia ipelekwe kwenye Tume ya Utumishi husika. Tume ya Utumishi husika pia itizame zile hoja ambazo zimejengwa na yule muajiri kwa nini huyu mtu aongezwe miaka miwili baada ya kustaafu kwa umri wake wa miaka 60.

Kwa hiyo, sio utaratibu tu wa hivi hivi ni utaratibu kidogo inajibu ile taasisi ijenge hoja. Tume ya Utumishi husika nayo izipitie zile hoja na ikikubaliana na zile hoja ndio inatoa idhini na kibali cha yule mtu kuongezwa miaka minne.

Sasa ni kweli hiyo sheria ipo na nikasema ukitizama *ratio* ya wale wanaotoka na wale wanaobaki, wale wanaobaki sio wengi Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli ni wachache tu wanaobaki na ni wataalamu kwenye fani fulani

wanaombwa waendelee na kazi kwa kipindi fulani. Kwa hiyo, nadhani hili nimelijibu vizuri Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante pamoja na maelezo mazuri ya Mwanasheria Mkuu sikatai lakini bado nashikilia pale pale kwamba ile sheria uliyosema kwamba itakuja ndani ya Baraza la Tisa ni lini, 2017, 2018, maana yake Baraza la Tisa lina miaka mitano isijekuwa mpaka tunamaliza hapa ile sheria haijaja itakuwa hatujatendewa haki, kwanza hilo.

La pili juu ya hii sheria ya mikataba. Nafikiri bado tukumbuke kwamba kuna kundi kubwa sana lina-*graduate* nje linataka nafasi, haiwezekani mtu kaanza kufanya kazi ana miaka 25 ikawa bado umuongezee kama ana uzoefu mkubwa. Je, huyu ambaye ataanza atapata lini uzoefu. Nafikiri bora sheria ile kwa sababu ni kandamizi kwa upande wa vijana ifutwe, tuletewe sheria mpya kwamba kusiwe na kitu kama hicho. Kwa sababu kuna kundi kubwa sana Mheshimiwa na kila siku tunasikia ajira, ajira, utakuta watu wanakaa mpaka masjala anaongezwa mkataba wa nini. Ni lini tutaletewa hii sheria ili sisi tuweze kukiachia hiki kifungu kiendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Maalim Haroun Ali Suleiman nadhani Mhe. Mjumbe keshakubali kwamba tuendelee au vipi?

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Aa, anijibu ni lini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimefurahi umeniita mwalimu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani hivi sasa sheria hii iko mikononi mwa Makatibu Wakuu kwa utaratibu wa kiserikali, ikitoka kule inakwenda serikalini inaletwa katika *senate* tunaijadili. Sasa inategemea ratiba yetu ya *cabinet agenda* ziko vipi, lakini *Inshaallah* kama tulivyoahidi tutajitahidi tuiharakishe tuilete kwa sababu ina umuhimu wake haraka iwezekanavyo katika kipindi hiki hiki cha mwaka huu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ni sheria ipi anayonambia anafanya haraka aniletee katika hizi mbili, kwa sababu nimezungumza sheria mbili Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Sheria ya udhalilishaji haijafutwa na inaendelea. Kwanza kwa *rare profession* ndio tunatoa ile *extended time,* kwa *professor* maalum na kama

kuna tatizo kwa mfano kuna mtu kachukuliwa kwa makosa sidhani kama hilo limetendeka kwa upande wetu hatujafanya makosa hayo. Tunachofanya sheria tunayoizungumzia tutaileta ni sheria ya ushahidi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, unajua sio kama namkomoa mwalimu wangu isipokuwa tupo katika taratibu. Kikubwa amesema inafanyiwa mori, unajua siku zote serikali majibu ya haraka haraka ya kisiasa ndio inatengeneza, tusubirini italetwa, nafikiri tuondokane kule. Kwa sababu mwisho wa siku Mhe. Mwenyekiti, kuna wanafanya, wanasema kwamba wanafanya busara zaidi, busara ni nafasi yake lakini katika masuala ya uongozi wa nchi hususan kwa kutetea wananchi wako tufuate taratibu na sheria zetu.

Kwa hivyo, mimi bado sijaridhika na suala lake anitajie muda gani italetwa hii katika kikao kinachokuja pengine baada ya bajeti mwaka 2017, 2018, hapo nitaweza kuridhika Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, serikali inaendeshwa kwa utaratibu na mimi naheshimu sana utaratibu wa serikali na nimekula kiapo kwamba nitaheshimu kanuni na Katiba. Kwa sababu siwezi kuja hapa nikasema kitu ambacho sina uhakika nacho kwamba lini nitaleta, nitakachosema ni kwamba tutaiwasilisha sasa inategemea na utaratibu wa kiserikali.

Sasa hivi ikitoka kwenye Makatibu Wakuu inakwenda kwa Baraza la Mawaziri, halafu baadae Baraza la Mawaziri tunauwasilisha mswada huu tunauleta hapa Barazani, siwezi kukaa nikasema mengine yoyote ambayo nitakuwa nadanganya na nitakuwa nakwenda kinyume na kiapo changu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hiyo *process* anayoizungumza iko nje ya *control* yake Mheshimiwa, kwa hiyo hawezi kukuhakikishia. Mimi nimeshawahi kuwa waziri najua, hawezi kukuhakikishia kwamba kikao fulani *absolute* itakuja lazima ipite kwenye hizo *process*. Kuna wataalamu wale sijui ndio Makatibu Wakuu wakimaliza wao iende kwenye BLM, ikitoka huko ndio ije huku, yaani ni *process* ambazo haziko kwenye *control* yake kabisa. Kwa hiyo, ukimtaka lazima akupe tarehe utamuonea mwalimu wako.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, sawa naridhia kwa hili tuendelee Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi) lakini *issue* moja tu.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, mimi *issues* zote nimeshazizungumza tena kwa nia njema kabisa.

Mhe. Mwenyekiti katika maelezo yangu nilipochangia jana mchana saa sita na nusu mpaka saa saba kasoro dakika tatu, ukurasa wa saba wa hotuba hii ya Mhe. Waziri moja katika kazi zake alizozungumza ni kusimamia utekelezaji wa Katiba ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na katika eneo moja lililo la sheria ni Sheria ya Uvuvi wa *Deep Sea Fishing*, mimi nikataka maelezo juu ya sheria hii tumefikia wapi, lakini alipozungumza japo juu juu tu alikuwa anieleze kwamba ana mpango gani juu ya hili hayo maelezo hayakutolewa kabisa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama atakumbuka Mhe. Mjumbe wakati Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi alipokuwa akichangia hoja hii alielezea utaratibu wa hii Sheria ya *Deep Sea Fishing*, alielezea. Sina hakika kama Mhe. Mjumbe alikuwepo lakini nadhani majawabu yametolewa juu ya utaratibu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti: Nakumbuka Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika mchango wake aligusia hicho kitu.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Naomba tuendelee.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimuuliza waziri kwa maandishi baadhi ya taasisi za serikali zimeruhusiwa kutengeneza sheria ndogo ndogo za kukusanya mapato.

Nilitaka nipate jibu hawa wanasheria wa kujitegemea wameweka ofisi zao za wanasheria lakini wanatengeneza mikataba ya kuuziana kama viwanja, magari na majumba. Je, wao wana sheria gani inayowaruhusu, na hizi fedha ambazo wanazipata zinaingia serikalini au zinaingia wapi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sheria inayowaongoza wanasheria wa kujitegemea inaitwa *Legal Practitioners Decree*, ya zamani kidogo ya muda mrefu na ni miongoni mwa sheria ambayo iko katika utaratibu wa kuifanyia marekebisho. Wao kwenye sheria ile ndio umewekwa utaratibu ule wa kutoza ada zao, kwa sababu ada zilizomo mule ni za zamani. Lakini nikubaliane naye kwamba kwa sasa hivi hakuna utaratibu maalum inategemea umekwenda kwa nani, ukienda kwa *firm* kidogo inajiweza iko vizuri *charge* zake zitakuwa kubwa, ukienda kwa mwengine kidogo ndio kwanza mpya anaanza *charge* zake zitakuwa ndogo. Sasa hili ni moja ya eneo ambalo kusema

kweli inabidi tuliratibu na tulishughulikie vizuri. Kwa hiyo, tutapoleta ule mswada wa sheria ya kufanya mabadiliko ya ile *Legal Practitioners Decree*, haya ni moja ya maeneo ambayo itabidi tuyaratibu vizuri. Nakushukuru.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, je, haoni kama anatunyima haki au mapato Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa sheria hiyo ambayo ilikuwa inatumika wakati huo kwa sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nadhani atakuwa ameliona hilo ndio maana anasema sasa wanataka kuliratibu walete sheria ya kurekebisha hiyo hali kama nitakuwa nimemfahamu vizuri Mheshimiwa. Wanajaribu kuliratibu sasa ili likae katika utaratibu huo ambao wewe unautaka.

Kifungu SG030101 Programu ndogo ya ubora na ufanisi wa huduma za kisheria

Jumla **Shs. 610,786,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PG 0302 Programu ya Utawala

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Mwanasheria Mkuu anamsaidia Mhe. Waziri kutoa majumuisho akaijibu hoja yangu niliyomuliza alikiri kamba wanapokea ada za usimamizi wa kesi kwa zile taasisi za umma. Lakini kwenye kitabu chake hazimo na zile pesa haziingii serikalini. Sasa nataka kujua kwa nini zile pesa haziingii serikalini. Nilikuwa naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Mhe. Mjumbe amekiri ni kweli nililitolea ufafanuzi jambo hili na nikasema kwenye zile taasisi ambazo zinajitegemea za serikali mfano Benki, Mashirika haya; *ZECO*, Shirika la Bima na mashirika haya mengi ya serikali ukitizama ule muundo wake wa kisheria mashirika yale yanajitegemea na yana hadhi ya kushitaki na kushitakiwa na yanaposhitaki au yanaposhitakiwa yana ruhusa ya kutafuta ushauri wa kisheria kwenye taasisi yoyote.

Kwa utaratibu ulivyo sasa hivi wa kisheria ni kwamba lazima sasa waishirikishe Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kwa sababu zile ni taasisi ambazo zinafanya biashara na zinaingiza pesa, wanachofanya kwetu sisi

tunawatoza ada tu ndogo ikiwa ni kama motisha ya wale wanasheria ambao wanashughulikia ile kesi, ni kama motisha tu. Wala si fedha nyingi ambazo tunawatoza na zinaingia kwenye mfuko wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazigawa kwa wanasheria ambao wanalisimamia jambo hili.

Sasa akisoma sheria yetu namba 6 ya mwaka 2013 imeeleza vizuri utaratibu wa jinsi gani Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa sababu sasa hivi tumeuweka kisheria. Mwanzo tukiufanya hivi hivi kiutaratibu limetoka toleo wizarani. Lakini sasa hivi tunaliratibu kisheria na zinazoingia zile fedha hatupeleki kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali zinaingia pale afisini na inakuwa ni kama moja ya motisha kwa wale wanasheria ambao wanasimamia kesi hiyo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Nakushukuru kwa majibu mazuri lakini haioni kwamba hizo fedha kuingia kwenye Mfuko wa Mwanasheria Mkuu na kuingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali huku ni bora zaidi kuliko kwa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa Mwanasheria Mkuu ni kama motisha kwa wale.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Amesema kama motisha lakini kwa taasisi nyengine kama ya *GAG* wanatoza zile *fees* kwa nini na wao basi wasitoe kama motisha wakawa wao *GAG* wanazipeleka kwenye Mfuko Mkuu wao wasizipeleke, basi na *GAG* nao waruhusiwe *audit fees* zile wapewe kama motisha.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hili la *GAG* nitamwachia mwenyewe Mheshimiwa atalijibu lakini sidhani kama Mhe. Mwenyekiti, alipochangia hoja yake alilizungumzia la *GAG*. Alichozungumzia ni Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, hoja ni ya Mwanasheria Mkuu sio.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ndio Mwanasheria Mkuu wa Serikali sio la *GAG*, kwa hiyo sidhani kama sasa hivi tunaweza tukalitolea majibu.

Lakini kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina *vote* yake ndio hii tunayoijadili, hii G03 na ndio hii tunaijadili kama nilivyosema ile inakuwa ni motisha kwa wale ambao wanazishughukia zile kesi kwa sababu wangeachwa kuja pale wangepelekwa watu wa nje kwanza gharama zake ni kubwa wangelipa pesa kubwa.

Lakini pia sisi tunavyofanya hizi kazi tunashirikiana na wale Wanasheria ambao wako kwenye zile kazi ili pia kuwajenga uwezo ili yanapotokea yale mambo kwa siku za mbele waweze kuyasimamia wao wenyewe. Kwa hiyo, hatupeleki, ni kweli kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na zinapoingia zinaingia kwenye *vote* ya G03 na zinagawanywa kwa utaratibu ambao nimeueleza. Nakushukuru.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mimi kwanza nataka nimsahihishe tu nilipokuwa najenga hoja hii nilitoa mfano wa *CAG* kwamba wao wanatoza kodi pamoja na Idara ya Upimaji kwamba nao wanatoza ada.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa lakini hapa hili fungu halihusiani na *CAG* tunapitisha mafungu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Huo ni mfano tu nimetoa kwamba kulinganisha kwamba *GAG* wao wanatoza...

Mhe. Mwenyekiti: Kwa sababu ulikuwa unaomba na *CAG* naye afanyiwe sio pahali pake hapa.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ndio mimi nimetoa mfano kwamba *AG* aige mfano wa *GAG* ndio hoja yangu iko hapa. Lakini zile pesa wanazotoza zile ziende kwenye Mfuko wa Serikali kama zinavyokwenda kwenye *audit fees*, ndio hoja yangu mimi iko hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, unataka vipi?

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Pesa wanazozitoza ziende Mfuko wa Serikali zisiende kwa Mfuko wa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Anataka hiyo motisha msiwe nayo ipelekeni kwenye Mfuko Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Sikumfahamu Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa yaani wapeleke kule, halafu iweje?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ni kama hoja sisi tumesema tunai- *retain* pale kwa sababu ya kutoa motisha kwa hawa watu ndio ku- *raise performance* ya hawa watu. Lakini pia kuwapa motisha kwamba jamani tunayasimamia haya

mashirika lakini kuna *token* ambayo tunapata haiendi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Sasa inawezekana hiyo hoja labda mimi sikuifahamu. Lakini ninachosema mimi utaratibu uliopo sasa hivi ni huu kama inapokuja ile inaingia kwa jina la Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameruhusiwa na serikali kuzitumia fedha hizi kwa utaratibu ambao nimeueleza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria Mkuu mimi rafiki yangu sana na namshukuru sana kwamba hoja yangu aliielewa na nimeijenga hapa sikuijenga katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu tayari tumeshapewa kazi na Mhe. Rais mimi na yeye Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Sasa lile agizo nadhani sijui tulifanye kwa maandishi au tufanye utaratibu gani lakini hapa pia ni pahala pake. Kwamba aliagiza Afisi ya Spika kwa kuwa Mwanasheria Mkuu tulipokuwa tumeipeleka sheria ile kwa Mhe. Rais yeye alikuwa bado ni mgeni, akasema basi na yeye aende akajifunze kwa sababu hoja tuliojenga kwamba Mawaziri wahusika tulikwenda nao pamoja na Mwanasheria Mkuu.

Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema basi sawa tuendelee na utaratibu lakini ile tuendelee na utaratibu hakufafanua tuendelee nao vipi. Sasa mimi nilikuwa na ushauri ile sheria imeshakaa muda mrefu na tunakwenda sasa hivi kutokuwa na sheria ile. Baraza la Wawakilishi tunakwenda nje ya maazimio ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola ambayo *conventions* zake ninazo hapa sina haja ya kuzisoma kwa sababu itachukua muda mrefu.

Sasa nilikuwa nataka Mhe. Mwanasheria Mkuu atusaidie kwa sababu suala la sheria hii linahusiana vile vile na vifungu vya Katiba na suala la vifungu vya Katiba lazima Afisi ya Mwanasheria Mkuu iweze kuhusika moja kwa moja. Sasa labda niambiwe tu kwamba suala la sheria hii ya Utawala na Utumishi wa Baraza la Wawakilishi iletwa lini.

Lakini vile vile je, sheria hii haioni sasa serikali iko haja ya kuirejesha kwenye mikono yetu ya Baraza la Wawakilishi ili kufuata matakwa ya Katiba Ibara ya 77 ili sheria hii tuweze kuja nayo na Baraza la Wawakilishi liwe na sheria yake ya Utawala. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na kama nilivyosema nimemshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma amerudi na kazi ile ile ambayo amemaliza nayo ya sheria hii kasi yake bado inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli toka tupate maelekezo na maagizo ya Mhe. Rais hatujakutana na kwa sababu kati kati mambo mengi yalitokea kulikuwa kuna uchaguzi. Kwa hiyo, hatukuweza kukaa tukalijadili kwa upana suala hili. Nitachofanya kama nitaiandikia barua Afisi ya Spika kuikumbushia yale maelekezo ambayo tulipewa na Mhe. Rais ili sasa tuanzishe tena mjadala wa kuishughulikia sheria ile, nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mjadala ulikuwa umeshakwisha ulikuwa utekelezaji. Sasa hili nilikuwa naomba tu msaada wa Afisi yako ya Mhe. Spika. Kwa sababu Afisi ya Mhe. Spika, ndio *facilitator* wa suala hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu yeye ataleta barua lakini mtekelezaji wa suala hili ni Afisi yako wewe Mhe. Spika, na hii sheria kwa kweli kama nilivyosema Baraza la Wawakilishi tumeachwa nyuma sana, na ile mikataba na maazimio ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

Sasa sijui kama kiti chako kinaruhusiwa na wewe kutoa kauli kwamba je, kwa sababu mimi nimependekeza kwamba sheria hii ije mwezi wa Oktoba. Kwa hiyo, hayo maagizo ya Mhe. Rais nafikiri ndani ya kipindi baada ya kumaliza Baraza Afisi yako iweze ku- *facilitate* ili inapokuja Oktoba tulete sheria hii ili tuweze kuwa na sheria ya Utawala wa Baraza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba maelekezo yako kwa sababu hapa inategemea nguvu yako. Mhe. Mwanasheria Mkuu kazi yake akishaleta barua kazi yake itakuwa ishamaliza, kazi inayobakia itakuwa ni kazi yako Afisi ya Baraza la Wawakilishi naomba maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi siwezi kukupa maelezo, mimi nitasubiri barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu. Hiyo barua yake ikifika kwangu mimi kazi ndio itaanzia hapo. (*Makofi*)

Kifungu SG 030201	Programu ndogo ya Utawala na Usimamizi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu	
	Jumla	Shs. 457,818,000
	Jumla Kuu	Shs. **168,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu G0401 *Administration* Unguja Shs. 47,900,000

Kifungu PG0401	Programu Kuu ya Uendeshaji na Usimamizi wa kesi za Jinai ...

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti hizi fedha tunaziona na najua Mhe. Waziri wa Fedha ameshatoa maelezo na katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha aliongea kwa mapana sana juu ya programu nzima juu ya Bajeti ya Serikali.

Hapa nilikuwa nataka kushauri tu endapo hali itaruhusu kuwa nzuri na kutokana na khofu na maelezo mengi waliyoongea Wajumbe pamoja na mimi mwenyewe hasa katika masuala ya madawa ya kulevya, na hapa kama ndipo kwenye kitovu juu ya hizi kesi basi naomba hawa waweze kuimarishwa, wasaidiwe kifedha ili mambo yawe mazuri. Tuendelee.

Kifungu SG040101	Programu Kuu ya Uendeshaji na Usimamizi wa kesi za Jinai	
Jumla		Shs. 1,163,569,000/-
Kifungu PG0402	Programu Kuu ya Mipango na Uendeshaji katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	
Kifungu SG 040201	Programu Kuu ya Mipango na Uendeshaji katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	Shs. 178,061,000/=
Kifungu SG 040202	Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Mashtaka Pemba	Shs. 307,971,000/-
Kifungu SG 040203	Programu ndogo ya kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar	Shs. 54,800,000/-
	Jumla	Shs.54,800, 3100
	Jumla Kuu	**Shs. 1,704,400,00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, wala sitaki kupiga buti wala sina nia ya kupiga buti. Hii ningemuomba Mwanasheria Mkuu tu kidogo kuna sheria nafikiria toka Hayati Mzee Abeid Karume hazijafanyiwa marekebisho.

Kuhusu sheria za mavazi nilipochangia jana nikazungumza kuwa sheria hizi ni za muda mrefu nafikiri toka Hayati Abeid Aman Karume hazijaletwa tena Barazani na Mwanasheria atatusaidia pengine mimi ni mshamba nimezaliwa shamba, natoka shamba, nimekuwa shamba atanisaidia kidogo.

Halafu vile vile kuna sheria ya kula mchana na keshokutwa tunakaribia mwezi mtukufu wa Ramadhani serikali nafikiri haijatoa kauli yoyote kuhusu suala hili. Wakati ule alikuwa Mhe. Abubakar Khamis alikuwa akilipigia kelele akilisimamia lakini nafikiri hakuna sheria vile vile. Mimi nilikuwa nataka ufafanuzi tu wala sina nia ya kutaka kupiga buti. Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa heshima naomba anifahamishe, elimu yangu ni ndogo mimi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Jaku Hashim Ayoub nadhani angeiga *sprit* ya Mhe. Hamza Hassan Juma ya kuleta mswada binafsi.

Sijui Mhe. Mwenyekiti, sijui Mhe. Jaku Hashim Ayoub anataka kitu gani kama kitu ambacho amekiona ambacho watu hawavai vizuri ili tulete hiyo sheria. Sijafahamu kidogo labda angekuwa muwazi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Inaonekana hizi sheria zipo labda kwa sababu hichi ni kifungu cha kurekebisha sheria. Mhe. Jaku Hashim Ayoub hebu mfafanulie kidogo Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa bahati nzuri nazungumza Kiswahili wala si kihindi wala kizungu. Mhe. Mwanasheria kwa heshima kabisa hapo zamani kama sikosei nilipokuwa nikihadhithiwa. Kuwa sheria ya Mhe. Mzee Abeid Aman Karume kulikuwa sijui kama kuna sheria au kanuni kuhusu mavazi ya nguo fupi. Hivi sasa tunaona mila na desturi zetu zinazidi kubomoka na maadili yetu ya Kizanzibari.

Sasa nataka kujua hii sheria ipo au haipo, haiko hai. Na vile vile tukashuhudia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani baadhi ya mahoteli kufungwa, sijui kuna kanuni au sheria na watu kula mchana wakikamatwa. Sijui kama umenielewa Mhe. Mwanasheria au nirudie tena.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda nimwambie Mhe. Jaku Jashim Ayoub kama hivi karibuni moja ya jambo ambalo tumelifanya kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Sherikali ni kupeleka mbele ya Baraza la Mapinduzi orodha zote za sheria ambazo ziko Zanzibar na zile ambazo zinahitaji marekebisho.

Na agizo ambalo limetoka Baraza la Mapinduzi kwamba sasa kila Waziri, kwa sababu tulizitaja ipi inasimamiwa na nani, ipi inasimamiwa na wizara gani na ipi inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Sasa nimuombe Mhe. Jaku Hashim Ayoub sina kumbukumbu, ninakumbuka kama alivyosema Mhe.Mwakilishi lakini kama ipo na imekabidhiwa kwa sekta basi hiyo sekta itatizama. Kama inaona kuna haja ya kuleta *amendments*, ninadhani italeta, ikiona watu wanavyovaa hivi siku hizi, wanavaa uzuri inatosheleza basi hawatoleta Mswada huo wa kufanya marekebisho ya sheria. Lakini nimuhakikishie kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 78 ya Kanuni zetu za Baraza yeye pia ana haki ya kuleta Mswada binafsi kama ambavyo Mhe. Hamza Hassan Juma ameanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe.Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kidogo nimemfahamu lakini siyo sana. Kwa hili kuhusu Sheria ya Kula Mchana Ovyo ipo sheria hiyo. Isiwe tunakamata watu tu tunawatia ndani wakati hatuna sheria, wakifika Mahakamani wakaachiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Kula mchana kwenye mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe.Mwenyekiti, katika kupitia sheria zetu za Zanzibar sikumbuki kuona kama kuna sheria hiyo ambayo Mhe. Jaku aliyoielezea. Lakini *of course* kutokana na mila na desturi zetu, Zanzibar ikiwa kama asilimia kubwa ni Waislamu, inapofika mwezi Mtukufu wa Ramadhani hutolewa tangazo maalum la Mhe.Waziri wa Katiba, Sheria la kuuelezea mwezi wa Ramadhani lakini maelekezo ya nini kinatakiwa kifanyike katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Moja ya maelekezo ambayo anatoa ni hayo kama katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani basi yale maduka ambayo yanauza vyakula, inabidi sasa yafungwe, yale ambayo wanauza *chips* mchana inabidi pia yafungwe. Sasa ipo ni katika desturi ambazo zinafanywa na serikali inapofika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, lakini sina kumbukumbu ya kama kuna sheria hiyo ambayo Mhe. Jaku anaelezea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana naye Mhe. Mwanasheria hana kumbukumbu ndiyo maana mengine mara nyingi huwa yanampita mpaka serikali akaishauri vyengine, mpaka sheria zika-*back date*.

Lakini kama Mwanasheria huna kumbukumbu wewe ikiwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ukiwa huna kumbukumbu wewe Mwanasheria, sisi tusemeje na tunakutegemea wewe katika chombo hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Basi na tuendelee. Mhe. Hamza.(*Kicheko*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na ninamshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu baada ya kumpa maelekezo Mhe. Mwanasheria Jaku Hashim Ayoub. Sasa naomba na mimi nipate maelezo kidogo kuhusu suala la marekebisho ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria ya *Political Party Act* ya 2002. Sheria hii imetupa nguvu za kisheria sisi wanasiasa kuunda vyama vya siasa baada ya kutekeleza au kufuata matakwa yote.

Sasa nilikuwa ninamuuliza Mhe.Mwanasheria Mkuu. Kwa sababu katika sheria ya *Political Party Act* nimejaribu kuangalia Kifungu cha 8(1) lakini vile vile nikaenda Kifungu cha 8(2) (a), halafu kidogo (i), (ii) na (iii). Labda naomba nivinukuu, nitavinukuu kwa Kiswahili, maana yake vimeandikwa kwa Kiingereza.

Kwamba vyama vyote ambavyo vimepata uhalali wa kusajiliwa visiwe na *affiliation* ya udini wala ubaguzi wowote wa aina, wa kabila, rangi au damu au upande wa mtu anayetoka. Lakini vile vile Kifungu (c) ndiyo hichi ambacho ninachotaka kujenga hoja yangu. Kinasema kwamba, "Chama chochote kisitumie nguvu au vurugu ili kutekeleza yale matakwa yao kisheria".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuuliza je, sheria hii kama kuna sheria nyengine ambayo iliyoifuta sheria hii. Na kama hakuna sheria nyengine iliyokuja kuifuta sheria hii. Ina maana sheria hii inakiukwa na mpaka sasa hivi wanaokiuka sheria wapo wanatamba na hatuoni kwamba utekelezaji wa sheria hii inafuatwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima huwa siku zote ninasema Zanzibar tuna sheria nyingi nzuri, lakini tatizo katika utekelezaji. Naomba maelezo katika sheria hii kama haijafutwa basi kwa nini sheria hii haitekelezwi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe.Mwenyekiti, kama ambavyo tunajua Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa ni sheria ya Muungano. Ni Sura 258 ndiyo Sheria inaitwa *Political Party Act*, Sheria ya Vyama vya Siasa na sheria ile ina msimamizi wake.

Na msimamizi wake ni Msajili wa Vyama vya Siasa. Sasa haya yote ambayo Mhe. Hamza ameyaeleza tumeyasikia na katika majumuisho ambayo Mhe. Waziri aliyasema ni kwamba kama serikali itapeleka hoja ambazo zimeelezwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na kukiukwa kwa masharti ya sheria ile. Na mwenye kusajili ndiyo mwenye haki ya kufuta. Kwa hivyo yatapelekwa maoni haya ambayo yametolewa na Baraza. Msajili atayapitia na yeye ndiye atakuwa na maelekezo ya mwisho na maamuzi ya mwisho kwa mujibu wa sheria ambayo yeye anasimamia.

Kwa hivyo haya tumeyasikia na Mhe. Waziri ameyapokea, na ninadhani tumekubali kama atampelekea Msajili wa Vyama vya Siasa hizi hoja zote za Waheshimiwa Wajumbe, halafu yeye Msajili wa Vyama vya Siasa sheria imemuelekeza vizuri utaratibu wa kufuata. Inabidi awaite awaeleze.

Kwa hivyo kuna utaratibu mzuri wa kisheria umeelezwa, lakini sisi kama serikali tutatimiza wajibu wetu kwa kumuandikia kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wameonesha *concerns* zao.(*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe.Mwenyekiti, ninashukuru sana maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Hii sheria kama ilivyosema ni Sheria Nam. 258 ya 2002 na ni kweli inasimamiwa na Msajili wa vyama ambaye yupo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini sheria hii inaeleza na Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini vitendo vinavyokiukwa katika sheria hii kuna suala la *violence*. Unapozungumza suala la *violence* hii haisubiri lazima Msajili afute. *Violence* hii inatakiwa ishughulikiwe pale pahali inaposhughulikiwa.

Kwa nini mpaka leo bado haya masuala ya *violence* ndiyo maana nikauliza hii sheria imefutwa. Kwa sababu ile *violence* inatokea katika pahala popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa je, hizi *violence* zinazotokea sasa hivi za kulazimisha jambo fulani, za kuwalazimisha watu wavunje sheria za nchi, wakatae kulipa kodi ambayo ni kinyume na sheria. Hili pia tunamsubiri Msajili wa Vyama vya Siasa. (*Makofi*)

Naomba maelekezo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza kama Sheria hii Sura ya 258 ni sheria ambayo inatumika pande zote mbili za Muungano. Pia nimrudishe Mhe. Hamza kwenye Kifungu cha 5 cha Katiba. Akisoma maelezo yaliyoelezwa katika Kifungu cha 5 cha Katiba, maelezo yake ni mazuri, kwa nini Zanzibar inafuata mfumo wa kidemokrasia wa vyama vingi. Imeelezwa maelezo mazuri.

Sasa ahadi ambayo imetoka kwa Mhe. Waziri ni kwamba ambayo Waheshimiwa wamezungumza, kwa sababu nguvu zile hazipo kwa Mhe. Waziri. Nguvu zile zipo kwa mtu mwengine. Kwa hivyo mwenye zile nguvu, kinachofanywa na serikali ni kama Mhe. Waziri ameahidi atampelekea barua na kumueleza hoja zimeelezwa na Wajumbe wa Baraza.

Kwa sababu yeye ndiye mwenye mamlaka haya kwa mujibu wa sheria atayapitia, halafu ninaahidi majibu ambayo yatatoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ninaamini Mhe. Waziri ataleta taarifa yake mbele ya Baraza. Lakini kwa hali ilivyo sidhani kama serikali kwa upande wetu sasa hivi tunaweza tukatoa *commitment* ya jinsi gani tunaweza kuyashughulikia haya yanayotokea kwa mujibu wa sheria hii, kwa sababu sheria hii hatuisimamii sisi.

Ni kweli yupo Naibu Msajili hapo wa Vyama vya Siasa, kwa sababu ukitazama ule muundo Msajili anapotoka upande mmoja basi Naibu Msajili anatoka upande wa pili. Lakini bado zibaki kwamba ni nguvu za Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye ndiye amepewa uwezo na nguvu kwa mujibu wa sheria hii. Kwa hivyo mimi ninadhani Mhe. Hamza atufahamu, sisi tumefahamu na Mhe. Waziri ameeleza vizuri. Sasa yaliyobaki ni utekelezaji, halafu taarifa zije zitolewe ndani ya Baraza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu Katiba ya Zanzibar. Katiba ya Zanzibar Ibara ya 5 ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameitaja nitasema ya 5(a) na (2) na (3) kwa faida ya Baraza hili.

> 5. "Zanzibar itafuata mfumo wa Demokrasia wa Vyama Vingi vya siasa vyenye kuheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu, usawa, amani, haki na uadilifu.
>
> (a) Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka ya tatu, mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria, mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki.

(2) Mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mamlaka ya kutunga sheria na utekelezaji wa shughuli za umma na Baraza la Wawakilishi, mamlaka ya utekelezaji wa utoaji haki ni Mahakama".

Sasa Mhe.Mwenyekiti hapa kuna vitu viwili. Mimi niliitaja Sheria ya Usajili wa Vyama ili kuwe kwamba je, hii sheria haijakiukwa. Lakini kukiukwa sheria ni jambo moja lakini *violence*, labda kwa kuwa nilizungumza Kiingereza, labda Kiingereza changu cha Shaurimoyo si kizuri. Suala la vurugu halihusu kufuta chama cha siasa, ile kama wamekiuka sheria Msajili aangalie.

Lakini suala la vurugu na kulazimisha kufanya vurugu kwa kulazimisha matakwa ya mtu fulani yanafanyika hapa Zanzibar na vyombo vipo vya kuweza kuzuia vurugu na kuchukua sheria. Kwa hivyo hili serikali inaweza ikachukua sheria bila ya hata hicho chama kipo. (*Makofi*)

Mimi nitatoa mfano mdogo kule Tanzania Bara Chama cha CHADEMA wanafanya vurugu, wanafanya nini, serikali inachukulia watu hatua na chama bado hakijafutwa. Hii hatulazimishi lazima chama kifutwe lakini tunataka serikali pale inapotokezea na hii sheria ipo wazi. Suala la ubaguzi wa dini, sasa hivi watu wanabaguliwa misikitini, suala la ubaguzi wa ukabila. (*Makofi*)

Vile vile kulazimisha vurugu. Mhe. Mwenyekiti, leo kuna kiongozi anapopita njia zote zinafungwa, shughuli za biashara zinafungwa ndiyo vurugu yenyewe. Hii pia mpaka tumsubiri Msajili wa Vyama afute chama. Hii kwa nini hatuwezi tukachukua sheria kumdhibiti huyu mtu na watu wake. (*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza alipopiga buti lake, alipiga buti na akasoma Sheria ya Vyama vya Siasa. Angeeleza tu kwa jumla bila ya ku-*refer* Sheria ya Vyama vya Siasa na tungemfahamu vizuri, wala nisingekaa kuueleza utaratibu mzima jinsi ya Sheria ya Vyama vya Siasa unavyoeleza.

Kwa sababu yeye ali-*refer* Sheria ya Vyama vya Siasa na mimi nikarudi kule kule kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa na kumueleza utaratibu ambao unatumika. Lakini haya mengine ambayo yanatumika kuna vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya kazi yake. Ninadhani wanafanya kazi vizuri, wapewe fursa waendelee kufanya kazi yao.

Lakini kwa sababu ali-*refer* sheria maalum na sheria mahususi, na mimi ndiyo nika-*refer* kwenye vifungu vya sheria ile ile ambayo Mhe. Hamza ameizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, *actually* alivyoitaja ile nikamuuliza Katibu hii sheria lakini mbona ya Muungano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe.Mwenyekiti, ninafikiri tumeelewana mimi na Mwanasheria Mkuu. Ahsante.

Na kwa sababu sisi tulipopewa hizi nondo na ulitukabidhi wewe hapo. Ulitukabidhi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar. Sasa kwa kuwa na yeye alinielewa kanifafanulia katika Sheria ya Vyama vya Siasa.
Pia ninashukuru kwamba amenieleza kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vipo makini tuwaachie wafanye kazi yao. Na kwa kuwa ametwambia vinafanya kazi nzuri, basi tunaangalia huu uzuri wa hiyo kazi inayofanywa na hivyo vyombo vya sheria. Na ninaamini labda hali itaweza kutulia kwa mujibu wa maelekezo yake.(*Makofi*)

Ninakushukuru sana.(*Makofi*)

SG 050101	Programu Ndogo ya Kufanyia Mapitio ya Sheria	Shs.382,500,000/-
	Jumla Kuu	**Shs.382,500,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote

SG 050201 Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji .

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kupata fursa hii. Nilipokuwa nikichangia niliuliza sheria ngapi Ofisi au Tume hii imerekebisha hizo sheria. Ninashukuru Mhe. Naibu Waziri amenijibu vizuri sana, ninamshukuru sana kwa idadi.

Lakini ninachoomba sasa, kwamba ninafuatilia sana vile vipindi vinavyotoa kwenye redio kutoa taaluma wapi, wapi. Pia ni nzuri sana lakini naomba sasa ile *speed* waongeze, tatizo lipo kwenye ile *speed* ya ile kazi yenyewe kwamba

wanachukua muda mkubwa kuelimisha jamii kuliko kufanya ile kazi ya wanasheria.

Kwa hivyo mimi nilitaka kushauri tu, wala sitaki kumsimamisha Mhe. Waziri. Nilitaka kutoa ushauri tu kwamba ile *speed* ya kazi ya kurekebisha zile sheria iende kwa kasi, ili kweli kama walivyozungumza wenzangu sheria nyingi zimepitwa na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee nilitaka kutoa ushauri huo tu basi. Ahsante. (*Makofi*)

SG 050201	Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji	Shs.126,000,000/-
	Jumla Kuu	**Shs.508,500,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote

FUNGU G 06 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

G 0601	Utawala Unguja	Shs.25, 864,000/-
	Jumla Kuu	Shs.25, 864,000/-

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote

FUNGU G 06 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

PG 0701	Programu Kuu ya Kupunguza Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nipatiwe ufafanuzi wa majibu sahihi kuhusu hatua zilizochukuliwa baada ya kugundulika mapungufu katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Serikali, ambapo kumeonekana kuna mapungufu kwa baadhi ya wizara na taasisi za serikali.

Katika majibu yake Mhe. Waziri mwalimu wetu alisema kwamba tuna haki sisi Wawakilishi kwenda kufuatilia mawizarani. Lakini mimi sikuuliza jibu lijalo, niliuliza jibu lililotangulia. Je, ni hatua gani zilizochukuliwa baada ya kukutikana mapungufu haya. Taasisi ambazo zilipata hati mbaya, hati zisizoridhisha na kwamba kuna viashiria vya upotevu wa fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilitaka nipate maelezo akanijibu kwenye jibu lake kwamba tuna mamlaka na tuna uwezo wa kufuatilia mawizarani. Hasa tukitilia maanani kauli ya Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein wakati wa uzinduzi wa Baraza letu tukufu la Wawakilishi, aliposema kwamba sasa umefika wakati wa kuyatumbua majipu yote na kuyatoa moyo.

Sasa hapa majipu haya yapo yanahitaji kutolewa moyo, kwani hawa wamevunja sheria ya fedha nambari 24, kifungu 2 sheria nambari 12 ya mwaka 2005, na zinatakiwa taasisi zote ziwasilishe hati zao za ukaguzi miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka. Kweli zilifanya hivyo na ripoti hii imeonesha wazi mapungufu makubwa yaliyotokea. Kwa hivyo, mimi naomba jibu, nilimpunguzia asilimia tano, sasa nambakishia mbili ili nipate majibu mazuri ili na mimi niunge mkono hoja. Hatua zilizochukuliwa kwa taasisi na wizara za serikali ambazo zimeonekana zina mapungufu humu, ili niweze kuunga mkono hoja hii. Mhe. Waziri naomba jibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Seif, kama kanisikiliza vizuri, wala sikusema kwamba Baraza la Wawakilishi lifuatilie.

Nilisema humu ndani kuna mawaziri, manaibu mawaziri na makatibu wakuu na watendaji wakurugenzi, kila mmoja katika taasisi yake imeguswa kwa njia moja au nyengine, basi wafuatilie na wachukue hatua. Lakini sisi ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Mahesabu zimeshawasilishwa kwenye kamati yetu ya *PAC* hapa. Sasa wao wataleta taarifa yao na sisi tutaileta serikalini, baadae tutawasilisha ripoti hapa na matokeo yake baadae tutaijadili na tutatoa maazimio yetu na kuona hatua gani tuchukue.

Mhe. Mwenyekiti, hiki kikundi ndio kimekuja sasa hivi tumekiwasilisha hapa kwa utaratibu wa kikatiba, baada ya kusoma bajeti baada ya siku 7 tunatakiwa tuiwasilishe na tumefanya hivyo.

Sasa muliuliza maswali na tumewajibuni, sasa hatua inayofuatia ni upande wa serikali na *PAC* na wao upande wao hapa tuiwasilishe taarifa yao kwa kupitia ripoti yao hapa ili tuijadili zaidi. Lakini kwanza serikali lazima ijadiliwe na

iletwe hapa baadae tuijadili vizuri, tutoe maazimio yetu na tuone kwa kiasi gani tutachukua hatua.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, lakini suala la msingi tumesema pesa za majimbo zimetumika vibaya, hilo nililisema wazi wazi na nikasema tuna wajibu wa kusimamia sisi kama Wawakilishi ili kuona kwamba pesa hizi zinatumika vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, mimi naridhika na majibu ya mwalimu, kwa sababu ni mwalimu Mhe. Waziri. Lakini bado ni muda mrefu, haoni kama huu muda mrefu na haya ndio yanayopelekea mizozo yetu tunayoishuhudia hapa leo, watu wengine wanafanya makosa halafu wanakuja kubebeshwa misalaba watu wengine. Hata yeye mwenyewe Mhe. Waziri anakuta msalaba huu tunaoujadili hapa sio wake, lakini kutokana na kuchelewa kwa mambo kama haya ndio yanayosababisha mizozo hii. Sasa wewe mwaka 2014 mwezi wa 9 mpaka leo watu hawa hakuna *action* yoyote iliyochukuliwa, unasubiri mpaka lini. Sasa watu hawa wakishakufa na pesa za serikali si ndio zimeshapotea kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kwamba suala hili lichukuliwe hatua za dharura, vyenginevyo Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai mwakani, siji kukutizama kama ni mwalimu wangu, nakuja kuzuia kikweli kweli. Ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa na langu moja ambalo nilizungumza kwa hisia na nafikiria nilifahamika. Swali langu lilikuwa dogo tu. Katika mchango wangu nilioutoa jana nilizungumza utaratibu mzima anaotumia Mkaguzi *CAG* katika kwenda kuzifanyia ukaguzi taasisi za serikali ambazo zinatakiwa zilipe fedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pesa. Nilisema taasisi hizi ambazo zinakwenda kukaguliwa na serikali, zinamlipa *CAG* kwa sababu *CAG* hana uwezo anahitaji kutumia *external auditors* kufanya hiyo kazi, ambapo yeye anatoa barua kwenda kwenye taasisi, halafu wanatakiwa walipe. Kwa bahati mbaya au nzuri zile taasisi za serikali zinakuwa zile fedha ambazo wanatakiwa walipe hawajaziweka katika bajeti zao za mwaka ule na fedha zenyewe sio kidogo.

Kwa hivyo, kwanza nilitaka kujua jumla ya fedha zote ambazo *CAG* amelipwa na taasisi za serikali ni kiasi gani, na katika fedha zile alizolipwa *CAG*, ni kiasi gani cha fedha wamezilipa hao *external auditors,* na katika hizo fedha zilizobakia amefanya nini, kama kafanya semina amezitumia kwa ajili ya

capacity building zilikuwa *amount* kiasi gani. Baada ya majibu hayo nitaweza sasa kutoa mchango wangu ambao nilikuwa nataka kutoa, kwa sababu hayo majibu sijayapata. Sasa naomba nipate hayo majibu, hayo majibu siyaombi nataka hayo majibu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimwambie Mhe. Simai Mohamed Said Mhe. mpendwa wa Jimbo la Tunguu kwamba, nakubaliana na maelezo yake ambayo ameyaeleza kwa kina na namuahidi kwamba tutampatia jawabu kwa njia ya maandishi ili aweze kuyafahamu zaidi. Ahsante.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naona kama moyo unaniuma. Mhe. Mwenyekiti, nasemaje mimi nimechangia jana saa 6:30 mpaka saa 6:55. Sasa naingia kwa undani hapa hatuondoki mpaka suala hili lieleweke. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kasoma bajeti, sisi huku wajumbe ma-*backbenchers* tumekwenda tumekagua mambo na tumefuatilia, wengine hili buku tulikuwa hatujui tumekwenda kusomeshwa. Tumeingia ndani tumefanya kazi, wote humu ndani wamekwenda kutafuta taarifa zao kwa kila njia ili tuweze kuisaidia serikali kutafuta hayo mapato na tumsaidie Waziri wa Fedha na Mipango.

Kuna fedha zimetumika ndani ya taasisi za serikali analipwa *CAG*, *CAG* anapokea pesa, nataka kujua ni kiasi gani, naambiwa nitaletewa kwa maandishi. Lakini hizi pesa zilizotumika zimetumika vibaya. Hapa sasa naanza kuona kuna mdudu mchafu. *CAG* amelipwa pesa ambazo hatujui zimetumika vipi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, taasisi za serikali naanza kuzitaja hapa *Zanzibar Revenue Board*, wanakusanya pesa wanasema wao ni wabaya, lakini wamelipa pesa nyingi sana kwa huyu *CAG, Zanzibar Insurance, State University of Zanzibar, Zanzibar Port Corporation*, sijui *ZAWA*, *ZECO*. Hawa wote wamelipa pesa kwa *Controller & Auditor General* ili wafanyiwe huo ukaguzi, hizi pesa yeye *CAG* anachukua *retainer* ili aweze kufanya yeye *training* kwa ajili ya hao wafanyakazi wake waliokuwa ndani. Lakini hizi pesa alizolipwa *CAG* sio pesa kidogo, na mimi kwa hesabu yangu nikizifikiria zinaweza kufika hata zaidi ya bilioni moja, lakini sina uhakika nazo. Kwa hivyo, nilitaka kujua hizi pesa zimetumikaje, na ni haki yetu sisi hapa kujua, kuambiwa zaidi ya mamilioni ya pesa nitajibiwa kwa maandishi. *This is the slap on my face*, napigwa kibao kwenye uso, palikuwa na masaa zaidi ya 24.

Leo Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anasema anahitaji pesa zaidi ya bilioni 800 kuendesha hii nchi kwa mwaka ujao. Tunataka kwenda kuwakamua wafanyabiashara wakati pesa inayotoka ndani ya serikali inatumika vibaya na hii sio pesa kidogo. Hapa lazima kieleweke, nataka majibu yangu, na muda ulikuwepo wa kutosha. Mimi siwezi kuunga mkono hapa suala la *CAG*, angalau nijue pesa zilikuwa kiasi gani ndio nitaridhika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, anapozungumza Mhe. Mjumbe kwamba tulikuwa na masaa 24, sio tatizo kusema tulikuwa na masaa 24, lakini tulitoa maelezo juu ya utaratibu unaotumika na naomba uniruhusu Mhe. Mwenyekiti, nisome hayo maelezo ambayo niliyatoa kwa ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti, kinachokosekana ni hizo *figures,* isingekuwa rahisi kwa mara moja, kwa sababu jana sisi tumeondoka saa 4:00 za usiku, hoja zilikuwa nyingi na leo asubuhi tumeanza na kazi hii tumekuja hapa hapa. Haiwezekani kuwa hapo na hapo tukaweza kufanya...

Mhe. Mwenyekiti: Hawakusikii vizuri Mhe. Waziri *mic*. Labda namuombea, waheshimiwa namuombea Mhe. Waziri aeleze akiwa kitako. Bora ukae Mhe. Waziri ili wakusike.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nilitoa maelezo ya ujumla na tunaambiwa kule tulikuwa masaa mengi, lakini tukumbuke kwamba hapa tumeondoka jana usiku, baada ya kumaliza nimekaa mimi na watendaji wangu mpaka usiku saa 4:00 ndio tumeondoka hapa. Tumerudi asubuhi mapema hapa kwa ajili ya kazi hii. Tumerudi mchana watu wameendelea kuchangia. Sasa ku-*accumulate* ile michango yote toka mchana hadi jioni saa 11:30 au 12:00 hadi saa 1:00, bado tunaendelea kukusanya, sio rahisi kupata hizi *data* kwa wakati mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, tumetoa maelezo ya jumla akiridhika nayo fahuwa, hakuridhika nayo tunamuambia tutamletea kwa maandishi hicho kiwango au *figures* anazosema.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya kazi zake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kwa mujibu wa sheria ya fedha ya 12 ya mwaka 2005. Kifungu namba 26(1)(c) kinampa uwezo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumruhusu mkaguzi au taasisi zenye sifa za ukaguzi kuchunguza na kukagua taasisi yoyote kwa niaba yake na hatimaye kuripoti kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, sheria imempa

uwezo huo kuchagua. Kuhusiana na mapato ya ukaguzi huingia moja kwa moja kwenye Mfuko mkuu wa Serikali.

Aidha, kuhusiana na malipo ya ukaguzi wa *ZRB* hadi hivi sasa hakuna malipo yoyote yaliyofanyika nasema tena Mheshimiwa. Aidha, kuhusianana malipo ya *ZRB* hadi sasa hakuna malipo yoyote yaliyofanyika. Utaratibu huu wa kuruhusu taasisi na ukaguzi kukagua kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi sio jambo geni duniani, ukaguzi ni jambo la kawaida.

Mfano wa taasisi kuu za ukaguzi zinatumia mfuko huu, *National Audit Office Tanzania*, *Auditor General* wa *South Africa, Auditor General* wa Nigeria. Mashirika ambayo yamekaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali kwa kutumia wakaguzi ambao wanafanya ukaguzi kwa niaba yake, Shirika la Bima, Benki ya Watu wa Zanzibar, Shirika la Umeme, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA*, Mfuko wa Barabara na Bodi ya Mapato.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa mwanzo wa wakaguzi walikuwa wakikagua kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, walikuwa wakikagua peke yao. Gharama na ada za ukaguzi huo zilikuwa zikilipwa kwa wakaguzi hao. Huu ndio utaratibu unaotumiwa na taasisi kuu zote za ukaguzi duniani.

Hata hivyo, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu nikaona iko haja ya kushirikiana na wakaguzi hao na kufanya ukaguzi wa pamoja, kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi wake na pia kuingiza mapato serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, mfano wa taasisi ambazo tunafanya ukaguzi wa mapato kwa pamoja ni Shirika la Bima, *SUZA*, Mfuko wa Barabara na sasa hivi tunaendelea na *ZRB*.

Mimi nadhani Mhe. Mjumbe aridhike kutokana na hali hiyo. Kwanza hao *ZRB* hawajatupa pesa hata moja haijafika kwa *CAG*, tutafanya tutakavyofanya zile ambazo tumezikagua kwa kutumia hao wakaguzi wa nje, tutakusanya hizo *data* kwa sababu si kidogo, tutakwenda nazo tutaleta kwa maandishi haraka iwezekanavyo.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, vitu viwili. Jambo la kwanza nilisema mwanzo sisi kama Wajumbe wa Baraza tunahitaji maelezo ya kina kujiridhisha. Matumaini wanayahitaji wananchi. Sasa kuna vitu viwili nataka nishauri.

Jambo la mwanzo hapa lipo jambo ndio maana na hizi *data* mimi sikuzipata tangu mwanzo, na nilizungumza tangu jana nilipoomba mchana. Nakubali mimi Mhe. Waziri hii wizara ni ngumu na ina mambo mengi na nampa pole kwa kazi nzuri aliyoifanya. Sasa kwa unyenyekevu mkubwa na kwa heshima kabisa, mimi nayakubali haya yote aliyoyazungumza na nitafurahi nikiyapata kwa maandishi. Lakini pia namshauri kitu kimoja, kwamba ikiwa kwa mujibu wa katiba ni kweli mkaguzi anatakiwa awe *independent* na afanye shughuli zake ili tuweze kupata taarifa kamili na sisi tuzipate.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu viwili kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu hana uwezo wa kuweza kufanya hii kazi, asichukue *External Auditor* kutoka nje, atafute njia ya kutafuta *Consultant* kuwafundisha vijana wetu, kwa sababu mwisho wa siku hapa kwenda taasisi mambo haya ya hesabu wako vijana ambao wataweza, wanahitaji usimamizi mzuri ili hizo ripoti zitoke ziwe zina uhakika na ziwe *independent.* Lakini hizi fedha ambazo zinakuwa kwa sisi na serikali ni fedha nyingi mno.

Kwa hivyo, watafute utaratibu baina ya serikali na *CAG* ili hichi kiwango ambacho hizi taasisi za serikali wanatakiwa walipe, japo kuwa kasema wengine hawajalipa, lakini wanachotakiwa wakilipe inawezekana kitakuwa ni kingi, angalau upatikane muafaka mzuri *CAG* afurahi hiyo *retainer* anayochukua iwe ya kiasi, afanye *capacity building*, baada ya mwaka mmoja au miwili tuwe tuna watu wetu, halafu hiyo kazi iende. Lakini kitendo cha pesa kulipwa kupita kiwango angalau kiangaliwe kwa hicho ambacho kitakuwa ni stahiki. Tumemalizana ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia nilimwambia Mhe. Waziri atakapokuja atwambie kwa sababu Ofisi ya *CAG* nayo inakaguliwa na ina ripoti yake inatakiwa iwasilishwe ndani ya chombo hiki. Sasa nilimuuliza Mhe. Waziri ni lini ripoti ya ukaguzi ya Ofisi ya *CAG* itawasilishwa Barazani, kwa maelezo hayo naomba kupata ufafanuzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri ni lini ripoti ya *CAG* itawasilishwa ndani ya Baraza ndio swali lenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, siwezi kutoa siku kwa sasa hivi, kwa sababu ni lazima nikae na *CAG* na wahusika ili tupange utaratibu mzuri. Kwa hivyo, itakapokuwa tayari wakati wowote naahidi kwamba itawasilishwa hapa, kwa

sababu kiutaratibu anaweza akakaguliwa hakuna matatizo, na hilo wala halina pingamizi. Lakini nilipitiwa labda sikuliandika vizuri, suala hili sikulifahamu inawezekana alivyochangia. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi tutalifanyia kazi na tutaliwasilisha tu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri, lakini namuuliza Mhe. Waziri haoni kwamba taarifa hiyo kutokuletwa hapa inakiuka sheria ya *Public Finance Act* Ibara ya 36 kifungu cha 4?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema, hili jambo tutalifanyia kazi kwa sababu sidhani kama imewahi kufanyika kazi kama hii ya kukaguliwa Ofisi ya *CAG*.

Mimi ndio nimelipata na nitalifuatilia ili kuhakikisha kwamba jambo hilo tunalifanya, kwa mujibu wa sheria tutafuata kutekeleza sheria na kanuni zetu zote, ili kuhakikisha kwamba taarifa hizo tunazileta hapa. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, sijasimama kwa ajili ya kupiga buti. Lakini nimesimama kwa ajili ya muongozo wako, naomba tutumie Kanuni ya 136 ili tuwaruhusu watendaji ambao wako juu ya wizara hii kuingia kwenye ukumbi kwa ruhusa yako, kwa kutumia Kanuni ya 136, ili iwe rahisi kumsaidia Mhe. Waziri baada ya *information* ambayo anatakiwa kujibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naona umeshangaa kidogo, hili jambo sio geni ni la kawaida tu.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, sijashangaa kwa sababu ya ugeni wake. Maana yake nafikiria ili tufanye hivyo, nirudi nikavae ili tulirejeshe Baraza.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Hapo hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Naam. Hapo hapo. Haya basi ruhsa. Mshangao wangu ni ule utaratibu tu.

Katibu Mezani: Wanaingia wanakaa nyuma kule.

(Anaongea kwa sauti ya chini na Mhe. Mwenyekiti).

Mhe. Mwenyekiti: Wanamsaidiaje.

Katibu Mezani: Kuandika *memo* kwa haraka kuliko kupanda juu kule inachukua muda mrefu.

(Anaongea kwa sauti ya chini na Mhe. Mwenyekiti)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa wakati hilo linafanyika tunaendelea Waheshimiwa Wajumbe.

FUNGU G06		AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI	
Kifungu	PG 0601	Programu Kuu ya Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma	
Kifungu	SG 060101	Progamu ndogo ya udhibiti wa Fedha na rasilimali za umma	1,106,765,000
Kifungu	PG 0602	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa udhibiti na ukaguzi	
Kifungu	FG 060201		

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kutokana na muda ulikuwa mdogo kuna baadhi ya maswali yangu niliyapeleka kwa maandishi kwa Mhe. Waziri, sasa nilikuwa tu nataka ufafanuzi, kwa sababu katika Baraza lililopita kutokana na kadhia ya ubadhirifu, tulimuomba *CAG* atufanyie ukaguzi ili kubaini kama kuna wafanyakazi hewa na mishahara hewa.

Sasa ile taarifa haijaletwa Barazani, na Mhe. Spika, alimuagiza *CAG* kupitia Waziri kipindi kile aende akafanye ukaguzi, na mimi nakumbuka ukaguzi ulifanywa na ile ilipelekea mpaka watumishi wakawa wanatakiwa waende na vitambulisho vya Uzanzibari na nini, ili ibainike kama kuna wafanyakazi hewa na mishahara hewa. Sasa hili hebu tulikuwa tunataka maelezo ili tuweze kujiridhisha baadae tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kwanza hicho ki-*note* alichoniletea Mheshimiwa mimi sikukipata, isipokuwa nataka nimjibu tu kwamba suala la wafanyakazi hewa sasa hivi tumempa kazi *CAG* aanze kufanya tena, ameshafanya hatua ya mwanzo lakini tungoje na hii ya pili ikamilike zije kwa pamoja, zote tuziwasilishe kwa pamoja hapa Barazani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Daa! Unajua nimeshituka sana Mhe. Waziri aliponambia *notes* zangu hakuzipata maana kulikuwa kuna hoja kama tatu nilizipeleka pale, sasa labda utaratibu wa humu sijui alikuwa anapokea nani, labda kuna Waziri wa Katiba na Sheria wawili humu, lakini basi mimi nafikiri nimeridhika na majibu yake kwa kuwa ile kazi imefanyika, na kwa kuwa amesema kwamba umefanyika ukaguzi wa mwanzo na unaendelea ukaguzi wa pili, labda ikishamalizika atueleze ukaguzi wa pili hiyo ripoti yake italetwa lini.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Huo ukaguzi wa pili ndio haujaanza utakapoanza tu tutawasilisha taarifa kwamba unaanza wajue tu kwamba unaanza, lakini ukishakamilika tu tutawasilisha ripoti hiyo msiwe na wasi wasi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa hivyo ina maana ule ukaguzi wa mwanzo utakusanywa au utakuwa ajuwar ama na wa pili utaletwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ukaguzi wa mwanzo ushakamilika tusubiri kabisa ufanywe na wa pili halafu walete kwa pamoja ndicho alichokizungumza Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kama ni hivyo mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti Tuendelee.

Kifungu SG 060201	Programu ndogo ya usimamizi na uendeshaji wa udhibiti na ukaguzi	641,741,000
Kifungu SG 060202	Programu ndogo ya udhibiti na ukaguzi Pemba	496,294,000
	JUMLA YA FUNGU	**1,138,035,000**
	JUMLA KUU	**2,244,800,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G O7 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI

Kifungu PG 0701	ProgramU kuu ya kupunguza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi	117,523,000

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti wakati nilipochangia niliuliza swali kwamba nilitaka nijibiwe wala rushwa na wahujumu uchumi wangapi wamehukumiwa, kwa sababu Serikali imekuja na azma njema kabisa ya kuanzisha hii taasisi, lakini *outcome* ya hii taasisi hatuioni, wezi wa kuku

tunawasikia wanatangazwa asubuhi kunako mawio, wezi wa ndizi tunawasikia. Lakini wala rushwa na wahujumu uchumi wapo na hatusikii kuhukumiwa, kwa hivyo nataka kujua wangapi wameshitakiwa mpaka leo.

Mhe. Mwenyekiti: Subiri Mheshimiwa atutafutie *data*, tustahamili Waheshimiwa tumeshamla ngombe mzima umebakia mkia.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, taarifa ambayo ilikuja ni suala la mapolisi na suala la rushwa ambalo ndilo tulilolitolea ufafanuzi, sasa hili jengine kama amelileta naomba aniite tena tuliangalie.

Mhe. Mwenyekiti: Ametaka kujua wahujumu uchumi wangapi waliohukumiwa au vipi?

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tunawasikia wezi wa kuku wanatangazwa kunako mawio, lakini mila rushwa na mihujumu uchumi ipo na hatusikii imeshitakiwa hata siku moja, tunataka kujua wangapi wameshtakiwa tangu hii taasisi imeanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa mkipiga makofi wakati anamalizia swali lake kipande hicho anakuwa hakisikii Mhe. Waziri, kwa hivyo anakuwa anashindwa kumjibu, mngemuacha akamaliza kwanza hilo swali halafu mkashangiria baadae.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako taarifa ambazo tumezipata zinasema kwamba hakuna hukumu iliyotolewa na kesi zinaendelea Mahakamani, na nyengine zinaendelea kwa uchunguzi, kwa hivyo hakuna hukumu iliyotolewa mpaka sasa hivi hata moja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, inaonesha hii kitu kama tunachezewa, kesi ziko Mahakamani tangu taasisi hii imeanzishwa, tunaomba apewe meno.

Mhe. Mwenyekiti: Naam!

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tunaomba tutafutiwe utaratibu wa kubadilisha Sheria kama kweli nchi hii imedhamiria kukomesha mila rushwa na mihujumu uchumi, ili wapewe meno hii taasisi wapeleke wenyewe Mahakamani hizi kesi.

Otherwise itakuwa tunachezea kwa sababu hii mila rushwa na mihujumu uchumi itaendelea kuwepo bila ya kuwapa meno.

Mheshimiwa tunaomba utafutwe utaratibu wa kuipa meno hii taasisi kama kweli tuna dhamira ya wakwezi na wakulima wawe salama katika hii nchi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na naamini kabisa Mhe. Hassan anatambua kama mashtaka ya jinai kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Katiba amepewa uwezo Mkurugenzi wa Mashtaka kuyashughulikia mashitaka yote ya jinai.

Kesi inazopokea kwenye mamlaka ya rushwa na uhujumu uchumi ni kesi za jinai, na ukisoma ile sheria yao pia wao kazi yao ni kufanya uchunguzi, wanapokamilisha uchunguzi wao wanapeleka sasa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye yeye kwa mujibu wa Katiba ndio mwenye mamlaka ya kufungua kesi hizi za jinai. Sasa huo ni utaratibu wa kikatiba ambao amepewa Mkurugenzi wa Mashtaka kushughulikia kesi hizi za jinai zikiwemo hizi ambazo zinatoka kwenye taasisi ya rushwa, sasa ni utaratibu kidogo wa kikatiba ambao umeelezwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Nimesikia majibu mazuri sana ya Mhe. *AG* lakini Katiba tumetunga wenyewe, na kila mtu anajua umuhimu wa kuyakomesha haya mala rushwa na wahujumu uchumi. Mhe. Rais Magufuli aliiomba nakumbuka siku aliyokutana na Mwanasheria Mkuu, alimuomba kwamba ianzishwe Mahakama Maalum, sasa uzuri wenyewe tunaye Mwanasheria Mkuu humu ndani, na leo kama sikosei iko Bungeni ile hoja ya kwenda kuanzisha Mahakama mpya.

Na mimi namuomba *AG* atafute mazingira au *process* ianze haraka iwezekanavyo kama kweli tuna nia njema, kama tumeweka tu haya, tuanzishe Mahakama ya wala rushwa na wahujumu uchumi na Mahakama wanaofanya vitendo vile vya kudhalilisha hasa watoto wadogo tuzianzishe hizo Mahakama kama kweli tuna lengo la kuvikomesha hivi vitu, kama tuna blaa blaa tu basi, lakini naomba Mwanasheria Mkuu atupe *process* ya kuanzisha hivi vitu.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee au vipi?

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sisi tunachotaka isipite kwa *DPP*, ikiwa mpaka leo mimi kama sikosei tangu imeanzishwa hii taasisi.

Mhe. Mwenyekiti: Nimeshakufahamu Mheshimiwa, ushaeleweka hivyo ulivyoliweka, lakini sasa nilichokuwa sijafahamu uliacha tuendelee au unataka bado kupata maelezo ya Serikali.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tunataka ufafanuzi wa *AG*, kwa sababu hii ni kadhia kubwa ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, tumeingia kwenye kuanzisha Mahakama au tuko wapi, maana lile la utaratibu wa kuendesha kesi za jinai nadhani nimelieleza, kama ni utaratibu wa kikatiba na mwenye mamlaka kwa mujibu wa Katiba ni Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Mwenyekiti: Ameshauri sasa tuanzishe Mahakama.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, jambo la kuanzisha Mahakama linaendana na *volume* ya kesi zenyewe ambazo zipo na ambazo zinatakiwa kushughulikiwa kwa uharaka wake, nadhani Mheshimiwa Waziri ametoa majibu mazuri, kama kwa sasa hivi kesi ambazo zinashughulikiwa bado hazijafika kwenye *volume* kubwa ya kufanya sasa tuwe tuna Mahakama maalum ya kushughulikia watu hawa.

Nadhani kesi hizi zitapozidi ukubwa wake, wala mimi sioni kama ni tatizo kubwa la kufungua Divisheni ya Mahakama Kuu ambayo itakuwa inasimamia kesi hizi maalum za rushwa, kwa sababu tu mambo yenyewe haya bado hayana *large scale* ya kuyashughulikia, ndio maana tumekuwa tunakwenda kwenye utaratibu huu huu wa Mahakama ambao upo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, anajitahidi Mwanasheria Mkuu lakini hili suala zito, kwa hivyo kama kuanzisha Mahakama ni *process* kubwa turekebishe sheria, sheria ije tena hapa tumruhusu Mwanasheria Mkuu kesi zake apande nazo mwenyewe Mahakamani kuliko kupitia *DPP*, kwa sababu inaonesha pale kwa *DPP* ndio zinakwama na zinakufa, mamlaka ya rushwa hii yaani iwe inapeleka wenyewe kesi zake Mahakamani, hizi sheria ni zetu tunaweza tukabadilisha kama kweli hili jambo tuna nia nalo safi sheria hiyo ije, kama Mwanasheria Mkuu anasema kuanzisha Mahakama ni *process* refu, basi ije sheria turekebishe tumpe meno mdhibiti rushwa aende mwenyewe Mahakamani, ili tupate kuwakomesha wakwezi na wakulima wanapata shida sana kwa wala rushwa, kazi zao zinabanwa kwa kitu hicho.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Hassan atakubaliana na mimi utaratibu wa kisheria ulivyo, kwa mfano nitoe tu mfano

sisi kazi zetu hapa ni kupitisha sheria lakini sisi sio tunaokaa hapa kutafsiri hizo sheria, kuna chombo chengine ambacho kinafanya kazi hizo nacho ni Mahakama.

Utaratibu wa kuendesha kesi za jinai ni hivyo hivyo, Polisi au Mkurugenzi wa Mamlaka ya Rushwa na taasisi yake wamepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya uchunguzi, wanapomaliza sio wao wanaoziendesha kesi zile. Inabidi sasa wao wakapeleke kwenye chombo chengine ambacho ni *independent* kitasimamia uendeshaji wa mashtaka. Na huko nyuma tulikotoka ndio maana tukaondoka kwenye huo utaratibu, ilikuwa kesi zote Polisi yeye ndio anashtaki, yeye ndio anayefanya uchunguzi, lakini tukasema utaratibu huo hautufai.

Na ndio utaratibu huu huu unaotumika kwa taasisi hizi nyengine ambazo zimepewa mamlaka ya kipolisi ya kuweza kufanya uchunguzi, sasa utaratibu uliokuwepo sasa hivi wa kisheria ni huo kama Mamlaka ya kuzuia rushwa na wahujumu uchumi mamlaka iliyopewa kwa mujibu wa sheria yao ni kufanya uchunguzi, na inapomalizika kuna chombo *independent* ambapo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ndio iliyopewa mamlaka tena ya Kikatiba ya kuendesha mashtaka yote ya jinai, sasa mimi sikuona kusema kweli kama utaratibu huu ni mbaya. Kwa sababu kama kuna ushahidi wa kutosha hata Mkurugenzi wa Mashtaka atazipeleka tu kesi hizo Mahakamani nakushukuru.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Majibu mazuri sana Mwanasheria Mkuu ameyatoa, yanapendeza, lakini hili jambo ni kubwa, sasa nataka kumpa ajifundishie wapi aende akasome kwa Wamarekani kesi ya madawa ya kulevya haipitii kwa *DPP* moja kwa moja, ina-*run* katika *court,* kwa hivyo hili jambo si jipya duniani bado linawezekana, nasema tena kama kweli tuna nia ya kufanya hilo jambo si jipya na linawezekana akajifunze Marekani naomba.

Kifungu FG 070101	Programu ndogo ya kupunguza vitendo vya rushwa na wahujumu uchumi	117,523,000
Kifungu PC 0702	Programu Kuu ya Utawala na uendeshaji katika mapambano ya rushwa na wahujumu uchumi	818,777,000
	JUMLA KUU	**936,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G 08 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu PG 0801	Programu kuu ya usimamizi wa mifumo ya Rasilimali watu katika utumishi wa umma	369,181,000
Kifungu PG 0802	Programu kuu ya Utawala na Uendeshaji Kamisheni ya Utumishi	440,019,000
	JUMLA KUU	**809,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU G 09 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Kifungu PG 0901	Programu Kuu ya usimamizi wa Watumishi Serikalini	123,900,000
Kifungu SG 090102	Programu ndogo ya usimamizi wa Uajiri kwa watumishi wapya Serikalini	57,520,000
	JUMLA KUU	**181,420,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PG 0902 Programu kuu ya utawala na uendeshaji wa Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa wakati nilipochangia hoja yangu nilieleza kuhusu Chuo cha Utumishi Serikalini, na Mhe. Waziri alikuja hapa akakiri kwamba yale yote niliyoyasema yalikuwa ni kweli, lakini akatoa mfano akasema wale wezi walioiba wamerejeshwa Wizara ya Fedha huko Wizara fedha ndio wakafanyiwe, sasa unapomrejesha mwizi kwengine pesa hizi zilizoibiwa za walipa kodi, kwanza suala la kwanza ndio zimerejeshwa.
Suala la pili alipoibiwa ni Taasisi yake, yeye anachukua hatua gani, kwanza hoja yangu ya kwanza pesa ni za walipa kodi kwanza lazima zirudi, kwa hivyo ana utaratibu gani wa pesa zile kurudi, lakini pili kaibiwa yeye sasa anamuachia mtu mwengine, yeye anachukua hatua gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, anazungumzia Chuo cha Utumishi hapa

tupo kwenye Tume ya Utumishi, sasa nadhani kifungu hichi anachokitaja sicho, naomba radhi sana kwamba hili si mahali pake twende kwa utaratibu na kanuni zetu, hapa sipo.

Mhe. Mwenyekiti: Unahoji pahala sipo umeulizia Chuo cha Utumishi hii ni Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, chuo kina fungu kwani hapa ni utawala na hichi Chuo sijaona fungu lake mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Ilikuwa ushike Mshahara wa Waziri.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hapa kushika kuna makosa gani kikanuni.

Mhe. Mwenyekiti: Hapo sipo.

Hassan Khamis Hafidh: Kikanuni Mheshimiwa hapa kupashika kuna makosa gani naomba nipate ufafanuzi?

Mhe. Mwenyekiti: Kwa sababu ni vifungu tunapitisha lile fungu linalohusika, kwa mfano kama lilikuwa halipo hapa ilikuwa ushike mshahara wa Waziri, lakini sasa tumeshapita kote huko, yaani wakati ule uliposhika mshahara wake wakati ule ndio ilikuwa ije hiyo hoja yako.

Kifungu FG 090201	Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Utumishi Serikalini	236,480,000
	JUMLA KUU	**417,900,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(*Baraza lilirudia)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali Makadirio hayo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba hoja iamuliwe wale wote wanaokubaliana na hiyo hoja wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi karibu ni saa 4.30. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, lakini pia nikupongezeni Waheshimiwa Wajumbe kwa ustahamilivu na mivutano ya hapa pale, lakini yote hiyo ni muhimu ili wananchi waone kwamba maana yake kuna watu wengine ndani ya vichwa vyao walihisi kwamba hii kazi itakuwa haifanyiki kwa nguvu kama hii, lakini sote tutakubaliana kwamba pamoja na kwamba tupo wenyewe lakini kazi imekuwa nzito.

Uzito huu pamoja na zile hoja mlizokuwa mkizitoa ni ushahidi tosha kwamba hiyo kazi waliyokutumeni wananchi mnaifanya kwa moyo mmoja. Bila ya kujali kwamba Serikali iliyoko Madarakani ni yenu nyinyi yaani ya Chama chenu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe mimi nina kumbukumbu niliwahi kuwa Waziri katika kipindi kama hichi, kipindi hicho ambacho tulikuwa wenyewe kilikuwa ni kipindi kigumu kuliko hicho kipindi ambacho walikuja na wenzetu tukashirikana nao kwenye kazi. Kwa hivyo napenda sana kuwaambia Waheshimiwa Mawaziri wajiandae vizuri sana, kwa sababu Waheshimiwa wapo hapa kwa ajili ya kazi.

Kwa hayo machache na baada ya kuwapongeza napenda sana nichukue nafasi hii pia nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili kwa kutustahamilia muda wote huo tuko nae, pamoja na Mawaziri wote kwa msaada ambao walikuwa wanautoa pale ambapo walikuwa wanahisi Waziri mwenzao anahitaji msaada, kwa hivyo walikuwa kitu kimoja katika kusaidiana kwenye hili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe pia nikushukuruni sana kwa namna ambavyo mlikuwa mnashirikiana kuhakikisha zile hoja zinapata majibu yale ambayo mnayataka. Kwa maelezo hayo machache Waheshimiwa Wajumbe napenda niahirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka kesho siku ya Ijumaa saa 3.00 Asubuhi.

(Saa 4:22 Usiku Baraza liliahirishwa mpaka
Tarehe 03/06/2016 Saa 3:00 Asubuhi)